**26 MEI, 2022**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

**Kikao cha Thelathini na Moja – Tarehe 26 Mei, 2022**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**MHE. JULIANA D. SHONZA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara

ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimuite sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa. *(Makofi)*

Tutaanza na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Jimbo la Tarime Vijijini.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba nimuulize swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali imetimiza sera muhimu ya uwekezaji nchini na hasa katika sekta ya madini. Katika kutimiza azima hiyo, wawekeza wamekuwa wakichukua maeneo ya watu maeneo kama kule Kabanga, Sumbawanga na kule Nyamongo, lakini maeneo hayo imechukua muda mwingi sana ama kuchelewa kulipwa au kutokulipwa kabisa fidia za wananchi.

Mheshimiwa Spika, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba wananchi ambao maeneo yao yametwaliwa kwa muda mrefu na wawekezaji waweze kulipwa fidia yao na waweze kutimiza kupata haki yao ya kukaa katika maeneo hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwita Waitara, Mbunge wa Tarime Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sera yetu, sheria za ardhi pamoja na uwekezaji nchini ziko wazi. Kwamba pale inapotokea mwekezaji yeyote anahitaji kutumia ardhi, ardhi ambayo ina mmiliki halali na shughuliki yake anaifanya, labda kwa kilimo, alijenga nyumba za makazi au uwekezaji kama ulivyosema, pindi ardhi hii inapotakiwa; iwe na Serikali au mwekezaji ni lazima apate fidia.

Mheshimiwa Spika, utaratibu unaotumika, baada ya kuwa mwekezaji ameomba kulitumia eneo hilo, uthamini utafanywa na mthamini wa Serikali, gharama zitapatikana na mhusika wa ile ardhi atahusishwa. Thamani ile ikishapatikana, kama ni Serikali, Serikali italipa, na kama ni mwekezaji atapewa ile gharama ya ule uthamini uliofanywa na atapaswa kulipa.

Mheshimiwa Spika, umetamka maeneo mengi, na mimi nimepata nafasi ya kupita maeneo kadhaa, tumekuta baadhi ya Watanzania waliokuwa wanamiliki ardhi kihalali wametoa ardhi yao kwa shughuli hizo za uwekezaji. Iwe ni kwenye madini au kwa shughuli nyingine yoyote ile ili mradi ni uwekezaji hawa wote wanapaswa kulipwa. Na nitoe wito kwa Wizara ya Ardhi ambayo ndiyo inasimamia sheria, kuhakikisha kwamba Watanzania ambao wanachukuliwa ardhi yao waliyomilikishwa kihalali, ni lazima walipwe fidia ya ardhi yao ili haki iweze kutendeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na ni muhimu sasa pia hata kwa mamlaka za Serikali za Mitaa pale ambako wananchi wapo wamechukuliwa ardhi yao kwa uwekezaji, kwa shughuli

nyingine yoyote ile na wanahitaji kulipwa fidia, ni lazima haki yao waipate kwa kulipwa fedha hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikuhakikishie kwamba inapotekea kuna madai kama bado madai yatolewe. Na hasa kama kumefanyiwa uthamini basi ile thamani ya ile ardhi au thamani ya ile mali iliyochukuliwa kwa ajili ya kupisha kwa shughuli nyingine ni lazima iweze kulipwa. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kunipa nafasi kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ongezeko kubwa sana la vituo vya afya na zahanati nchini baada ya kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ametoa fedha za UVIKO-19. Palipo na mafanikio changamoto hazikosekani. Kumekuwa na uhaba mkubwa wa watumishi wa kada ya afya.

Mheshimiwa Spika, je, ni nini mkakati wa Serikali kukabiliana na changamoto hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Mnzava, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza nikiri kwamba Serikali, na kwa maelekezo ya Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ya kutaka kuboresha huduma za afya Serikali imefanya uwekezaji mkubwa kwenye maeneo ya kutolea huduma, zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya, hospitali za mikoa na hospitali za kanda, lakini pia hospitali

kuu kama vile Benjamini Mkapa na maeneo mengine tumepanua maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, tunatambua uwekezaji huu ni mkubwa. Tumeanza na kuweka miundombinu, tumepeleka vifaa na maeneo mengine bado vifaa vinapelekwa, na mimi nimefanya ziara maeneo mengi, nimekuta vituo vya afya, zahanati hata hospitali bado tunaendelea kupeleka vifaa. Hata hivyo, vifaa hivi lazima viende sambamba na watumishi wa kada hii ya afya ambayo umesema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi wakati wa bajeti ya Wizara ya Afya hapa tumepata taarifa kwamba Mheshimiwa Rais, mama Samia Suluhu Hassan ameshatoa kibali cha ajira, na kibali hiki kiko kwenye sekta za afya, elimu, kilimo, fedha na utawala. Kwa hiyo, tunatarajia baada ya kibali hiki kuwa kimeshakamilika taratibu zake tutapeleka watumishi wa afya kwenye maeneo haya yote mapya ili huduma ianze kutolewa kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niungane na Watanzania wote wanamshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya kwenye sekta ya afya. Anataka kuona jamii ya Watanzania ikipata huduma kwenye maeneo yao kwa ukaribu, anataka kuona Watanzania wanatumia gharama ndogo kwa kupata huduma karibu na maeneo yao, na sisi tuendelee kumuunga mkono kama ambavyo tunamuunga mkono na tuamine kwamba mkakati huu wa Serikali wa kupeleka watumishi wa umma utakamilika katika kipindi kifupi sana kijacho. Hii ni kwa sababu tayari fedha ipo (Hapa ilikata) kwa sababu tayari fedha ipo na Waheshimiwa Wabunge mmeridhia. Jukumu letu kuanzia tarehe mwezi wa saba na kutoa fedha na ajira ipatikane na watumishi waanze kazi. Ahsante sana *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Assa Nelson Makanika, Mbunge wa Jimbo la Kigoma Kaskazini.

**MHE. ASSA N. MAKANIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inapitia katika wakati mgumu wa kuagiza mafuta ya kula nchi nyingine. Zaidi ya nakisi 250,000 mpaka 300,000 za mafuta ya kula zinaagizwa nchi zingine ambapo tunatumia zaidi bilioni 480 kuagiza nakisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika kupunguza uagizwaji wa mafuta ya kula, bonde la Tanganyika, kwa maana ya Mikoa ya Rukwa, Kigoma na Katavi, ina ardhi nzuri sana ambayo ikitumiwa vizuri inaweza ikasaidia nchi katika kupunguza nakisi hii. Je, ni nini mkakati wa Serikali katika kuwakaribisha wawekezaji wakubwa ili kuweze kusaidia kupunguza nakisi ya kuagiza mafuta hayo nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Makanika, Mbunge wa Kigoma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Makanika ni shahidi wa jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali sasa za kuhamasisha kilimo cha michikichi ambacho pia kinatoa mazao haya ambayo pia yanakamua mafuta kwa lengo kudhibiti nakisi hiyo tuliyonayo ya upungufu wa mafuta hapa nchini, au kupunguza kiwango cha uagizaji mafuta kutoka nje. Tayari zoezi hilo tumelisimamia vizuri na mimi mwenyewe nimekwenda Kigoma mara kadhaa, nimehamasisha kilimo, tumeanzisha kituo cha utafiti, tumezalisha na mbegu na tumesambaza kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, na sasa tumeanza kupata matumaini. Nimekwenda kwa mara ya mwisho nimekuta

michikichi inaanza kuiva, kwa hiyo, tayari sasa kwa jitihada hizi. Lakini chikichi haistawi tu pale Mkoani Kigoma, pamoja na mikoa hiyo ya Katavi na Mpanda lakini na miko yote ambayo inalima zao la nazi inaweza pia kustawisha zao la chikichi.

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kuwahamasisha wakulima waliopo maeneo hayo yanayolimwa minazi walime pia na michikichi. Tunaamini kampeni hii ambayo tunaendelea nayo ambayo pia Watanzania wanaopenda kilimo wakiendelea kupanda michikichi tutapunguza nakisi lakini pia tutaokoa na fedha tunazozitumia kuagiza mafuta nje. Sasa nini kinafanyika sasa, kwanza tunahamasisha wakulima wadogo wadogo wenye uwezeo wa kulima eka moja, mbili mpaka kumi, mia. Tunatoa wito kwa wawekezaji wa ndani na wa nje kuja kuwekeza nchini Tanzania. Tuna ardhi ya kutosha, hata kule Kigoma tuna ardhi ya kutosha Mpanda tuna ardhi ya kutosha, Katavi tuna ardhi ya kutosha, Sumbawanga nako pia tuna ardhi ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunatoa wito kwa wawekezaji kuja nchini Tanzania kuwekeza kwenye kilimo cha michikichi ili tuweze kuzalisha kwa wingi, tukamue na tuweze kupata mafuta yetu sisi wenyewe, na tunaamini gharama itakuwa ndogo na zile fedha ambazo tunapeleka nje kuagiza mafuta hazitakwenda tena na badala yake zitaingia kwenye mzunguko wa uboreshaji wa miradi ya utoaji huduma hapa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba kampeni ile inayoendelea Kigoma bado inaendelea kwa kutoa wito kwa wawekezaji. Ardhi tunayo, na wakuu wa mikoa na wakurugenzi wamepata taarifa; watenge ardhi kwa ajili ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, lakini sasa tunaenda kwenye viwanda vya ukamuaji. Kwamba, badala ya ile teknolojia ya

kushika miti wanazunguka hivi, ambayo nimeishuhudia kule Kigoma, nataka tubadilishe iwe mashine ili iweze kukamua kwa asilimia angalau 99 ya ukamuaji, badala ya ukamuaji wa sasa wa asilimia 70. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitoe wito kwa Watanzania kujitokeza kulima. Mara kadhaa nimesema, kama unataka kuwekeza kwa ajili ya manufaa ya mtoto wako ambaye yuko shule leo lima mchikichi, mpe shamba la mchikichi, mtoto huyo anapomaliza darasa la saba tayari ana shamba lake la eka mbili, tatu, nne, anapokwenda kidato cha kwanza mpaka cha nne anakuta shamba lake lipo, hata anapokwenda chuo kikuu anakuta shamba lake lipo na anaanza kuvuna yeye mwenyewe, na linavunwa lile zaidi ya miaka 30. Kwa hiyo, ni uwekezaji mzuri mkubwa na niendelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mbunge wa Jimbo la Bahi.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, nchi nyingi duniani zimerusha *satellite* angani kwa matumizi mbalimbali ikiwemo kupata takwimu sahihi za hali ya hewa. Katika anga la Afrika kwa sasa tuna *satellite* 41 na kati ya hizo 41 mbili zinatoka katika mataifa ya Afrika Mashariki. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuanza na programu ya kutengeneza *satellite* na baadaye tuweze kuirusha katika anga letu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kenneth Nollo, Mbunge wa Bahi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa anahitaji kujua maendeleo ya teknolojia kwenye mawasiliano. Ameeleza kwamba nchi nyingine tayari zimejitegemea katika kununu mitambo inayowezesha nchi husika kuboresha mawasiliano yake. Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo zinaendelea kwa kasi katika maboresho ya *TEHAMA,* na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kazi moja kubwa aliyoifanya ni kuanzisha Wizara ya Sayansi, Mawasiliano na Teknolojia ambayo pia ina habari mawasiliano na teknolojia ya habari ambayo pia inaendelea kufanya ufuatiliji wa maeneo ambayo tayari tunayo na maeneo ambayo bado hayapo kwa lengo la kufanya maboresho. Na Wizara, kama ambavyo inaendelea kufanya kazi yake na imeshapitishiwa bajeti yake, na Waziri hapa ameeleza maboresho makubwa yaliyofanywa nchini. Lengo hii teknolojia kufikisha kwa Watanzania mpaka vijijini. Tumeanza na teknolojia ambayo inawezesha kufanya mawasiliano maeneo yote, na tunapanua wigo huu mpaka kwenye ngazi za kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nikuhakikishie kwamba maeneo yote ambayo nchini sasa hayapo ambayo yanahitajika katika kuboreshwa mfumo mzima wa mawasiliano Serikali itafanya maboresho kutafuta fedha zaidi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba teknolojia tunaipandisha na teknolojia inawafikia wananchi wote mpaka kule vijiji, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kumuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwa vile nchi yetu ni ya pili katika Afrika kwa uzalishaji wa mifugo na kwa vile ina wafanyabiashara wengi wa mifugo wanaokwenda katika

nchi mbalimbali kama vile Kenya, Madagascar na Comoro. Je, Serikali ina mkakati kuimarisha usafirishaji wa mifugo hiyo na bidhaa zake ili kudumisha biashara hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge alipokuwa anazungumza kulikuwa na makofi mengi, kwa hiyo, sikumsikia vizuri maneno ya mwisho, naomba nilisikie lile swali ili niweze kulijibu vizuri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, rejea swali lako.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana; je, Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha usafirishaji wa mifugo na bidhaa zake kwenda nchi mbalimbali ili kuimarisha biashara hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwinyi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge amezungumzia sekta ya mifugo na pia ametaka kujua Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha usafirishaji, na vile vile amezungumzia masoko. Ni kweli kwamba nchi yetu ina mifugo mingi sana; ina ng'ombe wengi wa kutosha, mbuzi, kondoo na wameingia kwenye soko la kuuza ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kufanya maboresho makubwa kwenye biashara hii ambapo baadhi ya Watanzania wamejihusisha nayo kwa kusafirisha mifugo hii. Inaweza ikawa wanasafirisha mifugo hai au baada ya kuwa wamepitisha viwandani. Sasa mkakati wa kuboresha usafirishaji, wote tunajua, kuna kazi kubwa tunaifanya ya

kuboresha usafirishaji kwa njia ya ndege na sasa tunajenga pia reli ambayo inakwenda mpaka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, tunachokifanya sasa ni kuhakikisha kwamba tunatafuta masoko nje ili kuwezesha kufanya biashara hii na kila mmoja atatumia usafiri ambao anauona ni rahisi kufika kwenye nchi anakohitaji kupeleka mifugo hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali inachokifanya sasa, kwanza ni kuhakikisha ufugaji wa ndani unakuwa bora, unaweza kutoa mifugo yenye afya, uwezo na yenye thamani kubwa. Vile vile kazi kubwa tunayoifanya ni kuimarsiha mifugo hii iwe thamani kubwa kuhamasisha wafugaji kufuga kisasa zaidi ili mifugo hii iweze kuwa na thamani. Kwa hiyo, kazi zote ambazo tunazifanya kwa pamoja za kuimarisha ufugaji, ufugaji wa kisasa, kuhakikisha pia tunapeleka viwandani kwa wale wanaotaka kupata nyama au kusafirisha mifugo iliyo hai kupitia njia zetu za usafiri, sisi tumetoa kibali kwa Mtanzania yeyote anayetaka kuingia kwenye uwekezaji huo, afanye hilo ili iweze kumletea tija kwenye shughuli yake ya kila siku ya kibiashara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niendelee kutoa wito kwa wafugaji. Jana jioni nilikuwa na wafugaji kama 60 hivi tukizungumza namna bora ya uboreshaji wa mifugo hii. Kwa hiyo, naamini ufugaji kupitia Wizara ambayo imemaliza bajeti yake hapa jana, wataendelea kusikiliza maboresho yaliyotamkwa hapa ili wafugaji sasa waweze kuzalisha mifugo yenye thamani kubwa na usafirishaji upo kama ambavyo Serikali tunafanya ili waweze kutumia huduma hiyo waweze kupata tija zaidi. Huo ndiyo mkakati wa Serikali wa kuimarisha usafirishaji, pia kwenye masoko na ufugaji wa ndani wenye viwango, wenye kuleta faida kwa wafugaji, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa kuna miradi mingi ya miundombinu inayosubiri kutekelezwa kwa bajeti ya Serikali na bajeti ya Serikali; na bajeti ya Serikali imekuwa inatengwa kwa kutumia fedha za ndani na fedha za nje, lakini mfumo huu umeonesha kuchelewesha miradi na hata kupelekea gharama ya miradi kuwa kubwa:-

Je, Serikali haioni sasa ni muda muafaka wa kuanza kutumia mfumo wa *PPP* au mfumo wa *EPC plus finance* ambao ni mfumo wa *Engineering*, *Procurement* na *Construction* ambao umeonesha mafanikio makubwa sana kwa nchi za Afrika Mashariki na hata *SADC* ili kupunguza gharama za utekelezaji? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara zake, tunaleta bajeti zetu hapa na Waheshimiwa Wabunge mnapitisha bajeti hizi. Siwezi kusema kwamba bajeti hizo hazitoshi, lakini najua mahitaji ni makubwa, ni kweli tunahitaji fedha nyingi; na baadhi ya miradi tunapoitekeleza mwishoni mwa mwaka, mingine tunakuwa hatuikamilishi kwa sababu ya mwenendo wa makusanyo ambayo tulikuwa tunategemea kukusanya, kiwango hicho cha fedha ambacho tulikiomba hapa Bungeni, kinaweza pia kisitoshe.

Mheshimiwa Spika, iko mifumo mingine ambayo inawezesha pia kukamilisha bajeti zetu tunapopata fedha kutoka nje ya bajeti inayotegemea mapato ya ndani, kwa sababu bajeti zetu zinategemea mapato ya ndani, na pia tuna marafiki zetu wanaongeza mtaji na tunatekeleza majukumu yetu. Hii ndiyo tunafanya kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, sasa tunapokwenda kukusanya na tusifikie malengo, tunatafuta njia nyingine ikiwemo na hiyo ya *PPP* ambayo kwa muda mrefu tumeitekeleza, lakini imekuwa ngumu kidogo kutekeleza na tumebadilisha na sheria. Leo Mheshimiwa Njeza amependekeza mfumo wa EPC *plus finance,* najua Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi ameizungumzia sana mfumo huo juzi hapa wakati wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu unatafuta mwekezaji ambaye atakuwa tayari kutekeleza mradi wa aina fulani, anautengenezea mchoro wake, tunakaa naye, tunakubaliana naye, tunampa kazi hiyo ya manunuzi, ujenzi; na tunapokwenda kujenga, gharama ya mradi anaitumia yeye, na sisi tunaupokea mradi kwa yeye kuujenga, halafu kuufanyia kazi na wakati mwingine anaweza kuurudisha kwetu tuutumie baada ya kuwa ametumia kwa kipindi fulani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, miundombinu ile inabaki kwetu sisi. *BOT (Build, Operate and Transfer System),* hiyo inaweza kuwa inaendelea kutumika kwa utaratibu huo. Kwa hiyo, mfumo huo tunaukubali Mheshimiwa Njeza, ushauri wako nakuahidi tunauchukua, ni mfumo mzuri na Waziri wa Ujenzi yupo, Wizara ipo, itatumia mfumo huo na Wizara ya Fedha ipo, itaangalia mwenendo wa mapato yetu, nao ndio wanaoweza kuangalia mfumo huo tunaweza kupata kwa kiasi gani; na kama tunakopeshwa gharama yake ni kiasi gani? Kwa maana hiyo, tutakubali mfumo huo pale ambako tunaweza kupata mkopo huo wenye gharama nafuu ili tuweze kutekeleza miradi yetu.

Mheshimiwa Spika, nataka nimwakikishie Mbunge na Waheshimiwa Wabunge kwamba ile miradi yetu tuliyoipendekeza kuitekeleza kwenye bajeti hii, hata kama hatutakusanya kwa kiwango cha kutosha, mapato ambayo tunayo, tutatumia mfumo ambao Mheshimiwa Njeza ametupendekezea hapa kwa sasa, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Jimbo la Moshi Mjini.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kumwuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, urasimishaji wa makazi yaliyojengwa holela kwenye miji mingi katika nchi yetu ni zoezi ambalo lina gharama kubwa lakini mwisho wake yale makazi hayawi na ubora unaotakiwa hata kufikika na hata kwenye anuani za makazi yana shida kwa sababu barabara na huduma nyingine haziko vizuri:-

Mheshimiwa Spika, ni nini mpango wa Serikali wa kupima maeneo katika maeneo ya Miji, Manispaa pamoja na Majiji na yale maeneo ya pembezoni ili kuhakikisha sasa tunaipanga miji yetu vizuri na huduma zinawafikia wananchi? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge amezungumzia suala la upimaji wa ardhi kwenye maeneo yetu ikiwemo na maeneo ya miji ambayo yeye ameeleza. Nataka nimwakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mpango huu ni endelevu ndani ya Wizara yetu ya Ardhi, kuhakikisha kwamba tunapima maeneo yote ya ardhi nchini na kwenye vipimo hivi tunabainisha huduma zote zinazotakiwa kutumika kwenye ardhi hiyo; kwanza makazi, maeneo ya taasisi, maeneo ya huduma za jamii kama vituo vya mabasi na masoko na kila

kitu. Huo ndiyo mkakati ambao sasa unaendelea chini ya Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, sasa nini kinafanyika baada ya kuwa tumekamilisha kupima, tunakabidhi kwenye mamlaka ya Serikali za Mitaa ambapo wao ndiyo wanaitunza ile ardhi na kuitumia na kuitoa kwa Watanzania ambao wako kwenye maeneo hayo. Pia hata kwenye mamlaka yenyewe inaweza kuwa inapanga sasa mipango yake. Kwa mfano, pale Moshi Mjini, baada ya kuwa tumeupima ule mji na kupanga matumizi yake, tunawakabishi Manispaa ya Moshi ili waanze kupanga sasa, hapa panatakiwa masoko, hapa vituo vya mabasi, maeneo mengine makazi na kila kitu. Kwa hiyo, mkakati huu ni endelevu na siyo tu kwa maeneo ya miji, tunakwenda sasa mpaka vijijini.

Mheshimiwa Spika, tunataka Watanzania sasa wapate maeneo yaliyopimwa, yanayotambulika rasmi ili pia tuweze kuwapa hati. Ile hati inawasaidia pia kama mtaji wa kukopea kwenye mabenki na taasisi nyingine za fedha. Kwa hiyo, malengo yetu ni endelevu na ni mapana kidogo kwa sababu tunataka kila Mtanzania anufaike na ardhi iliyoko nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naitaka sasa Wizara ya Ardhi kuendelea kukamilisha zoezi hili ili Watanzania wanufaike na ardhi waliyonayo kwenye maeneo yao. Kwa kufanya hivyo, itawezesha pia hata wawekezaji kujua wanapofika wanaambiwa eneo la uwekezaji lile pale, litakuwa limeshapangwa tayari. Kwa hiyo, mnakamilisha kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo pia kuna Afisa wetu wa Ardhi. Hhii sera ni endelevu na itakuwa na msaada mkubwa kwa Watanzania, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu muda wako wa kujibu maswali umefikia mwisho. Tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* - KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali ya kawaida, tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, sasa aulize swali lake.

Na. 268

**Hitaji la watumishi wa afya – Kalambo**

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Watumishi wa Kada ya Afya Wilayani Kalambo kwa kuzingatia upungufu uliopo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Jimbo la Kalambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali katika mwaka huu wa fedha imepanga kuajiri watumishi wa kada ya afya 7,612 watakaopangiwa katika Halmashauri zote nchini ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephat Kandege, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Utakubaliana nami kwamba katika jibu ambalo limetolewa na Serikali, wanaongelea suala la kuajiri watumishi 7,612; na kitakachoenda kufanyika ni kugawa kwa kuzingatia *quality* na siyo *equity*. Katika swali langu la msingi nimeongelea juu ya upungufu mkubwa wa watumishi wa kada ya afya katika Halmashauri yetu. Hivi karibuni wamehama watumishi 33 na wakahamishiwa watumishi watatu tu: Je, Serikali katika mgao huu itaenda kuzingatia *equity* badala ya *equality*?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa watumishi ambao wamekuwa wakipelekwa katika maeneo yanayoonekana kama ya pembezoni wanaenda kuishi kule kama kupata *confirmation* na kupata ukuu wa idara na baadaye kuhama; je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba watumishi wote ambao wanapangwa katika maeneo hayo wanaenda kuishi kwa kipindi chote?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Jimbo la Kalambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, baada ya kumaliza mchakato wa ajira, maana yake kitakachofuata ni kugawanya katika Halmashauri zote nchini na tutagawa kulingana na mahitaji katika maeneo husika. Kwa hiyo, hatutakuwa na ile namba

kwamba tutagawa Halmashauri zote kwa usawa, Hapana, tutagawa kulingana na mahitaji. Tunatambua kabisa kwamba katika maeneo kama Kalambo kuna uhitaji mkubwa, kwa hiyo, tutawapa kulingana na hiyo idadi.

Mheshimiwa Spika, la pili, kwenye suala la kuhusu kuhama watumishi baada ya kwenda katika maeneo ya pembezoni, moja, ya utaratibu ambao tumeweka sasa, mtumishi haruhusiwi kuhama siyo chini ya miaka mitatu, lazima afanye kazi katika eneo alilopangiwa na baada ya hapo, labda kuwe na sababu za msingi sana ambazo zinapelekea mtu huyo apaswe kuhama. Kwa sasa ni kwamba tunafunga na wote wanakuwa na *commitment letter* ya kuhakikisha wanabaki katika maeneo hayo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Minza Mjika, swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda nielekeze swali langu katika Mkoa wa Simiyu Wilaya ya Busega: Ni lini Serikali itapeleka mashine ya *X-Ray* katika Wilaya ya Busega? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Minza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa hivi tuko katika mchakato wa kufanya manunuzi ya vifaa tiba, ninaamini mara baada ya mchakato huu kukamilika, basi tutalizingatia hilo nao tutawapatia hiyo X-*Ray*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aysharose Matembe, swali la nyongeza.

**MHE. AYSHROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mkoa wa Singida unakabiliwa na upungufu mkubwa wa wauguzi ambako zaidi ya wauguzi 800 wanahitajika: Je, ni lini Serikali itatuletea wauguzi wa kutosha ili kusaidia mkoa wangu kutoa huduma za afya na hususan kusaidia huduma ya mama na mtoto?

**SPIKA:** Mheshimiwa swali la nyongeza ni moja. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Aysharose Mattembe, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Singida, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali tunaajiri kulingana na bajeti na mapato kadri ambavyo tunapata na mahitaji yaliyoko. Kwa hiyo, tutakavyoajiri ikiwemo ajira 7,612 maana yake katika ule mgawanyo na Singida nao tutawapatia, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali kwa kushirikiana na wananchi wa Jimbo la Babati Vijijini wamekamilisha ujenzi wa zahanati za Guse, Hayamango na Yasanda, lakini zahanati hizo zimeshindwa kufunguliwa kwa sababu ya upungufu wa watumishi wa afya: Je, Serikali sasa ina mpango gani wa kuwapeleka watumishi ili zahanti hizo ziweze kufunguliwa na kuhudumia wananchi wetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Daniel Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, natambua kwamba kuna zahanati nyingi hazijafunguliwa kwa sababu ya kukosa watumishi, nasi kama Serikali tunalijua hilo na katika watumishi ambao tutawapeleka, tutawaagiza Wakurugenzi wawapangie katika zile zahanati ambazo zimekamilika ili ziweze kutoa huduma, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Furaha Matondo, swali la nyongeza.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe ina changamoto kubwa sana ya watumishi hasa kada ya afya na elimu: Je, ni lini Serikali itapeleka walimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe ili kukabiliana na changamoto kubwa sana ya watoto wetu kukosa elimu na elimu kushuka? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Furaha Matondo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ajira ziko katika hatua za mwisho na hizi ajira ni pamoja na kada ya afya na elimu, kwa hiyo, katika ule mgawanyo Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe vilevile tumeizingatia na itapata katika ule mgawanyo wa walimu pamoja na kada ya afya, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima James Mdee, swali la nyongeza.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nikiwa Mbunge wa Kawe, tumejenga hospitali kubwa sana ya mfano kupitia fedha za Halmashauri eneo la Mabwepande ambayo sasa hivi iko katika hatua za mwisho kabisa: Je, katika mchakato wa kugawa watumishi wa kada ya afya, Serikali mtazingatia hospitali hii kubwa ambayo itasaidia Wilaya za Bagamoyo na Kawe? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima Mdee, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, katika sehemu ya ajira ambazo tutazipanga na kupeleka katika Hospitali ya Mabwepande ni pamoja na hizi ajira mpya ambazo tutazitoa, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaingia kwenye swali lingine, niwakumbushe kwa sababu majibu yasipotoka mahususi ama sahihi kwa ajili ya maswali yenu, mnaomba miongozo. Kwa hiyo, tuyasome maswali ya msingi ili maswali ya nyongeza yatokane na swali la msingi.

Sasa swali linalofuata linahusu ujenzi wa shule za sekondari kwenye kata. Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge wa Ulyankulu swali.

Na. 269

**Hitaji la sekondari baadhi ya Kata - Ulyankulu**

**MHE. REHEMA J. MIGILLA** aliuliza:

Je, ni lini Serikali itajenga Shule za Sekondari katika Kata za Sasu, Nhwande, Makingi na Kanonge katika Jimbo la Ulyankulu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rehema Juma Migila, Mbunge wa Jimbo la Ulyankulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2021/2022, Serikali imetuma fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya za sekondari 15 kupitia mradi wa *EP4R* shilingi bilioni 15.0 na shule 232 kupitia mradi wa *SEQUIP* shilingi bilioni 109.57 katika kata ambazo hazina shule na maeneo ambayo yana wanafunzi wengi ukilinganisha na miundombinu ya shule zilizopo.

Mheshimiwa Spika, kati ya fedha zilizotumwa Jimbo la Ulyankulu limepokea fedha shilingi milioni 470 kwa ajili ya ujenzi wa shule moja ya sekondari ya kata. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kata zote zinakuwa na Shule za Sekondari nchini

zikiwemo Kata za Sasu, Nhwande, Makingi na Kanonge ambapo kupitia Mradi wa *SEQUIP* jumla ya shule za sekondari 1,000 zinatarajia kujengwa nchini ili kuwapunguzia umbali wa kutembea wanafunzi kufuata shule.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba George, Mheshimiwa nilishawaambia ukiwa na swali la nyongeza lazima usimame. Sasa naona ulikuwa unajitayarisha haya. Mheshimiwa Rehema Migilla swali la nyongeza.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, pamoja na majibu ya Serikali nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kata hizi ambazo nimezitaja kwenye swali langu la msingi ziko mbali sana na mojawapo ina mto katikati, kwa hiyo wanafunzi wanapata shida sana kwenda shuleni. Shule inayo-*accommodate* wanafunzi wa kata hizi ambazo hazina kabisa sekondari ni Shule ya Sekondari Mkindo. Sasa je kwa nini Serikali isione umuhimu wa kuifanya hii sekondari ya Mkindo kuwa ni sekondari ya bweni ili iweze kuwasaidia wanafunzi ambao wanatoka maeneo ya mbali waweze kufikia ndoto zao?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Serikali iliona umuhimu wa kujenga vituo vya afya kwa kupitia pesa za tozo lakini pia pesa za *COVID-19.* Je, kwa kata hizi zenye maeneo ambayo hayana sekondari, kwa nini isilete mpango mahsusi kama ilivyofanya kwenye Wizara ya Afya ili kuhakikisha na hizi kata ambazo hazina sekondari na zenyewe zinapata sekondari?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza

ya Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge wa Jimbo la Ulyankulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge amehitaji kwamba katika Kata ya Mikindo tuifanye kuwa shule ya bweni, tulipokee wazo hili na tutakwenda kufanya tathmini tutafute fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule hii.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Serikali ina mpango mahususi na mpango wetu ni kujenga sekondari 1,000. Mwaka wa fedha huu ambao unaisha 2021/2022 tumeshapeleka fedha katika kata 232, karibu bilioni 109.57 na katika mwaka wa fedha ambao Wabunge wameshatupitishia bajeti kwa maana ya 2022/2023 tutajenga shule za sekondari 234, manake tutapeleka katika kata zote katika majimbo ambayo bado hawajapata. Mwakani vilevile na mwaka kesho kutwa tutafanya hivyo hivyo. Kwa hiyo ndani ya miaka ya Mama Samia tutamaliza shule zote 1,000 ambazo Mheshimiwa Rais ameahidi kupitia mradi wa *SEQUIP*. Kwa hiyo nimwondoe shaka kwenye hilo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba George Luhoro, swali la nyongeza.

**MHE. NDAISABA G. LUHORO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Kata ya Nyamagoma ni miongoni mwa Kata za Wilaya ya Ngara ambazo hazina shule ya sekondari. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Nyamagona? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali dogo la nyongeza

la Mheshimiwa Ndaisaba George, Mbunge wa Jimbo la Ng'ara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kata ya Nyamagona ipo katika mpango ambao tunakwenda kujenga katika mwaka wa fedha unaokuja. Kwa hiyo nimwondoe shaka kwamba itajengwa katika mwaka wa fedha unaokuja wa 2022/2023.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaelekea Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Joseph Tadayo.

Na. 270

**Kurekebisha Sheria ya Utakatishaji Fedha**

**MHE. JOSEPH A. TADAYO K.n.y. MHE. DEODATUS P. MWANYIKA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itarekebisha Sheria ya Utakatishaji Fedha inayozuia dhamana kwa Watuhumiwa hata kwa makosa ya kawaida?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Hamad Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 12 cha Sheria ya Kudhibiti Utakasishaji wa Fedha Haramu, Ufadhili wa Ugaidi na Ufadhili wa Silaha za Maangamizi, Sura 423, kinabainisha makosa ya utakasishaji wa fedha haramu pekee. Sheria hiyo haihusishi makosa mengine yoyote, hususan kuzuia au kutozuia dhamana kwa watuhumiwa wa makosa ya kawaida. Aidha, utaratibu wa dhamana kwa makosa mbalimbali, ikiwemo utakasishaji wa fedha haramu unasimamiwa na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura 20.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, hakuna sababu ya kurekebisha Sheria ya Kudhibiti Utakasishaji wa Fedha Haramu, Ufadhili wa Ugaidi na Ufadhili wa Silaha za Maangamizi, Sura 423 kwa kuwa haizuii dhamana kwa watuhumiwa wa makosa ya kawaida. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Tadayo, naona umekaa kwa hiyo huna swali.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika...

**SPIKA:** Ngoja kwanza unalo swali la nyongeza au huna.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, sina kwa sababu…

**SPIKA:** Haya ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 271

**Changamoto zinazokabili viwanda vya kutengeneza nguo nchini**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza:

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua changamoto za Viwanda vya Nguo nchini kwani ni viwanda vitatu tu kati ya 33 vinafanya kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exaud Kigahe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sekta ndogo ya nguo na mavazi nchini ina jumla ya viwanda tisa vinavyofanya kazi hivi sasa. Serikali inaendelea kutatua changamoto zinazokabili viwanda vya nguo, ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara nchini, kudhibiti bidhaa zisizo na ubora na bidhaa bandia kutoka nje ya nchi, kuongeza ushuru wa forodha kwa kanga na vitenge vinavyotoka nje ya nchi, kuhamasisha Taasisi za Umma na Watanzania kwa ujumla kununua bidhaa za nguo zinazotengenezwa na viwanda vya hapa nchini na kuweka miundombinu wezeshi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Swali la kwanza; kumekuwepo na uingizaji wa nguo hasa vitenge na kanga kwa njia za magendo kutoka nje ambavyo vinapelekea ukwepaji wa kodi na hivyo kupoteza mapato, lakini pia vinasababisha viwanda vyetu nchini kutokuwa shindani. Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba inatokomeza biashara hii ya magendo ili kuweza kusababisha viwanda vyetu viweze kuzalisha kwa tija? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; nchi yetu imekuwa na viwanda maarufu sana Afrika Mashariki na Kati, kama vile *Kilitex*, Urafiki, *Mutex, Mwatex*, lakini viwanda hivi vimeshindwa kufanya kazi kwa changamoto mbalimbali ikiwepo mitaji. Ningependa kujua Serikali ina mkakati gani angalau kuweza kutoa dhamana za mikopo kwa viwanda hivi ili viweze kujiendesha kwa tija pia? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli sekta ya nguo na mavazi nchini imekuwa na changamoto kubwa ikiwemo hiyo ya kuingiza bidhaa hizo kwa njia ya magendo. Tunajua na tulishaanza kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kudhibiti mipaka au zile sehemu ambazo wanaingiza kiholela katika maeneo ya bandari bubu, lakini pia na mipaka ya kutoka nchi za jirani. Pia kwa sasa kumekuwa na tabia ya kuingiza, kupitisha nguo hizo kwenda nchi za jirani halafu kurudisha nchini. Kwa hiyo tumeshaanza kuchukua hatua ikiwemo kudhibiti kwenye sehemu zote zinazoingiza bidhaa, lakini kuongeza watumishi kwenye Taasisi zetu ikiwemo *TBS*, *FCC* na wengine, kuhakikisha tunaongeza udhibiti katika mianya

ambayo wanaingiza bidhaa hizo bandia hasa bidhaa za nguo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwanda ambavyo havifanyi kazi, ni kweli kuna viwanda ambavyo vimesimama ikiwemo kama alivyotaja ya Urafiki, lakini anajua Serikali tumekuwa na mkakati mara nyingi kuhakikisha tunavisaidia kwa kuweka dhamana na kuweza kuweka ruzuku mbalimbali ili viweze kufanya kazi. Ndiyo maana hivi viwanda tisa ambavyo vinaendelea kufanya kazi sasa, ni kutokana na juhudi hizi za Serikali mpaka vimefikia idadi hiyo kutoka vitatu mpaka tisa, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Mayenga, swali la nyongeza.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1998 Serikali ilitaifisha viwanda vikiwemo vya nguo na vingine. Mwaka 2017 viwanda hivi vilirejeshwa Serikalini katika Bajeti ya Viwanda na Biashara ya mwaka jana, Waziri alisimama hapa akasema viwanda hivi vitatangazwa kwa wawekezaji wenye uwezo ili waweze kuvifufua. Wananchi wetu na hasa vijana wanalalamika ajira, kwa nini Wizara iko kimya mpaka leo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa Lucy, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli viwanda ambavyo vilikuwa vimebinafsishwa na vikawa havifanyi kazi jumla viwanda kama 20 vilikuwa vimerejeshwa Serikalini. Kati ya hivyo 10

tutavitangaza, *notice* ilishatangazwa mwaka jana, lakini sasa tunaendelea na mchakato wa kupata wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, vingine ambavyo tunadhani ni muhimu kama Serikali tuendelee kuviendeleza, vitakuwa chini ya Mashirika mbalimbali ya Serikali ikiwemo *NDC*, maeneo yale ya uwekezaji kwa ajili ya wananchi *EPZA*, na kadhalika. Kwa hiyo, Serikali inaendelea na mchakato wa kuona tunapata wawekezaji mahiri, hatutaki tena kwenda haraka tukapata wawekezaji ambao badala ya kuendeleza viwanda watavidhoofisha zaidi kama ambavyo ilitokea huko nyuma. Kwa hiyo tunaendelea na mchakato huo kuhakikisha tunavitangaza viwanda hivyo kwa wawekezaji wenye tija na wenye nia ya kuendeleza viwanda hivyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Katika jibu la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri ametuambia kuwa viko viwanda tisa vinavyofanya kazi. Je, anaweza kututajia viwanda hivyo ili tupate ufahamu vizuri? *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa, sasa hiyo kwa sababu inahitaji orodha na hajavitaja hapo, atakupatia orodha tukishatoka hapa, atakupatia hiyo orodha Mheshimiwa Shally Raymond.

Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima, swali la nyongeza.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa asilimia 75 ya mafuta ya kupikia yanatoka nje ya nchi na kiwanda cha kuzalisha mafuta ya kupikia kilichopo katika Kata ya Wazo kinaitwa *Family* kimefungwa.

Je, Mheshimiwa Waziri ataambatana pamoja na mimi baada ya hapa ili kujua ni sababu gani kiwanda hicho kimefungwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba kujibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa Mchungaji Josephat Gwajima, Mbunge wa Kawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali sasa hivi mkakati wetu ni kuhakikisha tunajitolesheza kwenye mafuta ya kula. Kwa hiyo kama kweli kuna kiwanda ambacho kimefungwa na mimi kama Naibu Waziri kwenye sekta inayohusu viwanda, nitaambatana na Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kuona changamoto gani zinakikabili hicho kiwanda ili kiweze kuendelea kuzalisha mafuta ya kula ili kupunguza changamoto hii ya mafuta ya kula nchini, nakushuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, swali la nyongeza.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, nakushuru sana. Mahitaji ya vitenge nchini ni kontena 40 kwa mwezi, uzalishaji ni kontena kati ya sita hadi nane. Kwa hiyo yapo mahitaji makubwa sana ya vitenge nchini, lakini tulitengeneza sera ya kulinda viwanda vyetu vya ndani kwa kuongeza kodi ya vitenge kutoka nje. Je, wako tayari sasa hivi kukaa na Wizara ya Fedha kutokana na mahitaji kuwa makubwa kuitazama tena kodi iwe rafiki ili wananchi waweze kuendelea kupata huduma ya vitenge?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, unao uhuru wa kujibu hilo swali kama majibu unayo, kama huna nikupe muda ili hilo swali lije lijibiwe kama swali msingi.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naomba lije kama swali la msingi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa Serikali inayo dhamira ya dhati ya kufufua Kiwanda cha *Kilimanjaro Machine Tools* na tayari wameshaanza kuleta mitambo mbalimbali. Swali langu, Serikali iliahidi kutupa bilioni 1.6 kwa ajili ya kujenga *foundry machine* yaani kinu cha kuyeyusha chuma. Je, ni lini Serikali itatuletea fedha hizo ili kiwanda kiweze kufanya kazi kwa asilimia mia moja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli *Kilimanjaro Machine Tools* ni moja ya viwanda ambavyo vilikuwa vinazalisha vipuri kwa ajili ya kulisha viwanda vingine ambavyo vinazalisha bidhaa mbalimbali ikiwemo viwanda vya nguo na kadhalika. Lengo la Serikali kama nilivyosema ni kufufua viwanda vyote na kuhakikisha vinapata vipuli. Sasa hivi Serikali imeshatoa milioni 700, kwa hiyo bado milioni 800 na kidogo ambazo zitaenda kukamilisha ujenzi wa *foundry* hiyo katika kiwanda cha *KMTC*. Kubwa zaidi *commitment* imeshatoka, Wizara ya Fedha itatoa fedha hiyo ili *foundry* hiyo iweze kujengwa. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba nia ya Serikali na lengo la Serikali ni kulitimiza kadri ambavyo tumepanga kwenye bajeti zetu, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, sasa aulize swali lake.

Na. 272

**Kutekeleza Mradi wa Umwagiliaji Kijiji cha Arusha Chini**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA** aliuliza:-

Je, ni lini Mradi wa Umwagiliaji wa Kijiji cha Arusha Chini utatengewa fedha ili uanze kutekelezwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Umwagiliaji katika Kijiji cha Arusha Chini una jumla ya hekta 120 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Kati ya hizo hekta 48 zinamwagiliwa kwa kutumia mifereji ya asili ambayo chanzo chake cha maji ni chemichemi na mvua za msimu. Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa skimu hii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, kwanza niishukuru Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya kufanya usanifu kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, swali langu la kwanza kwa kuwa ekari zilizoorodheshwa hapa kwenye jibu la msingi ni 120 lakini kuna eneo kubwa ambalo linazunguka Kijiji cha Ngonja, Arusha Chini na Arusha Juu.

Je, Serikali ipo tayari kujumuisha eneo hilo wakati wa kufanya usanifu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini swali langu la pili, je, Naibu Waziri yupo tayari kuambatana na mimi baada ya kuahirisha Bunge hili la Bajeti ili akajionee uhalisia wa Mradi huu? Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tupo tayari kutoa maelekezo kwa timu yetu ambayo itafanya usanifu kuhakikisha kwamba inaligusa eneo kubwa kadri iwezekanavyo, kwa sababu ni maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwamba ifikapo mwaka 2025 tuwe tuna eneo ambalo linamwaagiliwa la hekta 1,200,000. Kwa kuongezeka kwa eneo ni sehemu ya tija ya uzalishaji kwetu pia, kwa hiyo wataalam wetu pia wataangalia eneo ambalo halijajumuishwa liweze kujumuishwa.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, niko tayari Bunge hili likifikia ukomo wake kwa maana ya vikao hivi vya Bajeti,

kuongozana na Mheshimiwa Mbunge kwenda kuangalia uhalisia wa Mradi husika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cosato Chumi swali la nyongeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, napenda kuishukuru sana Serikali imetenga zaidi ya shilingi milioni 700 kukamilisha mradi wa umwagiliaji wa Mtura. Kukamilika kwa mradi huu ili kuwe na tija kwa kilimo kile wananchi watahitaji mbolea.

Je, Serikali ipo tayari kuanza kuwapa mbolea hiyo ya ruzuku mapema mara tu mradi utakapokuwa umekamilika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge swali hilo linahusu kupewa mbolea, kwa hivyo litatafuta muda wa kujibiwa. Mheshimiwa Felista Njau swali la nyongeza.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Katika Mkoa wa Morogoro eneo la Chita kuna hekari 12,000 zenye miundombinu ya umwagiliaji ambapo sasa hivi zinamilikiwa na JKT, lakini kwa uwezo wao wameweza kulima ekari 2,500. Je, ni lini Serikali itawekeza nguvu yake pale ili kuweza kusaidia usalama wa chakula na kuongeza pato la Taifa? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felista Njau kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Fungu Namba 05 la Tume ya Umwagiliaji katika Randama ukiangalia Jedwali la Nne limeainisha moja kati ya miradi ambayo tutakwenda kuitekeleza katika mwaka ujao wa fedha ni mradi wa JKT –

Chita. Kwa hiyo, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge mradi upo katika mpango na utatekelezwa katika bajeti inayokuja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deus Sangu swali la nyongeza.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, skimu ya umwagiliaji wa Ilemba usanifu wa kina umekamilika kwa asilimia 100. Je, ni lini Serikali mtaanza ujenzi wa skimu hii ambayo ni muhimu sana kwa uchumi wa wananchi wa Kata ya Ilemba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deus Sangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi ambao Mheshimiwa Mbunge ameusema upo katika utekelezaji wa mwaka wa fedha unaokuja, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi huo utatekelezwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Serikali kwa muda mrefu sana imeahidi kuhusu ujenzi wa bwawa kwenye Bonde la Mto Mkomazi. Je, ni lini ahadi hii sasa itaanza kutekelezwa rasmi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Timotheo Mnzava Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli utekelezaji wa mradi wa Bonde la Mto Mkomazi umekuwa ni wa muda mrefu na Mheshimiwa Mbunge amekuwa akifuatilia sana, nataka nimhakikishie mbele ya Bunge lako Tukufu ya kwamba ifikapo mwezi wa Saba taratibu za awali za kumpata mshauri mwelekezi zitafanyika ili kazi ya usanifu na upembuzi yakinifu uanze na baada ya hapo tutaanza utekelezaji wa mradi huu mkubwa ambao wananchi wa Korogwe wanausubiri kwa hamu kwa sababu unagusa zaidi ya Kata 11 na una manufaa makubwa sana. Nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge tutaanza mwezi wa Saba mapema kabisa kumpata mshauri mwelekezi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Monni, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kijiji cha Kidoka na Takwa wanayo miradi maarufu ya umwagiliaji lakini mpaka leo Serikali haijawekeza chochote. Naomba kujua *commitment* ya Serikali katika kuwekeza kwenye miradi ya vijiji hivyo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mohamed Monni Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikirudia mara nyingi kusema ya kwamba tumedhamiria kuyagusa maeneo mengi ambayo yanafaa kwa ajili ya umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji wa mazao katika nchi yetu ya Tanzania, hatua ambayo inafanyika hivi sasa ni kwamba timu yetu imeendelea kuyapitia maeneo yote kufahamu *status* ya kila maeneo ambayo yanafaa kwa ajili ya umwagiliaji. Katika eneo ambalo Mheshimiwa amelitaja la Kidoka mimi na yeye tutatafuta muda hapa katikati tutaongozana pamoja na

wataalam kwenda kulitembelea na kuona uwezekano wa kufanya uwekezaji katika eneo hilo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Subira Mgalu swali la nyongeza.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona na kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, Serikali imeongeza kwa kiwango kikubwa bajeti ya umwagiliaji kutoka Shilingi Bilioni 46 mpaka Bilioni 361 na kwakuwa Wilaya yetu ya Bagamoyo tunayo skimu ya umwagiliaji - Ruvu inaitwa Chauru yenye wanachama zaidi ya 900 lakini inayo changamoto kubwa ya uchakavu wa miundombinu.

Je, Serikali inatoa ahadi gani kwa wanachama wa skimu hii ya umwagiliaji Chauru katika ukarabati wa miundombinu? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Subira Mgalu Mbunge, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, mradi huo tunaufahamu na changamoto iliyopo, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika miradi ambayo Tume imepanga kuifanyika kazi katika bajeti inayokuja mradi huo pia umeainishwa, kwa hiyo wakulima wa eneo hilo watapata nafasi ya kuweza kufaidika na uboreshaji wa miundombinu hasa baada ya kuanza utekelezaji kupitia bajeti inayokuja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu lakini na majibu kutoka upande wa Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo mambo mawili hapa, jambo la kwanza linahusu wageni waliopo hapa Bungeni na tutaanza na wageni walipo jukwaa langu pale juu.

Kwanza ni wageni 15 wa Spika ambao ni wawakilishi mafunzo ya *Mandela Washington Fellowship 2022* wakiongozwa na Ndugu Victoria Mwanziva ambaye ni Mratibu wa mafunzo na Katibu wa Uhamasishaji wa Chipukizi wa Umoja wa Vijana CCM – Taifa, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimia Wabunge, tunao pia wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula ambao ni viongozi na Watendaji wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo wakiongozwa na Dkt. Allan Kijazi ambaye ni Katibu Mkuu na Ndugu Nicholas Mkapa ambaye ni Naibu Katibu Mkuu. Wote wasimame kwa pamoja wageni kutoka Wizarani, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ameambatana na familia yake ambao ni ndugu zake, wote wasimame kwa pamoja. Karibu sana.  Pia Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete na yeye ameambatana na familia yake na ndugu zake, ndugu wa Mheshimiwa Naibu Waziri wasimame wote kwa pamoja, karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni mbalimbali pia ambao ni wa Wabunge, wageni wote wa Waheshimiwa Wabunge wasimame kwa pamoja, karibuni sana wageni wetu, karibuni sana nadhani mtapata nafasi ya kuwaona

Waheshimiwa Wabunge hapa ndani wakiwawakilishi vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunao wageni wawili kutoka Chuo cha *CBE* - Dodoma, wako wapi wa *CBE*, haya karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 50 na viongozi watano kutoka *Shiloh Child and Youth Development Center* ya Kinampanda - Singida, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wanafunzi 80 na walimu watano kutoka Shule ya Sekondari Nzuguni, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 27 kutoka Mkoa wa Tanga wanaosoma Chuo cha Mipango - Dodoma, karibuni sana pengine watapata nafasi baadae. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndio wageni tulionao hapa tunaendelea na marekebisho kwa sababu tulishasema hili Bunge kila mtu anaruhusiwa kuja, kwa hivyo hata wageni wanaotembelea kwa mafunzo mkija hapa msijisikie vibaya msipotajwa, tunatambua uwepo wenu na wote mtakuwa mnaingia kwenye Taarifa Rasmi za Bunge, siyo lazima kila kundi linaloingia hapa litangazwe kwa sababu makundi ni mengi yanayotaka kuja kuona namna ambavyo Bunge linafanya kazi, kwa hiyo, tutakapoacha kutangaza wageni waliokuja kwa ajili ya kutembelea Bunge msianze kuona sasa imekuwaje jamani, tunafanya marekebisho ili muda mwingi utumike kwa Wabunge kuwawakilisha ipasavyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na hilo tangazo la wageni ninao mwongozo mmoja hapa ambao uliombwa na Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum siku ya jana tarehe 25 Mei, 2022 katika Kikao cha 30 cha Mkutano wa Saba wa Bunge, kwa maana ya Mkutano wa

Bajeti, Mheshimiwa Agnes Elias Horokoro Mbunge wa Viti Maalum, aliomba Mwongozo wa Spika chini ya Kanuni ya 76 ya Kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka 2020.

Waheshimiwa Wabunge wakati wa kipindi cha Maswali na Majibu Mheshimiwa Agnes Hokororo aliuliza swali la msingi Namba 267 kuhusu utoaji na upatikanaji wa huduma za afya, swali lililoelekezwa kwa Wizara ya Afya ambapo Naibu Waziri wa Afya Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel alijibu kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya. Waheshimiwa Wabunge baada ya Mheshimiwa Agnes Hokororo kujibiwa swali la msingi alipata nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza ambapo aliuliza maswali yafuatayo nanukuu.

"Mheshimiwa Mwenyekiti Je, ni sheria ipi kati ya hizo sheria 30 inayosimamia wanawake na wajawazito wakati wa kujifungua wanapopata huduma zisizoridhisha, hilo ni swali la kwanza. Mheshimiwa Mwenyekiti swali la pili Je, sheria hizo zinaruhusu malipo ya fidia kwa wagonjwa wanaopata huduma zisizoridhisha au zisizo na ubora zinazopelekea athari za kiafya au hata kifo?"

Waheshimiwa Wabunge, Naibu Waziri alijibu maswali hayo kama ifuatavyo:-

Nanukuu; "Mheshimiwa Mwenyekiti kwanza nimpongeze kwa namna ambavyo anafuatilia wananchi wanavyotolewa huduma za afya katika eneo lake, ni kweli kwamba kumekuwepo na mambo anayoyasema kwa namna ya huduma ya mama na mtoto lakini siyo tu sheria za nchi yetu, taratibu za nchi yetu na Kanuni za Wizara ya Afya zinataka mama mjamzito na watoto chini ya miaka mitano wapate huduma bure.

Lakini sasa tunapokuja kujibiwa vibaya kujibiwa kwa masuala ya fedheha maana yake kuna sheria za kiutumishi ambazo zipo zimeonesha watu wanaofanya mambo

yanayofanana na hayo, lakini kuna sheria za maadili ya kitaaluma ambayo mara nyingi anapopatikana mtu ambaye amekuwa akijibu vibaya akifanya nini, wakati mwingine anapitishwa kwanza kwenye sheria ya maadili ya kitaaluma anawajibika, lakini anaachiwa. Vilevile sheria za kiutumishi zichukulwe mkondo wake.

Anaendelea kueleza anasema; ''Mheshimiwa Mwenyekiti kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge kama mdau mkubwa kwenye eneo hilo endelea kutusaidia na kutusaidia kutengeneza ushahidi wa kutosha kuwapata watu wa namna hiyo ili waweze kushughulikiwa kulingana na taratibu na sheria, ahsante.'' Mwisho wa kunukuu.

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na majibu hayo Mheshimiwa Agnes Hokororo aliomba mwongozo wa Spika akieleza, pamoja na mambo mengine kuwa haelewi kwamba ni swali namba moja au namba mbili kwenye maswali yake ya nyongeza kama yamepata majibu, hivyo Mheshimiwa Agnes Hokororo, akauliza kuwa Je, inaruhusiwa kwa Naibu Waziri kutojibu maswali na kutokusema kwamba swali hilo nitapata majibu baadaye.

Waheshimiwa Wabunge, nimepitia Taarifa Rasmi za Bunge yaani *Hansard* kuhusu majibu ya maswali ya nyongeza yaliyotolewa na Naibu Waziri na ni kweli kwamba swali halikujibiwa kikamilifu, kwa kuwa majibu ya maswali hayo hayaoneshi ni sheria ipi inayosimamia wanawake wajawazito wanaopata huduma zisizoridhisha wakati wa kujifungua na kama sheria hizo zinaruhusu malipo ya fidia kwa wagonjwa wanaopata huduma zisizoridhisha au zisizo na ubora kama ambavyo muuliza swali Mheshimiwa Hokororo alihitaji kufahamu. Aidha, majibu yaliyotolewa hayaeleweki kama ni ya swali la kwanza au ni majibu ya swali la pili.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa Mheshimiwa Hokororo alihitaji kujua kama jambo hili linaruhusiwa au

haliruhusiwi kwa mujibu ya Kanuni yetu ya 76. Hivyo namfahamisha Mheshimiwa Hokororo ama Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hilo haliruhusiwi na kwamba Naibu Waziri alipaswa kutoa majibu ya maswali hayo kwa ukamilifu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hivyo kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 53 ya Kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka 2020 naelekeza kwamba swali hilo lipatiwe majibu sahihi kama alivyoyahitaji Mheshimiwa Mbunge. Waheshimiwa Wabunge na hii ndiyo sababu tunasisitiza maswali ya nyongeza lazima yawe yanaendana na swali la msingi, lakini huyu muuliza maswali ya nyongeza alikuwa ni mwenye swali la msingi kwa hivyo majibu aliyapata kabla na akaandaa maswali ya nyongeza ambayo Naibu Waziri alipaswa kuyajibu kwa ukamilifu, kwa hiyo yatajibiwa upya maswali yake yote mawili ili apate majibu kwa ajili ya wananchi wake anaowawakilisha. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI *Ndc* – KATIBU WA BUNGE:** Maazimio ya Bunge, Azimio la Bunge la kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa miongozi kwa viongozi wenye ushawishi mkubwa Duniani na kupewa Tuzo ya mafanikio ya ujenzi wa miundombinu.

## MAAZIMIO YA BUNGE

### Azimio la Bunge la Kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwa miongoni mwa viongozi wenye ushawishi mkubwa Duniani na kupewa Tuzo ya mafanikio ya ujenzi wa miundombinu

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge Maazimio ya Bunge, kuna Azimio hapa la Mheshimiwa Zainab Athman Katimba. *(Makofi)*

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Spika, kama wote tunavyofahamu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yupo Nchini Ghana kuanzia tarehe 23 Mei, 2022 kwa ajili ya ziara ya kikazi ambapo pamoja na mambo mengine amehudhuria mdahalo wa Wakuu wa Nchi kujadili fursa zilizomo na changamoto zinazokabili Nchi za Afrika kama vile kuongezeka kwa athari za mabadiliko ya tabianchi, kupanda kwa bei ya vyakula na matumizi ya nishati endelevu.

Mheshimiwa Spika, vilevile tumeshuhudia tarehe 25 Mei, 2022 Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan akipewa Tuzo ya Mwaka 2022 ya Babacar Ndiaye kwa mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika Ujenzi wa Miundombinu ya usafirishaji ambayo kwa kawaida hutolewa kwa Mkuu wa Nchi iliyofanya vizuri katika sekta hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi ya kupewa tuzo hiyo, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ametajwa pia kuwa miongoni mwa Viongozi 100 wenye ushawishi mkubwa Duniani kwa mujibu wa Taarifa iliyotolewa na Gazeti maarufu la *TIME* la tarehe 24 Mei, 2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua sifa hiyo kubwa aliyoipata Rais wetu ambayo inailetea nchi yetu taswira nzuri

Kitaifa na Kimataifa, naomba kutumia fursa hii kuliomba Bunge hili Tukufu ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi, kuridhia Azimio la Kumpongeza Mheshimiwa Rais kama ifuatavyo.

Azimio la Bunge kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwa miongoni mwa Viongozi wenye ushawishi mkubwa Duniani na kupewa Tuzo ya mafanikio ya Ujenzi wa Miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tarehe 24 Mei, 2022 akiwa katika ziara ya Kikazi Nchini Ghana amepokea tuzo kuu ya Mjenzi Mahiri ya Babacar Ndiaye *(Africa Road Builders)* kwa mwaka 2022 inayotolewa na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB),* akiwa ni Rais wa 12 kupata Tuzo hiyo tangu ilipoanzishwa Mwaka 2016. *(Makofi)*

Na kwa kuwa tuzo hiyo imetolewa kwa kutambua mchango wake kama mwanamke mzalendo na Rais wa kwanza wa Tanzania kupata Tuzo hiyo akiwa anaongoza Serikali ya Awamu ya Sita kwa mafanikio makubwa katika kuendeleza sekta ya miundombinu na usafirishaji hususan eneo la barabara;

Na kwa kuwa Watanzania wote tunatambua juhudi kubwa anayoifanya Mheshimiwa Rais kuendeleza miundombinu ya usafirishaji ikiwemo kusimamia na kufungua miradi mbalimbali ya ujenzi wa barabara na reli hapa nchini;

Na kwa kuwa kwa hatua nyingine wakati wa tukio la kupewa tuzo hii Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ametambuliwa kama miongoni mwa viongozi wenye ushawishi mkubwa Duniani kwa mujibu wa Taarifa iliyotolewa na Gazeti la *TIME* la tarehe 24 Mei, 2022, jambo ambalo

linaendelea kumpatia sifa kubwa Rais wetu na Taifa kwa ujumla;

Kwa hiyo basi, Bunge hili katika mkutano wake wa saba, kikao cha Thelathini na Moja, tarehe 26 Mei, 2022 linaazimia kwa kauli moja: -

Kwanza, kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutambuliwa na kupewa Tuzo Kuu ya Mjenzi Mahiri ya Babacar Ndiaye kufuatia mafanikio makubwa ya Serikali ya Awamu ya Sita katika ujenzi wa miundombinu nchini Tanzania. *(Makofi)*

Pili, kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, kwa kutambuliwa kama miongoni mwa viongozi wenye ushawishi mkubwa duniani jambo linalolileteа sifa nzuri nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi/Vigelegele)*

Na tatu, kuendelea kumpa moyo Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa juhudi mbalimbali anazoendelea kuzichukua katika kuiletea nchi yetu maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja hii imeungwa mkono na Bunge zima. Sasa hii ni historia kwasababu haijawi kutolewa hoja hapa ikaungwa mkono na Bunge zima. *(Makofi)*

Haya, ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi/Vigelegele)*

Sasa kwa utaratibu wetu wa maamizio ili tuweze kufikia mahali ambapo tunaita sasa ni azimio la Bunge, kwasababu kwasasa ni mleta azimio au ni mtoa hoja, Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba, sasa utaratibu wetu ni kwamba tutafika mahali tutawahoji. Lakini kwasababu ni hoja ndiyo imetolewa kwa hiyo watu lazima wachangie kidogo ili tupate picha kabla sijawahoji waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Wabunge ambao watataka kuchangia kwenye hoja hii, wapo ambao baada ya kuona tu kwenye vishikwambi vyao kwamba kuna hoja hii basi wameleta majina hapa, lakini nitoe fursa kwa wale ambao pengine hawakuwa wametoa hiyo taarifa wasimame halafu nitawapa nafasi wachache kati yao.

Haya Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa Amar, Mheshimiwa Naibu Waziri naona umesimama Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu na Mheshimiwa Grace Tendega. Sasa hapo Katibu uwe unaandika hao ninaowataja maana mimi nipo *busy* kutaja sijawaandika hapa mbele. Mheshimiwa Omari, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mheshimiwa Jesca, Mheshimiwa Kirumbe Ng'enda.

Waheshimiwa Wabunge hawa watuwakilishe kwasababu ninayopia majina mengine hapa mbele kwa hiyo hawa niliyowataja wanatuwakilisha pamoja na haya niliyonayo hapa mbele. Tutaanza na Mheshimiwa Zahor Mohammed atafutiwa na Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, Mheshimiwa Cosato Chumi, ajiandae.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nikushukuru kwa kunipa heshima, hii ni heshima kubwa ambayo kwa kweli sikuidhania wala sikuiamkia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kusema kwa niaba yangu lakini kwa niaba ya Wabunge wenzangu,

kwamba Mama sisi kama Wabunge tunakupongeza sana sana sana. Kwa kawaida upo msemo wa Kiswahili unasema hakuna Nabii aliyewahi kupendwa kwao lakini mama sisi wenzako, Wabunge wenzako tunakupenda, tunakuthamini sana sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na kwenye hili nadhani ipo nafasi ya sisi kama Wabunge lakini sisi kama taifa kuanza kujitathimini upya kwasababu si lazima tusifiwe na wengine tunayo nafasi ya kujisifu na kusifu vya kwetu. Mheshimiwa Rais amefanyakazi kubwa, Mheshimiwa Rais anafanyakazi kubwa tunaiona, tunaithamini. Kwa hiyo, tunaomba tukupe moyo ili uendelee kufanya mema zaidi ili watanzania waendelee kufaidika kwa kuhakikisha kwamba unawaondoa walipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa maana yangu ni nini, zawadi au chombo hiki kilichotolewa ni kuashiria kazi kubwa aliyoifanya na anayoifanya mama kwaajili ya maslahi ya taifa lake. Mimi ningeomba mama yetu asirudi nyuma na sisi wabunge kwa kushirikiana na wananchi tuendelee kumpa moyo ili aone kwamba bado anahitajika kufanya mambo mazuri zaidi. Asiogope mama yetu kwasababu atakapofanya jema na sisi Wabunge tukaliona, tukamuunga mkono maana yake hili ndilo ambalo Watanzania wanalolitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niseme kwa ufupi hivi, kwamba kwasababu dunia imeona, kwasababu Afrika imeona, kwasababu Wabunge wenzangu mmeona maana yake ni nini, ni kuonesha kwamba mama yetu tokea ameteuliwa kuwa Makamu lakini pia kuteuliwa kushika nafasi ya chombo hiki kama taifa maana yake amekubali kuendeleza yale yote waliyoyapanga na yanakwenda mbio na hayasimami. Kwa hiyo, ningeomba sana sisi tumpongeze kwa kauli moja kama tulivyofanya lakini tumpe nguvu tukimuambia kwamba tupo pamoja na yeye, tutafanya naye kazi na hakika hatutamuangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa nafasi, lakini ningeomba niseme ni yeye pamoja na mawaziri wake lakini kwa kusaidiwa zaidi na Mheshimiwa Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Rais wa Zanzibar naye, kwasababu haya wanayafanya kwa umoja wao. Kwa hiyo, zawadi hii imetolewa kwa viongozi wetu wote ambao wanasaidia kuliongoza taifa hili. Nawapongeza, nawashukuru sana sana, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara atafuatiwa na Mheshmiwa Cosato Chumi, Mheshimiwa Grace Tendega, ajiandae.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, na mimi nichukue nafasi hii kuwaomba Wabunge wote kabisa tumpongeze Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, kwanza kabisa ametuheshimisha sana wanawake wa Tanzania na wanawake wa Afrika. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, kwanza hata katika teuzi ametuheshimisha, yaani ni kiongozi ambaye amesimama na kuona kwamba binadamu wote, wanaume na wanawake tunaweza tukafanyakazi. Pia tuangalie katika suala la miundombinu, miundombinu hii itawasaidia sana wanawake katika suala la uchumi. Kwa hiyo, ametuheshimisha kuona kwamba miundombinu yetu sasa inaendelea kukua vizuri na inaendelea kuboreshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambao Mheshimiwa Rais anastahili pongezi ni suala linalohusiana na eneo la afya. Mheshimiwa Rais amejipambanua sana kuona kwamba katika hospitali zetu, hasa maeneo ya wanawake kujifungua na watoto wadogo kupata huduma, amehakikisha kwamba zanahati zetu na vituo vya afya sasa hivi maeneo yote ukienda lazima yawe na sehemu ya wanawake kujifungua salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri sana anayoifanya upande wa miundombinu, afya na hata elimu. Kwa hiyo, anastahili pongezi na niwaombe Wabunge wote tuendelee kumtia moyo Mheshimiwa Rais, tumpongeze ili aendele kuboresha maeneo haya yote kwa manufaa ya wanawake na wanaume wote wa Tanzania, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Cosato Chumi, atafuatiwa na Mheshimiwa Grace Tendega, Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, ajiandae.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi napenda kutumia nafasi hii kwa niaba yangu mwenyewe na kwaniaba ya wananchi wa Mafinga kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa tuzo hii ambayo anaipata, akiwa ni kiongozi wa 12 katika Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuzo hii haitolewei tolewi tu, inatolewa kwa mtu ambaye kwanza amethibitisha dhamira yake katika kuendeleza miundombinu ya usafirishaji, hili si jambo dogo. Miundombinu ya usafirishaji na kuaminika huku kwa Mheshimiwa Rais kwanza kunalijengea taifa letu heshima lakini pia kunalijingea taifa letu kuaminika na kuaminiwa na vyombo vikubwa vya kimataifa duniani. Kama ambavyo tumeona, tuzo hii imetolewa na Benki ya Maendeleo ya Afrika, na tunafahamu mchango wa Benki ya Maendeleo ya Afrika katika ujenzi wa miundombinu katika taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwakutoa tuzo hii kwa Mheshimiwa Rais wetu si tu kwamba tunaendelea kuaminika katika Benki ya Maendeleo ya Afrika lakini pia tunaendelea kuaminika katika vyombo vingine vya fedha duniani. Kwasababu kama ambavyo tumeona kwenye bajeti yetu juzi

kila mbunge aliyesimama kilio kikubwa kilikuwa ujenzi wa barabara na kikubwa kilikuwa *resource* hazitoshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kuaminika na kwa kupata tuzo hii kwa kuheshimishwa kiasi hiki maana yake ni kwamba sasa kama taifa hata tunapoenda kuomba kama ni *grants* hata kama ni mikopo ya riba nafuu kwaajili ya ujenzi wa miundombinu ya taifa letu tutaweza kuaminiwa na kuaminika. Na hivyo, kwa kujenga miundombinu hiyo maana yake ni kwamba tutaweza kusafirisha bidhaa zetu kwa namna nyepesi, tutaweza kusafirisha mbolea zetu kuwafikia wakulima kwa namna nyepesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, itoshe kusema kabisa kwamba kama taifa, kama wabunge na kama Watanzania tujionee sifa kwa kuwa na kiongozi ambaye katika Afrika pekee mwaka huu ameenda kupewa tuzo hiyo. Ninaamini kabisa hata wana-Mafinga hapa ninapozungumza kuna ujenzi wa barabara zinaendelea pale Mafinga ni matokeo ya heshima hii ambayo tumepewa. Kwa hiyo, naunga mkono azimio hili na Mungu ambariki Rais wetu Mungu abariki Taifa letu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Grace Tendega atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, ajiandae.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Na mimi kwa niaba yangu binafsi lakini kwa niaba ya Watanzania nipende kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais Samia Suluhu Hassan kwa kweli kwa utekelezaji wa majukumu yake na hasa kwa tuzo kubwa aliyoipata. Tunaweza kuwa na changamoto ndani ya nchi lakini tunavyotoka nje hili ni la kupongeza kwa kweli kwa kupata tuzo hii. Ni sifa kubwa ametuletea Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuzo hiyo ya miundombinu ambayo ameipata; wananchi wengi mnaona changamoto ambazo tunazipata katika usafirishaji hasa wanawake katika kutatua changamo zao. Kwa hiyo tunapongeza sana kwa kupata hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hiyo amekuwa miongoni mwa viongozi mashuhuri 100. Kwa kweli ni kitu ambacho ni cha kupongeza sana, haijawahi kutokea. Lakini mama huwa anajali familia na anajali nje ya familia. Tunaona kwa vitendo jinsi ambavyo anafanya, tumeona Mheshimiwa Rais amejielekeza katika maendeleo ya watu, na tunaona katika sekta ya afya Rais anakwenda kujenga hata hospitali kubwa kwa ajili ya akina mama na Watoto. Hili ni jambo la kupongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye elimu ameangalia kila mkoa kwa kuhakikisha kwamba tunapata shule za wasichana. Hii itasaidia sana wanawake kuwa kuwa katika maamuzi katika maeneo mbalimbali. Tumeona pia kwenye sekta ya maji miradi mingi ya maji imeanzishwa, mingi inalenga kutimiza ile asilimia 85 vijijini na asilimia 95 mijini. Lakini pia mama ameleta mapinduzi katika kilimo, tumeona katika bajeti hii jinsi ambavyo amefanya. Cha muhimu ni kwamba fedha zikitoka tutaona matunda yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, licha ya hivyo tumeona mahusiano yake na mataifa ya nje. Ameonesha katika ziara zake anazokwenda ametoa fursa mbalimbali za kiuchumi na tunaona fursa za kiuchumi zinakuja katika nchi yetu. Ameimarisha mahusiano na nchi za nje, kwa mfano tumeshuhudia amehudhuria Mkutano wa Umoja wa Mataifa ambako alikwenda kuhutubia kwa umahiri mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumeona alihudhuria Mkutano wa Glasgow ambako kuna masuala ya mabadiliko

ya tabianchi. Huku tunaona ndiko gumzo kubwa sasa linalotokea katika mabadiliko ya tabianchi. Amehudhuria pia katika maonyesho ya kibiashara ya Dubai *(Dubai Expo)* ambapo wafanyabiashara wakubwa ulimwenguni wanakuja. Hili nalo limeleta umaarufu wa nchi yetu lakini tunajitoa kibiashara ili wananchi waweze kuja kuwekeza nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini alifanya ziara nchi za Ulaya, Ufaransa, na Ubelgiji. Hii yote ni kutanua wigo kuhakikisha wananchi wanaiona hiyo. Vilevile, umaarufu wa *Royal Tour;* kwa wale ambao wanaangalia sinema, ile tamthilia ya *revenge* kwenye king'amuzi cha Azam, jana Mellan alimwambia mchumba wake nikufanyie nini? au nikupeleke Tanzania. Kwa maana hiyo inaonyesha jinsi ambavyo ziara hii jinsi ambavyo ziara ya *Royal Tour* ilivyozaa matunda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninadhani kwa miaka ijayo Mheshimiwa Rais pamoja na kwamba alienda Marekani akakutana na Makamu wa Rais, lakini miaka ijayo mwakani labda anaweza akapata tuzo ya watu 20 hivi chini ya hapo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya Ahsanteni sana waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. Nilikuwa nimesha mtaja Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, ajiandae.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii. Nami niungane na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya heshima kubwa ambayo ameiletea nchi yetu. Tuzo hii ya Babacar N'Diaye, 2022 imetolewa kwa mtu mashuhuri. Nilikuwa naangalia tofauti kati ya mashuhuri na maarufu. Mashuhuri ni mtu ambaye amejulikana kwa jambo jema, maarufu anaweza akawa hata maarufu kwa mambo

mabaya. Kwa hiyo, sasa tuna Rais ambaye ni mashuhuri duniani amejulikana pamoja na mambo mengine ujenzi wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alipoapishwa mojawapo ya kauli mbiu zake kubwa sana ni kuifungua nchi na kukuza uchumi. Uchumi na miundombinu ni sawasawa na chakula na vyombo vya kulia chakula. Miundombinu ndiyo inayofikisha uchumi kwa wananchi. Kwa hiyo, mtu unaweza ukakuza uchumi wa nchi yako. Sasa, kama miundombinu hakuna faida zile zitashindwa kufika kwa wananchi wako. Kwa hiyo, tumpongeze sana Mheshimiwa Rais kwasababu amedhamiria kwamba uchumi huu unaokuzwa uwafikie wananchi hasa wale wa maeneo ya vijiji; na ndiyo maana tunapata fedha nyingi kwa ajili ya barabara za vijijini na maeneo mengine. Nchi hii ni pana sana, ina eneo kubwa, inahitaji mtu mashuhuri kuweza kutengeneza miundombinu ya kufikia nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli pamoja na yote ambayo yamesema juu ya miradi tunayoiona kwa macho yetu, miradi ya reli, ndege, meli na kadhalika lakini hayo sisi Watanzania tunayaona kabisa na wala hatuna haja ya kuambiwa na mtu. Kinachonifurahisha ni kwamba hata dunia imeona haya yanayofanyika na kuweza kumfikisha Mama hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, ningependa, kwa vile makao makuu ni hapa Dodoma na Bunge hili tunazungumzia kutoka Dodoma; nilisoma taarifa ya tathimini ya ile Tume iliyotoa zawadi hii, mojawapo ya vitu ambavyo walivizungumzia ni barabara hii ya *ring-road* ya Dodoma. Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba watendaji wetu watahakikisha kwamba inamalizika kwa wakati ili mwaka ujao tupate zawadi nyingine kubwa zaidi kuliko hii ambayo tumepata kwa sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie tu hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati anapokea tuzo hii jinsi ambavyo imetuma ujumbe kwa dunia. Jambo la kwanza ambalo nimeli-*note* kwa umuhimu sana, ni kwamba Mheshimiwa Rais wakati anapokea tuzo hii alitambua mchango wa watangulizi wake katika kufikia hapo alipofikia. Kipekee kabisa alitambua mchango wa Serikali ya Awamu ya nne chini ya Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, akatambua Awamu ya Tano chini ya Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu ni ujumbe kwa Afrika, kwamba nchi inapokuwa na utaratibu wa kubadilishana madaraka kwa amani na kwa katiba na sheria wananchi wanapata faida kubwa ya muendelezo wa mambo mema ambayo yalikuwa yakifanyika tofauti na pale ambapo tunabadilishana kwa kupambana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili liko jambo ambalo limejibiwa kwa vitendo na tuzo hii. Pamekuwa na dhana kubwa kwamba tunahitaji maono ya Kitaifa. *Fine,* lakini sasa hapa kuna majibu ya vitendo, kwamba kuna uendelezaji wa mambo ya awamu zilizopita, na siyo kwamba kila awamu inapokuja ina jambo lake. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kipekee kabisa, nalipongeze Bunge lako Tukufu kwa kuja na azimio hili, nampongeza kipekee dada yangu Mheshimiwa Zainab Katimba, kwa kutuongoza kwenye hili na ninaunga mkono hoja hii na ninaomba Waheshimiwa Wabunge tuunge mkono hoja hii kwa nguvu zetu zote, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jesca Msambatavangu atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Nassor Amar na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, ajiandae.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nami nichukue fursa hii kwa kweli kumpongeza Rais

wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa tuzo hii aliyoipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mimi ni Balozi wa Afya ya Akili, nitaomba nitumie mfano ili watu waelewe, kwa sababu kuna watu wengine huwa pia hawaelewi. Mimi niseme hivi, hii tuzo ni kama kombe ambalo huwa zinacheza ligi zetu humu ndani ya nchi. Hapa hii tuzo ilikuwa inagombaniwa na nchi 54. Nchi zote za Bara la Afrika na wachezaji walikuwa ni Wakuu wa Nchi kwenye timu hizo, lakini aliyekuwa kashikilia tuzo hii ilikuwa ni wenzetu *Nigeria*. Kwa hiyo, naweza nikaendelea kutoa mfano; nichukulie kama *Nigeria* ilikuwa ni Yanga na Mama Samia ni Simba; wameingia kwenye fainali. Zilikuwepo sheria, kama zilivyo sheria 18. Hapa kamati ile ikaangalia, maana kuna watu hawaelewi wanafikiri labda imetolewatolewa tu kwa sababu ya hivi hivi, hapana. *(Makofi/Kicheko/Kigelegele)*

Mheshimiwa Spika, jambo mojawapo Mbunge mwenzangu aliyemaliza kusema ameshamaliza. La kwanza, ilikuwa wameangalia shilingi milioni 290 ambazo Tanzania tume-*qualify* kwa vigezo kupewa na Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa ajili ya kuendeleza miundombinu chini ya usimamizi wa Rais Samia Suluhu Hassan, tukashinda kwa vigezo, tukaonekana tunafaa kupewa fedha hiyo kwa ajili ya kuendeleza miundombinu ya barabara, reli na usafiri wa anga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ya pili ikaangaliwa maono yetu baada ya kuwa tunajenga reli, tutai-*manage* vipi? Tutaiendeleza vipi? Tukaingia mkataba na kampuni nyingine ya China kutupatia *modern flit cars* kwa ajili ya kuendeleza sekta hii ya reli ambapo tutakuwa na magari 1,430 kwa ajili ya kusimamia uendelezaji wa sekta hii ya miundombinu ya reli. Hii iligharimu karibu dola milioni 172.2. Hayo ndiyo tuliyomtoa *knockout Nigeria. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ya tatu, ikaonesha nia ya Serikali ya Rais Samia; nimewahi sikia tetesi tetesi kwamba ule Mji Mkuu wa Nigeria, Abuja ule ramani yake inafanafana na *masterplan* ya Mji wa Dodoma. Sasa wao wamejenga ule Mji lakini walishindwa kwenye *ring road* hawajafanya. Sisi Tanzania tarehe 11 Februari, Rais wetu amezindua na kuanza rasmi ujenzi wa *ring road* katika Mji wetu wa Dodoma. Hiyo moja ilikuwa ni *credit. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ndugu zangu Watanzania tunaposema Mama anafanya kazi kubwa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hata vitabu vya Mwenyezi Mungu vinasema, wakati mwingine Nabii hapati heshima kwao. Ila mimi kama Balozi wa afya ya akili, naweza nikasema ni matatizo pia ya afya ya akili kutotambua kwamba una kitu cha thamani au una kiongozi bora ndani ya nyumba yako na kubeza juhudi za mama anapotoka kwenda kutafuta chakula; au baba anapotoka kwenda kupambana na maisha ili arudi na kitu kuendeleza familia. Ile nayo ni matatizo ya afya ya akili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ndugu zangu mama anapokuwa katika harakati za kuwepo ndani ya Tanzania, au anapokuwa katika harakati za kuwepo nje ya nchi ya Tanzania, ni kwa maslahi mapana ya Taifa letu. Leo hii katika hiyo fedha kila Mbunge hapa alipewa shilingi milioni 500 na wengine wamepewa shilingi bilioni moja. Leo hii nikifika Iringa, nikienda katika Kata yangu ya Mkimbizi pale, Namtivila kuna barabara tumejenga ambayo tumepeleka shilingi milioni 500 kutoka katika mgao huu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa kengele imeshagonga, ahsante sana.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa hiyo, nawaomba ndugu zangu tumuunge mkono mama, anaupiga mwingi!

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Hussein Amar atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, halafu Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, ajiandae.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu. Kwanza kabisa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Nyang'wale, tunaungana na Wabunge pamoja na wananchi wote kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan kwa tuzo ambayo ameipata na kuiletea heshima kubwa nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Mama anaupiga mwingi na anaupiga mwingi kweli kweli. Hapa sasa kwa lugha ya Kisukuma kama naruhusiwa kusema, wanasema "*shirikalewa mnzengo hatina mangaka.*" Maana yake ni kwamba, Askari wa Kijijini kwenu huwa hatishi, lakini Mama ametisha Kimataifa mpaka kupata tuzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuendelee kumuunga mkono kwa mambo mengi aliyoyafanya kwenye miundombinu mbalimbali mfano ujenzi wa reli ya *SGR,* ujenzi wa bwawa la umeme, ujenzi wa madaraja, ujenzi wa miundombinu ya afya, ujenzi wa miundombinu ya kilimo na mambo mengine mengi. Mama ameupiga mwingi ndiyo maana amepata tuzo, nasi kama Watanzania tuendelee kumuunga mkono mama yetu kwa kazi nzuri anazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina mengi yakusema, kwa niaba ya sauti ya wananchi wa Nyang'wale na Wabunge na

Watanzania wote tuendelee kumuuga mkono Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, atafuatiwa na Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda na Mheshimiwa Omar Omar, ajiandae.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru nami kupata nafasi ya kutoa pongezi kwa ajili ya tuzo ya Rais aliyoipata. Sisi kama wanawake kutoka *Beijing Platform* tulikuwa tunatamani sana wanawake kuwa viongozi kwenye ngazi za juu za maamuzi. Mheshimiwa Rais kwa kupata nafasi hiyo, ninaamini anaitendea haki na ndiyo maana leo tunazungumzia habari ya kupata tuzo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulikuwa tunasikia zamani Corazon Aquino kutoka Philippines kama Rais wa kule, tulikuwa tunasikia habari za akina Margaret Thatcher, lakini leo hii katika nchi yetu tuna Rais ambaye ni kiongozi. Vilevile leo tunapotoa pongezi hizi, kiongozi huyu amekuwa kiongozi wa 12 na inaonesha ni mwanamke wa kwanza kabisa kupata tuzo hii katika benki hiyo. Hii peke yake inamfanya yeye kuwa Balozi wa Afrika ili aweze kupata pesa za kuweza kujenga miundombinu tena Tanzania zaidi ya ile tuliyojenga, tuweze kupata maendeleo ya Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshauri Mheshimiwa Rais na kumpongeza kwamba yeye kama ni Balozi na amekuwa mwanamke wa kwanza kupata tuzo hiyo, basi nafahamu nchi za kwanza za dunia na za pili zitaona umuhimu wa kuleta *fund* katika nchi yetu ya Tanzania na kuweza kumsadia kumalizia majukumu yake hasa ya miundombinu ambayo bado kama Taifa tunahitaji kuijenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia kiongozi kupata nafasi, ni kusimamia kile ambacho watu wamekuamini wewe kukifanyia kazi. Nasi wanawake tuko vizuri sana kwenye maamuzi; tunapoamua kufanya kazi ya maamuzi tunasimamia kweli kweli. Mwanamke ana nguvu ya kuamua, mwanamke anapoamua kufanya kitu chake anaweza kufanya na akalisaidia Taifa kwa ajili ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe mwenyewe ni mwanamke, tunaona maamuzi unayofanya na kazi unavyoisimamia. Vivyo hivyo na sisi Wabunge wanawake tunapoamua; tukiamua, wako wanawake ambao hawaamui, lakini wanawake wanapoamua mambo yao, wakiona yana msingi kwa Taifa lao, wanasimamia wanachokiamini. *(Makofi/Vigelegele)*

**MBUNGE FULANI:** Haleluya! *(Vigelegele/Makofi)*

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, niseme hivi; Mheshimiwa Rais, sisi kama wanawake unachokisimamia, kisimamie; simamia Watanzania, tuzo uliyoipata ni ya kwako, lakini ni ya Watanzania, hususan wanawake. Tunakuamini kwa kile unachokifanya lakini hiyo iwe ni chachu ya kusimamia mambo makubwa ambayo yako mbele kama Taifa na kama wanawake tunaenda kuyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, nampongeza kwa tuzo hii na atakapofika *airport* ninaamini wanawake watakuwa wa kwanza kwenda kuipokea tuzo hiyo maana ni ya kwao. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda atafuatiwa na Mheshimiwa Omar Omar na Mheshimiwa Ummy Nderiananga ajiandae.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, naungana na wenzangu wote kwanza kutoa pongezi nyingi na kuunga mkono hoja iliyoletwa hapa ya kumpongeza Rais wetu kipenzi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilipotaka nianze mimi, ni kuwakumbusha Watanzania umuhimu wa kuwaandaa viongozi. Mama Samia Suluhu Hassan aliandaliwa kuwa kiongozi. Kwa hiyo, pongezi za kwanza kabisa tukipe chama ambacho kilimwandaa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuwa kiongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa nataka tukumbushane kwamba mwaka wa 2000, Mama Samia Suluhu Hassan alichaguliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na akapewa kuwa Waziri wa Afya katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mwaka wa 2005 akaendelea na nafasi hiyo ya uwakilishi na akawa Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mwaka wa 2010 akapewa kuwa Waziri katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anayehudumu kwenye shughuli za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengi tunakumbuka hapa mwaka wa 2014, wakati tunahangaika na suala la Katibu mpya, Mama Samia Suluhu Hassan alichaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge la Katiba. Ilipofika mwaka 2015, Mama Samia Suluhu Hassan alichaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa nini nimeyasema haya? Ukiona vimeelea ujue vimeundwa. Mama Samia Suluhu Hassan aliandaliwa na sasa ameonesha umahiri mkubwa sana katika uongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nije katika tuzo. Afrika peke yake ina nchi 54, lakini kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa, nchi zilizoko duniani ni 233. Rais wetu wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania anatajwa kuwa kiongozi mwenye ushawishi na maarufu katika dunia ambayo ni viongozi 100 tu ndiyo wamepata sifa hiyo katika Mataifa 233 duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niwakumbushe Watanzania, huu ushawishi Mama Samia ameuonesha kwa kiwango kikubwa wakati tunahangaika na mapambano ya *COVID-19*. Alikwenda katika Jumuiya ya Kimataifa kuomba fedha, wengine wakaomba fedha za barakoa, wengine wakaomba fedha za *sanitizer,* yeye akaomba fedha kwa ushawishi, wakamkubalia fedha hizo zisambae katika kupambana na *COVID* kwa kupeleka kwenye elimu, kwenye afya na kwenye maji. Kwa hiyo, tukawa tumepata faida mara mbili, kwamba tunapambana na *COVID* lakini tunasaidia kutatua changamoto katika sekta ya elimu, afya na maji. Huu ndiyo ushawishi unaozungumzwa kwa kiongozi wetu, anaweza akakaa na chombo chochote duniani akasema na akasikilizwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumefanikiwa katika miundombinu, wala hili halina ubishi. Nitumie nafasi hii kusema kwamba naunga mkono hoja iliyotolewa hapa ya kumpongeza Rais wetu na kwa kweli tujiandae kumpokea na kuendelea kumpa ushirikiano mkubwa, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Omar Omar, atafuatiwa na Mheshimiwa Ummy Nderiananga na Mheshimiwa Selemani Jafo ajiandae.

**MHE. OMAR ALI OMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nami nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nianze kwa kusema kwamba Waswahili wanasema, kizuri chajiuza, kibaya chajitembeza.

Pia kuna Mwalimu mmoja wa Kiswahili, Shaaban Robert katika kitabu chake cha Adili na Nduguze, alisema kwamba, haja ikishughulikiwa kwa matendo, humalizika upesi, lakini ikichelewa, huchelewa kama sadaka ikishughulikiwa kwa maneno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anafanya matendo. Anawaachia watu wakazungumza maneno; na nime-*quote speeches* zake nyingi anasema kwamba, "kuna watu watatusikia, watatuona kwa matendo yetu lakini walio wengi watatupongeza na walio wachache watasema watabeza."

Kwa hiyo, sote tuliomo katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumeziona juhudi za Mama Samia, amezifanya vizuri kabisa, hata kwenye Jimbo langu najisifia kwamba sasa hivi juhudi za Mama Samia naziona. UVIKO-19, kuna majengo ambayo yanajengwa ndani ya Jimbo langu kwa fedha za UVIKO-19. Zimetoka kwa nani? Kwa Mama. Kwa hiyo, ni kuonesha kwamba Mama ana juhudi kubwa kabisa ya kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe mfano mmoja mkubwa kabisa ambao huo ni kisa maarufu na kinaendelea mpaka leo duniani. Mama Hajra wakati alikuwa anatafuta maji, alikuwa anakwenda Kusini na Kaskazini, Mashariki na Magharibi kutafuta maji; nani aliyekuwa akitafuta maji? Ni mama. Matokeo yake maji yalipatikana. Kwa hiyo, hii ni kuonesha kwamba mapambano ya mama, ni mapambano makubwa na ataendelea kupambana mpaka dakika ya mwisho kwa ajili ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naunga mkono azimio hili kwa asilimia mia moja. Ni azimio ambalo lina mashiko, lina mwelekeo; na tumpe moyo Mama yetu aweze kutuongoza

vizuri, na kila mtu aliyekuwa ana nia mbaya kwetu sisi na kwa Tanzania hii, basi Mungu ndiye anayejua vipi anaweza kumshughulikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho nina ombi maalum kwa Bunge. Kwa vile tuzo aliyopewa mama ni ya kwetu, tutayarishe jambo maalum la kumpokea Mama katika tuzo hii ili tuone sasa kwamba kweli tunamthamini kwa tuzo hii aliyoipata ni ya Watanzania wote. Kwa hiyo, nasema kwamba Mheshimiwa Sophia Mwakagenda kasema wanawake waende, lakini na wanaume sote twende tukaipokee hiyo tuzo. *(Makofi/Kicheko/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Ummy Nderiananga, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Jafo na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma ajiandae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, nilishukuru sana Bunge lako Tukufu kwa kupitisha azimio hili la kumpongeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Serikali napenda nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan. Wabunge waliotangulia wamesema, nami niseme kwa lugha ya wenzetu, *a leader is the one who lead the way and show the way.* Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, ameyaonesha kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nirejee kipindi fulani nchi ya Marekani walipokumbwa na anguko la uchumi, walimpata Rais Franklin

Roosevelt. Rais huyu aliwaonesha namna ya kufufua uchumi wa Marekani, akawaambia kwamba *I will show you the new deal.* Mheshimiwa Rais Samia ameichukua nchi kipindi ambacho tupo katika janga kubwa la corona. Uchumi wetu umeanguka lakini Mheshimiwa Rais Samia ametuonesha njia, tumepanda kwenye uchumi wetu uliokuwa umeanguka kwa asilimia nne, sasa tuko 5.2 na dhamira yake ni kuupeleka kurudi kwenye 6.8. Nani kama Rais Samia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Samia Saluhu tuzo hii aliyopewa ni ya heshima kwake, kwa Watanzania, kwa wanawake na dunia. Nchi yetu tunajivunia sana kwa uwepo wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa sababu kwa kazi zake nyingi na kubwa alizozifanya Waheshimiwa Wabunge wamezieleza hapa, Mheshimiwa Rais kwenye elimu amefanya kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaalike pia wanaoendelea kutoa tuzo duniani kwenye elimu wamwone Mheshimiwa Rais Samia, kwenye afya wakitaka kutoa tunaye jemedali mpambanaji Mheshimiwa Rais Samia ambaye amefanya kazi kubwa na nzuri sana ya kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Samia toka amepewa kazi ya Urais halali, anachapa kazi usiku na mchana, Watanzania tumemwona, tumefurahia kazi yake, amefanya kazi kubwa sana kwenye *royal tour* na watalii wameanza kuja na kuiunga mkono Serikali yetu. Kwa kweli sisi sote tumefurahi tumefarijika sana kwa tuzo hii ya heshima kwa Mheshimiwa Rais, tunamwombea kwa Mwenyezi aendelee kumlinda, ambariki kwenye majukumu yake ili aweze kuendelea kuwaletea Watanzania maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kumuunga mkono Mheshimiwa Rais Samia, tunamwambia kazi iendelee na sisi

tunaoamini katika uongozi wa hoja na kazi, tunasema kazi yake inaendelea vizuri, hongera sana kwa Mama, Mungu ambariki sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Selemani Jafo atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Msukuma na Mheshimiwa Charles Mwijange ajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, awali ya yote ningependa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye ametufikisha siku ya leo, ambapo kwa ujumla wote tunaona Bunge bila kujali itikadi zetu za Vyama vya Siasa. Sote tunajadili ajenda kubwa ya kitaifa kuhusu suala hili la Mheshimiwa Rais. Hili jambo ni kubwa sana, Watanzania tuna kila sababu ya kujivunia. Heshima hii iliyotolewa kwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania watu waliipima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukumbuke kwamba Rais alipopata majukumu haya ya kuiongoza Jamhuri ya Muungano Tanzania, Taifa lilikuwa limekabiliwa na ujenzi wa miundombinu mingi iliyokuwa inaendelea, ukiangalia ujenzi wa reli *standard gauge,* barabara zinazofunganisha mikoa katika maeneo mbalimbali, endapo kipindi kile Rais asingekuwa Rais mwenye msimamo, mwenye kujali watu, mwenye kujali mustakabali wa Taifa hili, Taifa lingeenda mahali pabaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki tunaona ujenzi wa reli ulivyoshika hatamu katika maeneo yote. Tukumbuke tulikuwa na kipande cha kwanza tu kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro na kipande cha pili toka Morogoro mpaka Makutupola, lakini tunaona jinsi gani hii kazi inavyoendelea kuiunganisha nchi yetu katika *standard gauge.* Pia kuna suala zima la ujenzi wa miundombinu hii tunayozungumza, leo hii tumeshuhudia suala zima la mkataba mkubwa wa ujenzi

wa barabara ya *ring road* katika Mkoa huu na Jiji la Dodoma, tuna kila sababu ya kumpongeza sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, yapata wiki moja sasa imepita, tumemshuhudia Rais akiunganisha suala zima akizindua mradi mkubwa wa barabara unaounganisha Mkoa wa Singida na Mkoa wa Tabora, lakini Mkoa wa Tabora na Katavi, nani kama Mama Samia? Kungekosa udhibiti wa usimamizi wa maeneo hayo, hayo mambo tusingeyaona, lakini ukiangalia leo hii, watani zangu kule Wasukuma ukienda angalia lile Daraja la Busisi linavyojengwa kwa nguvu kubwa, hii yote ni kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati Rais anashika majukumu haya, tunafahamu ujenzi wa *Tanzanite Bridge* pale Dar es Salaam ulikuwa unaendelea, bila yeye kusimama kidete tungeona wakandarasi wale wanaondoka *site*. Tumeshuhudia daraja limekamilika daraja limefunguliwa, nani kama Mama Samia? Tukumbuke barabara zinazotuunganisha katika maeneo mbalimbali ya barabara za *TARURA* ambayo bajeti yetu tumehama kutoka bilioni 280 mpaka leo hii kuzungumzia bilioni 803, nani kama Mama Samia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii hata ukienda kule Mbuchi kwa ndugu zangu kule Kibiti watu waliokuwa wanahangaika nenda kaangalie daraja kubwa zaidi ya Shilingi bilioni sita, nani kama Mama Samia? Watu walikata tamaa, Rais asingekuwa na msimamo wa kusimamia miundombinu katika nchi yetu hii, hali yetu ingekuwa mbaya. Kwa kweli naomba niwaambie, hili jambo Mama ametuvisha nguo Watanzania, amefanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi iliyoanzishwa na viongozi wa awali mpaka yeye alipoipokea, wakati ujenzi wa miundombinu hii ukishika hatamu kipindi cha Mkapa, wakati wa Kikwete, wakati wa Marehemu Dkt. John Pombe

Magufuli, yeye akaiendeleza kwa kasi, leo hii Watanzania tumevishwa nguo, tunaenda vizuri zaidi. Tuna kila sababu ya kuliombea Taifa letu, lakini tuna kila sababu ya kumwombea Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu kuna kauli Wazaramo wanasema *kanoga afile,* watu hawasifiwi mpaka siku wametoka duniani. Leo hii tumeona dunia imemsifia Rais wetu akiwa hai, jamani! Katika hili niwaombeni Watanzania, jambo kubwa tuendelee kumuenzi na kumpa moyo Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kazi kubwa anayofanya, sidhani kama huyu mama analala, kwa hii kazi kubwa analiyoifanya tuna kila sababu kwa umoja wetu na kwa mapenzi yetu, tumwombee sana Rais Mama Samia Suluhu Hassan aendelee kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii tunaona faraja kubwa aliyopata mpaka hata kwa watoto wadogo, hapa tumezungumzia miundombinu ya barabara lakini leo ukiangalia mradi wa Shilingi trilioni 6.5 ujenzi wa Bwawa la Nyerere linaloendelea, zaidi ya *megawatts* 2,115 itazalishwa, nani kama Mama Samia? Leo hii ukiangalia manunuzi ya ndege hata bajeti iliyopita jana hapa, tumepitisha bajeti ya ununuzi ya ndege mpya lengo ni kwamba ajenda ya utalii iendelee kutamalaki katika Taifa letu. Katika hili hata kama tuna upungufu wetu wa hapa na pale, lazima Taifa tuungane kwa pamoja kuliombea Taifa letu na kumwombea Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukifanya hivi na kuondoa chuki zisizokuwa na sababu yoyote, tutalifikisha Taifa letu mbele. Hivyo, tusijiharibie sisi wenyewe, tunafanya vizuri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, naunga

mkono hoja na hongera sana dada yangu Katimba. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Charles Mwijage na mtoa hoja ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Rais. Kweli Watanzania tuna kila sababu ya kujivunia uongozi wa Mama Samia ukizingatia kwenye wakati tuliopita ni wakati mgumu sana, lakini hata baada ya kuondokewa na mpendwa wetu Mheshimiwa Magufuli, tumempata Rais ambaye ameenda kuonesha Afrika kwamba Tanzania ni nchi ambayo inadumisha amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimemsikiliza mchangiaji mmoja dada yangu Mheshimiwa Tendegu na mimi nimekuwemo Bungeni huu unaenda mwaka wa saba, ni azimio la kwanza kwenye Bunge linaungwa mkono na vyama vyote hata na upinzani ikiwemo CHADEMA, lakini amezungumza vizuri sana dada Mheshimiwa Tendegu kwamba wanawake wanaweza hasa wakiamua jambo lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikwambie, kwa uongozi wa Mama Samia, sio wanawake tu wanaoufurahia hata sisi wanaume tunamfurahia sana, hata Vvyama vya Upinzani, hebu angalia leo Mbowe ndio anaongoza kwenda Ikulu, najua alipa-*miss* sana, lakini amepata nafasi ya kuingia na kutoka zaidi ya mara tano. Hongera sana kwa Mama Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na ushindani wa nchi zaidi ya 54, lakini Mama Samia ameongoza, nafananisha na ligi ya Tanzania, kama alivyosema mama wa afya ya akili kwamba tumemnyang'anya Nigeria ambaye ndio alikuwa na tuzo hiyo. Ni sawa na Tanzania tu, tunatarajia kumnyanganya

mnyama *very soon* labda Jumapili na ningemwomba Mama Samia huko aliko anisikilize, najua atakuja, nimkaribishe sana Mwanza tumpe zawadi ya Kitanzania. Najua aliyopewa kule ni tuzo aje tumpe mnyama kesho kutwa hapa tunavyomchinja, apate zawadi. Najua tulimpa uwanja wa Taifa alipokuwa mgeni rasmi, aje na Mwanza kule Jumapili tutampa zawadi kama alivyozoea kupewa hata akiwa kule Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo ukizunguka kila jimbo hapa utakuta mtambo unatengeneza barabara. Nimekuwa Mbunge miaka saba, nimelia lami humu miaka saba, leo hata Jimbo la Geita Vijijini tuna kilomita 25. Kwa niaba ya wananchi wa Geita Vijijini, tunamwombea mema sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo ukienda vijijini pamoja na kwamba hatuwezi kujenga lami kila mtaa, kila kijiji, lakini leo tuna pesa za kutosha kujenga barabara zinazopitika mchana na usiku.

Mheshimiwa Spika, sasa utanisamehe sana sisi Wasukuma huwa tukifurahi hatuna maneno mengi, ningekuomba mimi sitaruka sarakasi, wala sipigi magoti, tukifurahi sisi Wasukuma wamo humu wenzangu watanisaidia tunafanyaje?

**WABUNGE FULANI:** Tunaimba.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Tunafanyaje.

**WABUNGE FULANI:** Tunaimba.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, sasa naomba niimbe wimbo, utaniruhusu? Tuna imani na Samia…

**WABUNGE FULANI:** Oyaa, oyaa, oyaa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma! Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Musukuma magoti na sarakasi haviruhusiwi humu ndani ni pamoja na kuimba, hairuhusiwi. (*Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, hii ni kwa sababu ili Mbunge mwingine aweze kuzungumza lazima mimi niwe nimemwita, sasa wewe ndio utakuwa umemwita ili akusaidie kuimba wimbo, kitu ambacho hakiruhusiwi. Ahsante sana.

Mheshimiwa Charles Mwijage, halafu mtoa hoja ajiandae.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Zainab Katimba kufuatia tuzo aliyoipata Mheshimiwa Rais kwenye kuimarisha au kujenga miundombinu.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru na wewe kipekee kwa kutaja jina langu na baada ya kulitaja ukanitamka nikiwa wa mwisho, matokeo yake nitakachosema hapa ni meseji nilizotumiwa na Wanajimbo wa Wilaya ya Muleba kwa ujumla na nyingine nimekurushia wewe.

Mheshimiwa Spika, Muleba wanasemaje kwenye tuzo hii? Wanasema jema lolote, lililoshindikana katika nchi hii sasa kwa Mama litalekelezwa, hiyo ni Muleba, jema lolote katika nchi hii lililofikiriwa na likashindikana kutekelezwa kwa Mama litatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Muleba ni kubwa mno, wanasema Mheshimiwa Rais sio kwamba amejenga barabara, amejenga barabara kule ambako watu hawakufiria. Ukienda kule Muleba kule ambako watu hawakufikiria, alipopaona Mjerumani Muleba kuna barabara, amejenga barabara katika Kata ya Kamachumu na Luanga kupita Kyaraburamula ameshuka akaenda Chuo cha Elimu Katoke

akajenga barabara mpaka ziwani Kamugaza. Wanasema Muleba, amejenga madaraja, barabara ya Kyamyolwa kwenda Kimeya, Kumuliza mpaka Kashebuko amejenga barabara. Kimbugo amejenga barabara, Mheshimiwa Rais amejenga barabara Kakindo mpaka Maziba, Mayondwe mpaka Bugasha, Muramura na Kyamyolwa. Mama anafungua barabara anakwenda kule ambako watu hawakufikiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, amejenga barabara kwenda Ngenge zaidi, wameniambia mama, wanavyosema ni *wagandagaza*, *wagandagaza* maana yake nini ukimuona mtu analia, ukampangusa machozi, unaitwa *uwagandagaza*. Anajenga barabara kwenda Rutoro, kwenye Kisiwa cha Bumbile, mama anafanya mambo tofauti lakini yaleyale yaliyozoeleka. Wananchi wa Muleba na Kagera kwa ujumla wanampongeza na wanasema mama isifike mwezi Oktoba hujafika, haya matatizo madogo madogo ya ardhi yatakuwa yanakuja, uje tusherehekee, wamkumbuke Baba wa Taifa wakati anasema Mwenge.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi/Vigelegele)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba aje ahitimishe hoja yake. *(Makofi)*

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Spika, azimio hili limechangiwa na Wabunge mbalimbali kwa sababu ya muda sitoweza kuwataja majina yao, lakini Wabunge hawa wote kwa kauli moja wamepongeza sana tuzo hii aliyoipata Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan na pia kwa kutambuliwa kwake kuwa miongoni mwa viongozi 100 wenye ushawishi mkubwa duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa wameenda mbali, si tu kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa umahiri wake kwenye kuboresha miundombinu, lakini wameenda zaidi kupongeza umahiri wake katika kuboresha sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Afya, Sekta ya Elimu, Sekta ya Maji na Sekta ya Kilimo ambazo ndio zinaenda kuchochea maendeleo ya nchi yetu kwa kasi sana na kuleta maendeleo ya watu na hasahasa wale wa vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ni kielelezo cha uongozi bora, uongozi mahiri, sio tu kwa Tanzania bali kwa dunia nzima. Pia Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ameonesha umahiri mkubwa sana katika kuboresha miundombinu katika nchi hii, jambo ambalo linaenda kuchochea uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ameonyesha uthubutu kwenye kuendeleza na kusimamia miradi mikubwa ya miundombinu ambayo inaenda kuibadilisha Tanzania. Miradi hiyo ni miradi ya kuunganisha mkoa kwa mkoa, miradi ya kuunganisha Tanzania na nchi jirani, ambapo ameendeleza miundombinu ya reli ya kisasa yaani *Standard Gauge Railway*, barabara na madaraja makubwa nchini. Yote haya yanaenda kuleta mageuzi makubwa sana kwenye nchi yetu na kuchochea sekta mbalimbali za uzalishaji ambazo zitaenda kuleta athari chanya kijamii lakini pia kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Watanzania tuna kila sababu ya kumuunga mkono Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan. Watanzania tumuunge mkono Mheshimiwa Rais kwa vitendo na vitendo hivyo ni kwa kila mmoja kutimiza wajibu wake; tufanye kazi kwa bidiii, tutimize wajibu wetu tunaopewa kwenye dhamana tulizokuwa nazo. Viongozi wote wa kila ngazi tuwahudumie wananchi, tumuunge mkono Mheshimiwa Rais kwa kuwahudumia wananchi. Nchi

hii itajengwa na sisi wote. Hapo pia wananchi tuna wajibu wa kutimiza majukumu yetu kama raia wema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuishukuru sana benki ya *AfDB (African Development Bank)* kwa mchango wake katika mafanikio haya. Naomba sana nichukue nafasi hii kuendelea kuwaomba sana benki ya *AfDB* iendelee kutoa ushirikiano mkubwa sana kwa Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan, kwa sababu dunia nzima imethibitisha kwamba fedha tunazozipata sisi kama Tanzania tunahakikisha zinaenda kwenye maendeleo ya watu. *(Makofi/Vigelelegele)*

Mheshimiwa Spika, sisi wote ni mashahidi kwamba Serikali ya Awamu ya Sita, Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan inasimamia matumizi bora ya rasilimali za Taifa, inasimamia na inapinga ufisadi na inasimamia utawala bora. Kwa hiyo tunaomba sana wadau mbalimbali waendelee kumuunga mkono Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ili aweze kuendeleza yale aliyoyaanza kwa kasi kubwa sana na sisi Watanzania tuendelee kuwa na imani naye, tuendelee kumwombea, naamini Mungu ataibariki Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana Mheshimiwa Zainab Athman Katimba. Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Ahsanteni sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa utaratibu wetu nitawahoji. Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki hoja ya Mheshimiwa Zainab Athman Katimba ya Azimio la Bunge la

kumpongeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa miongoni mwa viongozi wenye ushawishi mkubwa duniani na kupewa tuzo ya mafanikio ya ujenzi wa miundombinu waseme ndiyo, wasioafiki waseme siyo, hawapo. Kwa hiyo, walioafiki wameshinda. *(Makofi)*

*(Azimio la Bunge la Kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa miongoni wa viongozi wenye ushawishi mkubwa duniani na kupewa Tuzo ya Ujenzi wa Miundombinu Lilipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa umoja wenu niwapongeze sana namna mlivyoitikia hoja hii ya Mheshimiwa Zainab Athman Katimba ya kumpongeza Mheshimiwa Rais, mmefanya jambo la heshima kubwa sana kwa nchi hii pia kwake binafsi Mheshimiwa Rais kwa juhudi anazozifanya za kuliletea Taifa hili maendeleo. Maana kama isingekuwa Wabunge wote mmesimama kwenye kuunga mkono hoja yake alipoitoa mwanzo pengine kungekuwa na maswali maswali hivi, kumbe nchini kwake Mheshimiwa Rais wao wenyewe hawazioni barabara lakini sisi huku *AFDB* tumeziona hizo barabara. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mmefanya jambo la heshima sana na mimi niwapongeza sana. *(Makofi)*

Pia ninampongeza mtoa hoja Mheshimiwa Zainab Athman Katimba kwa kuileta hoja hii kwa umahiri mkubwa sana ambao umeashiria kwamba Mheshimiwa Rais kazi kubwa anayoifanya na watu wanaompongeza pia ni mahiri kama yeye, kwa hiyo nakupongeza sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mmezungumza mambo mengi nami naafikiana nanyi, watu watakuwa wamepata picha na Watanzania pia wamepata picha kwamba pamoja na changamoto tunazozizungumza huku za kwenye maeneo

yao kwamba zitaendelea kufanyiwa kazi lakini juhudi mbalimbali zinazoendelea kufanywa ni muhimu sana kama Taifa kuzitambua. Kama duniani hapa tupo watu karibia Bilioni 7.9, katika Bilioni 7.9 wapo watu 100 tu mashuhuri, katika hao 100 wamegawanywa makundi, Mheshimiwa Rais ni kati ya kundi la viongozi, hao viongozi wa dunia nzima wapo 23 tu waliotambuliwa mwaka huu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Suluhu Hassan Rais wetu tunampongeza sana, kwa sababu kuingia kwenye hiyo orodha ya watu 100, na kuingia kwenye hiyo orodha ya viongozi 23 siyo jambo dogo, kwa sababu viongozi wapo wengi sana. Nanyi Wabunge pia wananchi wanaweza kutazama waone viongozi waliopo kwenye hiyo orodha hao viongozi 23, halafu wamtazame pia Rais wetu kwamba katika hao 23 na yeye yumo ni jambo kubwa sana kwa nchi yetu, lazima tujue kwamba kazi nzuri anayoifanya hapa nchini wameitambua huko nje na bila shaka Watanzania tutaongoza katika kutambua hizo juhudi anazozifanya kwenye maeneo yote. *(Makofi/Vigelegele)*

Hapa wamezungumza baadhi ya Wabunge kwamba Bunge hili linao Wabunge wa Chama cha Mapinduzi na Wabunge wa Vyama vya Upinzani lakini kwenye hili tumeungana sote kwasababu ya Rais namna anavyofanya kazi nzuri. Kwa hiyo, niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge na tutaendelea kufanya hivi kwa kweli kutambua juhudi zake kwa sababu na yeye malaika ni mwanadamu, tukionyesha namna ambavyo tunatambua juhudi zake bila shaka atatia bidii zaidi na hivyo changamoto za wananchi wale tunaowawakilisha hapa zitafanyiwa kazi kwa upesi na kwa wepesi. Kwa hiyo, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi hiyo. *(Makofi)*

Waheshmiwa Wabunge, nilikuwa nimetoa maelezo ya jumla kuhusu matangazo ya wageni lakini wao wenyewe wageni wakija hapa wanaweza kuwa hawakusikia vizuri ama hawajamuelewa hivi Spika hajajua kama sisi tumo humu ndani. Wageni wetu msiwe na wasiwasi nimetoa maelezo

lakini nirejee tena Waheshimiwa Wabunge wanavyowaalika hapa ni kwa sababu wanawaheshimu sana ninyi wote, lakini tunajaribu kupunguza muda wa kuwatangaza ninyi, ili kwanza mnakuja wengi na Wabunge humu ndani tupo wengi kwa hiyo wote wanaleta wageni hapa na tunataka tutumie muda mrefu zaidi kwenye hoja ambazo mmewatuma Wabunge wenu kuja kuwawakilisha hapa ndani.

Kwa hivyo, nia ni njema lakini kipekee kabisa kwa sababu yupo Kiongozi wa Chama cha Mapinduzi kutoka Wilaya ya Bagamoyo na Chalinze karibu sana sana. Huyu ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Wilaya kwa hivyo, ameuongoza ujumbe wote wa kutoka huko pia ndugu zangu kutoka Ilemela naamini hili pia wamelielewa na wanatamani sana wamsikilize Mheshimiwa Waziri hapa akisoma hotuba kwa umahiri mkubwa sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kipekee nimtambulishe Mke wa Mhehimiwa Ridhiwan Kikwete Arafa Mohamed Kikwete. Karibu Sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema kwa sababu ili mtu azungumze humu ndani lazima awe ameitwa sasa ukisema hoyoo unataka na wenzio waitike hoyoo! jambo ambalo mtakuwa mnazikosea kanuni kwa sababu nitakuwa sijawaita kwamba wakujibu, kwa hiyo, hilo nalo Mheshimiwa Agnes.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninamuita sasa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula ili aje awasilishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kusoma hutuba yangu, naomba hotuba yote ichukuliwe kwenye *Hansard* kwa sababu ni ndefu yawezekana nisiyaguse yote.

Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo asubuhi ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu Na. 48) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu Na. 03), naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu sasa lipokee na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara (Fungu Na. 48) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) kwa mwaka 2021/2022. Aidha, naomba Bunge lako tukufu lijadili na kupitisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara (Fungu Na. 48) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (FunguNa. 03) kwa mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, napenda nitumie fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki wa Bunge la Kumi na Mbili, Mkutano wa Saba wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, kwa heshima na taadhima naomba

kutumia fursa hii kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa, kipekee kabisa kumshukuru sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Ninamuahidi kuwa nitatekeleza majukumu yangu kwa juhudi, maarifa, uaminifu na weledi mkubwa kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, nitumie fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu na Mbunge wa Ruangwa kwa uongozi wao mahiri. Aidha, nawashukuru kwa miongozo, maelekezo na ushirikiano wao unaoniwezesha kutekeleza majukumu ya kuongoza sekta hii vema.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ushindi mkubwa wa kishindo mlioupata umetokana na uzoefu mkubwa mlionao katika kusimamia shughuli za Bunge hivyo kukidhi matarajio ya Wabunge waliowachagua hongereni sana. Vilevile, nachukua fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Najma Murtaza Giga na Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile Mbunge, kwa kuchaguliwa na kendelea kuwa Wenyeviti wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunawaombea Mwenyezi Mungu awajalie afya njema na hekima katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, natoa pole kwako na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako tukufu kwa kuondokewa na

wapendwa wetu Mheshimiwa Elias Kwandikwa aliyekuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Mbunge wa Jimbo la Ushetu, Mheshimiwa William Tate Olenasha aliyekuwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji) na Mbunge wa Ngorongoro, Mheshimiwa Khatibu Said Haji aliyekuwa Mbunge wa Konde Zanzibar na Mheshimiwa Irene Alex Ndyamkama aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum. Aidha, napenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu kwa kuondokewa na wapendwa wao. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza pia Mheshimiwa Ally Juma Makoa Mbunge, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii na Mheshimiwa Shabani Omary Shekilindi kuwa Makamu Mwenyekiti, Wabunge wote Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, tunaahidi kuwapa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yenu ya usimamizi wa Sekta hii kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dkt. Allan H. Kijazi kuwa Katibu Mkuu na Ndugu Nicholas M. Mkapa kwa kuteuliwa na kuendelea kuwa Naibu Katibu Mkuu. Vilevile, nawapongeza Mawaziri wote, Naibu Mawaziri na Viongozi wengine walioteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali katika Serikali ya Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, nitumie fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Emmanuel Shangai kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Ngorongoro, Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Ushetu, Mohammed Said Issa Kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Konde na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania. Nawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yenu na ninaahidi kuwapa ushirikiano hususan kwa masuala yanayohusu sekta ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa dhamira na juhudi zake za kuendeleza Sekta ya Ardhi nchini. Katika kipindi chake cha mwaka mmoja toka ameingia madarakani ameiwezesha sekta ya ardhi kupata Shilingi Bilioni 345 kutoka Benki ya Dunia na Shilingi Bilioni 68.4 fedha za ndani kwa ajili ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi, kuimarisha utunzaji wa taarifa za ardhi, kuandaa taarifa za ramani kidigitali kwa ajili ya mfumo wa anuani za makazi na kuboresha miundombinu ya upimaji na ramani, tunasema ahsante sana kwa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, aidha nawapongeza kwa dhati Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa Hotuba yake ya Bajeti ambayo imetoa utekelezaji wa malengo ya Serikali katika mwaka 2021/2022 na mwelekeo wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2022/2023. Wizara inaahidi kutekeleza maelekezo yote aliyoyatoa hususani yanayohusu Wizara Ardhi.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa ushirikiano na ushauri ambao umetuwezesha kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, uchambuzi wao makini na ushauri walioutoa wakati tukipitia taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Wizara kwa mwaka 2021/2022 pamoja na Makadirio na Matumizi ya Wizara (Fungu Na. 48) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu Na. 03) kwa mwaka 2022/2023. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara itaendelea kuzingatia maoni, ushauri na maelekezo ya

Kamati ili kuboresha utendaji na hivyo kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma za sekta ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kwa dhati kabisa kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Ilemela kwa kuendelea kuniamini na kuwa Mwakilishi wao ninaishukuru familia yangu, viongozi wa dini kwa sala na dua za ambazo zimekuwa zikinipa nguvu ya kutenda kazi zangu nikiwa na hofu ya Mungu. Pamoja na shukrani hizo, kipekee namshukuru mtangulizi wangu Mheshimiwa William Lukuvi kwa kuwa Mwalimu mwema, amechangia kwa kiasi kikubwa katika kazi yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo ya utangulizi, naomba sasa nieleze kwa ufupi utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2021/2022 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na malengo ya mwaka 2022/2023 yanapatikana kuanzia aya 13 mpaka aya ya 16 kwenye kitabu. Katika mwaka 2021/2022, Wizara iliidhinishiwa jumla ya Shilingi bilioni 97.5. kati ya fedha hizo shilingi bilioni 33.9 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, shilingi bilioni 34.0 kwa ajili ya mishahara ya Wizara na shilingi bilioni 29.5 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika fedha za miradi ya maendeleo shilingi bilioni 18.3 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 11.3 ni fedha za nje. Aidha, kwa mwaka 2021/2022 Wizara iliongezewa bajeti ya shilingi bilioni 18.5 ambapo shilingi bilioni moja ilikuwa ni kwa ajili ya kulipa madeni ya watumishi na watoa huduma na shilingi bilioni 17.5 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Ongezeko hilo limefanya bajeti ya Wizara kufikia shilingi bilioni 116.1. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuweza kutoa pesa hiyo na kulipa madeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2022, Wizara ilipokea jumla ya shilingi bilioni 71.6 kati ya bajeti ya shilingi 116.1 sawa na asilimia 62 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa, shilingi bilioni 27.6 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo *(OC)* ya Wizara na Taasisi sawa na asilimia 77 ya bajeti. Shilingi bilioni 30 ni mishahara ya Wizara na Taasisi, sawa na asilimia 91 ya bajeti na Shilingi Bilioni 14 ni fedha za ndani, sawa na asilimia 30 ya bajeti ya yote ya Miradi ya Maendeleo ambayo pia ni asilimia 39 ya fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilipokea Shilingi Bilioni 54.8 fedha za ndani kupitia akaunti ya Amana ikiwa ni nyongeza ya bajeti katika Fungu 48. Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni 50 ni kwa ajili ya kuwezesha zoezi la kupanga, kupima na kumilikisha ardhi na shilingi bilioni 4.8 ni kwa ajili ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Wizara katika Mji wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022, Wizara ilipanga kukusanya shilingi bilioni 221 kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato yanayotokana na sekta ya ardhi. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2022, Wizara imefanikiwa kukusanya shilingi bilioni 115 sawa na asilimia 52 ya lengo. Miongoni mwa sababu za kutofikia malengo ni uwepo wa Taasisi na Mashirika ya Umma yapatayo 114 kuwa na malimbikizo makubwa ya kodi ambayo yanafikia shilingi bilioni 78 ni sawa na asilimia 35 ya bajeti yote.

Mheshimiwa Spika, ninatoa rai kwa mashirika haya waweze kutimiza wajibu wao na kuwezesha Serikali kufanya kazi yake. Aidha, wananchi wenye vipande vya ardhi waliopewa ankara kutolipa gharama za umilikishaji na wadaiwa kodi wa pango la ardhi kutolipa kwa wakati. Wizara inaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kulipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati. Kumekuwepo na makubaliano na Taasisi za Serikali ya kulipa kwa awamu madeni husika, kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wadaiwa

sugu, na kuweka mifumo rafiki ya kielekitroniki ya ukadiriaji na ulipaji ili kuongeza ufanisi. Utekelezaji wa mikakati hii unalenga kuongeza kasi ya makusanyo ili kufikia lengo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2022/2023, Wizara imeweka lengo la kukusanya shilingi bilioni 250.1, lengo hili litafikiwa kwa kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kuhuisha na kutunza kumbukumbu za wamiliki wa ardhi katika mfumo wa kielektroniki ili kurahisisha utumaji wa Ankara. Nyingine kuimarisha miundombinu ya TEHAMA, kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kumi kukusanya maduhuli, kutoa elimu ya mlipa kodi, kuandaa na kuhuisha viwango vya ukadiriaji kodi, kuhamasisha halmashauri na sekta binafsi kupima maeneo mapya ili kuongeza wigo wa makusanyo.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Wizara imeboresha utoaji wa ankara za malipo ya kodi ya pango la ardhi kwa wateja ambapo mteja anaweza kukadiria kodi ya ardhi kupitia tovuti ya Wizara *www.landrent.lands.go.tz* na kulipa kwa awamu. Nichukue fura hii kuwakumbusha wamiliki wote wa ardhi kulipa kodi ya pango la ardhi ili kuepuka kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara iliahidi kuendelea kuimarisha ofisi za ardhi za mikoa. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa hadi kufikia Mei 15 2022, ofisi za ardhi za mikoa ambapo mikoa yote 26 zimeimairishwa na zina wataalam wa kada zote, yaani mipangomiji, upimaji na ramani, uthamini, utawala wa ardhi na usajili. Aidha, Wizara imezipatia ofisi zote za mikoa vitendea kazi muhimu na kutoa mafunzo kwa watumishi pamoja rasilimali fedha na kuweka mifumo ya TEHAMA.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara kupitia Mradi wa Uboreshaji wa Milki za Ardhi imepanga kujenga ofisi za ardhi katika mikoa 25 ambazo hazina ofisi zitakazokidhi utoaji huduma kwa Mfumo Unganishi

wa Kuhifadhi Taarifa za Ardhi. Aidha, huduma zote za sekta zitakuwa zikitolewa katika majengo hayo ikiwemo huduma za mabaraza ya ardhi na nyumba.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara imepanga kutoa vyeti vya ardhi vya kijiji 100, hatimiliki za kimila 520,000, hatimiliki 500,000 na hati za sehemu ya jengo 1,000. Vilevile Wizara imepanga kusajili miamala ya hatimiliki na nyaraka za kisheria 100,000. Ili kuhakikisha kuwa malengo haya yanafikiwa, Wizara itatekeleza Mradi wa Uboreshaji Miliki za Ardhi na itaongeza kasi ya utekelezaji wa Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha, kuboresha miundombinu ya upimaji, na kuongeza kasi ya uandaaji wa matumizi ya ardhi. Pia kushirikisha wadau mbalimbali katika sekta binafsi, mathalan *UN-Women, LTA-NGO*, Ofisi ya Rais kupitia MKURABITA na kuzihimiza halmashauri kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya sekta ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, nitoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge ambao ni wajumbe wa Mabaraza ya Madiwani kuhakikisha kuwa halmashauri zetu zinatenga fedha katika bajeti zao kwa ajili ya kutekeleza shughuli za sekta ya ardhi kwa mujibu wa matakwa ya Sheria Na. 8 ya Mipango Miji ya mwaka 2007 kama Mamlaka za Upangaji. Takwa hili la kisheria mamlaka nyingi za halmashauri zetu zimekuwa hazitekelezi. Rai yangu ni kwetu kama Wabunge kuendelea kuwakumbusha tunapokuwa hasa katika vikao vyetu vya mabaraza ya Madiwani.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na utatuzi wa migogoro ya ardhi kiutawala; kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Wizara ilipanga kutatua migogoro 1,000 ya kiutawala. Hadi kufikia Mei 15, 2022 migogoro 1,635 imetatuliwa kati ya 1,898 iliyopokelewa. Wizara inaendelea na utaratibu wa kutatua na kudhibiti migogoro ya ardhi kwa kutumia njia mbalimbali na kuhusisha wizara za kisekta na wadau wa sekta ya ardhi. Njia hizo ni pamoja na kutoa elimu kwa umma kwa kushirikiana na

wadau mbalimbali, kuongeza kasi ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi, kubadilisha nyaraka za upangaji, upimaji na uimarishaji ardhi kutoka analojia kwenda dijitali kama mpango wa muda katika kupunguza migogoro.

Mheshimiwa Spika, mpango huu wa kuingia katika kidijitali na kutoka kwenye analojia utatuondolea pia changamoto ambayo imekuwepo kubwa ya kuwa na *double allocation,* lakini pia kutokuwa na nyaraka sahihi au watu kutokuwa na kumbukumbu sahihi. Tuna imani hili tatizo hilo litakuwa limepatiwa ufumbuzi. Aidha, madawati ya kushughulikia malalamiko katika ofisi za mikoa ambapo tumeanzisha pia rejista za migogoro ya ardhi kwa kila ofisi ya mkoa na halmashauri. Rejista hizi zinaonesha aina na hali ya mgogoro pamoja na namna unavyoshughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, tumelazimika kufanya hivyo kwa sababu migogoro mingi inakuwa inajirudia na hasa anapokuwepo kiongozi mgeni basi mgogoro unaibuka kama vile hujawahi kutatuliwa. Kwa hiyo rejista hizi zitaturahisishia kuweka kumbukumbu ili kusiwepo na kujirudiarudia kwa hoja ambazo zinakuwa zimeshapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975; napenda kutumia fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuelekeza na kuridhia vijiji 920 kati ya vijiji 975 kurasimishwa. Jambo hili ni jambo ambalo Mheshimiwa amelifanya kwa imani kubwa ya kuondoa migogoro katika watu ambao wamekuwepo katika maeneo hayo kwa muda mrefu. Kamati ya mawaziri nane wa kisekta inashiriki katika zoezi la kuelekeza uongozi wa mikoa kutekeleza zoezi hili ambalo ni maagizo ya Baraza la Mawaziri kwa njia shirikishi na kuendelea kufanya tathmini katika vijiji 55 vilivyobaki ili kumaliza migogoro.

Mheshimiwa Spika, viongozi mbalimbali katika ngazi ya mkoa, wilaya na taasisi wamekuwa wakishirikishwa, ikiwa ni pamoja na viongozi wa Chama Tawala kwa ngazi ya mkoa na wilaya pamoja na ngazi ya kitaifa ambayo ndiyo ilikuwa ya kwanza kushirikishwa kabla ya kushuka mikoani. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, Kamati ya Mawaziri Nane wa kisekta imekuwa na vikao katika mikoa 13, ambayo ni, Mkoa wa Pwani, Morogoro, Tanga, Manyara, Mara, Mbeya, Geita, Arusha, Tbora, Dodoma, Singida, Kilimanjaro na Kigoma. Aidha, Kamati ya Mawaziri itaendelea kutekeleza uamuzi wa Serikali katika mikoa iliyobaki. Ninawasihi sana wananchi wote kuwa na Imani na Serikali yao katika utekelezaji wa zoezi hili. Ninatoa tahadhari kwa wale ambao wamekuwa wakieneza taarifa zisizo sahihi na kusababisha taharuki kwa wanachi kuacha tabia hiyo mara moja. Serikali haitasita kuchukua hatua kwa wale wanaokwenda kudanganya wananchi na kuleta taharuki kwa maamuzi ambayo yamefikiwa na baraza na ambaya yanakwenda kutatua tatizo la migogoro katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uthamini na fidia; katika mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara iliahidi kuendelea kushughulikia malalamiko 100 ya uthamini wa fidia, kufanya uhakiki wa uthamini wa fidia katika maeneo 20, kuendelea kufanya utafiti na kuandaa viwango vya thamani ya ardhi katika mikoa yote 26 nchini. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, jumla ya malalamiko 51 ya uthamini wa fidia yamepokelewa na kushughulikiwa. Pia uthamini wa maeneo 15 ya miradi mbalimbali umefanyiwa uhakiki ili kutatua migogoro ya fidia.

Mheshimiwa Spika, Wizara imekuwa ikipokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi yanayohusiana na ucheleweshwaji wa kulipwa pungufu au kutolipwa fidia. Nasisitiza, taasisi za Serikali na kampuni binafsi kulipa fidia kwa wakati ili kuepuka ulipaji wa riba na malalamiko yanayotokana na ucheleweshaji wa ulipaji fidia. Kamwe Serikali haitaruhusu utwaaji wa ardhi bila kulipa fidia. Kwa

maana hiyo taasisi yoyote inayotaka kutoa ardhi iwe na uhakika imetenga fungu kwa ajili ya kulipa fidia, na wanapotwaa wanalipa fidia hiyo mara moja.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ardhi kwa mwaka 2021/2022 upande wa mabaraza ya ardhi na nyumba iliahidi kuongeza idadi ya mabaraza yanayotoa huduma, ambapo hadi kufikia tarehe 15 mabaraza mapya 20 yameanza kutoa huduma na hivyo kuwa na jumla ya mabaraza 80 yanayotoa huduma kati ya mabaraza 139 yaliyoanzishwa. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara inatarajia kuwezesha mabaraza mapya 59 kuanza kutoa huduma na hivyo kuwa na mabaraza yanayotoa huduma katika wilaya zote nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ifikapo Juni, 2022 Wizara itakamilisha ujenzi wa Mfumo wa Kusimika Mashauri katika Baraza la Ardhi na Nyumba ya Wilaya *(Integrated Land Cases Management System)* ambao utaanza kutumika katika mwaka wa fedha 2022/2023. Mfumo huo utarahisisha kiutendaji katika mabaraza ya ardhi na nyumba ya wilaya katika kutunza kumbukumbu za mashauri, kufungua mashauri mapya, kufuatilia utendaji kazi wa watumishi wa mabaraza na upatikanaji wa nakala za hukumu kwa wakati kwa njia ya mtandao. Hii itaondoa pia usumbufu wa wananchi pengine kulazimika kwenda kwenye baraza, bado anaweza aka-*file* kesi yake akiwa nyumbani na akafuatilia akiwa nyumbani.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto ya wazee wa mabaraza wanapomaliza muda wao huchukua muda mrefu kupatikana wengine. Nitoe rai kwenye mamlaka za mikoa na wilaya kuanza mchakato wa kupata wazee wa mabaraza wapya miezi sita kabla ya waliopo kumaliza muda wao ili kuepuka usumbufu kwa wateja kwa kuahirishwa mashauri yao mara kwa mara kwa kukosa wazee kwa kisingizo cha muda wao wa kuhudumu kuwa umekwisha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara pia iliahidi kufanya marekebisho ya Sheria za Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Na. 2 ya mwaka 2002 yanayoendelea kubadili mfumo wa ajira za wenyeviti wa mabaraza na kufanya mabaraza ya kata kufanya usuluhisho wa migogoro ya ardhi badala ya kutoa hukumu. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imefanya marekebisho katika sheria hiyo na kurekebisha mfumo wa ajira kwa wenyeviti wa mabaraza badala kutoka ajira ya miaka mitatu na kuwa na ajira ya kudumu.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa ajira za kudumu kwa wenyeviti wa mabaraza utaiwezesha Wizara kupata wenyeviti kutoka miongoni mwa wanasheria wenye sifa waliopo katika utumishi wa umma na kuwezesha usimamizi wa maadili ya wenyeviti wa mabaraza kwa kutumia sheria na kanuni za utumishi wa umma. Aidha, kupitia marekebisho haya mabaraza ya kata yameondolewa mamlaka ya kufanya maamuzi na yamebaki na mamlaka ya usuluhishi pekee katika mashauri yanayohusu migogoro ya ardhi. Wote tunatambua mabaraza ya kata yamekuwa ni chanzo pia cha kuendeleza migogoro ya ardhi kwa kufanya kazi za kuhukumu badala ya kuwa washauri. Hatua inayofuata ni kuandaa kanuni zitakazobainisha utaratibu wa usuluhishi katika mabaraza hayo ya kata.

Mheshimiwa Spika, sekta ya TEHAMA inapatikana aya ya 42 mpaka 49. TEHAMA ni nyenzo muhimu katika kuboresha huduma katika sekta ya ardhi. Katika kufanikisha azma ya matumizi ya TEHAMA, Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi (*Integrated Land Management Information System – ILMIS*) umeendelea kuboreshwa na kusambazwa kwa kutumia watalaam wa ndani.

Mheshimiwa Spika, vilevile, mfumo huo umeboreshwa kwa kuongeza moduli mbalimbali ikiwemo Moduli ya kiganjani *(ILMIS Mobile App.)* ambayo imewezesha uchukuaji

wa taarifa za upimaji moja kwa moja kutoka uwandani na kuzingizwa katika mfumo. Hatua hii imerahisisha ukusanyaji na uchakataji wa taarifa za utambuzi wa vipande vya ardhi kwa ajili ya utoaji wa leseni za makazi na hatimiliki za Kimila. Hadi kufikia tarehe 15 Mei jumla ya leseni 18,063 na hati za Hakimiliki za Kimila 6,861 zimetolewa kupitia mfumo katika Mikoa ya Mwanza, Arusha, Mbeya, Rukwa na Singida.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara iliahidi kuanza kutumia mfumo wa *ILMIS* kwa kutoa hati za kieletroniki katika Mkoa wa Dodoma na kuendelea kujenga na kusimika miundombinu wezeshi ya *TEHAMA* kwa awamu katika ofisi za ardhi za mikoa yote nchini. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi kupikia Mei 15, 2022, Hatimiliki za Kielektroniki 6,138 zimetolewa kupitia mfumo wa *ILMIS* katika Jiji la Dodoma na ujenzi wa miamala ya upili unaendelea. Aidha Wizara imeanza kujenga mtandao kiambo *(Local Area Network)* katika Ofisi za Ardhi za Mikoa ya Iringa, Lindi, Mwanza na Mbeya ambapo utakamilika ifikapo Juni, 2022. Mitandao hiyo itakapokamilika itaunganishwa na Kituo cha Taifa cha Ardhi.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara itaendelea kujenga miundombinu wezeshi ya *TEHAMA* kwa awamu katika ofisi za ardhi za mikoa na halmashauri nchini. Vilevile, ukarabati wa mtandao kiambo katika Ofisi za Halmashauri 47 zikiwemo Makao Makuu ya Mikoa ya Iringa, Lindi, Mwanza na Mbeya utafanyika.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa kutumia mifumo ya *TEHAMA*, Wizara imeendelea kuchambua, kufanya nakishi ya michoro *(scanning)* na kuhifadhi ramani za kumbukumbu za ardhi katika ofisi za ardhi za mikoa na halmashauri mbalimbali nchini kwa awamu. Katika kutekeleza azma hiyo, jumla ya michoro ya mipangomiji 25,744 yenye viwanja 7,013,474, ramani za upimaji 89,512 zenye viwanja 2,842,494, nyaraka za

umiliki 2,388,705 na makadirio ya vipande vya ardhi 1,000,000 katika maeneo ambayo hayajapangwa na kupimwa mijini. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, ubadilishaji wa michoro ya mipangomiji 5,649 yenye viwanja 1,758,424 na ramani za upimaji 31,500 zenye viwanja 598,000 katika halmashauri 38 umefanyika kutoka analojia kwenda digitali. Aidha, utambuzi wa vipande vya ardhi 52,648 katika Halmashauri za Jiji la Dodoma na Manispaa za Tabora, Shinyanga na Ilemela umekamilika.

Mheshimiwa Spika, zoezi la ubadilishaji wa michoro ya mipangomiji, ramani za upimaji na nyaraka za umiliki litakuwa na manufaa makubwa kwa wananchi, wawekezaji wa ndani na nje ya nchi na Taifa kwa ujumla kama ifuatavyo: -

(i) Kuwezesha uandaaji wa anwani za makazi na Sensa ya Watu na Makazi;

(ii) Kuwezesha Wizara kuunganishwa na mifumo mingine ya Serikali katika kubadilishana taarifa mathalan, mifumo wa *ILMIS* na *NaPA*;

(iii) Kuwezesha utunzaji wa kumbukumbu za ardhi kidigitali pamoja na utoaji wa Hatimiliki kwa njia ya kielektroniki;

(iv) Kurahisisha usimamizi, utoaji wa huduma na kufanya maamuzi;

(v) Kupunguza udanganyifu na kughushiwa kwa nyaraka mbalimbali za ardhi na hivyo kupunguza migogoro; na

(vi) Kurahisisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali ikiwemo utoaji wa ankara za kidigitali.

Mheshimwia Spika, upimaji na ramani vinapatikana aya ya 50 mpaka aya ya 55. Wizara ina jukumu la kusimamia na kuratibu upimaji wa ardhi nchini, upimaji wa mipaka kimataifa, kutafsiri matangazo ya Serikali ardhini kuhusu mipaka ya kiutawala pamoja na utayarishaji wa ramani za msingi kwa ajili ya shughuli mbalimbali. Aidha, Wizara ina wajibu wa kutoa miongozo ya upimaji ardhi na uandaaji wa ramani kwa taasisi mbalimbali za Serikali na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuweka miundombinu ya upimaji wa ardhi ikiwemo alama za msingi za upimaji ambazo zitarahisisha kazi, kupunguza muda na gharama ya upimaji katika kupima ardhi. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara iliahidi kusimika alama mpya za msingi 80 katika maeneo mbalimbali nchini. Hadi kufikia tarehe 15 Mei alama za msingi za upimaji 68 zilisimikwa katika Mikoa ya Dar es Salaam tano, Arusha nane, Dodoma 11, Mara saba, Njombe nane, Simiyu tatu, Kigoma nane, Manyara tano, Tanga tano, Geita nane na hivyo kuwa na alama za upimaji 939 nchini. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara itasimika alama mpya 80.

Mheshimiwa Spika, picha za anga ni nyenzo muhimu katika uandaaji wa ramani za msingi. Kwa mara ya mwisho picha za anga zilipigwa mwaka 1970. Kukosekana kwa picha za anga kulisababisha kutohuishwa na ramani za msingi zinazoonyesha hali halisi ardhini na hivyo kuathiri upangaji wa miji na uwekaji wa miundombinu.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara iliahidi kununua ndege ndogo isiyotumia rubani (drone) kwa ajili ya kupiga picha za anga zitakazowezesha uandaaji wa ramani za msingi. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba, Wizara tayari imenunua ndege kwa gharama ya shilingi milioni 189 kwa ajili ya kupiga picha za anga. Picha zilizoanishwa zinawezesha kuandaa ramani za msingi ambazo zinatumiwa katika Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Taarifa.

Ndege hii inawezesha upatikanaji wa taarifa zilizopo ardhini pindi zinapohitajika na picha hizo zina ubora kuliko taarifa zinavyoweza kupatikana. Picha hizi pia zitasaidia katika suala la fidia kwa kupiga picha mapema kabla ya kuchukua fidia kuepuka wale wanaotegesha kwa ajili ya kuiibia Serikali. Ndege hii imetumika kupiga picha katika eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 100 katika Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha ardhi katika Jiji la Dodoma. Aidha, Wataalam wawili wamehitimu mafunzo ya kurusha ndege za aina hiyo na kupata leseni kutoka Mamlaka ya Usalama wa Anga.

Mheshimiwa Spika, katika upimaji wa ardhi kwa nchi kavu, Wizara ina jukumu la kuratibu na kusimamia upimaji wa viwanja na mashamba unaofanywa na Mamlaka za Upangaji pamoja na sekta binafsi. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ilipanga na kuidhinisha ramani za upimaji wa viwanja na mashamba 500,000 pamoja na kutatua migogoro 25 ya mipaka ya vijiji, hifadhi na Wilaya. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, viwanja 298,232 na mashamba 356 vimeidhinishwa na kutunzwa kwenye kanzidata ya Wizara, Jedwali Na. 8 kwenye kitabu linaonesha.

Mheshimiwa Spika, vilevile, migogoro ya mipaka ya vijiji vinane katika Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze inaendelea kushughulikiwa na migogoro ya mipaka miwili katika Halmashauri za Wilaya za Nyang'hwale moja, na Nkasi moja, imetatuliwa. Aidha, migogoro ya Hifadhi za Msitu wa Kalambo na Kijiji cha Kasapa katika Wilaya ya Nkasi imeshughulikiwa. Pia mipaka ya maeneo ya kupumzishia mifugo ya Mkwese, Manyoni na Kinyangiri, Mkalama imehakikiwa.

Mheshimiwa Spika, zoezi la upangaji Miji na Maendeleo ya Miji linapatikana katika aya 56 - 76. Katika kulinda maeneo yanayochipukia kuwa miji, Wizara imeandaa mwongozo wa kusimamia uandaaji wa mipango ya uendelezaji wa makazi na ujenzi wa nyumba vijijini ambao unaelekeza namna ya

kupanga makazi vijijini kwa kuzingatia vigezo vilivyoainishwa. Ili kuwahakikishia utekelezaji wa mwongozo huo, Wizara imeandaa mafunzo kwa wananchi kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa upangaji na usimamizi wa miji midogo katika maeneo ya vijiji.

Mheshimiwa Spika, naelekeza Mamlaka za Upangaji kuendelea kutambua na kuwasilisha mapendekezo ya vijiji na miji inayokua katika kukidhi vigezo vya kutangazwa kuwa maeneo ya upangaji ili yaweze kuendelezwa kimiji; na tayari katika majedwali la 9(a) na 9(b) imeonesha maeneo ambayo yamepokelewa kwa ajili ya kutangazwa yapo 117 na maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya urasimishaji, yapo 190 katika Halmashauri 20 kwenye mikoa minane na mikoa minane kwenye upangaji pia.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara iliahidi kuendelea kuboresha taarifa za nyumba katika kanzidata ikiwa ni pamoja na kuhamasisha uundwaji wa vyama vya ushirika vya nyumba. Hadi kufikia Mei 15, 2022, taarifa za waendelezaji na wasimamizi milki 207 ambao wamejenga jumla ya nyumba 25,239 zimeingizwa katika kanzidata za nyumba.

Mheshimiwa Spika, aidha, Vyama vya Ushirika vya Nyumba 38 vyenye wanachama 2,247 ambavyo vimejenga jumla ya nyumba 1,056 katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Kagera, Musoma, Morogoro, Mwanza na Shinyanga vimeingizwa katika kanzidata. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Vyama vya Ushirika itaendelea kuhamasisha ujenzi wa nyumba kupitia vyama vya ushirika wa nyumba na kuvijengea mazingira ya kupata mikopo yenye masharti nafuu kutoka taasisi za fedha.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikikabiliwa na ukosefu wa takwimu sahihi za majengo nchini. Sensa ya

majengo ambayo itafanyika kwa mara ya kwanza tangu nchi ipate uhuru, itawezesha upatikanaji wa takwimu za hakika na sahihi za majengo kwa ajili ya mipango ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Upatikanaji wa takwimu sahihi na za uhakika ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya Mwaka 2000, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025. Ili kufanikisha zoezi la Sensa ya Majengo, Wizara imekamilisha maandalizi ya dodoso la majengo, mwongozo wa Wakufunzi na Makarani, Mwongozo wa Ukusanyaji taaarifa za majengo na kufanya kikao cha wadau wa sekta ya majenzi.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa sensa ya majengo na anwani za makazi, ni vyema maeneo ambayo ni hatarishi, hifadhi za miundombinu mbalimbali na maeneo yenye migogoro zoezi husika lifanyike baada ya kujiridhisha na uhalali ya maeneo hayo. Nawahimiza wamiliki wa majengo yote nchini kushiriki zoezi la sensa ya watu na makazi na kutoa taarifa sahihi za matumizi ya jengo, hali ya jengo na umiliki wake. Kwa majengo ambayo hayatumiki, ninaelekeza viongozi wa mitaa na vitongoji kuchukua taarifa za majengo hayo za wamiliki wake na kwa kuwapatia fomu maalum iliyoandaliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu Sekta ya Milki imekosa usimamizi, takwimu na taarifa sahihi, uratibu madhubuti kwa waendelezaji, taasisi za fedha, watumiaji na mawakala wa sekta. Changamoto hizi zimesababisha kutotambuliwa kwa mchango wa sekta hii katika uchumi wa nchi. Dhamira ya Serikali ni kuwa na mfumo madhubuti wa kitaasisi wa kusimamia na kuratibu uendeshaji sekta ya milki.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu huo, Wizara imeanzisha Kitengo cha milki *Real Estate Unit* ambacho kitasimamia pamoja na masuala mengine uwekaji wa mfumo wa uwazi na usawa katika biashara na huduma za kisekta ya milki nchini, ikiwemo kuhakikisha viwango vya kodi ya pango

la nyumba vinatozwa kwa mujibu wa soko na taratibu za ulipaji wa kodi hiyo haumuumizi mlaji. Kitengo hiki kitawajibika kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, kanuni na Miongozo mbalimbali kwa ajili ya kusimamia na kukuza sekta ya milki.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya Sera na Sheria yanapatikana aya ya 74 – 79. Ili kuendelea na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, maendeleo ya sayansi na teknolojia pamoja na changamoto zinazotokana na mabadiliko ya tabia nchi, katika mwaka 2021/2022 Wizara iliahidi kukamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995, kukamilisha uchambuzi wa maoni ya wadau kuhusu mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Makazi ya Mwaka 2000 na rasimu ya Sera ya Nyumba ambayo ni Sera mpya.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa mapitio ya Sera ya Taifa ya Ardhi yako katika ngazi ya maamuzi Serikalini. Aidha, marekebisho ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi na rasimu ya Sera mpya ya Taifa ya Nyumba, yako katika hatua ya ukamilishaji, uchambuzi wa maoni ya wadau kabla ya kuwasilishwa Serikalini kwa maamuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi yanayotokana na takwa la kisheria la kutoza riba baada ya miezi sita ndani ya mwaka wa fedha ambao kodi ya pango la ardhi inapaswa kulipwa. Ili kuondoa malalamiko hayo, Wizara inakusudia kufanya marekebisho ya Sheria ya Ardhi kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha ili riba ya kuchelewa kulipa kodi ya pango la ardhi ianze kutozwa baada ya kuisha kwa mwaka wa fedha badala ya inavyotozwa sasa kila baada ya miezi sita.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi unaendelea, ambapo katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara iliidhinishiwa

shilingi bilioni nane. Aidha, Wizara ilipokea shilingi bilioni 50 kwa ajili ya kukopesha Halmashauri na Taasisi kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii. Hadi kufikia 2015, kati ya fedha zilizoidhinishwa, Wizara imepokea shilingi bilioni 5.6 na hivyo kufanya kuwa na jumla ya shilingi bilioni 55.6 kwa ajili utekelezaji wa programu. Fedha hizi zimekopeshwa kwenye Halmashauri 92 nchini ambayo ipo katika mikoa 23 pamoja na Chuo cha Ardhi, Tabora.

Mheshimiwa Spika, kupitia programu hii tunatarajia kupata mapato ya shilingi bilioni 51.6. Pamoja na jitihada za Serikali za kutoa fedha kwa ajili ya kutekeleza shughuli za Sekta hii, natoa rai kwa Mamlaka za Upangaji kuhakikisha kuwa zinatenga fedha, asilimia 40 hadi 60 kwa faida ya fedha wanayoipata kutokana na mkopo huo kwa ajili ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi kwa kuzingatia Mwongozo wa Madaraja ya Halmashauri uliowekwa na Ofisi ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, kulingana na muda, nimeshasema mengine yatawekwa kwenye *Hansard* kama yalivyo, naomba niende kwenye mradi wa uimarishi mipaka Kimataifa ambapo tulikusudia kuimarisha urefu wa kilometa 100, lakini mpaka tunapoongea hivi sasa, napenda kuliarifu Bunge kuwa kilometa 83 za mpaka wa Tanzania na Kenya zimeimarishwa na kazi inaendelea; na ramani za msingi kwa kipande cha kilometa 238 kutoka Ziwa Victoria hadi Ziwa Natron zitatumika.

Mheshimiwa Spika, katika miradi ya kimkakati ya Kitaifa, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara imeendelea kushiriki kikamilifu katika kuwezesha utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati; Miradi hiyo ni Ujenzi wa Bwawa la Kuzalisha Umeme la Mwalimu Nyerere, Ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima - Uganda hadi Chongoleani – Tanga. Mradi wa Mwalimu Nyerere tumeweza kuufanya mipango kina katika vijiji vitatu yenye viwanja 2,041 na imeandaliwa katika Miji

Midogo ya Mloka na Ikwiriri. Upande wa Rufiji pia kazi hiyo imefanyika katika maeneo ya Wilaya ya Mbarali, Mufindi, Kilolo na Wangingo'mbe.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kushiriki katika utekelezaji wa mradi wa Reli ya Kisasa kutoka Morogoro hadi Makutupora kwa awamu hiyo. Usanifu wa michoro ya mipangomiji tisa; Dar es Salaam, Soga, Ruvu, Kwala, Morogoro, Kilosa, Chanzulu, Gulwe na Dodoma umekamilika. Aidha, usanifu wa michoro ya mipangomiji katika maeneo ya Dodoma; Igandu, Tura Tabora, Nkalalo Mwanza, Isaka na Ishololo, Shinyanga unaendelea. Vilevile, thamani ya uthamini wa mali tayari kwa wananchi wapato 1,462 umefanyika na shilingi bilion 34 za fidia tayari zimetolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa Bomba la Mafuta, tayari katika zoezi hilo, Wizara imeweza kukamilisha maeneo 14 ya kipaumbele ya mradi ambapo wananchi 350 wamefidiwa na jumla ya shilingi bilioni 1.6. Aidha, utwaaji ardhi ya Mkuza wa Bomba la Mafuta wenye urefu wa kilometa 1,147 umekamilika na vilevile, mipangokina 42 yenye viwanja 21,335 umefanyika. Tunafanya hivyo ili kuepuka migogoro ya ardhi katika Mkondo huo ambao ni miradi ya Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu shughuli zilizotekelezwa na Shirika la Nyumba, zinapatikana katika aya ya 96 – 106 ya kitabu kikubwa. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2022 utekelezaji wa miradi umefikia asilimia 93 na hii imetokana na Serikali kuruhusu Shirika kukopa shilingi bilioni 173.9 ili kukamisha miradi na mingine iliyokuwa imesimama tangu mwaka 2018 kwa kukosa fedha. Mpaka sasa Shirika limekopa shilingi bilioni 44.7 kati ya fedha hizo kwa ajili ya kukamilisha Miradi ya *Morocco Square* na Kiwanja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Shirika litaendelea na ujenzi wa nyumba 101 katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Jiji la Dodoma 103 na kuweza kukamilisha nyumba 1,000 kama ilivyopangwa. Napenda kuliarifu Bunge lako kuwa hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2022, ujenzi wa nyumba 100 na jengo la maduka katika Wilaya ya Chamwino umekamilika kwa asilimia 80 na ujenzi wa nyumba 300 na majengo matatu ya huduma za jamii katika Jiji la Dodoma, Iyumbu umekamilika kwa asilimia 90.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Shirika limepanga kutekeleza mambo kadhaa, ukiangalia katika kitabu chetu yameorodheshwa yote, naomba niyaruke.

Mheshimiwa Spika, kulingana na muda, naomba niruke maeneo mengine niende kwenye hitimisho. Napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika mwaka 2022/2023, Wizara itaendelea kufanya mageuzi ya kuboresha huduma zinazotolewa na sekta ya ardhi na kuendelea kuwekeza katika matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika utoaji wa huduma na pia kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi pamoja na udhibiti.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2022/2023; Wizara inatarajia kukusanya shilingi bilioni 250.1. Aidha, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi - Fungu Na. 48; na Fungu Na. 03 la Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kama inavyoonesha katika Jedwali. Jumla ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo, fedha zinazoombwa ni shilingi 105,455,777,000. Upande wa Matumizi ya Kawaida kwa Fungu Na. 03 zinaombwa shilingi 4,867,704,000. Jumla ya fedha zinazoombwa kwa Fungu Na.

48 na Fungu Na. 03 ili Bunge lako liweze kujadili na kuidhinisha ni shilingi 110,323,474,000.

Mheshimiwa Spika, naomba kuhitimisha hotuba yangu kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Pamoja na hotuba hii nimeambatisha majedwali ambayo yameainisha kwa kina takwimu pamoja na shughuli zilizotekelezwa na Wizara. Aidha, hotuba hii inapatikana kwenye tovuti ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI, MHESHIMIWA DKT. ANGELINE S.L. MABULA (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2022/23 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**UTANGULIZI**

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu **48**) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **03**), naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili taarifa za utekelezaji wa Bajeti ya Wizara (Fungu **48**) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **03**) kwa mwaka 2021/22. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara (Fungu **48**) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **03**) kwa mwaka 2022/23.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** Baada ya utangulizi huo, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki Mkutano wa Saba (**7**) wa Bunge la 12 la Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania. Aidha, kwa heshima na taadhima naomba kutumia fursa hii kipekee kumshukuru sana Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Ninamuahidi kuwa nitatekeleza majukumu yangu kwa juhudi, uaminifu na weledi mkubwa kwa maendeleo ya Taifa letu.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee, nitumie fursa hii kuwapongeza **Mhe. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango**, Makamu wa Rais; **Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na **Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa**, Waziri Mkuu na Mbunge wa Ruangwa kwa uongozi wao mahiri. Nawashukuru pia kwa miongozo, maelekezo na ushirikiano wao unaoniwezesha kutekeleza majukumu niliyokabidhiwa ya kuongoza sekta hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia uchaguzi uliofanyika katika Mkutano wa Sita (6) wa Bunge la 12, nakupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nampongeza Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb.), kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ushindi mkubwa wa kishindo mlioupata umetokana na uzoefu mkubwa mlionao katika kusimamia shughuli za Bunge hivyo kukidhi matarajio ya wabunge waliowachagua hongereni sana. Vilevile, nachukua fursa hii kuwapongeza **Mhe. Najma Murtaza Giga (Mb.)**, na **Mhe. David Mwakiposa Kihenzile (Mb.)**, kwa kuchaguliwa na kuendelea kuwa Wenyeviti wa Bunge. ***Tunawaombea Mwenyezi Mungu awajalie afya njema na hekima katika utekelezaji wa majukumu yenu.***

5. ***Mheshimiwa Spika,*** natoa pole kwako, Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na wapendwa wetu **Mhe. Elias Kwandikwa**,

aliyekuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Mbunge wa Jimbo la Ushetu; **Mhe.William Tate Olenasha** aliyekuwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji) na Mbunge wa Ngorongoro; **Mhe. Khatibu Said Haji** aliyekuwa Mbunge wa Konde Zanzibar na **Mhe. Irene Alex Ndyamkama**, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum. Aidha, napenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu kwa kuondokewa na wapendwa wao. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** Pia, ninampongeza **Mhe. Ally Juma Makoa (Mb.)**, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii na **Mhe. Shabani Omary Shekilindi (Mb.)**, kuwa Makamu Mwenyekiti. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote walioteuliwa kuwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, tunaahidi kuwapa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yenu ya usimamizi wa Sekta ya Ardhi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** nampongeza pia **Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete (Mb.)**, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, **Dkt. Allan H. Kijazi** kuwa Katibu Mkuu na **Bw. Nicholas M. Mkapa** kwa kuteuliwa na kuendelea kuwa Naibu Katibu Mkuu. Vilevile, nawapongeza Mawaziri, Naibu Mawaziri na Viongozi wengine walioteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali katika Serikali ya Awamu ya Sita. Aidha, nitumie fursa hii kuwapongeza **Mhe. Emmanuel Lekishon Shangai (Mb.)**, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Ngorongoro, **Mhe. Emmanuel Peter Chelehani** kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Ushetu, **Mohammed Said Issa** Kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Konde na **Mhe. Shamsi Vuai Nahodha (Mb.)**, kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa

majukumu yenu na ninaahidi kuwapa ushirikiano hususan kwa masuala yanayohusu Sekta ya Ardhi.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee nampongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa dhamira na juhudi zake za kuendeleza Sekta ya Ardhi nchini. Katika kipindi cha mwaka mmoja cha uongozi wake ameiwezesha Sekta ya Ardhi kupata shilingi bilioni **345** kutoka Benki ya Dunia na shilingi bilioni **68.4** fedha za ndani kwa ajili ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi; kuimarisha utunzaji wa taarifa za ardhi; kuandaa taarifa za ramani kidigitali kwa ajili ya Mfumo wa Anwani za Makazi; na kuboresha miundombinu ya upimaji na ramani.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa Hotuba yake ya Bajeti ambayo imetoa utekelezaji wa malengo ya Serikali katika mwaka 2021/22 na mwelekeo wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2022/23. Wizara inaahidi kutekeleza maelekezo yote yanayoihusu Sekta ya Ardhi.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** natoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa ushirikiano na ushauri ambao wamekuwa wakiutoa mara kwa mara katika kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, naishukuru Kamati kwa uchambuzi makini na ushauri iliyotoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2021/22 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara (Fungu **48**) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **03**) kwa mwaka 2022/23. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Wizara, itaendelea kuzingatia maoni, ushauri na maelekezo ya Kamati ili kuboresha utendaji na hivyo kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma za Sekta ya Ardhi.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** Aidha nitumie fursa hii kwa dhati kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Ilemela kwa ushirikiano wa karibu wanaonipa katika kutimiza majukumu yangu nikiwa Mbunge wao. Aidha, naishukuru familia yangu kwa kuendelea kuniunga mkono wakati ninapokuwa nikitekeleza majukumu yangu ya jimbo na ya kitaifa. Sala zenu za kila siku zimekuwa zikinipa nguvu na hamasa katika kutekeleza majukumu yangu. Niwashukuru pia viongozi wa dini kwa sala na dua zao ambazo zinanipa nguvu ya kutenda kazi zangu nikiwa na hofu ya Mungu. Vilevile, nakishukuru chama changu Chama cha Mapinduzi kwa kuniteua kugombea ubunge katika Jimbo la Ilemela, ninaahidi kutekeleza vyema Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo ya utangulizi, naomba sasa nieleze kwa ufupi utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2021/22, na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2022/23. Bajeti hii imeandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025); Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka (2020 - 2025); Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26); Sera, Sheria na Miongozo mbalimbali ya Sekta ya Ardhi; na maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Serikali.

## 1. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2021/22 NA MALENGO YA MWAKA 2022/23.

### Matumizi

13. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wizara iliidhinishiwa jumla ya Shilingi **97,548,698,000.00**. Kati ya fedha hizo, shilingi **33,918,651,000.00** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC); shilingi **34,079,748,000.00** kwa ajili ya Mishahara ya Wizara (PE); na shilingi **29,550,299,000.00** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Katika fedha za Miradi ya Maendeleo shilingi **18,300,000,000.00** ni fedha za ndani na

shilingi **11,250,299,000.00** ni fedha za nje. Aidha, katika mwaka 2021/22, Wizara iliongezewa bajeti ya shilingi **18,535,117,066.42**, ambapo shilingi **1,072,986,393.42** ilikuwa kwa ajili ya kulipa madeni ya watumishi na watoa huduma na shilingi **17,461,130,673.00** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Ongezeko hilo limefanya bajeti ya Wizara kufikia shilingi **116,082,815,066.42.**

14. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2022, Wizara ilipokea jumla ya shilingi **71,617,723,210.00** kati ya bajeti ya shilingi **116,082,815,066.42** sawa na asilimia 62 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa, shilingi **27,585,455,467.60** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) ya Wizara na Taasisi sawa na asilimia 77 ya bajeti; shilingi **30,016,307,292.60** ni Mishahara ya Wizara na Taasisi sawa na asilimia 91 ya bajeti; na shilingi **14,015,960,449.80** ni fedha za ndani sawa na asilimia 30 ya bajeti ya yote ya Miradi ya Maendeleo ambayo pia ni **asilimia 39** ya fedha za ndani **(Jedwali Na. 1).**

15. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara ilipokea shilingi bilioni **54.8** fedha za ndani kupitia akaunti ya Amana ikiwa ni nyongeza ya bajeti (Fungu **48**). Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 50 ni kwa ajili ya kuwezesha Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi na shilingi bilioni **4.8** ni kwa ajili ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Wizara katika Mji wa Serikali Mtumba.

**Ukusanyaji wa Maduhuli**

16. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wizara ilipanga kukusanya shilingi bilioni **221** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato yanayotokana na Sekta ya Ardhi. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2022, Wizara imekusanya shilingi bilioni **115** sawa na asilimia 52 ya lengo **(Jedwali Na.2)**. Miongoni mwa sababu za kutofikia malengo ni uwepo wa Taasisi na Mashirika ya umma yapatayo **114** kuwa na malimbikizo ya kodi ya shilingi bilioni **78**, wananchi wenye

vipande vya ardhi waliopewa ankara kutolipa gharama za umilikishaji na wadaiwa kodi ya pango la ardhi kutolipa kwa wakati. Wizara inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuongeza makusanyo ya mapato ikiwemo kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kulipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati; kuweka makubaliano na Taasisi za Serikali ya kulipa kwa awamu madeni husika, kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wadaiwa sugu; kusambaza hati za madai na kuweka mifumo ya kielekitroniki ili kuongeza ufanisi. Utekelezaji wa mikakati hii unalenga kuongeza kasi ya makusanyo ili kufikia lengo.




*Gari maalumu linalotumika katika kampeni ya kutoa elimu ya sekta ya ardhi mtaa kwa mtaa katika Jiji la Dodoma.*

17. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2022/23, Wizara imeweka lengo la kukusanya shilingi bilioni **250.1**. Lengo hili litafikiwa kwa kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kuhuisha na kutunza kumbukumbu za wamiliki wa ardhi katika mfumo wa kielektroniki ili kurahisisha utumaji wa ankara; kuimarisha miundombinu ya TEHAMA; kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kukusanya maduhuli; kutoa elimu ya mlipa kodi; kuandaa na kuhuisha viwango vya ukadiriaji kodi; na kuhamasisha Halmashauri na Sekta binafsi kupima maeneo mapya ili kuongeza wigo wa makusanyo. ***Nawakumbusha wamiliki wa ardhi kulipa kodi ya pango la ardhi ili kuepuka kuchukuliwa hatua za kisheria.***

## 2. UTAWALA WA ARDHI

18. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi zinazolenga kuimarisha usalama wa milki na kuendelea kuifanya ardhi kuwa moja ya nguzo kuu ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Katika kutoa huduma, Wizara inaongozwa na Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha kuwa huduma zinatolewa kwa misingi ya haki na usawa. Katika kufanikisha azma hiyo, Wizara imeendelea kutoa huduma kwa wananchi katika ngazi za Mikoa na Halmashauri zote nchini.

19. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wizara iliahidi kuendelea kuimarisha Ofisi za Ardhi za Mikoa ikiwemo kuwapanga watalaam wa Sekta ya Ardhi kwa uwiano mzuri ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi tarehe 15 Mei, 2022, Wizara imeendelea kuhuisha taarifa za mahitaji ya watumishi wa kada za ardhi katika Ofisi za Ardhi za Mikoa ambapo mikoa yote 26 ina wataalam wa kada za Mipangomiji, Upimaji na Ramani, Uthamini, Utawala wa Ardhi na Usajili. Kada hizi ni muhimu katika utoaji wa huduma za Sekta ya Ardhi. Aidha, Wizara imeendelea kuboresha utendaji kazi wa ofisi zake kwa kuzipatia vitendea kazi muhimu, kutoa mafunzo kwa watumishi, rasilimali fedha pamoja na kuweka mifumo ya TEHAMA.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Wizara itaendelea kuboresha utoaji wa huduma za Sekta ya Ardhi kwa wananchi kwa kuziwezesha Ofisi za Ardhi za Mikoa na Halmashauri kwa kuzipatia vitendea kazi, rasilimali fedha pamoja na kusimamia maadili ya watumishi. Aidha, Wizara itaendelea kuwapanga wataalam wa Sekta ya Ardhi kwa uwiano katika Halmashauri ili kuhakikisha utoaji wa huduma za ardhi unaimarika zaidi. Vilevile, kupitia Mradi wa Uboreshaji wa Milki za Ardhi (LTIP), Wizara imepanga kujenga Ofisi za Ardhi katika Mikoa **25** zitakazokidhi utoaji huduma kwa

Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Taarifa za Ardhi (ILMIS). Pia, huduma zote za sekta zitakuwa zikitolewa katika majengo hayo zikiwemo huduma za Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya.



*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Dkt. Angeline Mabula, akizungumza na wananchi wa Nyafula katika Manispaa Ilemela mkoani Mwanza wakati kamati ya kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii tarehe 17 Machi 2022.*

**Uandaaji wa Hati na Usajili wa Nyaraka za Kisheria**

21. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za uandaaji wa hati, kusajili na kutoa Hatimiliki na Hati za Hakimiliki kwa wananchi. kupitia hati hizo wananchi wanapata manufaa yakiwemo kuwa na usalama wa miliki zao hivyo kuwezesha kudhibiti na kupunguza migogoro ya ardhi; kudhibiti umegaji wa ardhi kiholela hivyo kuongeza tija katika matumizi ya ardhi; kuwezesha utambuzi wa maeneo katika zoezi la uwekaji wa Anwani za Makazi; na Wananchi kutumia ardhi kama dhamana katika Taasisi za fedha na vyombo vya sheria.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji iliahidi kuandaa na kusajili Vyeti vya Ardhi ya Kijiji 100, Hati za Hakimiliki za Kimila **520,000,** Hatimiliki **500,000** na Hati za Sehemu ya Jengo **1,000.** Aidha, Wizara iliahidi kusajili miamala na Nyaraka za Kisheria **100,000**. Hadi kufikia tarehe

15 Mei, 2022, Wizara imesajili Vyeti vya Ardhi ya Kijiji 142, Hati za Hakimiliki za Kimila **42,684,** Hatimiliki **65,441** na Hati za Sehemu ya Jengo **284.** Vilevile, miamala ya Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria **84,803** zilisajiliwa. **(Jedwali Na. 3A & 3B).**



*Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Ridhiwani Kikwete akiangalia sehemu ya hati na leseni za makazi zilizotolewa kwa wananchi wa halmashauri ya jiji la Mbeya wakati wa zoezi la utoaji hati na leseni za makazi katika viwanja vya Ruanda Nzovwu mkoani Mbeya.*

23. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wizara haikuweza kufikia malengo katika uandaaji wa Hatimiliki, na Hati za Hakimiliki za kimila. Hali hii imetokana na baadhi ya wananchi kutokamilisha ulipaji wa gharama za umilikishaji na Wadau wanaoshirikiana na Wizara (NGOs, CBOs) kupunguza ufadhili wa kuwezesha Vijiji kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi na uandaaji wa Hati za Hakimiliki za Kimila. Aidha, Mamlaka za Upangaji kutoweka kipaumbele katika uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ili kuwezesha utoaji wa milki za ardhi.

24. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Wizara itaandaa na kutoa vyeti vya ardhi ya kijiji 100, Hati za Hakimiliki za Kimila **520,000,** Hatimiliki **500,000** na Hati za Sehemu ya Jengo **1,000**. Vilevile, Wizara itasajili miamala ya Hatimiliki na nyaraka za kisheria **100,000.** Ili kuhakikisha kuwa

malengo haya yanafikiwa, Wizara itatekeleza Mradi wa Uboreshaji Miliki za Ardhi (LTIP); itaongeza kasi ya utekelezaji wa Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi; kuboresha miundombinu ya upimaji; na kuongeza kasi ya uandaaji wa matumizi ya ardhi; kushirikisha wadau mbalimbali na sekta binafsi mathalan UN-Women, LTA - NGO, Ofisi ya Rais kupitia MKURABITA na kuzihimiza Halmashauri kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya Sekta ya Ardhi. **Natoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge ambao ni wajumbe wa Baraza la Madiwani kuhakikisha Halmashauri zinatenga fedha katika bajeti zao kwa ajili ya kutekeleza shughuli za Sekta ya Ardhi kwa mujibu wa matakwa ya sheria Na. 8 ya mwaka 2007 ya Mipango Miji kama Mamlaka za Upangaji**

**Usimamizi wa Masharti ya Umiliki**

25. ***Mheshimiwa Spika,*** Sheria za Ardhi zinamtaka kila mmiliki wa ardhi kuzingatia masharti yanayoainishwa katika nyaraka za umiliki ikiwemo kuendeleza ardhi hiyo kwa wakati. Tatizo la ukiukaji wa masharti hususan katika mashamba umekuwa ukisababisha athari kubwa kiuchumi na kusababisha migogoro ya ardhi. Katika mwaka 2021/22, Wizara iliahidi kuendelea kufanya utambuzi na ukaguzi wa mashamba ili kubaini ukiukaji wa masharti na kuchukua hatua za kisheria. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2022, mashamba **106** yalitambuliwa na kukaguliwa. Kati ya mashamba hayo, mashamba **61** yenye ukubwa wa ekari **13,028** wamiliki wake walibainika kukiuka masharti ya uendelezaji na hatua mbalimbali za kisheria zimeendelea kuchukuliwa. Katika mwaka 2022/23, Wizara itaendelea kukagua mashamba **230** ili kubaini uzingatiwaji wa masharti ya uendelezaji.



*Baadhi ya Wananchi wakimsikiliza Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Ridhiwani Kikwete wakati alipofika kusikiliza changamoto mbalimbali zikiwemo za matumizi ya ardhi katika kijiji cha Kwakonje wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani tarehe 5 Machi 2022.*

**Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Kiutawala**

26. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kudhibiti migogoro ya ardhi kwa kutumia njia mbalimbali na kuhusisha Wizara za kisekta na wadau wa Sekta ya Ardhi. Njia hizo ni pamoja na kutoa elimu kwa umma kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, kuongeza kasi ya umilikishaji ardhi, kufanya utambuzi wa vipande vya ardhi kwenye maeneo yaliyoendelezwa, kuendelea kubadilisha nyaraka za upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi kutoka analogia kuwa za kidigitali, kuandaa na kusimamia mipango ya matumizi ya ardhi, kudhibiti uvamizi na kuchukua hatua za kisheria, kuwajengea uwezo watumishi ili kuimarisha utoaji huduma na kuimarisha utendaji wa madawati ya kushughulikia malalamiko katika Ofisi za Ardhi za Mikoa. Wananchi wamekuwa wakiwasilisha malalamiko yanayohusu masuala ya ardhi kwa njia mbalimbali ikiwemo kupitia sanduku la maoni, kukutana na viongozi katika ngazi mbalimbali za Wizara, Mikoa, Wilaya na Mitaa, madawati ya malalamiko katika Halmashauri, kituo cha mawasiliano kwa wateja na vyombo vya habari. Katika kuhakikisha kuwa kunakuwepo na

utunzaji wa taarifa za migogoro ya ardhi, Ofisi za Ardhi za Mikoa na Halmashauri zimeandaa kanzidata ya michoro iliyopo inayoonesha aina na hali ya mgogoro pamoja na namna ulivyoshughulikiwa.



*Kituo cha mawasiliano kwa wateja kilichopo Mtumba Jijini Dodoma*

27. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wizara ilipanga kutatua migogoro ya ardhi 1,000 kiutawala. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2022 migogoro **1,898** kati ya migogoro **1,635** iliyopokelewa na kutatuliwa **(Jedwali Na.4).** Aidha, Wizara iliendelea na utaratibu wa kutatua migogoro ya ardhi inayowasilishwa na wananchi. Kamati ya Ugawaji wa Ardhi

28. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kuteua Kamati za Kugawa Ardhi katika Halmashauri. Faida ya Kamati hizi ni kuongeza uwazi, kurahisisha upatikanaji wa ardhi na kuongeza uadilifu katika utoaji milki za ardhi. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, Wizara imeteua Kamati za Kugawa Ardhi katika Halmashauri **46** na hivyo kuwa na jumla ya Halmashauri **173** zenye Kamati hizi nchini, huku Halmashauri **11** zikisalia bila kuwa na Kamati hizo kutokana na Mamlakana hizo za Upangaji kutokuwasilisha majina ya Wajumbe wake wakiwemo Waheshimiwa Madiwani wawili (mme na mke) wanaotakiwa kwa mujibu wa Kanuni **(Jedwali Na. 5). Natoa Rai kwa Halmashauri 11 zilizobaki kuhakikisha kuwa Kamati zinaundwa kwa kuzingatia uwiano wa wanaume na wanawake kama ilivyoelekezwa katika Kanuni.**

## Usimamizi wa Ardhi ya Uwekezaji

29. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inasimamia uidhinishaji wa maombi ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji. Ardhi ya uwekezaji hutambuliwa, hutangazwa na kumilikishwa kwa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) au Mamlaka ya Ukanda Maalum wa Kiuchumi (EPZA) ambao hutoa Hatimiliki Isiyo Asili (Derivative Right) kwa wawekezaji. Kamati ya Taifa ya Ugawaji Ardhi iliyo chini ya Wizara huidhinisha maombi ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2022, Kamati ilifanya vikao vinne (**4**) na kuidhinisha maombi yote **151** yaliyowasilishwa yenye ukubwa wa hekta **42,174.41**. Uwekezaji uliokusudiwa ni ujenzi wa viwanda (**68**), kilimo (**12**), ufugaji (**7**), ujenzi wa majengo kwa ajili ya matumizi mbalimbali (**19**), bustani (**1**), makumbusho (**1**), maeneo ya dampo (**2**), taasisi (**3**) na hoteli (**32**).

30. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri, Kituo cha Uwekezaji (TIC) na Mamlaka ya Ukanda Maalum wa Kiuchumi (EPZA) hufanya uhakiki katika maeneo mbalimbali ya wawekezaji nchini ili kubaini hali ya uendelezaji wa maeneo hayo kwa mujibu wa Mipango ya Uwekezaji. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2022, Wizara imehakiki maeneo **27** yaliyotolewa kwa wawekezaji katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. Uhakiki umebaini kuwepo kwa manufaa mbalimbali yanayotokana na uwekezaji katika maeneo hayo. Manufaa hayo ni ujenzi wa viwanda **26** ambavyo vimetoa ajira za kudumu **3,786** na ajira za muda **3,250** kwa watanzania. Aidha, uwekezaji huo umewezesha ujenzi wa vyumba vya madarasa, Zahanati, Kituo cha Polisi, kiwanja cha michezo na ukarabati wa barabara. Katika mwaka 2022/23, Wizara itaendelea kufanya uhakiki wa uendelezaji wa ardhi ya uwekezaji katika mikoa mingine.

31. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na jitihada binafsi zinazofanywa na wawekezaji ili kupata ardhi, Wizara

imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ili kuhakikisha kuwa kuna ardhi kwa ajili ya uwekezaji. Mikakati hiyo ni pamoja kutenga ardhi kwa ajili ya uwekezaji kupitia Mipango Kabambe inayoandaliwa, miradi ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi na ardhi ya mashamba yaliyobatilishwa. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, ardhi yenye ukubwa wa ekari **247,899.59** imetengwa kwa ajili ya uwekezaji katika Kituo cha Taifa cha Uwekezaji (TIC), Mamlaka ya Ukanda Maalum wa Kiuchumi (EPZA), mikoa na Halmashauri mbalimbali nchini **(Jedwali Na. 6A).** Aidha, jumla ya hekta **27,956** zimetengwa kama ardhi ya akiba katika mikoa mbalimbali. **(Jedwali Na. 6B)**. Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ulipaji wa fidia ili ardhi iliyotengwa iwe huru kwa ajili ya uwekezaji.



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Dkt Allan Kijazi (Kulia) na Mkurugenzi wa Kampuni ya Tanzania Plantations Ltd wakionesha hati ya makubaliano ya makabidhiano ya mashamba ya Kampuni ya Tanzania Plantantions na serikali wilayani Arumeru mkoani Arusha.*

32. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa Serikali inakuwa na taarifa za pamoja na unganishi za masuala ya uwekezaji na wawekezaji, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara na Taasisi nyingine inaandaa Mfumo wa Tanzania Investment Electronic Window (TIEW). Mfumo huo utawezesha wawekezaji kupata taarifa

zote muhimu za uwekezaji ikiwemo maeneo yaliyotengwa na yaliyomilikishwa kwa ajili ya uwekezaji.

**Uhuishaji wa Kumbukumbu za Ardhi**

33. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuwa na kumbukumbu sahihi za wamiliki wa ardhi nchini, Wizara inaendelea kuhuisha kumbukumbu katika Mifumo ya TEHAMA inayotumika kuhifadhi kumbukumbu za ardhi. Zoezi hilo linahusisha uhakiki wa taarifa za wamiliki ili ziendane na taarifa za NIDA na mifumo mingine ya Serikali mathalan BRELA. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2022, Wizara imehuisha kumbukumbu za wamiliki wa ardhi **112,637**. Aidha, majina ya wamiliki wa ardhi **86,254** yalihakikiwa katika nyaraka za umiliki ili kuoanisha na taarifa za NIDA. Katika mwaka 2022/23, Wizara itaendelea kuhuisha kumbukumbu za wamiliki wa ardhi katika mifumo ya TEHAMA na kuendelea na zoezi la uhakiki wa taarifa za wamiliki kupitia zoezi la ubadilishaji wa nyaraka za umiliki kutoka analojia kwenda digitali na utambuzi wa maeneo yasiyopimwa.



*Bwana Chande Hemed Mkazi wa kata ya Toangoma Jijini Dar es salaam akichukuliwa taarifa za kumbukumbu kidigitali na Mtaalamu kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.*

**Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi katika Vijiji 975**

34. ***Mheshimiwa Spika,*** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mhe.Rais Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuridhia utekelezaji wa utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi kwa vijiji **975** ambapo vijiji 920 vitarasimishwa kwa njia shirikishi na kuendelea kufanya tathmini katika vijiji **55** ili kuishauri Serikali hatua za kuchukua. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta inaendelea kuratibu utekelezaji wa maelekezo ya Serikali kuhusu utatuzi wa migogoro hiyo. Sehemu kubwa ya migogoro hiyo ni ile inayohusisha maeneo ya hifadhi, mashamba, vyanzo vya maji, ranchi za Taifa na maeneo ya vyombo vya ulinzi na usalama. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2022, Kamati ya Mawaziri wa Kisekta tayari imekwishafanya ziara kwenye Mikoa 12 ya Dodoma, Singida, Manyara, Tabora, Mara, Geita, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Mbeya, Pwani na Morogoro. Kazi zinazofanyika ni kuishirikisha Mikoa kuhusu uamuzi wa Serikali na kujadiliana namna bora ya utekelezaji, kutembelea baadhi ya maeneo na kutoa elimu kwa wananchi na kuelekeza kuendelea kufanya tathmini kwenye baadhi ya maeneo yanayohitaji maelekezo zaidi ya Serikali. Aidha, Kamati ya Mawaziri itaendelea kutekeleza uamuzi wa Serikali kwa mikoa iliyosalia baada ya Bunge la bajeti. Kwenye baadhi ya maeneo yakiwemo ya Pori la akiba Mkungunero na bonde la Usangu/Ihefu, tathmini ya kina inaendelea kufanyika kwenye maeneo hayo ili kuishauri serikali hatua stahiki za kuchukua. **Nawasihi wananchi wote kuwa na imani na Serikali yao katika utekelezaji wa zoezi hili na natoa rai kwa wale ambao wamekuwa wakieneza taarifa zisizo sahihi na kusababisha taharuki kwa wananchi kuacha kufanya hivyo mara moja.**



*Mawaziri wa Wizara za Kisekta wakiwa katika mkutano wa wananchi wa kata ya Makurunge katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani walipokwenda kupeleka mrejesho wa maamuzi ya Baraza la Mawaziri kuhusiana na migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975 tarehe 24 Machi 2022.*



*Sehemu ya wananchi wa kata ya Makurunge katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani wakiwasikiliza Mawaziri wa Kisekta katika ziara ya kutafuta ufumbuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975 tarehe 24 Machi 2022.*

**Uthamini wa Mali**

35. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inasimamia uthamini wa mali zinazohamishika na zisizohamishika, uidhinishaji wa taarifa za uthamini na uandaaji wa viwango vya bei ya soko la ardhi, mazao na majengo. Viwango vya bei ya soko ndivyo

hutumika kufanya uthamini ili kuwezesha ulipaji wa fidia, utozaji wa ushuru wa Serikali unaotokana na mauzo au uhamisho wa umiliki wa mali, utozaji wa malipo ya awali (premium) wakati wa kutoa milki, mizania ya hesabu, kuweka mali rehani, mirathi, kinga ya bima na utozaji kodi ya pango la ardhi.

36. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wizara iliahidi kuratibu uandaaji na uidhinishaji wa taarifa za uthamini **50,000** ambazo kati ya hizo uthamini wa kawaida ni **20,000** na uthamini wa fidia ni **30,000**. Kadhalika, Wizara iliahidi kuendelea kushughulikia malalamiko **100** ya uthamini wa fidia, kufanya uhakiki wa uthamini wa fidia katika maeneo **20**, kuendelea kufanya utafiti na kuandaa viwango vya thamani ya ardhi katika mikoa yote nchini. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, Wizara imeidhinisha Taarifa za Uthamini **46,910** ambapo kati ya hizo taarifa za uthamini wa kawaida ni **18,881** na uthamini wa fidia **28,029**. Aidha, jumla ya malalamiko **51** ya uthamini wa fidia yalipokelewa na kushughulikiwa. Pia, uthamini wa maeneo **15** ya miradi mbalimbali umefanyiwa uhakiki ili kutatua migogoro ya fidia. Aidha, Wizara imekuwa ikipokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi yanayohusiana na kucheleweshewa, kulipwa pungufu au kutolipwa fidia. **Nasisitiza taasisi za Serikali na kampuni binafsi kulipa fidia kwa wakati ili kuepusha ulipaji wa riba na malalamiko yanayotokana na ucheleweshaji wa ulipaji fidia. Kamwe Serikali haitaruhusu utwaaji wa ardhi bila kulipa fidia.**

37. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Wizara itaratibu na kusimamia uandaaji wa taarifa za uthamini **54,000** ambazo kati ya hizo uthamini wa kawaida ni **20,000** na uthamini wa fidia ni **34,000**. Kadhalika, Wizara itaendelea kushughulikia malalamiko yatokanayo na uthamini wa fidia, kuboresha kanzidata ya viwango vya thamani ya ardhi na mazao pamoja na kuhuisha viwango vya kodi ya ardhi.

**Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya**

38. **Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Sheria ya Mahakama za Ardhi Na. 2 ya mwaka 2002, Wizara ina jukumu la kuanzisha, kusimamia na kuhudumia Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kwa lengo la kutatua migogoro ya ardhi nchini. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara imeunda Mabaraza **80** kati ya Mabaraza **139** yanayotakiwa kisheria ambayo yamekuwa yakipokea, kusikiliza na kuamua mashauri ya ardhi. Katika mwaka 2021/22, Wizara ilipanga kushughulikia mashauri **27,801**. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2022 mashauri **20,180** yalishughulikiwa na kutolewa maamuzi. Aidha, mashauri mapya **17,698** yalifunguliwa. **(Jedwali Na. 7).**

39. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kusogeza huduma karibu na wananchi, Wizara katika mwaka 2021/22 iliahidi kuongeza idadi ya Mabaraza yanayotoa huduma ambapo hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2022, Mabaraza mapya **20** yameanza kutoa huduma na hivyo kuwa na jumla ya Mabaraza **80** yanayotoa huduma kati ya Mabaraza **139** yaliyoanzishwa. Katika mwaka 2022/23, Wizara inatarajia kushughulikia mashauri **33,250** na itawezesha Mabaraza mapya **59** kuanza kutoa huduma na hivyo kuwa na Mabaraza yanayotoa huduma katika Wilaya zote nchini.




*Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Dkt Angeline Mabula akiwa na wakazi wa wilayani ya Sengerema mkoani Mwanza baada ya kuzindua Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya na kugawa miongozo ya uendeshaji wa Mabaraza tarehe 21 Machi 2022.*

40. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22 Wizara iliahidi kuanza kutumia mfumo wa kielektroniki katika kutoa huduma za Mabaraza. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara itakamilisha ujenzi wa Mfumo wa Kusimamia Mashauri katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya (Intergrated Land Cases Management System) ifikapo Juni, 2022 ambao utaanza kutumika katika mwaka 2022/23. Mfumo huo utarahisisha utendaji kazi wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya katika kutunza kumbukumbu za mashauri, kufungua mashauri mapya, kufuatilia utendaji kazi wa watumishi wa Mabaraza na upatikanaji wa nakala za hukumu kwa njia ya mtandao.

41. Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto ya wazee wa baraza wanapomaliza muda wao, huchukua muda mrefu kupatikana wengine, ***nitoe rai kwenye mamlaka za mikoa na wilaya kuanza mchakato wa kupata wazee wa mabaraza wapya <u>miezi sita (6)</u> kabla ya waliopo kumaliza muda wao ili kuepuka usumbufu kwa wateja kwa kuahirishwa mashauri yao mara kwa mara kwa kukosa wazee kwa kisingizo cha muda wao wa kuhudumu kuisha.***

## 3. HUDUMA ZA TEHAMA

42. ***Mheshimiwa Spika,*** TEHAMA ni nyenzo muhimu katika kuboresha huduma katika sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Ardhi. Kutokana na umuhimu huo, Wizara imeendelea kutumia mifumo ya TEHAMA katika kuchakata, kutunza kumbukumbu na kutoa huduma kwa wananchi. Katika kufanikisha azma ya matumizi ya TEHAMA, Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi (Integrated Land Management Information System – ILMIS) umeendelea kuboreshwa na kusambazwa kwa kutumia watalaam wa ndani.

43. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, mfumo huo umeboreshwa kwa kuongeza moduli mbalimbali ikiwemo Moduli ya kiganjani (ILMIS Mobile App.) ambayo inawezesha uchukuaji wa taarifa za upimaji moja kwa moja kutoka uwandani na kuingizwa katika mfumo. Hatua hii imerahisisha ukusanyaji na uchakataji wa taarifa za utambuzi wa vipande vya ardhi kwa ajili ya utoaji wa Leseni za Makazi na Hati za Hakimiliki za Kimila. Hadi kufikia tarehe 15 Mei 2022, jumla ya Leseni za makazi **18,063** na Hati za Hakimiliki za Kimila **6,861** zimetolewa kupitia mfumo katika mikoa ya Mwanza, Arusha, Mbeya, Rukwa na Singida.



*Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Dkt Angeline Mabula na Mkurugenzi wa Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Korea (KOICA) Kyuchoel Eo akitoa hati kwa mkazi wa Ikungi wakati wa hafla ya utoaji hatimiliki za kimila mkoani Singida tarehe 15 Machi 2022.*

44. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wizara iliahidi kuanza kutumia mfumo wa ILMIS na kutoa hati za kieletroniki katika mkoa wa Dodoma na kuendelea kujenga na kusimika miundombinu wezeshi ya TEHAMA kwa awamu katika Ofisi za Ardhi za Mikoa yote nchini. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi tarehe 15 Mei, 2022, Hatimiliki za Kielektroniki **6,138** zimetolewa kupitia Mfumo wa ILMIS katika Jiji la Dodoma na ujenzi wa miamala ya upili unaendelea. Aidha, Wizara imeanza kujenga mtandao kiambo (Local Area Network) katika Ofisi za Ardhi za Mikoa ya Iringa, Lindi, Mwanza na Mbeya ambao utakamilika ifikapo Juni, 2022. Mitandao hiyo itakapokamilika itaunganishwa na Kituo cha Taifa cha Taarifa za Ardhi.

45. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliahidi kuendelea kuboresha huduma kwa wateja kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ikiwa ni pamoja na kusimika vifaa vipya vya TEHAMA katika Kituo cha Huduma kwa Wateja kilichopo katika Ofisi ya Ardhi ya Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Mawasiliano kwa Wateja (***Call Centre* Na. 0739 646 885**) kilichopo Makao Makuu ya Wizara Dodoma. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Kituo cha Mawasiliano kwa Wateja kimejengwa na tayari kinatoa huduma. Kituo hiki kimeongeza wigo wa kutoa huduma kwa kuwezesha mawasiliano ya moja kwa moja na wateja popote walipo kwa simu na kutatua changamoto zinazowakabili bila kulazimika kufika katika Ofisi za Ardhi. Utaratibu huu umewapunguzia wananchi kero, gharama za usafiri na muda wa kupata huduma. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2022, kupitia Kituo hiki Wizara imepokea na kushughulikia malalamiko **3,947**. Aidha, uboreshaji wa Kituo cha Huduma kwa Wateja katika Ofisi ya Mkoa wa Dar es Salaam utakamilika ifikapo Juni, 2022. Vilevile, Wizara imeboresha utoaji wa ankara za malipo ya kodi ya pango la ardhi kwa wateja ambapo mteja anaweza kukadiria kodi ya ardhi kupitia tovuti ***www.landrent.lands.go.tz*** na kulipa kwa awamu.

46. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Wizara itaendelea kujenga, kusimika na kuimarisha miundombinu wezeshi ya TEHAMA kwa awamu katika Ofisi za Ardhi za Mikoa na Halmashauri nchini. Aidha, huduma kwa wateja zitaendelea kuboreshwa kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Vilevile, ukarabati wa mtandao kiambo katika Ofisi za Halmashauri **47** zikiwemo Makao Makuu ya Mikoa ya Iringa, Lindi, Mwanza na Mbeya utafanyika.

**Ubadilishaji wa Michoro ya Mipangomiji, Ramani za Upimaji na Nyaraka za Umiliki kutoka Analojia kwenda Digitali**

47. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa kutumia mifumo ya TEHAMA, Wizara imeendelea kuchambua, kufanya nakishi ya michoro (scanning) na kuhifadhi ramani na kumbukumbu za Ardhi katika Ofisi za Ardhi za Mikoa na Halmashauri mbalimbali nchini kwa awamu. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara imefanya uchambuzi wa Michoro ya Mipangomiji, ramani za upimaji na nyaraka za umiliki na kubaini kuwa kuna jumla ya Michoro ya Mipangomiji **25,744** yenye viwanja **7,013,474,** ramani za upimaji Ardhi **89,512** zenye viwanja **2,842,494,** Nyaraka za umiliki **2,388,705** na makadirio ya vipande vya ardhi **1,000,000** katika maeneo ambayo hayajapangwa na kupimwa mijini. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2022 ubadilishaji wa michoro ya mipangomiji **5,649** yenye viwanja **1,758,424** na ramani za upimaji **31,500** zenye viwanja **598,000** katika Halmashauri **38** umefanyika kutoka analojia kwenda digitali. Aidha, utambuzi wa vipande vya ardhi **52,648** katika Halmashauri za Jiji la Dodoma na Manispaa za Tabora, Shinyanga na Ilemela umekamilika.

48. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatarajia kukamilisha kazi ya kubadilisha Michoro ya Mipangomiji **20,095** yenye viwanja **5,255,050**, Ramani za upimaji Ardhi **63,113** zenye viwanja **1,478,957**, Nyaraka za umiliki **2,388,705** zilizobaki kutoka analojia kwenda digitali na kutambua vipande vya ardhi

**947,352** katika maeneo ambayo hayajapangwa na kupimwa ifikapo Mei, 2022.

49. ***Mheshimiwa Spika,*** zoezi la ubadilishaji wa michoro ya mipangomiji, ramani za upimaji na nyaraka za umiliki litakuwa na manufaa makubwa kwa wananchi, wawekezaji wa ndani na nje ya nchi na Taifa kwa ujumla kama ifuatavyo;

(i) Kuwezesha uandaaji wa anwani za makazi na Sensa ya Watu na makazi kwa mwaka 2022;

(ii) Kuwezesha Wizara kuunganishwa na mifumo mingine ya Serikali katika kubadilishana taarifa mathalan, Mfumo wa ILMIS na NaPA;

(iii) Kuwezesha utunzaji wa kumbukumbu za ardhi kidigitali pamoja na utoaji wa Hatimiliki kwa njia ya kielektroniki;

(iv) Kurahisisha usimamizi, utoaji wa huduma na kufanya maamuzi;

(v) Kupunguza udanganyifu na kughushiwa kwa nyaraka mbalimbali za ardhi na hivyo kupunguza migogoro; na

(vi) Kurahisisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali ikiwemo utoaji wa ankara kidigitali.

## 4. UPIMAJI ARDHI NA UTAYARISHAJI WA RAMANI

50. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kusimamia na kuratibu upimaji wa ardhi, upimaji wa mipaka ya kimataifa, kutafsiri matangazo ya Serikali ardhini kuhusu mipaka ya kiutawala, pamoja na utayarishaji wa ramani za msingi kwa ajili ya shughuli mbalimbali. Aidha, Wizara ina wajibu wa

kutoa miongozo ya upimaji ardhi na uandaaji wa ramani kwa taasisi mbalimbali za Serikali na Sekta Binafsi.




*Ramani ya Rasmi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoonesha mipaka ya kiutawala*

## Uwekaji wa Alama za Msingi za Upimaji Ardhi

51. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuweka miundombinu ya upimaji wa ardhi ikiwemo alama za msingi za upimaji. Alama hizi hurahisisha kazi, kupunguza muda na gharama za upimaji ardhi. Katika mwaka 2021/22, Wizara iliahidi kusimika alama mpya za msingi **80** katika maeneo mbalimbali nchini. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2022 alama za msingi za upimaji **68** zilisimikwa katika Mikoa ya Dar es Salaam (5), Arusha (8), Dodoma (11), Mara (7), Njombe (8), Simiyu (3), Kigoma (8), Manyara (5), Tanga (5), na Geita (8) na hivyo kuwa na alama za upimaji 935 nchini. Katika mwaka 2022/23 Wizara itasimika alama mpya za msingi **80**.



*Muonekano wa alama ya mpaka ardhini (BP MWISHONI) eneo la Kirongwe lililopo wilaya ya Rorya mkoani Mara na Muhuru Bay iliyopo Kaunti ya Migori upande wa Kenya.*

52. ***Mheshimiwa Spika,*** picha za anga ni nyenzo muhimu katika uandaaji wa ramani za msingi. Kwa mara ya mwisho picha za anga zilipigwa mwishoni mwa miaka ya 1970. Kukosekana kwa picha za anga kumesababisha kutohuishwa kwa ramani za msingi zinazoonesha hali halisi ardhini hivyo kuathiri upangaji wa miji na uwekaji wa miundombinu. Katika kukabiliana na changamoto hii, Wizara inatekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo ununuzi wa vifaa vya kisasa vya kupiga picha za anga na kuchakata ramani.

53. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wizara iliahidi kununua ndege ndogo isiyotumia rubani (drone) kwa ajili ya kupiga picha za anga zitakazowezesha uandaaji wa ramani za msingi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara imenunua ndege kwa gharama ya shilingi milioni **189** kwa ajili ya kupiga picha za anga. Picha zinazozalishwa zinawezesha kuandaa ramani za msingi zinazotumiwa katika Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Taarifa za Ardhi. Ndege hii inawezesha upatikanaji wa taarifa zilizopo ardhini pindi zinapohitajika na picha hizo zina ubora kuliko taarifa zinazopatikana kwa picha za satellite. Ndege hii imetumika kupiga picha katika eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba **100** katika Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha ardhi katika Jiji la Dodoma. Aidha, Wataalam wawili (**2**) wamehitimu mafunzo ya kurusha ndege za aina hiyo na kupata leseni kutoka Mamlaka ya Usalama wa Anga (TCAA**).**

**Upimaji wa Ardhi Nchi Kavu**

54. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kuratibu na kusimamia upimaji wa viwanja na mashamba unaofanywa na Mamlaka za Upangaji pamoja na sekta binafsi. Katika mwaka 2021/22, Wizara ilipanga kuidhinisha ramani za upimaji wa viwanja na mashamba **500,000** pamoja na kutatua migogoro **25** ya mipaka ya vijiji, hifadhi na Wilaya. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, viwanja **298,232** na mashamba **356** ziliidhinishwa na kutunzwa kwenye kanzidata ya Wizara **(Jedwali Na. 8).** Vilevile, migogoro ya mipaka ya vijiji nane (**8)** katika Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze inaendelea kushughulikiwa na migogoro ya mipaka ya vijiji viwili (**2)** katika Halmashauri za Wilaya za Nyang'hwale (1) na Nkasi (1) imetatuliwa. Aidha, mgogoro wa Hifadhi za Msitu wa Kalambo na Kijiji cha Kasapa katika Wilaya ya Nkasi umeshughulikiwa. Pia, mipaka ya maeneo ya kupumzishia mifugo ya Mkwese (Manyoni) na Kinyangiri (Mkalama) imehakikiwa.

**Tafsiri na Uhakiki wa Mipaka ya Kiutawala na Hifadhi**

55. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kutafsiri ardhini Matangazo ya Serikali (GN) yanayohusu mipaka ya maeneo ya utawala, Hifadhi za Misitu na Wanyamapori. Jukumu hili linatekelezwa na Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta, Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Mamlaka mbalimbali ili kutatua migogoro ya mipaka. Aidha, tafsiri hizo zimewezesha kutatua migogoro ya mipaka baina ya vijiji, wilaya na mikoa na kati ya vijiji na hifadhi. Hadi tarehe 15 Mei 2022, Tafsiri ya mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Mwalimu Nyerere na Mapori Tengefu ya Makere (Uvinza) na Litumbandyosi (Songea) imefanyika. Vilevile, uhakiki na tafsiri za mipaka ya Mapori Tengefu **14** yanayoandaliwa kuwa Mapori ya Akiba imefanyika. Aidha, mipaka ya vijiji **39** imepimwa katika Mikoa

ya Tabora (6), Mbeya (3), Singida (6), Arusha (4), Kigoma (10), Rukwa (3), Katavi (1), Dodoma (2), Iringa (1) na Ruvuma (3).

## 5. UPANGAJI MIJI NA MAENDELEO YA MAKAZI

56. ***Mheshimiwa Spika,*** Ongezeko la idadi ya watu nchini linaongeza mahitaji ya msingi katika huduma za jamii, miundombinu, mahitaji ya makazi, viwanda, maeneo ya wazi na uhifadhi. Ili kukabiliana na ongezeko hilo, Wizara itaendelea kutekeleza Miradi na Programu mbalimbali za kupanga, kupima na kumilikisha ardhi na kuboresha Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo ili kuwa na miji endelevu. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI itaendelea kuboresha mikakati ya kusimamia uendelezaji wa miji ili kupunguza ujenzi usiozingatia taratibu za mipangomji.

### Utangazaji wa Maeneo ya Upangaji Miji

57. ***Mheshimiwa Spika,*** utangazaji wa maeneo yaliyoiva kimji unazingatia vigezo mbalimbali. Vigezo hivyo ni pamoja na uwepo wa Kituo cha Afya, Shule ya Sekondari, Shule ya Msingi, Soko, Maduka ya rejareja yenye leseni yasiyopungua 20 na idadi ya watu 10,000. Aidha, eneo lolote linaweza kutangazwa kuwa la upangaji maalum iwapo lina sifa za kipekee au muhimu za kiuchumi, kimaendeleo au kimazingira. Katika mwaka 2021/22, Wizara iliahidi kuendelea kushirikiana na mamlaka za upangaji kutambua, kupokea mapendekezo na kutangaza maeneo yaliyoiva kimipangomiji. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2022 maeneo **117** ya upangaji yaliyoiva kimipangomiji yalipokelewa kwa ajili ya kutangazwa kuwa Maeneo ya Upangaji na maeneo **190** yalipokelewa kwa ajili ya kutangazwa kuwa maeneo ya Urasimishaji Makazi yalipokelewa kutoka Mamlaka za Upangaji kati hayo maeneo **110** yalitangazwa. **(Jedwali Na. 9A, B & C)**. Katika mwaka 2022/23, Wizara itaendelea kushirikiana na Mamlaka za Upangaji kutambua, kupokea na kutangaza maeneo yaliyoiva kimipangomiji ili yaendelezwe kwa mujibu wa sheria

na kanuni za mipangomiji hivyo kudhibiti ukuaji holela wa vijiji na miji nchini.

58. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kulinda maeneo yanayochipukia kuwa miji, Wizara imekwisha andaa mwongozo wa kusimamia uandaaji wa mipango ya uendelezaji wa makazi na ujenzi wa nyumba vijiji. Ili kufanikisha utekelezaji wa mwongozo huo, Wizara itandaa mafunzo kwa wananchi kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa upangaji na usimamizi kwa miji midogo katika maeneo ya vijiji. **Nazielekeza Mamlaka za Upangaji kuendelea kutambua na kuwasilisha mapendekezo ya vijiji na miji inayokua na kukidhi vigezo vya kutangazwa kuwa maeneo ya upangaji ili kuyaendeleza kimji.**



*Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Dkt Angeline Mabula akiwa katika picha ya pamoja na wananchi wa vijiji vya Ntondo na Nkwea mkoani Singida baada ya kukabidhiwa hatimiliki za kimila wakati wa ziara ya kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii tarehe 15 Machi 2022.*

## Uandaaji wa Mipango Kabambe

59. ***Mheshimiwa Spika,*** maendeleo endelevu ya miji huwezeshwa kwa kuandaliwa Mipango Kabambe inayotoa dira ya ukuaji wa miji, utoaji wa huduma mbalimbali za kiuchumi na kijamii na usalama wa miji na watu wake. Katika mwaka 2021/22, Wizara iliahidi kuendelea kushirikiana na Mamlaka za Upangaji katika uandaaji na utekelezaji wa Mipango Kabambe kwa mujibu wa sera, sheria, kanuni na miongozo iliyopo. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, Mipango Kabambe mitano (5) ipo katika hatua mbalimbali za uandaaji katika Halmashauri za Manispaa za Moshi na Kahama, Mji wa Mafinga, Bagamoyo na Chalinze. Aidha, katika kipindi hicho Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Mipango Kabambe katika Jiji la Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na Mbeya, Manispaa ya Bukoba, Musoma na Mji wa Geita. Katika mwaka 2022/23, Wizara itaendelea kushirikiana na Mamlaka za Upangaji kufuatilia uandaaji, ukamilishaji na utekelezaji wa Mipango Kabambe kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo iliyopo. **Nazihimiza Mamlaka za Upangaji nchini kutenga fedha kwa ajili ya uandaaji, utekelezaji na udhibiti uendelezaji miji ili kuwezesha miji yetu kusanifiwa na kuendelezwa kwa kuzingatia Mipango Kabambe**.

## Upangaji wa Mji wa Tanzanite

60. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu uaandaji wa Mpango Kabambe, Mpangokina na upimaji wa Mji wa Kibiashara wa Tanzanite uliopo eneo la Mirerani Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara ili kuhakikisha biashara ya madini ya Tanzanite inafanyika kwa ufanisi katika eneo lililopangwa na hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi. Hadi tarehe 15 Mei, 2022 jumla ya viwanja **335** vya matumizi mbalimbali yakiwemo masoko ya madini, makazi, hoteli za kitalii na za kawaida, huduma za jamii burudani na michezo vimepangwa na kupimwa. Aidha, viwanja **526** vimepangwa na umilikishaji unaendelea katika eneo linalozunguka mji huo.

**Uandaaji wa Mipangokina**

61. ***Mheshimiwa Spika,*** mipangokina huandaliwa na Mamlaka za Upangaji kwa lengo la kuelekeza ukuaji na uboreshaji wa makazi, kuhifadhi mazingira, kuondoa ukinzani wa matumizi ya ardhi na kutoa uhakika wa upatikanaji wa maeneo kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo ya uwekezaji na huduma za jamii mijini na vijijini. Katika mwaka 2021/22, Wizara ilipanga kukagua na kuidhinisha michoro ya mipangokina **2,000** kutoka katika Mamlaka za Upangaji nchini. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, michoro ya Mipangokina **1,121** yenye viwanja **197,126** ilidhinishwa. Katika mwaka 2022/23, Wizara inatarajia kuidhinisha michoro ya mipangokina **2,000** kutoka katika Mamlaka za Upangaji nchini.

**Urasimishaji Makazi**

62. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imeendelea kuboresha makazi ya wananchi wanaoishi katika maeneo yasiyopangwa kupitia Programu ya Urasimishaji Makazi iliyoanza kutekelezwa kuanzia mwaka 2013 hadi 2023. Tangu kuanza kwa Programu hii hadi 15 Mei, 2022 milki za wananchi **2,145,100** zimetambuliwa na viwanja **1,002,391** vimepimwa. Aidha, jumla ya ankara **408,030** za viwanja zimetolewa kwa wananchi kwa ajili ya kulipia gharama za umilikishaji ambapo wananchi **142,833** wamekamilisha malipo na kuandaliwa Hatimiliki. Aidha, Wizara kupitia Ofisi za Ardhi za Mikoa itaendelea kuwahamasisha wananchi kulipia viwanja vyao na kuzishirikisha Taasisi za Fedha katika kuwawezesha kugharamia urasimishaji makazi. Ushirikiano baina ya wananchi na Taasisi za fedha ni muhimu katika kuwezesha kukamilisha zoezi la urasimishaji makazi nchini. **Natoa wito kwa wananchi wote ambao wamepewa ankara za malipo kulipia Ankara hizo ili wamilikishwe maeneo yao na hivyo kuongeza usalama wa milki zao.**

63. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2021/22, Wizara ilipanga kuendelea kuratibu shughuli za urasimishaji makazi zitakazotekelezwa na Mamlaka za Upangaji na Sekta Binafsi nchini. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji iliandaa michoro ya urasimishaji **932** yenye jumla ya viwanja **380,272 (Jedwali Na. 10).** Katika mwaka 2022/23, Wizara itaendelea kuratibu shughuli za urasimishaji makazi **300,000** nchini kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji na sekta binafsi ikiwa ni hatua ya kukamilisha Programu ya Kurasimisha Makazi na Kuzuia Makazi Yasiyopangwa Mijini (2013 - 2023). Baada ya muda uliopangwa kutekeleza programu ya urasimishaji kuisha, Wizara itafanya tathmini ya mafanikio na changamoto ya utekelezaji wa programu hii. **Natoa rai kwa Mamlaka za Upangaji nchini kuhakikisha zinasimamia kikamilifu sheria, kanuni na taratibu zinazohusu uendelezaji miji ili kudhibiti ujenzi holela kwa lengo la kuwa na miji nadhifu.**



*Kazi ya urasimishaji makazi ya wakazi wa Kivule Jijini Dar es salaam likiendelea*

**Udhibiti na Uendelezaji wa Miji**

64. ***Mheshimiwa Spika,*** upangaji na uendelezaji wa miji ni suala mtambuka ambalo hushirikisha wadau mbalimbali wakiwemo wamiliki wa ardhi, taasisi zisizo za kiserikali, sekta binafsi, asasi za kijamii na taasisi zinazotoa huduma za

miundombinu kama vile barabara, umeme, maji na mawasiliano. Katika mwaka 2021/22, Wizara iliahidi kuendelea kuratibu uidhinishaji wa maombi **300** ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, jumla ya maombi **252** ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi kutoka Mamlaka za Upangaji yaliidhinishwa.

**Usimamizi na uratibu wa uendelezaji Sekta ya Nyumba**

65. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Nyumba ni miongoni mwa sekta muhimu katika kukuza pato la Taifa, kuongeza ajira na kuboresha maisha ya wananchi. Wadau wanaoshiriki katika ujenzi wa nyumba na majengo ya biashara ni pamoja na Wizara kupitia Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) lililoanzishwa kwa sheria Na. 2 ya mwaka 1990 (National Housing Act) ambalo kwa mujibu wa sheria hiyo limepewa mamlaka ya kujenga nyumba kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Aidha, Wakala wa Taifa wa Majengo (TBA), Watumishi Housing Company, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Sekta Binafsi na watu binafsi. Pamoja na juhudi za ujenzi wa nyumba zinazofanywa na taasisi hizo na sekta binafsi bado kuna upungufu wa nyumba takriban **200,000** kwa mwaka.

66. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya upatikanaji wa huduma za uendelezaji nyumba nchini. Huduma hizo ni pamoja na upatikanaji wa mikopo ya masharti nafuu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba; ubunifu wa nyumba za gharama nafuu pamoja na Mwongozo wa Upangaji na Ujenzi wa Nyumba Bora Vijijini ambao unaelekeza namna ya kupanga makazi vjijini kwa kuzingatia vigezo vilivyoainishwa. Wizara imeendelea na uratibu wa utekelezaji wa Mwongozo huo katika kuhakikisha nyumba bora za gharama nafuu zinajengwa katika maeneo ya vijiji ili kuboresha makazi na maisha ya wananchi. Aidha, katika utafiti wa mapato na matumizi ya kaya binafsi *(Household budget Survey)* nchini uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu

mwaka 2017/2018 imebainisha kuwa kuna ongezeko la matumizi ya vifaa bora vya ujenzi wa nyumba vijiji. Kwa mujibu wa utafiti huo nyumba zilizoezekwa kwa bati ni asilimia **76.6,** nyumba zenye kuta zilizojengwa na saruji asilimia **70.5** na nyumba zenye sakafu iliyoboreshwa ni asilimia **32.1.** Katika mwaka 2022/23, Wizara itaendelea kusimamia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa zoezi hili ili kubaini changamoto zilizopo na namna ya kukabiliana nazo.

67. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wizara iliahidi kuendelea kuboresha taarifa za Nyumba katika kanzidata ikiwa ni pamoja na kuhamasisha uundwaji wa vyama vya ushirika wa nyumba. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, taarifa za waendelezaji na wasimamiaji milki **207** ambao wamejenga jumla ya nyumba **25,239** zimeingizwa katika kanzidata ya nyumba. Aidha, Vyama vya Ushirika wa Nyumba **38** vyenye wanachama **2,247** ambavyo vimejenga jumla ya nyumba **1,056** katika Mikoa ya Dar es salaam, Dodoma, Iringa, Kagera, Musoma, Morogoro, Mwanza, na Shinyanga vimeingizwa katika kanzidata. Katika mwaka 2022/23, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Vyama vya Ushirika itaendelea kuhamasisha ujenzi wa nyumba kupitia vyama vya ushirika wa nyumba na kuvijengea mazingira ya kupata mikopo yenye masharti nafuu kutoka taasisi za fedha.

**Mikopo ya ujenzi wa nyumba**

68. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wizara ilipanga kuwezesha kuboreshwa kwa mazingira ya upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba kupitia Tanzania Mortage *Refinance Company (TMRC)*. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, Serikali kupitia TMRC imewezesha taasisi za fedha 32 kutoa mikopo yenye riba nafuu kiasi cha shilingi bilioni **496.61** kwa wananchi **6,177** kwa ajili ya ujenzi wa nyumba. Aidha, katika mwaka 2022/23, Wizara itaendelea kuratibu utoaji wa mikopo ya ujenzi wa nyumba yenye riba nafuu kutoka Taasisi za fedha. Vilevile, Wizara itakamilisha

Miongozo ya Ujenzi wa Nyumba za Gharama Nafuu na kuisambaza kwa wadau **(Jedwali Na. 11).**

**Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali**

69. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ilianzisha Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa nyumba kupitia Waraka wa Utumishi Na. 8 wa mwaka 1992. Lengo la mfuko huo ni kukabiliana na changamoto ya upungufu wa nyumba kwa watumishi wa Serikali. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, watumishi **30** walipatiwa mikopo yenye thamani ya shilingi milioni **315**. Aidha, jumla ya shilingi bilioni **9.09** zimetolewa kwa watumishi **1,567** tangu Mfuko ulipoanzishwa mwaka 1992.

**Sensa ya Majengo**

70. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imekuwa ikikabiliwa na ukosefu wa takwimu sahihi za majengo nchini. Sensa ya majengo ambayo itafanyika kwa mara ya kwanza tangu nchi ipate uhuru itawezesha upatikanaji wa takwimu za uhakika na sahihi za majengo kwa ajili ya mipango ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Upatikanaji wa takwimu sahihi na za uhakika ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020 – 2025. Ili kufanikisha zoezi la Sensa ya Majengo Wizara imekamilisha maandalizi ya dodoso la majengo, mwongozo wa Mkufunzi na Makarani, mwongozo wa ukusanyaji taaarifa za majengo na kufanya kikao cha wadau wa sekta ya majenzi. Katika utekelezaji wa sensa ya majengo na anwani za makazi ni vyema maeneo ambayo ni hatarishi, hifadhi za miundombinu mbalimbali pamoja na maeneo yenye migogoro zoezi husika lifanyike baada ya kujiridhisha na uhalali ya maeneo hayo. **Nawahimiza wamiliki wa majengo nchini kushiriki zoezi la sensa na kutoa taarifa sahihi za matumizi ya jengo, hali ya jengo na umiliki wake. Kwa majengo ambayo hayatumiki,**

**ninaelekeza viongozi wa mitaa na vitongoji kuchukua taarifa za majengo hayo na wamiliki wake kupitia fomu maalum iliyoandaliwa.**



*Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Ridhiwani Kikwete akiwa pamoja Wadau wa Sensa ya majengo walipokutana jijini Dodoma tarehe 21 Aprili 2022. Ushirikiano na Taasisi za Kimataifa Katika Uendelezaji wa Makazi*

71. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekuwa na ushirikiano wa muda mrefu na mashirika ya kimataifa ikiwemo Shirika la Makazi Duniani (UN-HABITAT) na Taasisi ya Shelter Afrique. Ushirikiano huo pamoja na kuongeza mahusiano ya kidiplomasia baina ya nchi yetu na nchi zingine duniani katika usimamizi na uendelezaji wa miji. Kutokana na ushirikiano huo, Shirika la Nyumba la Taifa lilipata mkopo wenye masharti nafuu wa Dola za Marekani milioni **14.5** kutoka Taasisi ya Shelter Afrique. Aidha, Taasisi hii ilinunua hisa za shillingi bilioni **1.859** kutoka *Tanzania Mortage Refinancing Company.* Vilevile, Serikali ilipata Dola za Marekani **13,000** ikiwa ni gawio kutoka Taasisi hii linalotokana na michango inayotolewa na Serikali. Kwa kuzingatia umuhimu wa Shelter Afrique kwa Serikali ya Tanzania, Serikali imelipa kiasi cha Dola za Kimarekani **3,074,859.19** ikiwa ni deni katika taasisi hiyo.

Malipo hayo yameiwezesha Serikali kuongeza kiwango cha hisa zake na kuongeza fursa kwa taasisi mbalimbali kupata mikopo kwa ajili ya uendelezaji wa sekta ya milki nchini.

72. ***Mheshimiwa Spika,*** Vilevile, Wizara imeandaa taarifa ya kitaifa ya utekelezaji wa Agenda Mpya ya Miji na kuiwasilisha Shirika la Umoja wa Mataifa linalosimamia maendeleo ya makazi (UN-HABITAT). Taarifa hii inabainisha hatua iliyofikiwa na nchi katika utekelezaji wa lengo Na. 11 la Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) linaloelekeza kuwa na miji na maendeleo ya makazi jumuishi, salama, stahimilivu na endelevu. Serikali imepata mafanikio katika utekelezaji wa agenda mpya ya miji ikiwa ni moja ya nchi nane (**8)** kati ya **54** za Afrika zilizowasilisha taarifa hiyo. Vilevile, utekelezaji wa agenda mpya ya miji, umechangia kupunguza kiwango cha umasikini kutoka asilimia **28.2** (2011/12) hadi **26.4** (2017/2018). Katika mwaka 2022/23, Wizara itaendelea kusimamia na kuratibu ushirikiano na Taasisi mbalimbali za kimataifa kwa lengo la kutekeleza malengo na mikakati inayoandaliwa na taasisi hizo.

**Usimamizi wa Sekta ya Milki**

73. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa muda mrefu Sekta ya Milki imekosa usimamizi, takwimu na taarifa sahihi, uratibu madhubuti kwa waendelezaji, Taasisi za fedha, watumiaji na mawakala wa sekta. Changamoto hizi zimesababisha kutotambuliwa kwa mchango wa sekta hii katika uchumi wa nchi. Dhamira ya Serikali ni kuwa na mfumo madhubuti wa kitaasisi wa kusimamia na kuratibu uendelezaji sekta ya milki nchini. Kwa kutambua umuhimu huo, **Serikali imeanzisha Kitengo cha milki *(Real Estate Unit)* ambacho kitasimamia pamoja na masuala mengine uwekaji wa mfumo wa uwazi na usawa katika biashara na huduma za sekta ya milki nchini, ikiwemo kuhakikisha viwango vya kodi ya pango la nyumba vinatozwa kwa mujibu wa soko na taratibu za ulipaji wa kodi hiyo haumuumizi mlaji.** Kitengo hiki kitawajibika

kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, kanuni na Miongozo mbalimbali kwa ajili ya kusimamia na kukuza sekta ya milki. Sheria itakayotungwa itasimamia pia utendaji na shughuli za wadau na wataalam wa sekta wakiwemo mawakala wa miliki (Real Estate Agents) ili kuhakikisha wajibu, haki na maslahi ya wadau zinatekelezwa na kulindwa ipasavyo. katika mwaka 2022/23 Wizara itaendelea kukiboresha na kukijengea uwezo Kitengo cha Sekta ya milki ili kiweze kusimamia kikamilifu Sekta ya milki inayojumuisha masuala ya majengo, mawakala, waendelezaji milki, Taasisi binafsi za fedha pamoja na uratibu wa Taasisi za Kitaifa na Kimataifa.

**Mapitio ya Sera na Sheria**

74. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendana na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, maendeleo ya sayansi na teknolojia pamoja na changamoto zinazotokana na mabadiliko ya Tabia nchi; katika mwaka 2021/22 Wizara iliahidi kukamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995, kukamilisha uchambuzi wa maoni ya wadau kuhusu mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 na rasimu ya Sera mpya ya Nyumba. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mapitio ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 yako katika ngazi ya maamuzi serikalini. Aidha, marekebisho ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 na rasimu ya Sera mpya ya Taifa ya Nyumba yako katika hatua ya kukamilisha uchambuzi wa maoni ya wadau kabla ya kuwasilishwa serikalini kwa maamuzi.

75. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa sheria na kanuni za Sekta ya Ardhi zinaakisi hali halisi ya kiuchumi, kijamii na kiteknolojia kwa kuzifanyia marekebisho. Ili kutekeleza azma hiyo, katika mwaka 2021/22, Wizara imefanya marekebisho ya Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi, Na. 2 ya mwaka 2002 kuruhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili katika uendeshaji wa mashauri, uandishi

wa hukumu na kumbukumbu za mashauri. Marekebisho haya ni kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wananchi wanapata haki zao ikiwa ni pamoja na kuelewa hukumu zinazotolewa na mahakama.

76. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/22, Wizara iliahidi kufanya marekebisho ya Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Na. 2 ya mwaka 2002 yanayolenga kubadili mfumo wa ajira za wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi na kuyafanya Mabaraza ya Kata kufanya usuluhishi wa migogoro ya ardhi badala ya kutoa hukumu. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Serikali imefanya marekebisho katika sheria hiyo kwa kurekebisha mfumo wa ajira za Wenyeviti wa Mabaraza kutoka ajira ya mkataba wa miaka mitatu (**3**) na kuwa ajira za kudumu. Mfumo wa ajira za kudumu kwa Wenyeviti wa Mabaraza utaiwezesha Wizara kupata Wenyeviti kutoka miongoni mwa wanasheria wenye sifa waliopo katika Utumishi wa Umma na kuwezesha usimamizi wa maadili ya Wenyeviti wa Mabaraza kwa kutumia Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma. Aidha, kupitia marekebisho haya Mabaraza ya Kata yameondolewa mamlaka ya kufanya maamuzi na yamebaki na mamlaka ya usuluhishi pekee katika mashauri yanayohusu migogoro ya ardhi. Hatua inayofuata ni kuandaa kanuni zinazobainisha utaratibu wa usuluhishi katika Mabaraza ya Kata.

77. ***Mheshimiwa Spika,*** Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.1 ya mwaka 2021 imeelekeza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika sheria zote za nchi. Katika kutekeleza matakwa ya sheria hiyo na maelekezo ya Serikali kwamba sheria zote ziandikwe kwa lugha ya kiswahili; Wizara yangu imefanya mapitio ya sheria 14 za Sekta ya Ardhi na kuandaa tafsiri kwa lugha ya Kiswahili na kuwasilisha Wizara ya Katiba na Sheria kwa mapitio zaidi. Lengo la kufanya tafsiri hiyo ni kuzifanya sheria zetu ziwe rafiki na zieleweke kwa wananchi wengi.

## Utozaji Riba katika Kodi ya Pango la Ardhi

78. ***Mheshimiwa Spika,*** Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 imeweka utaratibu wa kukadiria, kutoza, muda wa kulipa na hatua za kuchukuliwa kwa mmiliki atakayeshindwa kulipa kodi hiyo kwa wakati. Kwa mujibu wa Kifungu cha 33(1) cha Sheria hii, mmiliki wa ardhi anatakiwa kulipa kodi ya pango la ardhi kwa mwaka kama ilivyoainishwa chini ya masharti ya Sheria ya Fedha za Umma.

79. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa muda mrefu kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi yanayotokana na takwa la kisheria la kutoza riba baada ya miezi sita ndani ya mwaka wa fedha ambao kodi ya pango la ardhi inapaswa kulipwa. Ili kuondoa malalamiko hayo, Wizara inakusudia kufanya marekebisho ya Sheria ya Ardhi ili riba ya kuchelewa kulipa kodi ya pango la ardhi ianze kutozwa baada ya kuisha kwa mwaka wa fedha.

80. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2022/23, Wizara itaendelea na maboresho ya sheria za Sekta ya Ardhi ili kongeza usalama wa milki, kuwezesha wananchi wengi kuwa na ardhi iliyopangwa na kupimwa, kuvutia uwekezaji, kuwa na miji iliyopangwa na kuongeza mapato ya Serikali.

## 6. MIRADI YA MAENDELEO

81. ***Mheshimiwa Spika*** ili kuimarisha usalama wa milki, miundombinu ya upimaji na ramani, kudhibiti na kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi, kuimarisha utunzaji wa kumbukumbu za ardhi kwa kutumia mifumo ya TEHAMA, kuimarisha mipaka ya ndani ya nchi ya kiutawala na kimataifa, kuongeza ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali pamoja na kuwawezesha wananchi kiuchumi. Ili kutimiza malengo haya, Wizara itatekeleza miradi ya maendeleo ya kupitia Program ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi,

mradi wa kuboresha miundombinu ya upimaji na ramani na mradi wa kuimarisha usalama wa milki za ardhi.



*Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Ridhiwani Kikwete akikagua vigingi vya alama za mipaka zinazotengenezwa na Halmashauri ya mji Bunda vitakavyotumika katika Mradi wa kupanga,kupima na kumilikisha ardhi.*

82. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi unaendelea ambapo katika mwaka wa fedha 2021/22, Wizara iliidhinishiwa shilingi bilioni **8**. Aidha, Wizara ilipokea shilingi bilioni **50** kwa ajili ya kukopesha Halmashauri na Taasisi kwa ajili ya utekelezaji wa Programu hii. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, kati ya fedha zilizoidhinishwa, Wizara imepokea shilingi bilioni **5.6** hivyo kufanya kuwa na jumla ya shilingi bilioni **55.6** kwa ajili utekelezaji wa Programu. Fedha hizi zimekopeshwa kwenye Halmashauri **92**, Vyuo vya Ardhi vitatu (**3**) na Ofisi ya Ardhi ya Mkoa wa Iringa ili kuwezesha upangaji, upimaji na umilikishaji wa viwanja takriban **373,155.** Vigezo vilivyotumika kutoa mikopo ni pamoja na uwepo wa andiko la mradi linaloonesha uwezo wa kurejesha, historia ya Halmashauri/ Taasisi kwenye urejeshaji wa mikopo, uwepo wa vifaa vya upimaji na

wataalamu na utayari wa Halmashauri/Taasisi husika kwenye utekelezaji wa miradi. Vigezo hivi vitaendelea kuhuishwa na kuboreshwa kwa kuzingatia uzoefu uliopatikana kutokana na utelezaji wa Programu katika Halmashauri mbalimbali.

83. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia programu hii Serikali inatarajia kupata mapato yenye jumla ya shilingi **51,604,155,169 (**baada ya urejeshwaji mkopo) kwa mwaka wa kwanza na kuongeza wigo wa mapato kwa wastani wa kiasi cha shilingi **5,597,325,000** kwa mwaka kwa miaka inayofuata, kupunguza migogoro ya ardhi na kuwapatia wananchi fursa ya kuwa na hati miliki za makazi. Pamoja na jitihada za Serikali za kutoa fedha kwa ajili ya kutekeleza shughuli za Sekta ya Ardhi, Mamlaka za Upangaji zina jukumu la kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kwa mujibu wa Sheria. **Natoa rai kwa Mamlaka za upangaji kuhakikisha kuwa zinatenga fedha asilimia 40 hadi 60 ya faida ya fedha za mkopo kwa ajili ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi kwa kuzingatia Mwongozo wa Madaraja ya Halmashauri uliotolewa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI.**

84. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23 Wizara itaendelea na jukumu la kutambua, kupanga, kupima na kumilikisha vipande vya ardhi kwa ajili ya matumizi mbalimbali kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji na sekta binafsi. Vilevile, itaandaa mipango minne (**4**) ya uendelezaji upya wa maeneo kongwe katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza na Arusha; na Mipango kina mitano (**5**) ya uendelezaji wa visiwa na fukwe kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

85. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na jitihada zinazofanywa na Wizara za kuzikopesha Halmashauri fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi, jitihada hizo bado hazikidhi matarajio katika kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi nchini. Ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi hiyo katika Halmashauri, Wizara

imeanza kuzishirikisha Taasisi za Fedha ili kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wananchi hasa kwenye miradi ya urasimishaji.

**Mradi wa Uboreshaji wa Milki za Ardhi - LTIP**

86. ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa Uboreshaji Milki za Ardhi umesainiwa na Serikali Februari, 2022 na utaanza kutekelezwa na Wizara yangu kwa kushirikiana na Benki ya Dunia katika mwaka 2022/23. Mradi huu utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2022/23 – 2027/28) na unalenga kuimarisha usalama wa milki za ardhi; kuboresha usimamizi wa taarifa za ardhi ikiwemo Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Taarifa za Ardhi (ILMIS); kuimarisha miundombinu ya Upimaji na Ramani; na kujenga majengo ya Ofisi za Ardhi za Mikoa 25.



*Hafla ya utiaji saini mkopo wa kuboresha milki za ardhi nchini wa shilingi Bilioni 345 iliyofanyika jijini Dar es Salaam.*

87. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Wizara imepanga kujenga majengo ya Ofisi za Ardhi za Mikoa **25**; kuboresha mfumo wa ILMIS; kutoa Hatimiliki **150,000** katika Halmashauri **10**; kutoa Hati za Hakimiliki za Kimila **50,000** katika Vijiji **50**; kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji **50** katika Wilaya sita (6) na Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya hizo; na kutoa Leseni za Makazi **250,000**. Katika

utekelezaji wa kazi hizi, Wizara inatarajia kutoa fursa za ajira za muda mfupi **2,300** na vibarua **4,200**.




*Mchoro wa Jengo la Ofisi za Ardhi zinazotarajiwa kujengwa katika mikoa 25 nchini*

**Mradi wa Uimarishaji wa Mipaka ya Kimataifa**

88. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wizara iliahidi kuendelea na uimarishaji wa mipaka ya nchi kavu yenye urefu wa kilometa **100** kati ya Tanzania na Burundi na kilometa **128** kati ya Tanzania na Kenya kwa kushirikiana na mamlaka za Serikali za nchi hizo. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi tarehe 15 Mei, 2022, kilometa **83** za mpaka wa Tanzania na Kenya zimeimarishwa na kazi inaendelea. Pia, ramani za msingi za mpaka kwa kipande cha kilometa **238** kutoka Ziwa Viktoria hadi Ziwa Natron ambazo zitatumika kuandaa Mkataba wa mpaka zimeandaliwa.




*Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Ridhiwani Kikwete akiwa na baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi Maliasili na Utalii katika mpaka wa Tanzania na Kenya ndani ya mbunga ya Serengeti mkoani Mara.*




*Timu ya Wataalam wa upimaji kutoka nchi za Tanzania na Kenya ikiangalia muelekeo wa mpaka wa nchi hizo katika eneo la Serengeti/ Masai Mara.*



*Alama za mpaka wa Kimataifa kati ya Kenya na Tanzania uliopo Serengeti Mkoani Mara*

89. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2022/23, Wizara itaendelea kuimarisha mpaka wa Tanzania na Kenya kutoka Namanga hadi Tarakea wenye urefu wa kilometa **110** pamoja na kuchora ramani za msingi za kipande cha kilometa **110** kutoka Ziwa Natron hadi Namanga. Aidha, Wizara itaendelea na uimarishaji wa sehemu ya mpaka wa Tanzania na Burundi wenye urefu wa kilometa **100** kutoka ukingoni mwa Ziwa Tanganyika (kijiji cha Kagunga) hadi unapoanzia Mto Malagarasi (kijiji cha Manyovu) mkoani Kigoma.

90. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na malengo yaliyopo katika mwaka wa fedha 2022/23, Wizara inatambua umuhimu wa kukamilisha kwa haraka zoezi la uimarishaji wa mipaka ya kimataifa ili kuimarisha mahusiano ya kidiplomasia, ulinzi na usalama, na mahusiano baina ya jamii zinazoishi maeneo ya mipakani. Ili kuongeza kasi na kuhakikisha kwamba kazi ya uimarishaji mipaka inakamilika ifikapo 2027 kama ilivyokubaliwa na Umoja wa Afrika (AU), Serikali inaandaa mkakati utakaowezesha upatikanaji wa rasilimali kwa ajili ya kuimarisha na kuweka miundombinu ya barabara na mawasiliano.

**Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Upimaji na Ramani – NSDI**

91. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wizara ilipanga kuanza utekelezaji wa Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Upimaji na Ramani kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Korea Kusini kupitia Benki ya Exim. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Mradi huu uko katika hatua za mwisho za ukamilishaji wa Hati ya Makubaliano ya Mkopo (Loan Agreement) ambapo Wizara inatarajiwa kupatiwa mkopo wa masharti nafuu wa dola za Kimarekani **milioni 65**. Utekelezaji wa Mradi huu unatarajiwa kuanza katika mwaka 2022/23. Utekelezaji wa mradi huu utawezesha kuongeza kasi ya upangaji na upimaji ardhi, uwezo wa kuandaa ramani za msingi kwa nchi nzima ambazo zinahitajika kwa matumizi mengine hususan ya ujenzi wa miundombinu msingi ya umma.

**Miradi ya Kimkakati ya Kitaifa**

92. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wizara imeendelea kushiriki kikamilifu katika kuwezesha utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati ya Kitaifa. **Miradi hiyo ni Ujenzi wa Bwawa la Kuzalisha Umeme la Julius Nyerere, Ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani - Tanga nchini Tanzania na ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR).**

**Mradi wa Uzalishaji Umeme wa Julius Nyerere**

93. ***Mheshimiwa Spika,*** katika uendelezaji wa eneo la mradi, Wizara inaendelea kuandaa mpango wa uendelezaji wa ukanda wa mradi (Corridor Development Plan) utakaowezesha mamlaka za upangaji kuandaa mipangokina katika miji midogo na mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji katika ukanda huu. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2022 mipangokina mitatu (**3**) yenye viwanja **2,141** iliandaliwa

katika Miji Midogo ya Mloka na Ikwiriri. Vilevile, Vijiji **69** vimeandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo yanayozunguka na kutiririsha maji katika kidakio cha mto Rufiji kwenda katika Bwawa la Ufuaji wa Umeme la Julius Nyerere (JNHPP) katika wilaya ya Mbarali (**14**), Mufindi (**11**) Kilolo (**8**) na Wangingo'mbe (**36**).

**Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa**

94. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushiriki katika utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Reli ya kisasa kutoka Morogoro hadi Makutupora kwa awamu ya pili na Isaka hadi Mwanza awamu ya tano. Usanifu wa michoro ya mipangomiji katika vituo tisa (**9**) vya Dar es Salaam, Soga, Ruvu, Kwala, Morogoro, Kilosa, Chanzulu, Gulwe na Dodoma umekamilika. Aidha, usanifu wa michoro ya mipangomiji katika maeneo ya vituo vya Igandu (Dodoma), Tura (Tabora), Nkalalo (Mwanza), Isaka na Ishololo (Shinyanga) unaendelea. Vilevile, uthamini wa mali umefanyika katika kipande cha kuanzia Morogoro hadi Makutupora ambapo wananchi **1,462** wamefanyiwa uthamini wenye thamani ya shilingi **34,383,421,262** na kipande cha kutoka Isaka hadi Mwanza wananchi **5,846** wamefanyiwa uthamini wenye thamani ya shilingi **20,363,846,496** na kazi ya uthamini inaendelea. Pia, vijiji 22 vimeandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi katika Halmashauri za Wilaya ya Kibaha (**10**), Chamwino (**8**) na Mpwapwa (**4**).

95. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na taasisi nyingine za Serikali inaendelea kufanya maandalizi ya kuandaa Mpango Maalum wa Uendelezaji Kiuchumi Ukanda wa Reli ya Kisasa. Mpango huu utawezesha sekta mtambuka kubainisha mahitaji ya ardhi kwa ajili ya matumizi mbalimbali ili kuleta tija katika ukanda wa reli ya kisasa. Katika mwaka 2022/23 Wizara kwa kushirikiana na Wizara za kisekta itakamilisha kuandaa mipangokina katika maeneo ya miji na

mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo ya vijiji vilivyo katika ukanda wa Reli ya Kisasa.

**Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta**

96. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushiriki katika utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani jijini Tanga. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, Wizara imekamilisha uthamini wa mali katika maeneo **14** ya kipaumbele ya Mradi ambapo wananchi **350** wamefidiwa jumla ya shilingi **1,582,949,599**. Aidha, utwaaji ardhi ya Mkuza wa Bomba la Mafuta wenye urefu wa kilometa **1,147** umekamilika. Vilevile, mipangokina **42** yenye viwanja **21,355** pembezoni mwa Mkuza wa Bomba la Mafuta imeandaliwa. Katika mwaka 2022/2023, Wizara itaendelea na utekelezaji wa shughuli zinazohusiana na sekta ya ardhi kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji katika Mikoa inayopitiwa na Mradi.

## 7. SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

**SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA**

97. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia shughuli za Shirika ambalo pamoja na mambo mengine lina jukumu la kuwezesha ujenzi wa majengo kwa matumizi mbalimbali hususan makazi, ofisi na biashara. Majukumu ya Shirika yanatekelezwa kwa kuzingatia Mpango Mkakati wa Shirika wa Miaka 10 (2015/16 – 2024/25) ambao unalenga kukamilisha miradi ya Shirika iliyo katika hatua mbalimbali; kufanya ukarabati wa majengo ya shirika; kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vya uzalishaji wa vifaa vya ujenzi; kujenga majengo ya biashara na nyumba za gharama nafuu katika maeneo mbalimbali; kuendeleza Miji ya Pembezoni *(Satellite Towns);* na kutekeleza miradi mbalimbali ya ukandarasi.

**Ujenzi wa Nyumba**

98. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Shirika lilipanga kukamilisha Mradi wa Morocco Square Jijini Dar es Salaam. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi tarehe 15 Mei, 2022, utekelezaji wa Mradi umefikia asilimia **93.** Hatua hii imetokana na Serikali kuruhusu Shirika kukopa shilingi bilioni **173.9** ili kukamilisha Mradi huu na miradi mingine iliyokuwa imesimama tangu mwaka 2018 kwa kukosa fedha. Mpaka sasa Shirika limekopa shilingi bilioni **44.7** kati ya fedha hizo kwa ajili ya kukamilisha Miradi ya *Morocco Square* na Kiwanja Na. 300 *Regent Estate*.



*Maendeleo ya Ujenzi wa Mradi wa Morocco Square unaotekelezwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC)*

99. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Shirika lilipanga kuanza ujenzi wa nyumba za gharama nafuu katika Halmashauri za Sumbawanga pamoja na kuendeleza Miji midogo ndani ya Mji Mkubwa *(Satellite Towns)* ya Uvumba (Kigamboni), Kawe (Kinondoni), Burka/Matevesi (Arusha Jiji) na eneo la *Usa River* (Meru). Napenda kuliarifu Bunge lako kuwa Shirika liko katika hatua za ukamilishaji wa taratibu za umiliki na upembuzi yakinifu katika eneo la Luguruni. Aidha, uendelezaji wa Miji Midogo ndani ya Miji Mikubwa uko katika

hatua mbalimbali ambapo kwa eneo la Kawe, uandaaji wa michoro ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu unaendelea. Vilevile, upembuzi yakinifu unaendelea ili kuanza utekelezaji wa Mpango Kabambe wa eneo la Uvumba. Katika eneo la Burka/Mateves uandaaji wa Mpango Kabambe umekamilika na uuzaji wa viwanja katika sehemu ya eneo hilo unaendelea. Aidha, Mpango wa ujenzi wa nyumba za awali unaendelea katika eneo la *Usa River*.



*Maendeleo ya mradi wa Ujenzi wa (Satellite Town) Kawe jijini Dar es salaam*



*Ujenzi wa nyumba za gharama nafuu katika Halmashauri za Sumbawanga*

100. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Shirika lilipanga kuendelea na ujenzi wa nyumba katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino (**101**) na Jiji la Dodoma (Iyumbu - **303**) kwa ajili ya kupangisha na kuuza ikiwa ni utekelezaji wa mradi wa nyumba **1,000**. Napenda kuliarifu Bunge lako kuwa hadi tarehe 15 Mei, 2022, ujenzi wa nyumba **100** na jengo la maduka katika Wilaya ya Chamwino umekamilika kwa asilimia **80** na ujenzi wa nyumba **300** na majengo matatu (**3**) ya huduma za kijamii katika Jiji la Dodoma (Iyumbu) umekamilika kwa asilimia **90**.



*Ujenzi wa nyumba za Iyumbu-Dodoma*

101. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Shirika lilipanga kuendelea na ujenzi wa majengo ya biashara katika Halmashauri za Manispaa za Lindi na Bukoba pamoja na kutekeleza miradi ya ukandarasi katika maeneo mbalimbali nchini. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, usanifu wa jengo la biashara katika Halmashauri ya Manispaa ya Lindi umekamilika na marekebisho ya michoro yanaendelea kufanyika ili kuendana na taarifa ya uchunguzi wa udongo. Aidha, usanifu wa jengo la biashara katika Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba umefanyika na taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata mkandarasi zinaendelea. Kuhusu utekelezaji wa Miradi ya ukandarasi; Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa Mwalimu Nyerere (Mara) Awamu ya IV umekamilika kwa asilimia **96** na Mradi wa ujenzi wa Soko la Kimataifa la Mifugo la Buzirayombo (Geita) umekamilika kwa asilimia **94**. Vilevile, Shirika linaendelea na mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Rais, Muungano na Mazingira kama Mshauri Elekezi. Pia, mapitio

ya michoro na gharama za Mradi wa ujenzi wa majengo ya Wizara ya Fedha na Mipango katika eneo la Mji wa Serikali – Mtumba yamefanyika.

**Uandaaji wa Mipango Kabambe**

102. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na utekelezaji wa miradi mbalimbali, katika mwaka 2021/22, Shirika lilipanga kuandaa mipango ya uendelezaji wa maeneo mbalimbali nchini pamoja na kutekeleza Mpango wa Uendelezaji wa maeneo ya Chuo Kikuu cha Dodoma (Institutional master 76 plan) ambao unahusisha utekelezaji wa Muundo Jumuishi (Integrated System) wa TEHAMA. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, Shirika lilishiriki katika uandaaji wa Mipango Kabambe ya Uendelezaji wa maeneo ya Kwala (Pwani) na Mji wa Tanzanite wa Mirerani (Manyara). Aidha, uandaaji wa Mpangokina kwa ajili ya uendelezaji wa maeneo ya Chuo Kikuu cha Dodoma unaendelea.

**Ujenzi wa Viwanda vya Vifaa vya Ujenzi**

103. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kutimiza azma ya kujenga nyumba za gharama nafuu nchini hususan kwa ajili ya wananchi wa kipato cha chini, Shirika limeanza kutekeleza mpango wa kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vya kutengeneza vifaa vya ujenzi hususan kokoto, matofali na mabati. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, Shirika limenunua maeneo kwa ajili ya uchimbaji mchanga na uzalishaji wa kokoto pamoja na kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kupata idhini ya utekelezaji wa miradi hiyo. Mpango wa Shirika ni kuhakikisha viwanda vya uzalishaji wa vifaa vya ujenzi vinaanza kufanya kazi mwaka 2022/23. Ukusanyaji wa Mapato

104. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Shirika lilipanga kukusanya shilingi bilioni 105.6 kutokana na kodi ya pango. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, Shirika limekusanya shilingi

bilioni 76.22 sawa na asilimia 72.1 ya lengo. Matarajio ya Shirika ni kufikia lengo hilo ifikapo Juni, 2022.

**Ukarabati wa Nyumba**

105. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na utekelezaji wa miradi ya ujenzi, Shirika limeendelea kufanya ukarabati wa nyumba zake kupitia Mpango wa Ukarabati unaoendelea kutekelezwa katika mikoa mbalimbali nchini. Ili kuhakikisha kwamba kazi hii inatekelezwa kwa ufanisi, katika mwaka 2021/22, Shirika lilitenga shilingi bilioni nane (**8**) kwa ajili ya ukarabati wa nyumba **350**. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, shilingi bilioni tatu (**3**) zimetumika kukarabati nyumba **53** katika mikoa ya Kilimanjaro, Dar es Salaam na Katavi. Katika mwaka 2022/23, Shirika litakarabati nyumba **180** katika mikoa ya Dar es Salaam, Iringa, Tabora, Arusha, Kigoma, Morogoro, Lindi, Tanga, Mbeya, Mwanza, Singida na Kagera kwa gharama ya shilingi bilioni nane (**8**).

106. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Shirika limepanga kutekeleza kazi zifuatazo: -

i) Kukusanya shilingi bilioni **268.03** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato;

ii) Kuendelea kukamilisha mradi wa ujenzi wa nyumba 300 kati ya nyumba 1,000 za gharama nafuu Jijini Dodoma kwa ajili ya kuuza na kupangisha;

iii) Kukamilisha ujenzi wa Mradi wa Morocco square na kuendelea na Miradi katika Kiwanja Na. 711 Kawe, Golden Premier (GPR-Project) na ujenzi wa nyumba 500 katika eneo la Kawe kwa ajili ya wananchi wa kipato cha kati cha chini ambapo nyumba 360 zitajengwa awamu ya kwanza na nyumba 140 zitajengwa awamu ya pili;

iv) Kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa michoro katika miji ya pembezoni (Satellite Cities) ya Kwala – Ruvu, Mbezi One Riffle Range (Dar es Salaam) na Kawe;

v) Kuendelea na ujenzi wa majengo ya biashara katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Bukoba, Mwanza, Dodoma, Kahama, Morogoro, Masasi na Lindi;

vi) Kuandaa Mpango Kabambe wa matumizi ya ardhi katika maeneo ya Iwambi na Mwashiwawala – Mbeya, Uvumba – Dar es Salaam na Mafuru Village - Morogoro;

vii) Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya ukandarasi ikiwemo ujenzi wa Majengo ya Ofisi za Wizara nane (8) Jijini Dodoma, ujenzi wa Jengo la Shule ya Uchumi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Ujenzi wa majengo matano (5) ya Wakala wa Ununuzi wa Serikali (GPSA), ujenzi wa jengo la TANZANITE Mirerani, ujenzi wa Jengo la Kitengo cha Moyo cha Jakaya Kikwete (JKCI) na miradi mingine itakayojitokeza;

viii) Kuendelea na usimamizi wa miradi mbalimbali ya kimkakati ikiwemo Soko la Kariakoo;

ix) Kuendelea kutekeleza Mpango wa miaka mitano wa ukarabati wa nyumba za Shirika unaoishia mwaka 2027;

x) Kununua ardhi ekari 400 katika maeneo mbalimbali ya kimkakati kwa ajili ya ujenzi wa nyumba na akiba ya ardhi;

xi) Kuanza utekelezaji wa Sera ya Ubia itakayoruhusu Sekta Binafsi kushiriki katika uendelezaji wa maeneo ya Shirika;

xii) Kuendelea na ujenzi wa viwanda vya kuzalisha vifaa vya ujenzi hususan kokoto na matofali; na xiii) Kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya nyumba na kulitangaza Shirika na Sekta ya Milki nchini kupitia vyombo vya habari.

**Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi**

107. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria ya Upangaji wa Matumizi ya Ardhi, Na.6 ya mwaka 2007, Mpango wa Matumizi ya Ardhi wa Taifa (2013 - 2033), Mpango wa III wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26) na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2020 - 2025). Majukumu hayo ni pamoja na kuandaa, kuratibu, kuwezesha na kusimamia mipango ya matumizi ya ardhi kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji na wadau mbalimbali nchini. Mipango hii inawezesha kutenga maeneo kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya ardhi ikiwemo makazi, kilimo, nyanda za malisho, uwekezaji, uhifadhi, ardhi ya akiba na mapito ya wanyamapori. Mipango hiyo inawezesha kudhibiti migogoro ya ardhi, kulinda ikolojia na mazingira, kutoa milki salama kwa wananchi na hivyo kuongeza tija katika matumizi ya ardhi, uzalishaji mali na kuinua uchumi wa jamii na Taifa.



*Bango linaloonyesha moja ya eneo lillotengwa kwa ajili ya Uhifadhi lililosimikwa mara baada ya kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji cha Igandu Wilayani Chamwino likionyesha kupiga marufuku shughuli yoyote katika eneo hilo*

108. ***Mheshimiwa spika,*** Ardhi ni rasilimali muhimu inayopaswa kupangwa na kulindwa kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vijavyo. Azma hii itafikiwa kwa kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi katika ngazi ya Taifa, Kanda, Wilaya na Vijiji. Uandaaji wa mipango katika ngazi hizi unajumuisha kutenga maeneo kwa matumizi mbalimbali, upimaji wa mipaka ya Vijiji, utatuzi wa migogoro ya mipaka na matumizi ya ardhi, utoaji wa elimu kwa Mamlaka za Upangaji, utoaji wa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji na utoaji wa Hati za Hakimiliki za Kimila.



*Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi Maliasili na Utalii Ally Makoa akitoa hati kwa mkazi wa kijiji cha Ntondo mkoani Singida wakati wa ziara ya kamati hiyo ya kukagua mradi wa mipango ya matumizi ya ardhi tarehe 15 Machi 2022.*

109. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na kuratibu uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya ardhi, Tume ina jukumu la kufanya tafiti, kuimarisha mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu za Mipango ya Matumizi ya Ardhi, kuratibu shughuli za Wadau, kufanya tathmini na ufuatiliaji wa mipango ya matumizi ya ardhi na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimkakati ikiwemo ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), Reli ya Kisasa (SGR) na Bwawa la Julius Nyerere (JNHPP).

**Uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ngazi ya Wilaya**

110. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Tume kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji na wadau wa kimkakati ilipanga kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya Wilaya tatu (**3**). Hadi tarehe 15 Mei, 2022, Tume imeandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya mbili (**2**) katika Halmashauri ya Tanganyika (Katavi) na Uvinza (Kigoma). Mipango hii imefanya kuwa na Wilaya **44** zenye mipango ya matumizi ya ardhi nchini. Katika mwaka 2022/23, Tume imepanga kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika Wilaya nne (**4**) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

**Uwezeshaji wa Mamlaka za Upangaji**

111. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ina jukumu la kuziwezesha na kuzijengea uwezo Mamlaka za Upangaji katika kuandaa, kupanga, kutekeleza na kusimamia mipango ya matumizi ya ardhi nchini. Katika mwaka 2021/22, Tume ilipanga kuziwezesha na kuzijengea uwezo Timu Shirikishi za Upangaji wa Matumizi ya Ardhi za Halmashauri za Wilaya **20**, Wajumbe **3,420** wa Halmashauri za Vijiji **171**, Wajumbe **1,368** wa Kamati za Usimamizi wa Matumizi ya Ardhi, Wajumbe **1,197** wa Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji pamoja na kutoa miongozo na elimu kwa umma kuhusu masuala ya sheria, kanuni na taratibu za upangaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi.



*Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Dkt Angeline Mabula akipata maelezo kutoka kwa mwenyekiti wa kamati ya uhifadhi wa mazingira Mufindi mkoani Iringa Waston Mkane alipokwenda kukagua Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi kwenye eneo la chanzo cha maji cha mpogolo kijiji cha Idetelo kata ya Mbalamaziwa wilayani Mufindi mkoani Iringa.*

112. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi tarehe 15 Mei, 2022, Tume imeziwezesha na kuzijengea uwezo Timu Shirikishi za Upangaji wa Matumizi ya Ardhi za Halmashauri za Wilaya **31** zenye wajumbe **248**, wajumbe **4,640** kutoka Halmashauri za Vijiji **232**, wajumbe **1,856** wa Kamati za Usimamizi wa Matumizi ya Ardhi na wajumbe **1,624** wa Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji. Aidha, Tume imehuisha Mwongozo wa Uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi katika ngazi mbalimbali ili kujumuisha hatua ya utoaji wa Hati za Hakimiliki za Kimila. Pia, elimu kwa umma imetolewa kupitia vyombo mbalimbali vya habari ambapo vipindi **43** vimerushwa kupitia luninga, redio, magazeti na mitandao ya kijamii.



*Wananchi wa Kijiji cha Nyichoka kilichopo Wilaya ya Serengeti Mkoani Mara wakiwa kwenye Mkutano Mkuu wa kijiji kwa ajili ya kujadili na kupitisha mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji chao ambao umewasilishwa kwao na Kamati ya Usimamizi wa Mpango wa Matumzi ya Ardhi ya Kijiji (VLUMC) kwa kushirikiana na Halmashauri ya Kijiji ya kijiji hicho.*

113. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume imeziwezesha Halmashauri mbalimbali za Wilaya kwa kuzipatia mafunzo kuhusu matumizi ya teknolojia rahisi na ya kisasa ya uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, Tume imeziwezesha Halmashauri za Wilaya **31** kutumia picha za anga na simu janja (Satelite image na smartphone) katika utambuzi wa maeneo wakati wa kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi. Teknolojia hii imewezesha kupunguza muda wa kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi kutoka siku **25** hadi wastani wa siku **15** kwa kijiji. Halmashauri hizi ni pamoja na Kigoma, Songea, Uvinza, Ikungi, Singida, Sumbawanga, Nkasi, Mbeya, Kalambo, Mufindi, Wanging'ombe, Mbarali, Kibaha, Kilolo, Chamwino, Mpwapwa, Namtumbo, Ruangwa, Tunduru, Kilindi, Nachingwea, Mbinga, Njombe, Ludewa, Mwanga, Same, Nyasa, Liwale, Butiama, Kilosa na Chalinze.



*Baadhi ya wananchi wa kijiji cha Lumage wilayani Makete wakishiriki zoezi la uandaaji wa mpango wa matumizi ya ardhi kwa kutumia picha ya anga (satellite image)*

**Uwezeshaji na Uratibu wa Uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji**

114. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume imeendelea kuwezesha na kuratibu Mamlaka za Upangaji na Wadau mbalimbali katika uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji. Katika mwaka 2021/22, Tume ilipanga kuwezesha Mamlaka za Upangaji na wadau mbalimbali kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya vijiji **171**. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, Tume **87** imewezesha na kuratibu uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya vijiji **232** ambapo **141** imeandaliwa kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na wadau 91 imeandaliwa kupitia miradi ya kimkakati ya EACOP, SGR na JNHPP **(Jedwali Na. 12A & 12B)**. Hivyo, vijiji vyenye mipango ya matumizi ya ardhi vimeongezeka kutoka **2,347** mwaka 2020/21 hadi **2,579** mwaka 2021/22.

115. ***Mheshimiwa Spika****;* Serikali inatambua uwepo wa wadau wanao shirikiana na Tume na Mamlaka zingine za Upangaji katika kuwezesha Uandaaji wa Mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Aidha, changamoto

inayoonekana ni kwa wadau hawa kutofikia hatua ya kuandaa mipango kina ya matumizi ya Ardhi inayowezesha utoaji wa Hati Miliki za Kimila na Upangaji wa maeneo ya Vijiji. Vilevile, Wadau wengi kuwa na malengo yasiyoakisi matakwa halisi ya Wananchi ya kuwainua kiuchumi na miliki salama ili kutimiza malengo ya Serikali ya kuwezesha Wananchi kiuchumi kupitia rasimali ardhi. **Natoa rai kwa wadau na Mamlaka za Upangaji zinazohusika uandaaji, usimamizi na utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi katika ngazi ya Taifa, Kanda, Wilaya na Vijiji kuzingatia Miongozo ya Serikali na Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka mitano (2021/22 – 2025/26) unaolenga pamoja na mambo mengine kuwezesha wananchi kiuchumi, Kijamii na kuwa na Milki salama.**

116. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume imeendelea kuwezesha Mamlaka za Upangaji kutenga maeneo kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya ardhi, upimaji wa mipaka ya Vijiji, utoaji wa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji na Hati za Hakimiliki za Kimila katika vijiji **232** katika Halmashauri **31** nchini. Jumla ya ardhi yenye ukubwa wa hekta **487,634** imetengwa kwa ajili ya kilimo, hekta **137,404.37** kwa ajili ya nyanda za malisho, hekta **254,366.59** kwa ajili ya makazi na kilimo na hekta **28,666.10** kwa ajili ya ardhi ya akiba ikiwemo uwekezaji. Katika mwaka 2022/23, Tume kwa kushirikiana na wadau itaendelea kuwezesha uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji **200** katika Mamlaka mbalimbali za upangaji nchini.

117. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na umuhimu wa vijiji vyote nchini kuwa na Mipango ya Matumizi ya Ardhi upo umuhimu kwa Mamlaka za Upangaji kutenga fedha kila mwaka za kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya na Vijiji. Utaratibu huo utawezesha kuongeza kasi ya uaandaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi nchini. **Natoa rai kwa Halmashauri zote za wilaya nchini, kuhakikisha zinatenga**

**fedha kwa ajili ya kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi.**

**Tafiti**

118. ***Mheshimiwa Spika,*** Tafiti ni nyenzo muhimu ya kuleta maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla. Katika mwaka 2021/22, Tume ilipanga kufanya tafiti na kusambaza matokeo ya tafiti kwa wadau. Napenda kuliarifu Bunge lako kuwa hadi tarehe 15 Mei, 2022, Tume imefanya utafiti kuhusu utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi katika Halmashauri **10** za Karatu, Longido, Chamwino, Chemba, Uyui, Nzega, Magu, Bunda, Kilombero na Mvomero. Matokeo ya utafiti huo yameonesha kuwa maeneo yenye mipango ya matumizi ya ardhi inayotekelezwa ipasavyo yana migogoro ya ardhi michache ikilinganishwa na maeneo yasiyo na mipango. Aidha, utafiti umebaini kuwa baadhi ya Mamlaka za Upangaji pamoja na wananchi hawazingatii mipango hii suala linalohitaji elimu zaidi. Katika mwaka 2022/23, Tume kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali imepanga kufanya tafiti kuhusu Ukuaji wa Miji na athari zake kwa Maendeleo ya Vijiji katika Halmashauri mbalimbali nchini.

**Uimarishaji wa Mfumo wa Utunzaji wa Kumbukumbu za Mipango ya Matumizi ya Ardhi**

119. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume, imeendelea kuboresha na kusimamia Mfumo wa Taifa wa Taarifa za Matumizi ya Ardhi (NLUIS) ili kuwezesha maandalizi ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi na utunzaji wa kumbukumbu. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, Mfumo umeboreshwa na kuwezesha kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji kwa kutumia teknolojia ya kisasa inayotumia vishikwambi na simu janja. Aidha, Mwongozo wa Watumiaji wa Mfumo umeandaliwa na mafunzo kwa watumishi wa Tume yametolewa ili kwenda kuzijengea uwezo wa kutumia mfumo Mamlaka za Upangaji ili kupunguza gharama za uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi.

Katika mwaka 2022/23, Tume itaendelea kukusanya, kuchakata na kuhifadhi kwenye Mfumo wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi takwimu za mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **800**.

**Ufuatiliaji na Tathmini ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi**

120. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume, imeendelea kutekeleza jukumu la Ufuatiliaji na Tathmini ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi inayoandaliwa na Mamlaka za Upangaji na Wadau mbalimbali nchini. Katika mwaka 2021/22, Tume ilipanga kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **200** na Wilaya mbili (**2**). Hadi tarehe 15 Mei, 2022, vijiji **45** vimefanyiwa ufuatiliaji na tathmini. Katika mwaka 2022/23, Tume itafanya ufuatiliaji na tathmini katika vijiji **210** kwa kushirikiana na wadau. Vilevile, Tume itaendelea kuzijengea uwezo Mamlaka za Upangaji katika uandaaji, utekelezaji, usimamizi na uzingatiaji wa mipango ya matumizi ya ardhi na kutoa elimu kwa umma kwa kuzingatia sheria, miongozo na taratibu.

**Vyuo vya Ardhi**

121. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inasimamia Vyuo vya Ardhi Morogoro (ARIMO) na Tabora (ARITA). Vyuo hivi vinatoa mafunzo ngazi ya Astashahada na Stashahada katika fani za Mipangomiji; Upimaji Ardhi; Urasimu Ramani; Ubunifu na Uchapishaji; na Usimamizi wa Ardhi, Uthamini na Usajili. Katika mwaka 2021/22, Wizara iliahidi kudahili jumla ya wanafunzi **2,200** ambapo Chuo cha Ardhi Tabora wanafunzi **1,600** na Chuo cha Ardhi Morogoro wanafunzi **600**. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, Chuo cha Ardhi Tabora kilidahili wanafunzi **1,250** na Chuo cha Ardhi Morogoro wanafunzi **476**. Katika mwaka 2022/23 Chuo cha Ardhi Tabora kitadahili wanafunzi **1,600** na Chuo cha Ardhi Morogoro wanafunzi **700**. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara iliahidi kufanya mapitio ya sheria na miundo ya Vyuo vya ARITA na ARIMO ili kuboresha usimamizi

na utendaji kazi. Hatua iliyofikiwa ni kupokea maoni ya wadau ili kuboresha Rasimu ya Sheria itakayoimarisha usimamizi na utendaji wa vyuo hivyo.

**Bodi za Usajili wa Wataalam wa Fani za Ardhi**

122. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inasimamia shughuli za Bodi mbalimbali za Wataalam wa Sekta ya Ardhi ambazo ni Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji, Bodi ya Usajili wa Wathamini na Baraza la Taifa la Wapima Ardhi. Majukumu ya Bodi hizi ni kusajili wataalam wa sekta na kampuni za kitaalam, kusimamia weledi wa wataalam na kutoa adhabu kwa ukiukwaji wa maadili ya kitaaluma.

**Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji**

123. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Bodi iliahidi kusajili wataalam **50** na kampuni **10**. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, wataalam **62** na kampuni nne (**4**) zimesajili hivyo kuwa na jumla ya wataalam **455** na kampuni **81** zilizosajiliwa. Aidha, Bodi inachunguza kampuni mbili (**2**) chini ya Kamati ya Kusimamia sheria kutokana na ukiukaji wa maadili na masharti ya taaluma. Vilevile, Bodi imemfutia usajili mtaalam mmoja (**1**) kutokana na ukiukaji wa maadili na masharti ya taaluma.

**Bodi ya Usajili wa Wathamini**

124. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/22, Bodi ya Usajili wa Wathamini imesajili wathamini wa ngazi ya kudumu **123**, ngazi ya awali **71**, wathamini wasaidizi **12**, kampuni mbili (**2**) za uthamini na hivyo kufanya wathamini wa ngazi ya kudumu kufikia **238**, wathamini wa ngazi ya awali **663**, wathamini wasaidizi **57** na kampuni za uthamini **52**. Aidha, Bodi imetoza faini kampuni sita (**6**), imetoa onyo kwa kampuni nne (**4**) na kusitisha leseni kwa muda wa miezi sita (**6**) kwa wathamini wawili (**2**) kutokana na kukiuka maadili ya taaluma.



*Baadhi ya Wahitimu wa Mafunzo ya Usajili wa Kudumu wa Uthamini kwa mwaka 2022.*

**Baraza la Taifa la Wapima Ardhi**

125. ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza la Taifa la Wapima Ardhi linasimamia taaluma ya Wataalam wa Upimaji Ardhi. Katika mwaka 2021/22, Baraza limesajili Wapima Ardhi **50** na kutoa usajili wa muda kwa Wapima Ardhi **20**. Aidha, Baraza limetoa leseni za kufanya kazi kwa Wapima Ardhi **15** na kuzitambua kampuni **10** za upimaji.

**8. MASUALA MTAMBUKA**

**Utawala na Rasilimali Watu**

126. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa huduma za utawala na kusimamia rasilimali watu kwa madhumuni ya kuboresha utendaji kazi unaolenga kuongeza tija na ufanisi katika Wizara, Ofisi za Ardhi za Mikoa na Halmashauri. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, Wizara ina jumla ya watumishi **2,381** ambapo wa sekta ya ardhi ni **1,797** ikilinganishwa na watumishi **5,028** wa sekta Ardhi wanaohitajika **(Jedwali Na. 13A).** Aidha, Wizara imeajiri watumishi **64** ili kujaza nafasi zilizoachwa wazi kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo watumishi kufariki, kustaafu, kufukuzwa au kuacha kazi.

Vilevile, Taasisi zilizo chini ya Wizara zina watumishi **607**, ikilinganishwa na mahitaji ya watumishi **1,121 (Jedwali Na. 13B)**.

**Utawala Bora na Uwajibikaji**

127. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatambua umuhimu wa kuimarisha mifumo ya utawala bora, uwajibikaji na kudhibiti ukiukwaji wa maadili kwa watumishi wa sekta ya Ardhi. Katika kutekeleza dhamira hiyo, Wizara imeendelea kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi wanaokiuka maadili ya utumishi wa umma. Aidha, Wizara inayo Kamati ya Kuthibiti Uadilifu yenye lengo la kusimamia maadili ya watumishi pamoja na viashiria vya rushwa. Katika mwaka 2022/23, Wizara itaanzisha Mfumo wa Usimamizi wa Sekta ya Ardhi (Land Governance Framework) ambao utaongeza uwajibikaji, uwazi na ufanisi katika kutoa huduma za sekta na itaendelea kusimamia utekelezaji wa ahadi zilizoainishwa kwenye Mkataba wa Huduma kwa Mteja kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

128. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wizara imeendelea na utekelezaji wa mikakati ya kuimarisha masuala ya utawala bora na maadili kwa watumishi ikiwa ni pamoja na kushughulikia viashiria vya rushwa katika sekta ya ardhi kupitia Kamati ya Kudhibiti Uadilifu pamoja na kushirikisha wadau mbalimbali. Aidha, Wizara imeendelea kuimarisha madawati ya kushughulikia malalamiko katika Ofisi za Ardhi za Mikoa pamoja na Kituo cha Mawasiliano kwa Mteja kilichopo Makao Makuu ya Wizara. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, elimu kuhusu utawala bora na mapambano dhidi ya rushwa imetolewa kwa makundi mbalimbali ya watumishi ikiwemo Wasajili na Wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya na Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara. Aidha, baadhi ya watumishi wamepata mafunzo ya muda mfupi katika Chuo cha Ulinzi cha Taifa. Vilevile,

watumishi **46** wamechukuliwa hatua mbalimbali za kinidhamu kutokana na kukiuka maadili ya utumishi wa umma.

**Stahili na Mafunzo kwa Watumishi**

129. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wizara iliahidi kutoa mafunzo kwa watumishi **700** kwa kuzingatia mahitaji na Mpango wa Mafunzo wa Wizara. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, Wizara imewezesha utoaji wa mafunzo kwa watumishi **415**. Kati ya hao, watumishi **332** walipatiwa mafunzo ya muda mfupi na watumishi **83** walipatiwa mafunzo ya muda mrefu. Aidha, katika kipindi hicho, watumishi **714** walipandishwa madaraja na **64** walibadilishwa kada. Pia, watumishi **396** walilipwa stahili zao ambapo **274** walilipwa stahili ya likizo, **107** walilipwa stahili ya uhamisho na misiba **15** ya watumishi na wategemezi ilihudumiwa. Katika mwaka 2022/23, Wizara itaendelea kuwezesha utoaji wa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa kuzingatia mahitaji yaliyopo kwenye mpango wa mafunzo, kutoa stahili mbalimbali, kuhamasisha watumishi kupima afya kujilinda na kuzingatia kanuni za afya ya magonjwa ambukizi ikiwemo UVIKO 19 na kutoa lishe kwa watumishi wanaoishi na Virusi vya UKIMWI.



*Baadhi ya Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi wakiwa na Naibu Waziri wa Ardhi Mhe. Ridhiwani Kikwete baada ya kikao cha Baraza hilo jijini Dodoma tarehe 21 Aprili 2022.*

## Habari na Elimu kwa Umma

130. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wizara iliahidi kuendelea na utaratibu wa utoaji elimu kuhusu masuala ya Sekta ya Ardhi. Napenda kuliarifu Bunge lako kuwa, hadi tarehe 15 Mei, 2022, Wizara iliandaa na kusambaza nakala **23,830** za vipeperushi vyenye jumbe za kuelimisha umma kuhusu huduma zinazotolewa na sekta ya ardhi na nakala **7,500** za machapisho mengine kuhusu shughuli za Sekta ya Ardhi. Aidha, vipindi na matangazo **132** ya luninga na **89** vya redio **98** kuhusu shughuli za Wizara viliandaliwa na kutangazwa.

131. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuelimisha wananchi kupitia mitandao ya kijamii ikiwemo facebook, instagram, youtube na twitter. Hadi tarehe 15 Mei, 2022, Wizara ilitoa taarifa **561** kwenye mitandao ya kijamii na tovuti. Pia, makala **462** za elimu kuhusu masuala ya Sekta ya Ardhi ziliandaliwa, kuchapishwa na kusambazwa kwa wadau. Kwa mwaka 2022/23, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala mbalimbali ya Sekta ya Ardhi.

## 9. SHUKRANI

132. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kumalizia hotuba yangu kwa kumshukuru tena Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo mahsusi kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara pamoja na Serikali kwa ujumla. Aidha, nawashukuru Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo na ushauri katika kuimarisha usimamizi wa shughuli za Sekta ya Ardhi. Vilevile, namshukuru Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo na maelekezo ya mara kwa mara yaliyowezesha kuboresha utendaji wa Wizara.

133. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee nakushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri na uongozi thabiti katika kusimamia shughuli za Bunge. Kadhalika, naishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii inayoongozwa na Mwenyekiti Mhe. Ally Juma Makoa (Mb.) na Makamu Mwenyekiti Mhe. Shabani Omary Shekilindi (Mb.) na Wajumbe wa Kamati kwa maoni na ushauri wanaotoa katika kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu. Aidha, nawashukuru kwa dhati Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na Makatibu Wakuu kutoka katika Wizara mbalimbali tulioshirikiana katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali. Napenda pia kuwashukuru Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge na Wabunge wote kwa michango, maoni na ushauri wenu.

134. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kwa umuhimu wa pekee kutambua mchango wa viongozi wenzangu katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Ninamshukuru Naibu Waziri, Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete (Mb.), kwa kunisaidia katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa Katibu Mkuu Dkt. Allan H. Kijazi, Naibu Katibu Mkuu Bw. Nicholas M. Mkapa, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Prof. Wakuru Magigi, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Taifa la Nyumba Bw. Nehemiah Kyando Mchechu, Kamishna wa Ardhi Bw. Nathaniel Mathew Nhonge, Mkuu wa Chuo cha Ardhi Tabora Bw. Biseko Musiba na Mkuu wa Chuo cha Ardhi Morogoro Bw. Huruma Lugalla kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Taasisi zake.

135. ***Mheshimiwa Spika,*** Vilevile, napenda kuwashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo pamoja na watumishi wote wa Wizara, kwa kuendelea kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Vilevile, nawashukuru Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya kwa kazi kubwa ya utatuzi wa migogoro ya ardhi

wanayoifanya hususan kwa kutenga siku maalum ya kusikiliza wananchi wenye changamoto za migogoro ya ardhi.

136. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, napenda kuwashukuru wadau wote wa Sekta ya Ardhi wanaojumuisha Mamlaka za Serikali za Mitaa, sekta binafsi, Bodi za Kitaaluma, Kamati za Ugawaji Ardhi, washirika wa maendeleo wa ndani na nje na wananchi kwa michango yao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Tunatambua na kuthamini michango yenu katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu yetu kwa maslahi ya wananchi na Taifa.

## 10. HITIMISHO

137. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika mwaka 2022/23, Wizara itaendelea kufanya mageuzi kwa kuboresha huduma zinazotolewa katika Sekta ya Ardhi kwa kuendelea kuwekeza katika matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika utoaji wa huduma na pia kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi pamoja na udhibiti wa migogoro ya matumizi ya ardhi. Mageuzi haya yanalenga kuwapunguzia wananchi gharama, kuimarisha usalama wa milki za ardhi pamoja na kuongeza thamani ya ardhi na hivyo kukuza kipato cha mwananchi mmoja mmoja na pato la Taifa.

## 11. MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23

138. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Wizara inatarajia kukusanya shilingi **bilioni 250.1** kutokana na maduhuli ya Sekta ya Ardhi kwa kutekeleza mikakati ambayo imeainishwa katika hotuba hii. Aidha, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu **48**) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **03**) kama ifuatavyo: -

***Fungu 48: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo Makazi***

| | MAPATO | SHILINGI |
|---|---|---|
| A | Mapato ya Serikali | **250,100,000,000** |
| | **MATUMIZI** | |
| B | Matumizi ya Kawaida: | |
| | Mishahara | 44,383,797,000.00 |
| | Matumizi Mengineyo | 33,918,651,000.00 |
| | **Jumla Ndogo** | **78,302,448,000.00** |
| C | Matumizi ya Maendeleo: | |
| | Fedha za Ndani | 14,006,000,000.00 |
| | Fedha za Nje | 13,147,322,000.00 |
| | **Jumla Ndogo** | **27,153,322,000.00** |
| | **JUMLA MATUMIZI (B+C)** | **105,455,770,000.00** |

Jumla ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya Fungu 48 ni shilingi 105,455,770,000/=.

***Fungu Na. 03: Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi.***

| **Aina ya Bajeti** | | | **2022/23 (Shs)** |
|---|---|---|---|
| **1. Mapato** | | | 4,873,704,000 |
| **JUMLA YA MAPATO** | | | 4,873,704,000 |
| **2. Matumizi ya Kawaida** | Mishahara | PE | 1,977,882,000 |
| | **Jumla ya Mshahara** | | **1,977,882,000** |
| | Matumizi Mengineyo | OC | 1,479,822,000 |
| | **Jumla ya Matumizi Mengineyo** | | **1,479,822,000** |
| **JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA** | | | **3,457,704,000** |
| **3. Matumizi ya Maendeleo** | | Ndani | 1,410,000,000 |
| | | Nje | 0 |
| **JUMLA YA MATUMIZI YA MAENDELEO** | | | **1,410,000,000** |
| **JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MATUMIZI YA MAENDELEO** | | | **4,867,704,000** |

Jumla ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya Fungu **03** ni shilingi **4,867,704,000/=.**

139. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla kuu ya fedha zinazoombwa na Wizara (Fungu **48** na Fungu **03**) ili Bunge liweze kujadili na kuidhinisha ni shilingi **110,323,474,000/=**

140. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kuhitimisha hotuba yangu kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa

Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Pamoja na hotuba hii yameambatishwa majedwali ambayo yameainisha kwa kina takwimu pamoja na shughuli zilizotekelezwa. Aidha, hotuba hii inapatikana kwenye tovuti ya Wizara ambayo ni *www.lands.go.tz.*

141. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Sasa nimwite Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Ali Juma Makoa. *(Makofi)*

**MHE. ALI J. MAKOA - KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba taarifa hii iingie yote kwenye *Hansard* za Bunge kama ilivyowasilishwa mezani kwako.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, katika kusimamia masuala ya kibajeti, Kamati imechambua Fungu Na. 48 ambalo ni Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Fungu Na. 03 ambalo ni Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi.

Uchambuzi huu umefanyika baada ya Kamati kufanya ziara za kujiridhisha na hali halisi ilivyo katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo chini ya vifungu vilivyotajwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/2022, uchambuzi ulifanyika ili kujenga msingi wa kufanya ulinganisho na makadirio kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Maeneo yaliyochambuliwa ni ukusanyaji wa maduhuli, upatikanaji wa fedha za matumizi ya kugharamia miradi ya maendeleo na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukusanyaji wa maduhuli; katika mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilijiwekea lengo la kukusanya jumla ya shilingi 221,000,000,000. Hadi kufikia mwezi Machi, 2022 Wizara iliweza kukusanya shilingi bilioni 91.9 sawa na asilimia 42 ya malengo yaliyokusudiwa. Jedwali Na. 01 linaonesha uhalisia.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa makusanyo kwa mwaka huu wa fedha si wa kuridhisha kwani Wizara imekusanya asilimia 42 peke yake. Aidha, makusanyo haya hayaendani na matarajio na malengo ya Wizara. Hali hii imetokana na mwamko mdogo wa wananchi kulipa Kodi ya Ardhi. Kwa upande mwingine, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi - Fungu Na. 03 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 706,000,000. Hadi kufikia Machi 5, 2022 Tume ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi 360.37 sawa na asilimia 51, Jedwali Na.2 linaonesha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Tume ya Kukusanya Kodi ya Pango kwa asilimia 155, Kamati ina maoni kuwa mwenendo wa ukusanyaji wa mapato kwa ujumla kwa mwaka huu hauridhishi na hautoi mwelekeo wa kufikia lengo kulingana na muda uliobaki wa utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inatekeleza miradi minne katika Fungu 48. Jumla ya bajeti iliyoidhinishwa ni Shilingi bilioni 47 sawa na asilimia 40 ya bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Fungu Na. 03, inatekeleza mradi mmoja wa uandaaji wa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi katika Vijiji vinavyozunguka Miradi ya Kimkakati. Mradi huu uliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 1.5.

Mheshimiwa Spika, kwa madhumuni ya kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni ya Kudumu ya Bunge, Kamati ilitembelea miradi mitatu ya Wizara katika Mikoa ya Singida, Mwanza na Mara kama ifuatavyo: Mradi wa kwanza ni Mradi Na. 2325 – Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi Katika Mikoa ya Mwanza na Mara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, mradi huu uliidhinishiwa 8,000,000,000 kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha katika Mikoa ya Mwanza na Mara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kwanza; Utekelezaji wa Mradi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ilemela; Mkoa wa Mwanza. Wizara iliipatia Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela mkopo wa shilingi bilioni 3.59 kwa malengo ya kupima viwanja 3,500 katika eneo la Isazu, Ilekako, Igalagala, Ilalila na Nyafura. Utekelezaji wa mradi huu upo katika hatua ya upimaji wa viwanja. Kamati ilibaini kuwa ucheleweshaji wa fedha umeathiri utekelezaji wa mradi. Kutokana na kazi ya upimaji na uratibu wa urasimishaji zinavyoendelea, Kamati imeridhishwa na matumizi ya mkopo huo kwa hatua ya utekelezaji wa mradi kulingana na kiasi cha fedha kilichotolewa.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Pili; Utekelezaji wa Mradi Katika Wilaya ya Bunda – Mkoa wa Mara; Halmashauri ya Wilaya ya Bunda ilipata mkopo wa Shilingi milioni 493.99 kwa ajili ya kupima viwanja 7,450 katika Kata tisa za Wilaya hiyo. Kata hizo ni Manyamanyama – Mtaa wa Mbugani, Manyamanyama – Mtaa wa Shuleni, Manyamanyama – Mtaa wa Katoliki, Sazira – Mtaa wa Ruselu, Bunda Stoo – Mtaa wa Kilimani, Nyasura – Mtaa wa Zanzibar, Balili – Mtaa wa Balili, Bunda Stoo – Mtaa wa Idara ya Maji na Guta – Mtaa wa Guta. Utekelezaji wa mradi huu upo katika hatua ya upimaji ambapo kiasi cha fedha shilingi milioni 144.99 sawa na asilimia 29.3 kimetolewa katika upimaji, upangaji, uelimishaji, kulipa wataalam na vibarua wanaotekeleza mradi huu.

Mheshimiwa Spika, Mradi mwingine ambao Kamati iliutembelea ni Mradi Na. 4951 – Uaandaji wa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi katika Vijiji Vinavyozunguka Miradi ya Kimkakati katika Mkoa wa Singida. Mradi wa Upangaji wa Matumizi ya Ardhi *(Land Use Planning Project Number 4951)* umebuniwa na Tume ya Mipango ya Ardhi kupitia Wizara yake mama kuanzia mwaka 2018/2019 na kupangiwa kutumia shilingi bilioni 32.21 hadi utakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2021/2022, Mradi huu ulitengewa shilingi bilioni 1.5 peke yake kutekeleza huo mpango wa upangaji matumizi ya ardhi. Hadi tarehe 10 Machi, 2022, Tume ilikuwa imeshapokea shilingi milioni 844.46 sawa na asilimia 56.29 ya fedha iliyoidhinishwa. Kamati ilitembelea mradi huu katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida katika Vijiji vya Nkwae na Ntondo ambavyo ni miongoni mwa vijiji 16 vilivyoandaliwa Mpango ya Matumizi ya Ardhi katika Vijiji vinavyopitiwa na Mkuza wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima, Uganda hadi Chongoleani, Tanga. Mradi unaendelea vizuri na unatoa mwelekeo na matokeo mazuri sana.

Mheshimiwa Spika, Mradi mwingine ni Mradi Na. 2324 – Uimarishaji wa Mipaka ya Kimataifa kati ya Tanzania na Kenya, Eneo la Serengeti. Mpaka wa Tanzania na Kenya una urefu unaokadiriwa kuwa na kilometa 817.71 ambapo kati ya hizo, kilometa 758 ni sehemu ya mpaka wa nchi kavu na kilometa 59.71 ni sehemu ya mpaka wa majini.

Mheshimiwa Spika, mradi huu unajielekeza katika Kuimarisha Mpaka wa Kimataifa kati ya Tanzania na Kenya katika Mkoa wa Mara. Katika mwaka wa fedha, 2021/2022, Mradi huu ulitengewa shilingi bilioni 5.4, hadi kufikia Machi, 2022, ulikwishapatiwa shilingi 2.7 sawa na asilimia 51.

Mheshimiwa Spika, licha ya kuwa utekelezaji wa mradi huu unaendelea vizuri na kwa ufanisi, lakini unakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Ukosefu wa miundombinu ya barabara kwa ajili ya kusafirisha vifaa;

(ii) Baadhi ya wananchi wa pande zote mbili kuendesha shughuli za kilimo juu ya mipaka;

(iii) Ukosefu wa elimu kuhusu mambo ya mipaka kwa jamii zinazozunguka mipaka; na

(iv) Kasi ndogo ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla hali ya upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo haukuwa kama ilivyotarajiwa. Kiasi kilichopatikana cha asilimia 51 ni kidogo ambacho hakiwezi kukidhi mahitaji ya utekelezaji wa miradi iliyokusudiwa na hivyo kupunguza ufanisi na tija ya kazi zilizokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida; Fungu Namba 48 na Fungu Na.3 yote yalipatiwa

fedha za matumizi ya kawaida kwa kiwango kinachoridhisha. Uchambuzi unaonesha kuwa kwa ujumla mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa Fungu Namba 48 na Fungu Na.3 unaonesha kuwa utekelezaji wake unaakisi malengo.

Mheshimiwa Spika, Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati; wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu Namba 48 na Fungu Na.3 kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kamati ilishauri mambo mbalimbali ambayo Serikali iliyazingatia kama ilivyofafanuliwa katika Taarifa. Kamati imejiridhisha na imeridhika kwamba, ushauri wake unaendelea kuzingatiwa na Wizara pamoja na Tume katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Maduhuli ya Matumizi; kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara inategemea kukusanya Shilingi bilioni 250.1, kiasi ambacho ni ongezeko la asilimia 11.63 ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/2022. Jedwali Na.4 linafafanua.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2021/2022, kufikia asilimia 42 peke yake ndani ya robo tatu ya muda wa lengo, Kamati haioni uwezekano wa kufikia lengo la makusanyo lililowekwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Pamoja na nia njema ya kuongeza makusanyo ya Wizara, ni vema Serikali ikazingatia changamoto zilizosababisha makusanyo kuwa chini ya lengo na kuzingatia uhalisia katika kupanga makisio yao.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Fungu Na.03, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi inakadiriwa kukusanya shilingi milioni 706 ambayo ni sawa na lengo la maduhuli kwa mwaka uliopita. Jedwali Na.5 linaonesha.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2021/2022, ambao ni asilimia 51 ndani ya robo tatu ya kipindi cha utekeleaji haitakuwa rahisi kufikia lengo la ukusanyaji kwa mwaka 2022/2023, haitakuwa rahisi kufikia lengo la ukusanyaji kwa mwaka 2022/2023 ikiwa mikakati ya ukusanyaji na vyanzo ni vilevile vilivyotumika katika mwaka unaoisha. Kwa ujumla Kamati inaona kuwa ni muhimu Tume ikajiwekea mikakati itakayoiwezesha kuongeza makusanyo ya maduhuli kwa mwaka huu wa fedha ili kuleta tija iliyokusudiwa. Aidha, makadirio ya makusanyo yazingatie uhalisia ili utekelezaji wake uwe ni rahisi.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Matumizi ya Kawaida; taarifa iliyotolewa na Wizara mbele ya Kamati ilibainisha kuwa, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inakadiria kutumia jumla ya shilingi bilioni 78.3. Kiasi hicho ni ongezeko la matumizi kwa asilimia 13 ikilinganishwa na bajeti iliyopita. Kati ya Fedha hizo Shilingi bilioni 44.38 ni kwa ajili ya mishahara na Shilingi bilioni 33.92 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hali hiyo ililinganishwa na uzoefu wa upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2021/2022 ili kuona uwezekano katika hali halisi. Mchanganuo huo umeoneshwa katika Jedwali Na.6.

Mheshimwa Spika, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Fungu Na.3, imekadiriwa kutumia shilingi bilioni 3.46 sawa na ongezeko la asilimia 28.3 ikilinganishwa na Bajeti ya mwaka 2021/2022. Mgawanyo wa fedha za matumizi ya kawaida upo kwenye Jedwali Na.7.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali chini ya Rais Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuona umuhimu wa Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi na kuanza kuiongezea nguvu ya kibajeti kwenye matumizi ya kawaida. Aidha, nyongeza hii bado haikidhi mahitaji ya Tume iliyonayo kulingana na Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa miaka

mitano 2020 - 2025. Ni maoni ya Kamati kuwa, nyongeza ya makadirio ya fedha za kawaida itaendana pia na upatikanaji wa fedha hizo kwa wakati na kwa kiwango stahiki katika hatua ya utekelezaji ili lengo lililokusudiwa liweze kutimia.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo; maelezo yaliyotolewa na Wizara mbele ya Kamati yalibaini kuwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Fungu Namba 48 imetengewa jumla ya Shilingi bilioni 27.15 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo ni pungufu ya asilimia 8.1 na Shilingi bilioni 1.4 kwa ajili ya miradi ya Tume Fungu Namba 03 ambayo ni pungufu ya asilimia sita ikilinganishwa na Bajeti ya 2021/2022. Jedwali Na.8 linaonesha.

Mheshimiwa Spika, kwa uchambuzi huu, ni wazi kuwa Tume kwa ujumla wake itatekeleza miradi yake kwa uchache kutokana na mkazo mdogo uliowekwa kwenye bajeti ya maendeleo. Ni maoni ya Kamati kuwa, ili Serikali iweze kufanikiwa katika kutekeleza sehemu ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2020 - 2025) ambapo Serikali inatakiwa kuandaa Mpango wa Matumizi ya Ardhi nchini kwa asilimia 50 ya vijiji 12,319 vilivyopo nchini ifikapo mwaka 2025, ni muda sasa wa kuongeza bajeti ya maendeleo ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ili malengo ya Mpango huo yaweze kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati; baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa bajeti pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara pamoja na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, naomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Fungu Namba 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

(i) Kutopatikana kwa wakati kwa fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kunasababisha utekelezaji wa miradi hiyo kusuasua. Hivyo, Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati na kwa kiwango kilichokusudiwa ili kukidhi matarajio;

(ii) Mwenendo wa makusanyo ya maduhuli usioridhisha unaathiri lengo la makusanyo hayo na kupunguza ufanisi. Hivyo, Serikali iweke mikakati madhubuti ya kuhakikisha kuwa lengo la makusanyo ya maduhuli linafikiwa na makadirio ya makusanyo hayo yanaakisi uhalisia;

(iii) Kuondolewa kwa fedha asilimia 30 *(retention)* ya makusanyo zilizokuwa zinabakia katika zoezi la makusanyo kumesababisha utendaji kazi wa halmashauri kuwa mgumu na kuzorotesha ukusanyaji wa maduhuli. Hivyo, Serikali ifanye mapitio ya sheria na kuona umuhimu wa kurejesha asilimia 30 ya makusanyo ili kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa ufuatiliaji wa makusanyo hayo ya maduhuli;

(iv) Kutotolewa kwa wakati fedha za mkopo kwa ajili ya miradi ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha ardhi, kunasababisha miradi hiyo kutotekelezwa kwa wakati. Hivyo, Serikali ihakikishe inatoa kwa wakati fedha za mkopo huo ili utekelezaji ufanyike kwa wakati. Aidha, utekelezaji wa miradi uanze mara moja bila kuchelewa mara tu baada ya fedha kupatikana;

(v) Kutorejeshwa kwa mikopo inayotolewa na Serikali kwa ajili ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha ardhi kwa wakati, kunasababisha kutofikiwa kwa lengo la kuendelea kukopesha halmashauri zingine nchini.

Hivyo, Serikali iziwekee halmashauri utaratibu mzuri wa kurejesha mikopo hiyo ili kuhakikisha kwamba, lengo la kukopesha halmashauri zote nchini linafikiwa;

(vi) Halmashauri nyingi zimekuwa zikipata faida inayotokana na mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha ardhi na kuelekeza faida hiyo kwenye shughuli zingine badala ya kuendeleza sekta ya ardhi ambayo ina uhitaji mkubwa wa fedha. Hivyo, faida inayopatikana kwenye mauzo ya maeneo yanayopimwa kutokana na mkopo wa KKK, ipangiwe matumizi yanayolenga kuendeleza sekta ya ardhi ikiwemo kuweka miundombinu kwenye maeneo yanaliyopimwa badala sasa ambapo fedha hizo hazina maelekezo ya namna ya kuzitumia;

(vii) Manufaa yaliyoanza kupatikana kutokana na utekelezaji wa mradi wa KKK yamebainisha kuwa bado kuna uhitaji mkubwa wa fedha ili kuweza kuzifikia halmashauri zote nchini. Hivyo, Serikali iharakishe kuanzisha Mfuko wa KKK kama ulivyo Mfuko wa Maji ambapo Mfuko huo utatumika katika kufanikisha kazi hiyo hasa vijiji-miji *(growing towns)* na kupunguza au kuondoa kabisa makazi holela na kuongeza wigo wa walipa kodi;

(viii) Kasi ndogo ya utoaji wa hati milki za ardhi, inaisababishia Serikali kukosa mapato yanayotokana na kodi ya kila mwaka ya viwanja. Hivyo, Serikali iongeze kasi ya utoaji wa hati miliki za ardhi ili kuongeza mapato yatokanayo na kodi ya viwanja. Aidha, maeneo yaliyopimwa yawekewe miundombinu muhimu kama barabara, umeme na maji itakayohamasisha wamiliki kuendeleza maeneo yao;

(ix) Mwamko mdogo wa kulipa kodi ya pango la ardhi nchini unatokana na elimu na uhamasishaji usioridhisha wa sekta ya ardhi juu ya umuhimu wa kulipa kodi ya ardhi kwa wakati. Hivyo, Serikali iharakishe kuandaa mfumo mahsusi utakaotumika katika kuwakumbusha wateja kulipa kodi ya pango la ardhi kama zinavyofanya baadhi ya mamlaka;

(x) Mkanganyiko wa kimuundo wa Mabaraza ya Ardhi ya Kijiji na Kata ambayo yapo chini ya TAMISEMI na yale ya Wilaya ambayo yapo chini ya Wizara ya Ardhi, yanasababisha changamoto katika usimamizi stahiki wa kisekta jambo linalopunguza ufanisi. Serikali ihamishie Mabaraza yote ya Ardhi chini ya usimamizi wa mamlaka moja ili kuboresha utendaji;

(xi) Uhaba wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba katika kila Wilaya nchini kumesababisha mashauri mengi kutotatuliwa kwa wakati na wananchi kulazimika kusafiri umbali mrefu kusikiliza mashauri yao. Hivyo, Serikali ihakikishe inaanzisha Mabaraza haya katika kila Wilaya nchini ili kusogeza huduma hiyo karibu na wananchi. Vile vile, Serikali iwekeze zaidi katika Mabaraza yanayotembea *(Mobile Land Tribunal)* ili kuwafikia wananchi wengi kwenye vijiji na kata; na

(xii) Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yanakumbana na changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na tuhuma za vitendo vya rushwa vinavyosababisha kutopatikana kwa haki. Hivyo, Serikali iweke mifumo mizuri ya uendeshaji wa Mabaraza ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi ili kuondoa vitendo vya rushwa vinayoathiri haki za wananchi.

Mheshimiwa Spika, Fungu Na.3. Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi:-

(i) Serikali itenge na kutoa bajeti itakayokidhi mahitaji halisi ya Tume ambayo inakabiliwa na upungufu mkubwa wa rasilimali fedha, rasilimali watu na vitendea kazi muhimu. Kwa mujibu wa mapendekezo ya bajeti kwa mwaka wa fedha, 2022/2023, fedha za miradi zilizotengwa ni shilingi bilioni 1.4 tu. Kiasi hiki hakiakisi uhalisia wa mahitaji ya Tume ambayo kwa mujibu wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2020 – 2025), unaitaka Serikali kuvipangia matumizi angalau asilimia 50 ya vijiji vyote 12,319 nchini nzima ifikapo mwaka 2025. Kufikia lengo hili Tume inahitaji shilingi bilioni 10.79 kwa mwaka na hivyo kwa bajeti hii kuwa na upungufu wa bilioni 9.34. Aidha, mahitaji halisi ya watumishi ni watumishi 179 lakini Tume leo ina watumishi 79 peke yake;

(ii) Mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli hauendani na matarajio na hivyo kupunguza ufanisi. Tume ijiwekee mikakati ya kuhakikisha kuwa makusanyo ya maduhuli yaliyowekwa yana uhalisia na yanafikiwa kwa wakati; na

(iii) Muundo wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi hauiwezeshi Tume kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa kuwa Tume ina Bodi ya Ushauri badala ya Bodi ya Utendaji. Kamati inaishauri Serikali kuwa, ifanye marekebisho ya sheria ili kuanzisha Bodi ya utendaji itakayayoipa nguvu ya kisheria katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, hitimisho napenda kukushukuru sana wewe kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha taarifa hii,

kwa niaba ya Kamati napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii ambao maoni yao, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyoorodheshwa katika taarifa hii yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*), Wajumbe hao ni kama walivyoorodheshwa hapo chini.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Lubala Mabula, Mbunge, Naibu Waziri, Mheshimiwa Ridhiwan Jakaya Mrisho Kikwete, Mbunge, Katibu Mkuu Dkt. Allan Kijazi, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Nicholaus Mkapa pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge - Ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc*, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge. Ninamshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein (Ndc), Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Dickson Bisile na Makatibu wa Kamati hii Ndugu Ramadhan Abdallah, Ndugu Elieka Saanya na Ndugu Rehema Kipera wakisaidiwa na Ndugu Mwimbe John, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee taarifa hii ili lijadili na kukubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**26 MEI, 2022**

**MAONI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKADHI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA JUMLA**

## 1.0 MAELEZO YA JUMLA

### 1.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2021/2022, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii ina sehemu kuu Nne. Sehemu ya kwanza ni utangulizi, sehemu ya pili inabainisha uchambuzi wa namna bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2021/2022 ilivyotekelezwa na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2022/2023. Sehemu ya Tatu inahusu maoni na mapendekezo ya Kamati na sehemu ya nne inahusu Hitimisho.

### 1.2 Msingi wa Uchambuzi wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 6(6) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, vinaipa Kamati jukumu la kufanya uchambuzi huu. Aidha, Kanuni ya 117(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yaliyotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Wizara hii kuchambuliwa na

Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba Bunge lijadili hoja ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa pamoja na Taarifa hii.

### 1.3 Mawanda ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Katika kusimamia masuala ya kibajeti, Kamati imechambua **Fungu 48** ambalo ni Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na, **Fungu 03** ambalo ni Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Uchambuzi huu ulifanyika baada ya Kamati kufanya ziara za kujiridhisha na hali halisi ilivyo katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo chini ya mafungu yaliyotajwa hapo juu.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI

### 2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Uchambuzi ulijielekeza katika maeneo makuu mawili ambayo ni Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

### 2.2 Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi ulifanyika ili kujenga msingi wa kufanya ulinganisho na makadirio kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Maeneo yaliyochambuliwa ni ukusanyaji wa maduhuli,upatikanaji wa fedha za matumizi ya kugharamia miradi ya maendeleo na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi kwa mwaka wa Fedha 2021/2022.

2.2.1 **Ukusanyaji wa Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa Fedha 2021/2022 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilijiwekea malengo ya kukusanya jumla ya **shilingi 221,000,000,000**. Hadi kufikia mwezi Machi, 2022 Wizara ilikuwa imekusanya **shilingi 91,926,073,996.12** sawa na aslimia 42 ya malengo yaliyokusudiwa.Mchanganuo wa makusanyo hayo unaonekana katika **Jedwali Na.01**

**Jedwali Na. 1: Fungu 48 - Makadirio na Makusanyo Halisi katika mwaka wa fedha 2021/2022**

| **UKUSANYAJI WA MADUHULI HADI KUFIKIA 22 MACHI, 2022** | | |
|---|---|---|
| **MAKADIRIO (Tsh.)** | **MAKUSANYO (TSh.)** | **ASILIMIA** |
| 221,000,000,000 | 91,926,073,996 | 42 |

***Chanzo:*** *Randama ya bajeti ya 2021/2022 fungu 48*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa makusanyo ya maduhuli unaonesha kwamba:-

(a) Jumla ya makusanyo ya maduhuli umefikia **asilimia 42** tu ya lengo hadi kufikia Machi, 2022 ambayo ni ndani ya robo tatu ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara;

(b) Mwenendo huu wa makusanyo ya maduhuli hauridhishi kwani ni chini ya lengo la makusanyo kulingana na muda uliotumika ambao ni karibu asilimia 75 ya muda wa utekelezaji;

**Mheshimiwa Spika,** mwenendo wa makusanyo kwa mwaka huu wa fedha si wa kuridhisha kwani Wizara imekusanya asilimia 42 tu. Aidha makusanyo haya hayaendani na

matarajio na malengo ya Wizara. Hali hii imetokana na mwamko mdogo wa Wananchi kulipa Kodi ya Ardhi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Fungu-03 ilikadiriwa kukusanya jumla ya **shilingi 706,000,000.** Hadi kufikia Machi, 2022 Tume ilikuwa imekusanya jumla ya **shilingi 360,367,136.12** sawa na asilimia 51. **Jedwali Na.2** linaonesha mchanganuo huo

**Jedwali Na. 2: Fungu 03 Makadirio na Makusanyo Halisi kwa mwaka wa fedha, 2021/2022:**

| Vifungu | Ufafanuzi wa Vifungu | Kilicho idhinishwa (Tsh.) | Kilicho kusanywa hadi Machi,2022 (Tsh.) | % |
|---|---|---|---|---|
| 140103 | Rent- Government Quarters and offices | 6,000,000 | 9,300,000 | 155 |
| 140369 | Other collections (strategic Partiners) | 700,000,000 | 351,067,136.92 | 50.15 |
| | **Jumla ya fungu 03** | **706,000,000** | **360,367,136.92** | **51.04** |

***Chanzo;*** *Randama ya Bajeti ya 2021/2022 Fungu 03*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi unaonesha kuwa:-

(a) Jumla ya makusanyo ya maduhuli imefikia asilimia 51 ya lengo hadi kufikia Machi, 2022 ambapo ni robo tatu ya utekelezaji wa majukumu iliyojiwekea;

(b) Kwa muda uliobaki wa utekelezaji ambao ni chini ya asilimia 30, ni vigumu kwa Tume kufikia lengo liliokusudiwa; na

(c) Makusanyo ya kodi ya pango(*Rent – Government Quarters and Offices*) taarifa zimeonesha kuwa Tume imevuka lengo la ukusanyaji wa maduhuli kwa kufikisha asilimia 155. Mwenendo huu wa makusanyo unaendana na matarajio.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Tume ya kukusanya kodi ya pango kwa asilimia 155 Kamati ina maoni kuwa mwenendo wa ukusanyaji wa mapato kwa ujumla kwa mwaka huu hauridhishi na hautoi mwelekeo wa kufikia lengo kulingana na muda uliobaki wa utekelezaji. Hii imetokana na changamoto zinazoikabili Tume kama vile upungufu wa rasilimali watu, rasilimali fedha na vitendea kazi.

2.2.2 **Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inatekeleza jumla ya miradi 4 ya Fungu- 48. Jumla ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya kugharimia miradi hiyo ni shilingi **47,011,429,673.00** sawa na asilimia 40 ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Fungu – 03, inatekeleza mradi mmoja wa uandaaji wa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi katika Vijiji vinavyozunguka Miradi ya Kimkakati. Mradi huu uliidhinishiwa jumla ya **shilingi 1,500,000,000.**

**Mheshimiwa Spika**, kwa madhumuni ya kuzingatia masharti ya kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea miradi 3 ya Wizara katika mikoa ya Singida, Mwanza na Mara kama ifuatavyo:-

**(a) Mradi Na. 2325 – Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK) Katika Mikoa ya Mwanza na Mara**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 mradi huu uliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 8,000,000,000/=** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha katika Mikoa ya Mwanza na Mara kama ifuatavyo:-

**i. Utekelezaji wa Mradi katika Halmashauri ya Wilaya ya Ilemela - Mkoa wa Mwanza**

**Mheshimiwa Spika**, Wizara iliipatia Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela mkopo wa **Shilingi 3,589,774,000/=** kwa lengo la kupanga, kupima na kumilikisha ardhi. Halmashauri iliweka lengo la kupima viwanja 3,500 katika eneo la Isazu, Ilekako, Igalagala, Ilalila na Nyafura. Utekelezaji wa mradi huu upo katika hatua za upimaji wa viwanja. Kamati ilibaini kuwa ucheleweshaji wa utekelezaji wa mradi umetokana na kutopatikana fedha kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na kazi za Upimaji na Uratibu wa Urasimishaji zinavyoendelea, Kamati imeridhishwa na matumizi ya mkopo huo kwa hatua ya utekelezaji wa mradi kulingana na kiasi cha fedha kilichotolewa.

**ii. Utekelezaji wa Mradi Katika Wilaya ya Bunda – Mkoa wa Mara.**

**Mheshimiwa Spika,** Halmashauri ya Wilaya ya Bunda ilipata mkopo wa **Shilingi 493,989,000/=** kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi pamoja na Kurasimisha makazi. Halmashauri iliweka lengo la kupima viwanja 7450 katika Kata tisa za Wilaya hiyo. Kata hizo ni Manyamanyama – Mtaa wa Mbugani, Manyamanyama – Mtaa wa Shuleni , Manyamanyama – Mtaa wa Katoliki, Sazira – Mtaa wa Ruselu, Bunda stoo – Mtaa wa Kilimani (Bungutu), Nyasura – Mtaa wa Zanzibar, Balili – Mtaa wa Balili , Bunda Stoo – Mtaa wa Idara ya Maji (Virian), na Guta – Mtaa wa Guta. Utekelezaji wa mradi upo katika hatua za upimaji ambapo kiasi cha fedha kilichotumika ilikuwa ni **Shilingi**

**144,599,000/=** sawa na asilimia 29.3 katika upangaji na upimaji, uelimishaji na kulipa wataalam na vibarua wanaotekeleza mradi huu. Ucheleweshaji wa utekelezaji wa mradi umetokana na ucheleweshaji wa upatikanani wa fedha.

**(b) Mradi Na. 4951 – Uaandaji wa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi katika Vijiji Vinavyozunguka Miradi ya Kimkakati katika Mkoa wa Singida**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Upangaji wa Matumizi ya Ardhi (Land Use Planning Project Number 4951) umebuniwa na Tume ya Mipango ya Ardhi kupitia Wizara yake mama kuanzia Mwaka 2018/2019 na kupangiwa kutumia **Shiling**i **32,214,378,810/=** hadi utakapokamilika.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha, 2021/2022 Mradi huu kwa ujumla wake umeidhinishiwa kutumia **Shilingi 1,500,000,000/=** kutekeleza upangaji wa matumizi ya ardhi. Hadi tarehe 10 Machi, 2022 Tume ilikuwa imeshapokea **Shilingi 844,457,500/=** sawa na asilimia 56.29 ya fedha iliyoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea mradi huu katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida katika vijiji vya Nkwae na Ntondo ambavyo ni miongoni mwa vijiji 16 vilivyoandaliwa Mipango ya Matumizi ya Ardhi katika Vijiji vinavyopitiwa na Mkuza wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima Uganda hadi Chongoleani, Tanga.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi unaendelea vizuri na unatoa mwelekeo na uzoefu wa utatuzi wa migogoro ya mipaka baina ya vijiji hivyo kupelekea kuwa wa mafanikio makubwa katika usimamizi wa matumizi bora ya ardhi.

**(c) Mradi Na. 2324 – Uimarishaji wa Mipaka ya Kimataifa: Kati ya Kenya na Tanzania (Eneo la Serengeti)**

**Mheshimiwa Spika,** Mpaka wa Tanzania na Kenya una urefu unaokadiriwa kuwa na Kilomita 817.71 ambapo kati ya hizo, Kilomita 758 ni sehemu ya mpaka wa nchi kavu na kilomita 59.71 ni sehemu ya mpaka ya majini (Ziwa Victoria).

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu, unajielekeza katika Kuimarisha Mpaka wa Kimataifa kati ya Tanzania na Kenya, katika Mkoa wa Mara. Mpaka huu una urefu wa kilometa 72 za nchi kavu, unaanzia eneo la Kinyangara hadi Makuka.

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha, 2021/2022 Mradi huu umetengewa bajeti ya **Shilingi 5,400,000,000/=.** Hadi kufikia Machi, 2022 ulikwishapatiwa **Shilingi 2,771,979,783/=** sawa na asilimia 51.

**Mheshimiwa Spika**, Licha ya kuwa utekelezaji wa mradi huu unaendelea vizuri na kwa ufanisi lakini unakabiliwa na changamoto zifuatazo;-

a) Ukosefu wa miundombinu ya barabara kwa ajili ya usafirishaji wa vifaa;
b) Baadhi ya wananchi wa pande zote mbili kuendesha shughuli za kilimo juu ya mipaka;

c) Ukosefu wa elimu kuhusu mambo ya mipaka kwa jamii zinazoishi mipakani; na

d) Kasi ndogo ya utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla hali ya upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo haukuwa kama ulivyotarajiwa. Kiasi kilichopatikana cha asiimia 51 ni kidogo ambacho hakiwezi kukidhi mahitaji ya utekelezaji wa miradi iliyokusudiwa na hivyo kupunguza ufanisi. Ni maoni ya Kamati

kwamba mafanikio ya miradi yataleta maana ikiwa utekelezaji wake utafanyika kama ulivyopangwa.

2.2.3 **Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, **Fungu 48 -** Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iliidhinishiwa na Bunge Bajeti ya **Shilingi 69,071,385,393.42** sawa na asilimia 59.5 ya bajeti yote kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Machi, 2022 Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 49,607,417,141.36** kwa ajili ya Matumizi ya kawaida sawa na asilimia 72 ya bajeti iliyotengwa. Jedwali lifuatalo linaonesha mwenendo wa upatikanaji wa fedha wa Fungu 48 kwa Mwaka 2021/2022.

**Jedwali Na. 3: Fungu 48 - Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida**

| MATUMIZI | KILICHOIDHINISHWA (Tsh.) | KILICHOPOKELEWA Tsh.) | ONGEZEKO/PUNGUFU ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| MISHAHARA | 34,079,748,000.00 | 22,706,302,651.62 | 79 |
| OC | 34,991,639,393.42 | 26,901,114,489.74 | 65 |
| **JUMLA** | **69,071,385,393.42** | **49,607,417,141.36** | **72** |

**Chanzo**: *Randama za Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/22.*

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unaonesha kuwa:-

(a) Upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida ni asilimia 72 ya fedha iliyotengwa; na

(b) Mwenendo huu wa upatikaji wa fedha unatoa mwelekeo mzuri wa ukamilishaji wa lengo lililokusudiwa ikiwa tu utaenda sambamba na upatikaji wa fedha za maendeleo kwa wakati na kwa kiwango Kinachotarajiwa.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Fungu 03 - Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2,476,888,000** pamoja na

nyongeza ya **Shilingi 711,181,577.62** na kufanya jumla ya Fedha za matumizi ya kawaida kuwa **Shilingi 3,188,069,577** sawa na asilimia 68 ya Bajeti yote ya Tume.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unaonesha kuwa, kwa ujumla mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa Tume unaonesha kwamba utekelezaji wa lengo unaweza kufikiwa.

2.2.4 **Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu -48 na Fungu -03 kwa mwaka wa fedha, 2021/2022, Kamati ilishauri mambo mbalimbali ambayo Serikali iliyazingatia.

**Mheshimiwa Spika** mfano wa ushauri wa Kamati uliozingatiwa ni kama ifuatavyo:-

(a) Serikali imefanya marekebisho ya sheria na kufanya ajira za Wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya kuwa ya kudumu kama Kamati ilivyoshauri;

(b) Wizara kupitia Ofisi ya Rais-TAMISEMI ilizielekeza Halmashauri zote nchini kuandaa angalau mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji sita kwa mwaka ili kuongeza kasi ya uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi kufikia vijiji 810 kwa mwaka katika Halmashauri 185 zilizopo nchini;

(c) Wizara ilitoa elimu ya mamlaka za upangaji nchini kuhusu matumizi ya teknolojia ya kisasa na rahisi katika uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi; na

(d) Serikali imehuisha muundo wa Tume kwa kuanzisha Ofisi saba za kanda nchini ambazo ni Kanda ya Kaskazini (Kilimanjaro), Mashariki (Morogoro), Kusini (Mtwara), Nyanda za Juu Kusini (Mbeya), Magharibi (Tabora), Kanda ya Ziwa (Mwanza) na Kanda ya Kati (Dodoma)

**Mheshimiwa Spika**, Katika hatua mbalimbali, Kamati imeridhika kwamba ushauri wake unaendelea kuzingatiwa na Wizara pamoja na Tume katika utekelezaji wa majukumu yao.

## 2.3 Makadirio ya Maduhuli na Matumizi

### 2.3.1 Makadirio ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Ardhi,Nyumba na Maendeleo ya Makazi katika Fungu -48 inategemea kukusanya jumla ya **Shilingi 250,100,000,000**. Kiasi kinachotarajiwa kukusanywa ni ongezeko la asilimia 11.63 ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Mchanganuo wa lengo la makusanyo kwa fungu unaonekana katika **Jedwali Na.4** hapa chini.

**Jedwali 4: Fungu 48 – ulinganisho katika Makusanyo ya Maduhuli**

| CHANZO | 2021/2022 (Tsh.) | 2022/2023 (Tsh.) | Nyongeza/ Pungufu (Tsh.) | Nyongeza/ Pungufu% |
|---|---|---|---|---|
| Utawala na Rasilimali Watu | 2,000.00 | 2,000.00 | - | - |
| Idara ya Utawala wa Ardhi | 203,512,496,000.00 | 232,612,496,000 | 29,000,000,000 | 12.5 |
| Idara ya Upimaji na Ramani | 1,175,000,000.00 | 1,175,000,000.00 | - | - |
| Kitengo cha Usajili wa Hati | 8,375,000,000.00 | 8,375,000,000.00 | - | - |
| Kitengo cha | 6,875,000,000.00 | 6,875,000,000.00 | - | - |

| CHANZO | 2021/2022 (Tsh.) | 2022/2023 (Tsh.) | Nyongeza/ Pungufu (Tsh.) | Nyongeza/ Pungufu% |
|---|---|---|---|---|
| Uthamini wa Mali | | | | |
| Maendeleo ya Makazi | 1,062,500,000 | 125,000,000.00 | 937,500,000 | -88.2 |
| Mabaraza ya Ardhi na Nyumba za Wilaya | 937,500,000.00 | 937,500,000.00 | - | - |
| **Jumla Kuu** | **221,000,000,000.00** | **250,100,000,000.00** | **29,100,000,000** | **11.63** |

***Chanzo**: Randama ya Fungu -48*

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unaonesha kuwa:-

(a) Kwa ujumla makadirio ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2022/2023 yameongezeka kwa **asilimia 11.63** ikilinganishwa na lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022;

(b) Kutokana na mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kufikia **asilimia 42** tu ndani ya robo tatu ya muda wa lengo, Kamati haioni uwezekano wa kufikia lengo la makusanyo lililowekwa kwa mwaka wa fedha,2022/2023 kwa kuzingatia uzoefu wa makusanyo ya mwaka uliotangulia;

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kuwa, pamoja na nia njema ya kuongeza makusanyo ya Wizara, ni vema Serikali izingatie changamoto zilizosababisha makusanyo kuwa chini ya lengo na kuzingatia uhalisia katika kupanga makisio hayo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa **Fungu -03** Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi inakadiriwa kukusanywa

jumla ya **shilingi 706,000,000** ambayo ni sawa na lengo la maduhuli kwa mwaka wa fedha 2021/2022. **Jedwali Na. 5** linaonesha mchanganuo wa makadirio hayo.

**Jedwali Na. 5: Fungu 03 Ulinganisho katika Makadirio Maduhuli**

| CHANZO | 2021/2022 (Tsh.) | 2022/2023 (Tsh.) | Nyongeza / Pungufu% |
|---|---|---|---|
| Rent - Government Quarters and Offices | 6,000,000.00 | 6,000,000.00 | - |
| Receipts from Sales of Publications | 0 | 0 | - |
| Other Collections (Strategic Partners) | 700,000,000.00 | 700,000,000.00 | - |
| **Jumla Kuu Fungu 03** | **706,000,000.00** | **706,000,000.00** | **-** |

***Chanzo***: *Randama ya Fungu – 03*

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unaonesha kwamba:-

(a) Kwa ujumla makadirio ya maduhuli kwa mwaka 2022/2023 yanalingana na lengo la maduhuli ya mwaka wa fedha,2021/2022;

(b) Kutokana na mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambao ulifikia asilimia 51 tu ndani ya robo tatu ya kipindi cha utekelezaji, haitakuwa rahisi kufikia lengo la ukusanyaji kwa mwaka 2022/2023 ikiwa mikakati ya ukusanyaji na vyanzo ni vilevile vilivyotumika katika mwaka unaoisha.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla Kamati inaona kuwa ni muhimu Tume ikajiwekea mikakati itakayoiwezesha kuongeza makusanyo ya maduhuli kwa mwaka huu wa fedha ili kuleta tija iliyokusudiwa. Aidha makadirio ya makusanyo yazingatie uhalisia ili utekelezaji wake uwe rahisi.

2.3.2 **Uchambuzi wa Matumizi ya Kawaida**

**Mheshimiwa Spika**, taarifa iliyotolewa na Wizara mbele ya Kamati ilibainisha kuwa, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inakadiria kutumia jumla ya **shilingi 78,302,448,000.** Kiasi hicho ni ongezeko la matumizi kwa **asilimia 13** ikilinganishwa na bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 44,383,797,000** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 33,918,651,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hali hiyo ililinganishwa na uzoefu wa upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2021/2022 ili kuona uwezekano katika hali halisi.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, iwapo mwenendo wa upatikanaji wa fedha utakuwa kama ilivyo kwa mwaka wa fedha unaoisha, ukadiriaji wa matumizi ya kawaida unaonesha kuwa na uhalisia na kwamba utekelezaji wa lengo unaweza kufikiwa. **Mchanganuo huo wa makadirio hayo unaonekana katika** Jedwali Na.06

**Jedwali Na. 6: Fungu 48 - Ulinganisho katika Bajeti kwa mwaka wa fedha,2021/2022 na 2022/2023**

| **ULINGANISHO WA BAJETI FUNGU 48 KWA MWAKA 2021/2022 NA 2022/2023** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **MATUMIZI** | **2021/2022 (Tsh.)** | **2022/2023 (Tsh.)** | **ONGEZEKO/ PUNGUFU (Tsh.)** | **ONGEZEKO/PUNGUFU%** |
| Mishahara | 34,079,748,000 | 44,383,797,000 | 10,304,049,000 | 23 |
| OC | 33,918,651,000.00 | 33,918,651,000.00 | 0 | 0 |
| **Jumla ya ulinganifu** | **67,998,399,000** | **78,302,448,000** | **10,304,049,000** | **13** |

***Chanzo***: *Randama ya Wizara Fungu – 48*

**Mheshimwa Spika**,Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Fungu – 03 imekadiriwa kutumia kiasi cha **shilingi 3,457,704,000** sawa na ongezeko la **asilimia 28.3** ikilinganishwa na Bajeti ya mwaka 2021/2022. Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,977,882,000** ni kwa ajili ya Mishahara sawa na

asilimia 24.3 na **Shilingi 1,479,822,000.00** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo sawa na asilimia 33.8. Mgawanyo wa fedha za matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 ni kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na.7** hapo chini.

**Jedwali Na. 7: Fungu 03 – Ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida.**

| ULINGANISHO WA BAJETI KWA MWAKA 2021/2022 NA 2022/2023 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **MATUMIZI** | **2021/2022 (Tshs)** | **2022/2023 (Tshs)** | **ONGEZEKO/ PUNGUFU (Tshs)** | **ONGEZEKO/PUNGUFU%** |
| Mishahara | 1,497,066,000.00 | 1,977,882,000.00 | 480,816,000 | 24.3 |
| OC | 979,822,000.00 | 1,479,822,000.00 | 500,000,000.00 | 33.8 |
| **Jumla ya ulinganifu** | **2,476,888,000.00** | **3,457,704,000.00** | **980,816,000.00** | **28.3** |

***Chanzo***: *Randama ya Fungu -03*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali chini ya Rais Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuona umuhimu wa Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi na kuanza kuiongezea nguvu ya kibajeti kwenye matumizi ya kawaida. Aidha, nyongeza hii bado haikidhi mahitaji ya Tume iliyonayo kulingana na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano (2020-2025). Ni maoni ya Kamati kuwa, nyongeza ya makadirio ya fedha za kawaida utaendana pia na upatikanaji wa fedha hizo kwa wakati na kwa kiwango stahiki katika hatua ya utekelezaji ili lengo lililokusudiwa liweze kutimia.

### 2.3.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Maelezo yaliyotolewa na Wizara mbele ya Kamati yalibainisha kuwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Fungu-48 imetengewa jumla ya **Shilingi 27,153,322,000** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo ni pungufu ya **asilimia 8.1**, na **Shilingi 1,410,000,000** kwa ajili ya miradi ya Tume fungu -03 ambayo ni

pungufu ya **asilimia 6** ikilinganishwa na Bajeti ya 2021/2022. **Jedwali Na.8** linafafanua hapo chini.

**Jedwali Na. 8: Fungu 48 na Fungu 03- Ulinganisho katika Makadirio ya fedha za Maendeleo**

| Na. | Fungu | MAKADIRIO KWA MWAKA 2021/2022 (Tsh.) | MAKADIRIO KWA MWAKA 2022/2023 (Tsh.) | ASIIMIA KATIKA ONGEZEKO |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Fungu - 48 | 29,550,299,000 | 27,153,322,000 | -8.1 |
| 2. | Fungu - 03 | 1,500,000,000 | 1,410,000,000 | -6. |
| | **Jumla** | **31,050,299,000** | **28,563,322,000** | **-8.0** |

***Chanzo:*** *Randama za Fungu – 48 na Fungu – 03*

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unaonesha kwamba:-

(a) Bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ujumla imepungua kwa **asilimia 8.** Upungufu huu unaweza kumaanisha kuwa thamani ama idadi ya miradi itakayotekelezwa imepungua ikilinganishwa na mwaka wa fedha,2021/2022;

(b) Bajeti ya fungu - 03 kabla ya kupungua kwa asilimia 6 ilikuwa tayari ina uhitaji wa kuongezewa bajeti ya maendeleo ili kuendana na malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2020 - 2025. Kwa mwenendo huu wa fedha zinazotengwa, ni dhahiri kuwa lengo hili litatekelezwa chini ya matarajio;

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huu, ni wazi kuwa Tume kwa ujumla wake itatekeleza miradi yake kwa uchache kutokana na mkazo mdogo uliowekwa kwenye bajeti ya maendeleo. Ni maoni ya Kamati kuwa, ili Serikali iweze kufanikiwa katika kutekeleza sehemu ya Mpango wa

Maendeleo wa Miaka Mitano 2020-2025 ambapo Serikali inatakiwa kuandaa Mpango wa Matumizi ya Ardhi nchini kwa **asilimia 50** ya vijiji 12,319 vilivyopo nchini ifikapo mwaka 2025, ni muda sasa wa kuongeza bajeti ya maendeleo ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ili malengo ya Mpango huo yaweze kufikiwa.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa Bajeti pamoja na makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara pamoja na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, ninaomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati kama ifuatavyo: -

3.1 **Maoni na Ushauri wa Kamati**

**A. Fungu 48 – Wizara ya Ardhi,Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

(i) Kutopatikana kwa wakati kwa fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kunasababisha utekelezaji wa miradi hiyo kusuasua. Hivyo,serikali ione umuhimu wa kutoa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati na kwa kiwango kilichokusudiwa ili kukidhi matarajio;

(ii) Mwenendo wa makusanyo ya maduhuli usioridhisha unaathiri lengo la makusanyo hayo na kupunguza ufanisi. Hivyo, Serikali iweke mikakati madhubuti ya kuhakikisha kuwa lengo la makusanyo ya maduhuli linafikiwa na makadirio ya makusanyo hayo yaakisi uhalisia;

(iii) Kuondolewa kwa fedha **asilimia 30** *(retention)* ya makusanyo zilizokuwa zinabakia katika zoezi la makusanyo zimesababisha utendaji kazi wa halmashauri kuwa mgumu na kuzorotesha ukusanyaj ya maduhuli.

Hivyo, Serikali ifanye mapitio ya sheria na kuona umuhimu wa kurejesha **asilimia 30** ya makusanyo ili kuboresha mazingira ya utendaji kazi wa ufuatiliaji wa makusanyo ya maduhuli;

(iv) Kutotolewa kwa wakati fedha za mkopo kwa ajili ya mradi wa Kupanga, Kupima na Kumiikisha ardhi, kunapelekea miradi hiyo kutotekelezwa kwa wakati. Hivyo, Serikali ihakikishe inatoa kwa wakati fedha za mkopo huo ili utekelezaji ufanyike kwa wakati. Aidha, utekelezaji wa miradi uanze mara moja bila kuchelewa baada ya kupokea fedha hizo;

(v) Kutorejeshwa kwa mikopo inayotolewa na Serikali kwa ajili ya Kupanga, Kupima na Kumiikisha (KKK) ardhi kwa wakati, kunapelekea kutofikiwa kwa lengo la kuendelea kukopesha halmashauri zingine nchini. Hivyo, Serikali iziwekee Halmashauri utaratibu mzuri wa kurejesha mikopo hiyo ili kuhakikisha kwamba lengo la kukopesha Halmashauri zote nchini linafikiwa;

(vi) Halmashauri nyingi zimekuwa zikipata faida inayotokana na mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha na kuelekeza faida hiyo kwenye shughuli zingine badala ya kuendeleza sekta ya ardhi ambayo ina uhitaji mkubwa wa fedha. Hivyo, faida inayopatikana kwenye mauzo ya maeneo yanayopimwa kutokana na mkopo wa KKK, ipangiwe matumizi yanayolenga kuendeleza ardhi ikiwemo kuweka miundombinu kwenye maeneo yanayopimwa badala ya ilivyo sasa ambapo fedha hizo hazina maelekezo ya namna ya kuzitumia;

(vii) Manufaa yaliyoanza kupatikana kutokana na utekelezaji wa mradi wa KKK, yamebainisha kuwa bado kuna uhitaji mkubwa wa fedha ili kuweza kuzifikia halmashauri zote nchini. Hivyo, Serikali iharakishe kuanzisha Mfuko wa KKK kama ulivyo Mfuko wa Maji ambapo mfuko huo

utatumika katika kufanikisha kazi hiyo hasa vijiji - Miji (Growing towns) na kupunguza au kuondoa kabisa makazi holela na kuongeza wigo wa walipa kodi.

(viii) Kasi ndogo ya utoaji wa hati milki za ardhi, inaisababishia Serikali kukosa mapato yatokanayo na kodi ya kila mwaka ya viwanja. Hivyo, Serikali iongeze kasi ya utoaji wa hati miliki za Ardhi ili kuongeza mapato yatokanayo na kodi ya viwanja. Aidha, maeneo yaliyopimwa yawekewe miundombinu muhimu kama barabara, umeme na maji itakayohamasisha wamiliki kuendeleza maeneo yao;

(ix) Mwamko mdogo wa kulipa kodi ya pango la ardhi nchini unatokana na elimu na uhamasishaji usioridhisha wa sekta ya ardhi juu ya umuhimu wa kulipa kodi ya ardhi kwa wakati. Hivyo, Serikali iharakishe kuandaa mfumo mahsusi utakaotumika katika kuwakumbusha wateja kulipa kodi ya pango la ardhi kama zinavyofanya baadhi ya mamlaka za maji ili kufikia lengo la makusanyo na kuongeza mapato.

(x) Mkanganyiko wa kimuundo wa mabaraza ya ardhi ya Kijiji na Kata ambayo yapo chini ya TAMISEMI na yale ya Wilaya ambayo yapo chini ya Wizara ya Ardhi, yanapelekea changamoto katika usimamizi stahiki wa kisekta jambo linalopunguza ufanisi. Serikali ihamishie mabaraza yote ya ardhi chini ya usimamizi wa mamlaka moja ili kuboresha utendaji wake;

(xi) Uhaba wa mabaraza ya ardhi na nyumba katika kila wilaya nchini umepelekea mashauri mengi kutotatuliwa kwa wakati na wananchi kulazimika kusafiri umbali mrefu kusikiliza mashauri yao. Hivyo, Serikali ihakikishe inaanzisha Mabaraza haya katika kila Wilaya nchini ili kusogeza huduma hiyo karibu na wananchi. Vile vile, Serikali iwekeze zaidi katika Mabaraza yanayotembea (Mobile

land tribunal) ili kuwafikia wananchi wengi kwenye Vijiji na Kata; na

(xii) Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yanakumbana na changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na tuhuma za vitendo vya rushwa vinavyopelekea kutopatikana kwa haki. Hivyo, Serikali iweke mifumo mizuri ya uendeshaji wa Mabaraza ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi ili kuondoa vitendo vya rushwa vinayoathiri haki za wananchi.

**B. Fungu 03: Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi**

(i) Serikali itenge na kutoa bajeti itakayokidhi mahitaji halisi ya Tume ambayo inakabiliwa na upungufu mkubwa wa rasilimali fedha, rasilimali watu na vitendea kazi muhimu. Kwa mujibu wa mapendekezo ya bajeti kwa mwaka ujao wa fedha, 2022/2023, fedha za miradi zilizotengwa ni **shilingi 1,410,000,000/=**tu. Kiasi hiki hakiakisi uhalisia wa mahitaji ya Tume ambayo kwa mujibu wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2020 – 2025),unaitaka Serikali kuvipangia matumizi angalau **asilimia 50** ya vijiji vyote 12,319 nchini ifikapo mwaka 2025. Kufikia lengo hili Tume inahitaji **shilingi 10,785,000,000** kwa mwaka na hivyo kuwa na upungufu wa **shilingi 9,375,000,000.** Aidha, mahitaji halisi ya watumishi ni **watumishi 179** lakini Tume ina **watumishi 79** tu.

(ii) Mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli hauendani na matarajio na hivyo kupunguza ufanisi. Tume ijiwekee mikakati ya kuhakikisha kuwa makusanyo ya maduhuli yaliyowekwa yana uhalisia na yanafikiwa kwa wakati; na

(iii) Muundo wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi hauiwezeshi Tume kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa kuwa Tume ina Bodi ya Ushauri badala ya

Bodi ya Utendaji. Kamati inashauri kuwa Serikali ifanye marekebisho ya Sheria ili kuanzisha Bodi ya utendaji itakayayoipa nguvu ya kisheria katika kutekeleza majukumu yake.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha taarifa hii. Kwa niaba ya Kamati napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo orodheshwa katika taarifa hii yaingie kwenye taarifa rasmi za Bunge (Hansard), wajumbe hao ni kama walivyoorodheshwa hapa chini :-

1. Mhe. Ali Juma Makoa, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Shabani Omar Shekilindi, Mb – Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Jafari Wambura Chege, Mb
4. Mhe. Soud Mahammed Jumah, Mb
5. Mhe. Phillipo Augustino Mulugo, Mb
6. Mhe. Khalifa Salum Suleiman, Mb
7. Mhe. Maida Hamadi Abdallah, Mb
8. Mhe. Godwin Emmanuel Kunambi,Mb
9. Mhe. Neema William Mgaya, Mb
10. Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb
11. Mhe. Flatei Gregory Massay, Mb
12. Mhe. Mwanakhamis Kassim Said, Mb
13. Mhe. Hassan Seleman Mtenga, Mb
14. Mhe. Asia Abdulkarimu Halamga, Mb
15. Mhe. Juliana Daniel Shonza, Mb
16. Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb
17. Mhe. Suleiman Haroub Suleiman, Mb

18. Mhe. Oliver Daniel Semuguruka, Mb
19. Mhe. Lucy Thomas Mayenga, Mb
20. Mhe. Vedastus Manyinyi Mathayo,Mb
21. Mhe. Asya Mwadini Mohammed, Mb
22. Mhe. Agnes Mathew Marwa, Mb
23. Mhe. Munira Mustafa Khatib, Mb
24. Mhe. Dr. Florence G. Samizi,Mb
25. Mhe. Joseph Zacharius Kamonga,Mb
26. Mhe. Timotheo Paul Mnzava, Mb

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Dkt. Angelina Sylvester Lubala Mabula (Mb), Naibu Waziri, Mhe. Ridhiwan Jakaya Mrisho Kikwete (Mb), Katibu Mkuu Dkt. Allan Kijazi, Naibu Katibu Mkuu Ndg. Nicholaus Mkapa pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi ndc, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Huseni,ndc Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Dickson Bisile na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Ramadhan Abdallah, Ndg. Elieka Saanya na Ndg. Rehema Kipera wakisaidiwa na Ndg. Mwimbe John, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu lipokee taarifa hii ili lijadili na kukubali kuidhinisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Ali Juma Makoa, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII**
Mei, 2022

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa kuwasilisha mawazo ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaanza na uchangiaji na kama tulivyokuwa tumeshataarifiana uchangiaji ni dakika 10, kwa hivyo Wabunge ambao waliomba kuchangia leo wale ambao hawatapata fursa wataendelea kuchangia siku ya kesho kwa maana ya uchangiaji sasa pia uchangiaji jioni tutakaporejea halafu na kesho kwa sababu Wizara hii tunayo kwa siku mbili.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, atafuatiwa na Mheshimiwa Halima James Mdee.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kupata hii fursa ya kuwa mchangiaji wa kwanza kwenye Wizara hii muhimu sana ambayo imebeba maslahi mapana ya Watanzania. Kwanza naomba niungane na wewe na niungane na Bunge lako Tukufu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa tuzo ya mafanikio ya ujenzi wa miundombinu na kuwa miongoni mwa viongozi 100 wenye ushawishi mkubwa duniani. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais, tuzo hii anaistahili sana.

Mheshimiwa Spika, pia kuna jambo jingine halijasemwa lakini mimi kwenye kupitia pitia tu mitandao nimeona

Mheshimiwa Waziri Stergomena Tax ameonyesha tuzo nyingine ambayo ameipata Mheshimiwa Rais kwenye *Pan African Woman Organization,* ametambuliwa kama Rais wa kwanza mwanamke katika Afrika Mashariki, Rais mwanamke pekee kwa mwaka 2022 pia kwa kuonyesha uwezo mkubwa wa kufanyakazi kama kiongozi Mkuu wa Serikali. Hayo yote naomba yaunganishwe kama pongezi kwa Mheshimiwa Rais kwa kutambua mchango wake mkubwa kwa maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo nilitaka nichangie na niliombe Bunge lako Tukufu litoe maelekezo kwa Serikali linahusu hali halisi ya eneo letu tunalofanyia kazi eneo la Bunge. Upande wangu huu wa kulia tuna barabara ya Dodoma – Morogoro, Waheshimiwa Wabunge wengi wamepaki magari ng'ambo ya pili ya barabara na siku za karibuni kumekuwa na ajali mbalimbali, siku mbili tatu zilizopita pia Mheshimiwa Francis Ndulane alipata ajali pale, yeye ni mmoja katika Wabunge kadhaa ambao wamekuwa wanapata ajali eneo lile kwa sababu ndani ya eneo la Bunge hatuna maegesho ya kutosha, maeneo ya kuegesha magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia upande huu wa mbele katika geti la Mheshimiwa Waziri Mkuu kuna barabara ambayo inatoka Hazina inakwenda kuungana na barabara ya Morogoro, eneo hilo wanapita watu wa aina mbalimbali lakini Bunge lako Tukufu kwa mazingira yaliyopo na umuhimu wake na Viongozi waliopo humu wanahitaji ulinzi na usalama wa hali ya juu. Lakini pia leo Wabunge wako ili waweze kushiriki kwenye mazoezi ya kujenga afya zao waweze kulitumikia Taifa hili vizuri wanalazimika kwenda nje ya maeneo haya, wanakodi viwanja maeneo mbalimbali ya Mji, eneo hili lingeweza kutosha kwa huduma kama hizo.

Mheshimiwa Spika, zipo hoja nyingi ambazo zinaonyesha kwamba eneo hili la Bunge halitoshi kutoa huduma za kisasa,

tunazo changamoto za ofisi za Wabunge, Wabunge hawana ofisi huku, hata wananchi wangu wa Madaba wakija hapa nakutana nao *canteen,* mimi ni Mbunge nilihitaji nikae nao katika maeneo ambayo tunaweza kuongea masuala ya maendeleo. Kwa hiyo, moja katika mambo yatakayoliwezesha Bunge lako Tukufu kufanya kazi vizuri ni kuwa na mazingira rafiki salama yatakayowafanya Wabunge wafanye kazi kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninatambua hatua ambazo Bunge limefanya moja ni kwamba limejaribu kutathmini na kuthaminisha maeneo haya ya Bunge yenye majengo na viwanja vilivyo wazi. Hiyo kazi najua Bunge wamemaliza lakini niiombe Wizara sasa ichukue jukumu hili la kuisaidia Bunge kwa haraka zaidi kuyapata hayo maeneo ili tuweze kuwa na Bunge la kisasa linaloweza kutoa huduma bora kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naelewa tupo kwenye hatua za mwisho za kupitisha bajeti yawezekana jambo hilo kibajeti halijakaa vizuri. Bunge lako lina mamlaka linaweza kuitisha Kamati ya Bajeti ikakaa na Serikali tukafanya *amendment* ambazo zitaruhusu kuingiza hizo bajeti za kumaliza hili tatizo ambalo litaenda kuboresha utendaji wa Bunge lako na hivi Watanzania watapata huduma bora wanazozihitaji, hilo lilikuwa ombi langu la pili.

Mheshimiwa Spika, ombi la tatu kama kuna Wizara imeweza kuitikia wito wa Watanzania kuhusu migogoro mbalimbali ni Wizara hii ya Ardhi na hizi *credit* zimwendee kwanza Mheshimiwa Waziri wa sasa, Dada yangu Mheshimiwa Angelina Mabula, pia mtangulizi wake Mheshimiwa Lukuvi, kwa kweli hawa wamefanyakazi kubwa sana nchi hii. Mimi nimepata bahati ya kuhusika katika kupanga na kuleta majina ya watu watakaozungumza kwa mara ya kwanza nimeona mapendekezo machache sana ya watu wanaotaka kuongea kwenye Wizara hii, kwa sababu

migogoro mingi imetatuliwa na Serikali kupitia Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana mtangulizi wake Mheshimiwa Mabula, yeye mwenyewe Mabula na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Ridhiwani wanafanyakazi nzuri sana. Ninazo salamu mahsusi toka Madaba wananchi wa Madaba walipomuona Mheshimiwa Mabula ameenda Mbeya walivyomuona ameenda Mwanza walivyomuona ameenda maeneo mbalimbali akitatua migogoro ya wananchi wakasema tunatamani Mheshimiwa Waziri aje na Madaba kwa sababu wanayo imani nae sana.

Mheshimiwa Spika, migogoro ya ardhi haiwezi kuendelea kutatuliwa na Mahakama pekee, Mahakama zina utaratibu ambao unachelewesha sana, tujifunze kwa Mzee Lukuvi wakati ule anakwenda ndani ya Mkoa, anakaa na wananchi anatatua mgogoro mpaka leo hatujasikia kelele katika maeneo hayo. Huduma kama hii kwa Madaba na Mkoa wa Ruvuma bado hatujaipata kikamilifu. Mheshimiwa Waziri ninakuomba wananchi wanayo imani kubwa sana na wewe, wananchi wanaimani kubwa sana na Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan, wananchi wanayo imani sana na Watendaji wako wanaamini ukiendelea kwa mwendo uleule Tanzania hii migogoro itapungua kwa kwa asilimia kubwa.

Mheshimiwa Spika, sehemu kubwa ya migogoro ambayo utaikuta kwenye maeneo yetu inachangiwa na taasisi zingine za Serikali, mimi ninaamini dhamana ya ardhi imekabidhiwa Wizara ya Ardhi hii ni Wizara ya kisekta. Mwananchi mwingine yeyote na idara nyingine yoyote na Wizara nyingine yoyote ya Serikali ni watumiaji wa ardhi, wana mamlaka sawa kama mwananchi mwingine mwenye ardhi. Pale inapotokea mwananchi ana matumizi na ardhi, Serikali kupitia Idara zake wanaihitaji hiyo ardhi basi Wizara ya Ardhi isimame kama Hakimu anayetenda haki kwa kila

pande. Madaba tuna mgogoro wa ardhi kati ya wananchi wa Kipingo na watu wa hifadhi lakini watu wa hifadhi wametumia ubabe kuchukua maeneo ya wananchi, utaratibu huu hauwezi kuleta afya.

Mheshimiwa Spika, wewe unajua Mheshimiwa Rais ni kipenzi cha watanzania wanyonge, ni Mama mpenda haki hataki kuona Mtanzania yeyote anaonewa ndani ya nchi hii, Mama Mabula naomba endelea kumsaidia Mheshimiwa Rais kuwasimamia wananchi kupata haki zao za ardhi wakiwemo wananchi wa Kipingo, wananchi wa Ngadinda, wananchi wa Mkongotema, wananchi wa maeneo yote ya Madaba na Mkoa mzima wa Ruvuma na Tanzania katika ujumla wake

**SPIKA:** Sekunde 30 malizia sentensi

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Halima James Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru nikiongezea kwa hoja ya Mheshimiwa Mhagama kuhusiana na eneo la Bunge, nakumbuka wakati wa hotuba ya Waziri Mkuu, Kamati ya Bajeti ilieleza suala hili kwa kina na tukaambiwa kwamba hoja hii imepelekwa Wizara ya Ardhi, kwa mantiki ya dhamira ya kutwaa maeneo. Sasa nilikuwa nadhani kwa sababu Wizara yenyewe mko hapa ni wakati muafaka wa kulitolea majibu hili ili kama kuna namna ya hatua za ziada kama ambavyo imependekezwa na Mheshimiwa Mbunge, iweze kufanyika kwa haraka, kwa sababu siku hazigandi na thamani ya ardhi inapanda kila siku kwa hiyo lazima uamuzi ufanyike na ufanyike haraka kwa maslahi mapana ya Taasisi ya Bunge lakini na wananchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili jana nilisikiliza kwa makini Wizara ya Mifugo, migogoro ya ardhi ilizungumzwa ikashikwa Shilingi hapa ikapigwa juu kwa juu kimtindo, lakini dhamira ilikuwa ni kuwapa somo wajifunze tunakoelekea inakuwaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo nikisoma hotuba ya Waziri, migogoro ya ardhi vilevile imezungumzwa na Waziri anasema kabisa kwamba katika mwaka 2021/2022 walitarajia kutatua migogoro 1,000 lakini wakatatua migogoro 1,800. Sasa ukimsoma nae Waziri wa Mifugo jana anasema alifanya mikutano 28 kwa ajili ya kutatua migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine, yaani ni kama vile kutatua migogoro ni sifa. Mawaziri wameacha kufanya shughuli zao za msingi wanaenda kutatua migogoro. Tumesikiliza taarifa ya Kamati ya Ardhi imesema…

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY NDERIANANGA):** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Anayesema taarifa kasimama upande gani? Aah! Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Ummy Nderiananga.

**T A A R I F A**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY NDERIANANGA):** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Dada yangu Halima Mdee kwamba kati ya majukumu mengine ambayo Waheshimiwa Mawaziri walipewa, wamepewa kwa mujibu wa kanuni na utaratibu waendelee kufanya zoezi hilo. Kwa hiyo, asiseme kwamba wameacha majukumu yao ni kati ya sehemu ya majukumu yao kufanya shughuli hizo. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Siwezi kuipokea mdogo wangu alitakiwa asubiri kwanza niendelee ajue najengaje hoja. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati amesema hapa, kuna tatizo kubwa sana la kibajeti kwenye Tume inayowajibika kupanga nchi. Hili tatizo tunalizungumza leo kwa sisi wakongwe ni mwaka wa 15, sasa Mheshimiwa kama tusipojua *principle* moja kama Taifa, wananchi tunaongezeka ardhi haiongezeki. *(Makofi)*

Mheshimiwa kwa takwimu za Wizara yenyewe wakati tunapata uhuru mwaka 1961 watu walikuwa Milioni 10.3, ukigawa maeneo ambayo tunatakiwa tutumie ukiacha hifadhi na mambo mengine, ilikuwa gawio la ardhi kwa kila mtu ni wastani wa eka 8.4 mwaka 1961. Sensa 2012 tunaambiwa tulikuwa Milioni 43, kwa takwimu ya ardhi gawio ni hekta Mbili kwa kila mmoja tunazidi kudondoka, leo tunaenda sensa 2022 *possibly* ya Watanzania kufika Milioni 100 ni kubwa tutafika wapi? Mipango ya matumizi bora ya ardhi mifugo tunazungumza migogoro ya mifugo na wakulima, tunaambiwa 1978 tulikuwa tuna mifugo Milioni 21, mwaka 2012 tuna mifugo Milioni 43. Jana nimejumlisha kwa mujibu wa Waziri wa Mifugo ukichanganya ng'ombe, kondoo, mbuzi, kuku na kitimoto tuna jumla ya mifugo 1,165,000. Ninasema hivi nchi *square meter* ni zile zile *square* kilomita zile zile 945,000 lakini tume-*shift from* 10 Milioni Mungu anajua sensa itatuambiaje.

Mheshimiwa Spika, tume-*shift from* 20 *and so now* tuko 1,165,000, tunaambiwa hapa tumepitisha sisi wenyewe mpango wa miaka mitano, Tume yetu inahitaji Bilioni 15 tu kwa mwaka kuweza kufanikisha baada ya miaka mitano tuweze kupima vijiji 6,160. Bilioni 10 hivi leo kweli eneo hili muhimu ambalo tumejipangia kupima vijiji 719 kila mwaka tutimize *target* ya miaka hivi hatuna Bilioni 10? Halafu

mnatuambia kwenye hotuba zenu hapa eti mnapiga maziara hivi hizo ziara mlizozipiga nyie wakubwa, tokea tumeanza kutatua migogoro ya ardhi nchi, hii hivi mmetumia shilingi ngapi? Au kwangu mimi kwa tafsiri yangu tu ya kawaida, ni hivi migogoro ya ardhi tunatumia kama dili kimtindo na kuweza kupata shughuli za kufanya.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu huwezi kuniambia tunakosa 10 Bilioni ambayo mimi nahakika Lukuvi pale kwa uzoefu wake, kwenye akaunti yake ana Bilioni 10 kama mimi ninayo kidogo dogo yeye anakosaje? Kwenye eneo ambalo tunatakiwa, nasema na nasisitiza kama kuna eneo ambalo tunaiomba Kamati ya Bajeti *on a very serious note* iende ikaliangalie katika mtindo huo huo wa maeneo ya Bunge tuliozungumza, kama tunaweza tukaenda tukafanya mambo ninaomba tumsaidie Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najua Waziri anaandika lakini anachekelea si tunamtafutia hela, tumsadie Waziri apate Bilioni 10 tuondokane na matatizo ya migogoro ya ardhi nchi hii, wananchi wetu wanateseka, wakulima wanateseka, wafugaji wanateseka, lazima tuonyeshe *leadership for once,* haiwezekani Mkapa akashughulikia migogoro, Mzee wetu Mwinyi kashughulikia migogoro, Kikwete kashughulikia migogoro, Marehemu Magufuli kashughulikia migogoro na Mama Samia naye? Sasa si tumepiga Azimio leo asubuhi si ndiyo?

**MBUNGE FULANI:** *Yes*!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Tukamsifu Mama anaupiga mwingi si ndiyo? Sasa kuupiga mwingi siyo kwa mabarabara, kuupiga mwingi ni kwa agenda zinazogusa Watanzania. Wafugaji walio wengi, wakulima walio wengi, wachimbaji madini walio wengi na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninaomba sana nimelizungumza hili kwa sababu *it pains*, watu wanaumia halafu vijisenti vidogo vidogo tunashindwa kuvitoa ili kusaidia hili tatizo litatuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ni suala la mradi wa Kawe. Kwanza nitambue baada ya kuhangaika sana hatimaye *project* ya *National Housing* 7111, 7112 ya Shilingi Bilioni 45 inaenda kufanyakazi. Kwa hiyo, niwapongeze Wizara japokuwa tulizembea nchi ikapata hasara Bilioni 100, tusifanye uzembe wa namna hii tunaliumiza Taifa kwa kuchelewa kufanya maamuzi makini kwa wakati makini na kwa dhamira njema kusaidia nchi.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha kwanza kwa siku ya leo na Wabunge wameshaanza kuchangia, nitawataja wachache ambao tutaanza nao mchana ambao ni Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mheshimiwa Benaya Kapinga, Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mheshimiwa Bahati Kenneth Ndingo, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara na wengine wataendelea kutajwa kadri muda utakavyokuwa unakwenda.

Mheshimiwa Waziri umepewa hapo ushauri kwamba kumbe una Wabunge wazito sana humu ndani, ambao ukizungumza vizuri wanaweza kurekebisha mambo hapo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni leo.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11:00 Jioni Bunge Lilirejea)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae.

Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano yetu tutaanza na Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mheshimiwa Benaya Kapinga, na Mheshimiwa Joseph George Kakunda ajiandae.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma aliyenijalia afya njema hadi siku ya leo nikafika kwenye mkutano wetu huu. Pili nimshukuru Mheshimiwa Rais wote ni mashuhuda hakika anaendelea kufanya kazi nzuri ya kuendelea kutuletea maendeleo Watanzania. Niipongeze Wizara kwa maana ya Waziri mwenye dhamana Naibu wake kaka yangu Wakili Msomo Ridhiwan Kikwete lakini pia na watendaji wote wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku ya leo kwa kweli tunaona kuna *improvement* kubwa kwenye Wizara hii. Kwa sababu hadi mwaka wa fedha uliopita, nilikuwa najaribu kuangalia takwimu, viwanja vilivyopimwa nchini vilikuwa takribani milioni sita, lakini leo hii tumeona hapa kwenye hotuba ya Waziri wa

Ardhi sasa tunakwenda milioni saba, tunaona kuna *improvement*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kwa historia tu nieleze, hapa nchi yetu ilianza kupimwa mwaka 1896 ndipo kiwanja cha kwanza kilipimwa hapa nchini, sasa ukiangalia muda hadi sasa tulipofikia unaona bado tunakazi kubwa ya kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nirejee maneno ya Hayati Baba wa Taifa, alisema nchi yoyote ili iweze kupiga hatua ya maendeleo lazima iwe na siasa safi kwa maana ya utawala bora, lakini watu na mwisho ardhi. Ardhi ni hazina kubwa sana kwa Taifa letu, na kila kitu unachokitaja kipo kama sio chini basi juu ya ardhi. Tukizungumzia madini ardhi, mito ardhi, kwa hiyo ardhi imebeba uchumi wa nchi yetu. Baada ya kueleza haya naomba nifanye *comparison* hapa na wenzetu jirani wa Kenya; nijaribu kuoanisha takwimu za Kenya na nchi yetu, *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 24 Aprili, 2021 saa Nne usiku Waziri wa Ardhi wa Kenya akihojiwa na Television ya *the citizen* alieleza kwamba nchi ya Kenya mpaka sasa wana hati miliki milioni 11. Sasa najaribu kulinganisha Kenya na sisi nikirejea kwetu mpaka leo tunapozungumza kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri tuna hatimiliki yaani wananchi waliomilikishwa ardhi ni Milioni 2.3 utaona wenzetu wapo mbali sana, lakini naona kuna jitihada. Nimeeleza, mwaka uliopita hatimiliki nchini zilikuwa 1,500,000 tu lakini leo tunazungumzia milioni 2,000,000, kuna *improvement.* Sasa ushauri wangu ninaokwenda kutoa ni kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwenye sekta hii ya upimaji Wizara ya Ardhi kama *custodian* au kama ndiyo mamlaka ya usimamizi wa sekta ya ardhi nchini, ushauri wangu kwake ingeendelea kubaki hivyo inavyofanya

kuratibu na kusimamia sekta ya ardhi, na mamlaka za upimaji kwa maana ya Halmashauri kwa mujibu wa Sheria ya Mipango Miji Namba 8 ya Mwaka 2007 mamlaka za upangaji ni halmashauri. Sasa hoja ninayokwenda kushauri hapa ni lazima sasa Wizara Ofisi ya Rais TAMISEMI na Ardhi waje pamoja wawe na mpango wa pamoja. Kwa sababu kule kwenye halmashauri, halmashauri ziko chini ya Wizara TAMISEMI lakini ardhi ipo Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Wizara hizi zinatakiwa zifanye kazi pamoja. Kwa mfano ukienda kwenye *level* za mikoa wasimamizi wa sera na shughuli za Serikali kwenye *level* ya mkoa ni Wakuu wa Mikoa. Ni muhimu sasa wakashirikishwa, wawe na *ownership* ya upimaji ili wasimamie vizuri zaidi. Serikali peke yake haiwezi kufanikisha jambo hili, lazima kuwa na *engagement* ya *private* sekta. Kuna kampuni za upimaji, hapo awali kulikuwa na hoja ya kwamba kampuni za upimaji hizi zimekuwa zikiwadhulumu wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa Waziri atakuwa ni shahidi, tulikosea mahali. Hapo nyuma ilikuwa kampuni zilikuwa zinakwenda moja kwa moja kukutana na wananchi, kamati za ardhi zinaundwa katika *level* ya vijiji au mitaa, halafu wanaingia mkataba ambao kimsingi hakuna mashiko ya kisheria kwamba anaweza kuwa huyo mkandarasi akikataa kufanya kazi na akiwadhulumu anaweza kuwajibika mahali popote pale. Sasa hivi naona kuna mfumo mzuri sasa, na mimi nishauri eneo hilo. Kwamba Wakurugenzi wa Halmashauri ndio waingie mikataba sasa na hivi kampuni au kandarasi za upimaji, mwananchi yeye asubiri huduma tu. Hii itatusaidia kudhibiti wizi au dhuluma kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze faida za upimaji, ardhi ikipimwa kwa Serikali lakini pia kwa wananchi. Mwananchi akipimiwa ardhi yake iwe shamba anapata hati anakwenda benki anakopesheka, na jitihada za Wizara ya Kilimo maana

yake mwananchi mwenye shamba anaweza pia akakopesheka na akaendelea kulima na nadhani nchi ikaendelea vizuri. Lakini pia si tu mkulima, mwananchi wa kawaida anaweza kufanya biashara. Akiwa na hati miliki anakopesheka, ardhi inapanda thamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tukiongeza kasi upande wa Serikali, kwenye ardhi kuna tozo mbalimbali. Kwa mfano, mathalani kwa Mkoa wa Dar es Salaam. Mkoa wa Dar es Salaam una idadi ya watu takribani milioni sita. Tuchukue tu, tufanye *sampling* watu 1,000,000 tuwape hatimiliki za Dar es Salaam, hiyo fedha kiasi gani? tukipata milioni moja tu wenye hati miliki kwa Mkoa wa Dar es Salaam watatusaidia kuwa na *sustainability* mapato kwenye tozo za adhi. Kwa mfano kuna *land rent* mtu analipa, akifanya *transaction* ya kuuza kiwanja au nyumba analipa *capital gain tax* analipa *stamp duty;* hivi fedha zote ni maduhuli ya Serikali. Kwa hiyo mimi niendelee kusema tu kwamba pamoja na pongezi zangu kwa Wizara ya Ardhi tuna kazi ya kufanya ili kuongeza kasi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni eneo la mfumo wa *ILMIS. ILMIS (Integrated Land Management Information system)* ni mfumo ambao una hifadhi taarifa za sekta ya ardhi; na huu mfumo umeleta matunda bora. Leo Mheshimiwa Waziri amezungumza hapa, tunaona mafanikio ya hati hizi za kwenye mtandao; mwananchi akipimiwa; kwa mfano tunazungumzia viwanja milioni saba na tunazungumzia umilikishaji millioni mbili, kuna *gape* kama milioni tano hawana hati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukiongeza kasi hapo kwa mfumo wa *ILMIS.* tuka-*integrate* nchi nzima; na nimuombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa sababu yupo hapa, na ananisikia; tukiongeza fedha kwenye Wizara ya Ardhi tukawawezesha wakai-*integrate* mfumo huu wa *ILMIS,* nchi nzima, na mtanzania akawa na uhakika akipimiwa kiwanja

atapata hati miliki tutakuwa mbali sana. Kwa hiyo tuwekeze nguvu hapo kama Serikali ili tuweze kufanikiwa eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende haraka haraka kwenye eneo lingine, eneo la sekta binafsi nimeeleza lakini niombe kitu kimoja; sekta binafsi bado ina hali ngumu tutafute namna bora ya kuiwezesha, hasa kampuni za upimaji; kama kwa ruzuku au njia yoyote bora ambayo tunaweza kupeleka fedha au mikopo nafuu ili mtu akopesheke. Hii kampuni ya kijana wa Kitanzania aliyesajili kampuni yake, amejiajiri na anaajiri watu wengine, akiwezeshwa, kwa maana ya kama si ruzuku basi apewe mkopo nafuu; anaweza akafanya vizuri zaidi na nchi yetu ikapimwa kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende eneo lingine la migogoro ya ardhi, kumradhi migogoro ya ardhi ni matokeo tu ya *failure sekta,* tukiri kabisa, wananchi wanakimbia sana kuwekeza wanakimbilia sana kwenye ardhi, sisi kama Serikali bado tupo nyuma. Kwa hiyo migogoro ya ardhi ni matokeo ya *failure* ya sekta ya ardhi, wala si chochote, kwa hiyo tukisimama ardhi hii tukai-*manage* vizuri, tukaipima nchi nzima hata migogoro ya ardhi itakwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hapa nirejee eneo moja; nimpongeze Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan. Mheshimiwa Waziri ameeleza hapa kulikuwa na migogoro ya ardhi kwenye vijiji 975, Mheshimiwa Rais mwenye mapenzi mema na Watanzania amesema sasa katika vijiji hivi havifutwi vyote Watanzania, vijiji 920 anasema vikarasimishwe, jambo hili ni la kumpongeza Mheshimiwa Rais, katika hili tumpongeze Mheshimiwa Rais; na siasa zetu zingekuwa ngumu kidogo kama vingefutwa hivi vijiji. Kwa hiyo leo hii, nadhani hata wananchi wa Jimbo la Mlimba wananisikia; kuna changamoto moja tu ambayo nimuombe Mheshimiwa Waziri aifanyie kazi. Bado kuna maeneo pale Jimboni kwangu yanashida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Kata ya Mofu Kijiji cha Ikwambi na Karenga, leo hii watu wa *TAWA* bado wanawasumbuwa. Kwa hiyo nadhani ni muhimu sasa, kwa kuwa Serikali inakwenda kurasimisha vijiji hivi wenzetu hawa wa maliasili wangetulia kidogo na wananchi watulie kidogo mpaka Serikali itimize wajibu wake kwenye eneo hilo. Sasa, utekelezaji bado. Kwa hiyo *pending* ya utekelezaji ni muhimu sasa watu wa *TAWA* lakini pia na wananchi wangu wa Ikwambi na maeneo hayo niliyoyataja watulie kusubiri utekelezaji wa Serikali kwa kuwa Mheshimiwa Rais mwenye mapenzi mema na Watanzania amesema virasimishwe. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kengele ilikuwa imepiga ya pili nilikuwa nakuachia umalizie.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuhitimisha. Kata nyingine ni Kata ya Mchombe Kijiji cha Mbasa Kitongoji cha Shamba la Saba, Utengule na Ipugasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niunge mkono hoja na Mheshimiwa Waziri naona hii *chemistry,* aa' bwana, Mungu awabariki tu. Huko tunakokwenda naona tunakwenda kulamba asali. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Godwin Kunambi.

Kabla sijaendelea na mchangiaji niliyemtaja kuna tangazo dogo hapa kuna gari namba T117DSJ, ipo benki tunaomba ikaondolewe pale. Tunaendelea na Mheshimiwa Benaya Kapinga, na Mheshimiwa Joseph Kakunda pamoja na Mheshimiwa Bahati Kenneth Ndingo ajiandae.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi. Awali ya yote na mimi niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri Dkt. Angeline umefanya kazi kubwa sana katika Wizara hii, hongera sana. Mimi nakumbuka ukiwa Naibu Waziri tumefika hadi huko Masasi kwenye vitongoji huko kutatua migogoro, ukiwa na nguvu timamu kabisa kwakweli hongera sana mama yetu. Lakini pia nampoingeza pia Naibu Waziri, kwa muda mfupi tu ame-*cope* na Wizara hii, hongera sana Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza makatibu na naibu katibu. Pia naipongeza Serikali kwa kufanya uamuzi ule wa kumrejesha Mkurugenzi wa Shirika la Nyumba. Uamuzi ule ni wa manufaa sana kwa nchi yetu. Waswahili wanasema uchungu wa mwana anaujua ni mzazi. Tunajua mkurugenzi yule ndiye aliye lihuisha lile Shirika, kwa hiyo mambo mengi na miradi mingi alikuwa anaifahamu. Kwa hiyo nawapongeza sana nakupongeza Waziri lakini naipongeza Serikali kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niungane na wenzangu pamoja na Bunge hili kwa uzito mkubwa kumpongeza Rais wetu kwa ushindi Mkubwa wa hii Tuzo ambayo ameipokea. Ushindi huu ni mkubwa kwa nchi yetu lakini kwa maendeleo ya Taifa letu. Kwa niaba yangu mimi mwenyewe lakini kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbinga Vijijini natoa hongera sana sana sana kwa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitajikita kwenye maeneo mawili. Eneo la kwanza ni eneo hili la maduhuli ya Serikali. Ninaipongeza Serikali, naona wanafanya jitihada mbalimbali za makusanyo lakini bado tupo nyuma sana kama taarifa ya Waziri inavyosema na hata taarifa ya Kamati imeeleza hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka uliopita tulitarajia kukusanya kwa asilimia 100, lakini kwa bahati mbaya sana tumefikia asilimia 42. Hata hivyo bado mwaka huu nimeona tumejiwekea malengo ya ongeleko la asilimia 11. Mimi hofu yangu tu ni kwamba, ikiwa mwaka jana hatukufikia malengo hata kwa nusu kwanini awamu hii tumejiwekea malengo yanayozidi tena kwa asilimia 11? Ipo mikakati gani, mikakati ipi tumejiwekea ya kwenda kuyafikia haya malengo ya mwaka huu? Kwa hiyo niombe Wizara kwa dhati kabisa, wenzangu wamesema hapa, na mzungumzaji aliyetangulia amesema hapa; sisi kule vijijjni wananchi wetu wapo tayari kumiliki ardhi lakini tunanyimwa fursa hii wananchi wetu hawana hati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa hawana hati tunawanyima fursa nyingine lakini pia sisi Serikali tunajinyima fursa ya kupata haya maduhuli ambayo pengine tungefikia haya malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niiombe niiombe sana sana sana Serikali, kama tumejiwekea ongezeko hili la asilimia 11 basi tuone na mikakati ya dhati kabisa, kabisa kabisa; na mimi nawaamini, ninamuamini Mheshimiwa Waziri lakini ninamuamini Mheshimiwa Naibu Waziri, uwezo huo mnao, nawaomba sana tufanya mabadiliko. Tumeona kwenye kilimo mambo yanakwenda, tuone pia hapa kwenye ardhi; hili ongezeko hili la asilimia 11 tuweze kulifikia. Na hatuwezi kulifikia kwa kuzungumza tu hapa, tunataka tuone mikakati ya dhati. Hivyo nikuombe Mheshimiwa Waziri utakapokuja kuhitimisha hoja hapa kesho utueleze mikakati inayowezesha kufanikisha mpango huu kwa sababu fursa zipo kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni kuhusu migogoro. Ninaiona jitihada ya Serikali ya kutatua hii migogoro ya ardhi, ipo, lakini migogoro hii utatuzi wake unachelewa sana. Tumesikia kuna Tume, kuna Kamati lakini majibu mpaka leo

hakuna. Na tutambue ndugu zangu, kucheleweshwa kwa haki hizi tunawachelewesha Watanzania fursa nyingine; tunawachelewesha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na wanasema haki iliyocheleweshwa ni sawa na haki iliyopotea. Kwa hiyo niwaombe sana ndugu zangu, niombe Wizara tufanye juu chini migogoro hii itatuliwe kwa wakati. Nitaomba pia Mheshimiwa Waziri utupe hatua gani utachukua ili kuharakisha utatuzi wa migogoro hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitolee mfano kwenye jimbo langu pale upo mgogoro tangu miaka iliyopita na mimi nimeukuta. Wamekuja viongozi, upo, mpaka leo hii, katika Kijiji cha Ndika. Ndika hii niliisemea mwaka jana, na naishukuru Wizara, kwa sababu mlikuwa wote na Mheshimiwa Lukuvi, alijaribu kutoa maelekezo yalipunguza migogoro zaidi kwa sababu ilifikia hatua watu walikuwa wanarushiana risasi pale. Risasi zilipigwa na mapanga yalipigwa kwasababu maeneo ya watu ya kulima yamechukuliwa bila hata yakufuata utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi hapa niombe sana mnisaidie mgogoro huu huishe, kwa sababu mpaka ninavyosema sasa hivi wananchi wamejipanga kuacha kupeleka watoto shule wakisema tutapelekaje watoto shule wakiwa wana njaa? Kwa sababu maeneo yao waliyokuwa wanalima siku zote hawalimi tena, ni miaka zaidi ya mitano hawalimi wanakaa tu kusubiri Serikali itatuondolea kero hii, Serikali itatatua mgogoro huu, mgogoro hautatuliki mpaka leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe sana Wizara. Jitihada mwaka jana ilionekana lakini haijafikia mwisho. Kwa hiyo niombe sana Kijiji cha Mkuka, Kijiji cha Mkuani lakini pia kata ya Jirani ya Langilo na kata ya Kipapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi inafika sehemu, kwa sababu watu wa TFS wao ndio wanaoonekana kufanya ulinzi eneo lile, wananchi hata kupita njia wanahofu. Na ni kweli ukipita wanakufanyisha mazoezi ya kichurachura sijui na nini! Kwa kweli niombe Wizara tutatue migogoro hii haraka haraka. Kwa kuchelewesha kutatua migogoro hii, kama nilivyosema pale mwanzo, watu wanakosa fursa ya kimaendeleo kwa sababu hawazalishi. Watu wanakosa chakula, na ndiyo maana sasa wamesema Mheshimiwa Mbunge sisi hatutapeleka watoto wetu shule, hatuwezi kupeleka watoto shule wakiwa na njaa. Miaka mitano hadi sita mgogoro tu wa eneo la wakulima hautatuliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimshukuru Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya, amekuja naye muda mfupi pale ameanza kuchukua hatua. Kwa ushirikiano wetu, kwa maana ya Wizara naye pengine tutayafikia haya majibu haraka au kwa wepesi zaidi. Kwa hiyo, nawaomba sana Mheshimiwa Waziri utakapokuja kujumuisha hapa, unipe majibu ya namna ambavyo tunaenda kumaliza huu mgogoro. Kwa leo nilikuwa sina mengi, nilitaka nisema haya, nawashukuruni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Benaya Kapinga, tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Kakunda, Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo na Mheshimiwa Mwita Waitara, wajiandae.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nianze tu kwa kusema kwamba hii Tuzo ya Babacar Ndiaye ambayo Rais alitunukiwa juzi ni kielelezo kwamba Afrika na Dunia inatambua kwamba viongozi wetu wa Chama cha Mapinduzi na Serikali ya Tanzania wanafanya kazi zao kwa maslahi ya wananchi walio wengi.

Hongera sana Rais Samia pamoja na Serikali nzima kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tamko la Azimio la Arusha lililopitishwa kule Arusha tarehe 29 mwezi wa Kwanza mwaka 1967 na kutangazwa na Mwalimu Nyerere pale Dar es Salaam tarehe 5 mwezi wa Pili mwaka 1967 kama uamuzi wa Watanzania kuondoa unyonge wao kiuchumi bado baadhi ya mauzui yake yana umuhimu sana hadi leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Azimio la Arusha, sura inayozungumzia wananchi na kilimo ukurasa wa 22; Mwalimu Nyerere anasema, nanukuu: "Maendeleo ya nchi huletwa na watu, hayaletwi na fedha. Fedha ni matokeo, siyo msingi wa maendeleo." Anasema, ili tuendelee twahitaji vitu vinne; kwanza watu; pili, ardhi; tatu, siasa safi; na nne, uongozi bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imepita miaka 55 tangu Azimio la Arusha, na kadri miaka inavyosonga mbele ndani ya mageuzi ya kiuchumi na kisiasa yaliyoanza katikati ya miaka ya 1980, nchi yetu kama sehemu ya dunia kwa sasa inazidi kutambua nguvu ya mtaji katika maendeleo, na hasa katika uwekezaji, mitaji ya uwekezaji kwenye sekta za kilimo, viwanda na biashara. Polepole tunaanza kutambua kwamba tunahitaji mitaji ili tufanye kazi za maendeleo hasa kwenye uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, misingi ya uwekezaji nayo ipo minne. Msingi wa kwanza wa uwekezaji ni gharama nafuu za usafiri na usafirishaji na ndiyo maana Serikali inawekeza sana kwenye miundombinu, sitaki kuitaja. Msingi wa pili ni gharama nafuu za huduma za uendeshaji wa mitambo, maana yake hapo utahitaji mafuta; upatikanaji wa mafuta wa uhakika, utahitaji maji ya uhakika, umeme wa uhakika na mambo mengine yanayofanana na hayo kwa ajili ya kuendesha mitambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa tatu wa uwekezaji ni upatikanaji wa uhakika wa malighafi viwandani kwa mwaka mzima na hapo ndipo unakuta kuna umuhimu wa kuwekeza kwa ajili ya kuongeza uzalishaji katika Sekta ya Kilimo. Kilimo kinalimwa vijijini, hakilimwi mjini; hapo ndiyo *point* yangu ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa nne wa uwekezaji ni nguvu kazi yenye ujuzi ambayo ni ya uhakika. Ndiyo maana Serikali inatakiwa kuwekeza sana kwenye vyuo vya ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukiwa na misingi hiyo minne kwenye uwekezaji tutafanya vizuri. Sasa tatizo liko wapi? Kama alivyosema Mwalimu Nyerere, tunahitaji watu, ardhi safi na uongozi bora, tatizo kubwa lipo kwenye ardhi mpaka sasa hivi. Ni rahisi mtu kusema mbona ardhi tunayo ya kutosha? Unawezaje kui-*transform* ardhi ilete nguvu ya kiuchumi katika nchi? Iweze kusisimua uchumi wa nchi? Ndiyo maana huwa naamini kila siku kwamba Waziri wa Ardhi ndio Waziri wa Uchumi, kwa sababu hakuna *activity* yoyote inayoweza ikafanyika katika dunia hii nje ya ardhi. Hata kama ni madini, lazima uyachimbe kupitia ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ardhi ndipo penye tatizo la msingi. Hadi sasa Watanzania wanaomiliki ardhi ni chini ya asilimia 10. Hili ni tatizo kubwa. Tuna sheria zetu kuu mbili za ardhi; Sheria Na. 4 ya vijiji na Sheria Na. 5 ya Ardhi ya jumla kwenye miji na maeneo mengine yaliyohifadhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kwenye miji lina unafuu kidogo kuliko tatizo lililopo vijijini, kwa sababu mjini mtu akikomaa katika kufuatilia ardhi yake atapatiwa hati, lakini kijijini hata ukikomaa, kama kijiji chako hakijapimwa mpango wa matumizi bora ya ardhi, huwezi kupata hati ya kimila. Hapo ndiyo tatizo lipo. Kwa sababu tuna fursa nyingi sana sasa hivi za mitaji kupitia benki, hata Serikali imewezesha benki kama *CRDB* na *NMB* zinatoza 9% tu kwenye mikopo ya kuwekeza kwenye kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa fursa kama ipo kwenye kilimo, na kilimo kinalimwa vijijini, watu watawekezaje kwenye kilimo kama hawawezi kukopa kwenye benki? Hapo ndiyo tatizo la msingi lipo. Watu wanaomiliki ardhi kwenye vijiji ambavyo havijapimwa, hawawezi kuitumia fursa hiyo kwa sababu sheria ya mikopo inayohusu kuweka rehani chini ya masharti maalumu; "*The Mortgage Financing (Special Provisions) Act,* ya mwaka 2008 inaweka utaratibu ni namna gani mtu atumie hati yake kuweka rehani nyumba, ardhi au kitu chochote kisichohamishika. Sheria hii inawapa unafuu watu wa mijini. Watu wa vijijini hawana unafuu wowote kama kijiji hakijapimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naweka *point* yangu vizuri, na ninaomba sana Serikali iweke kipaumbele katika kupima ardhi ya vijijini. Aidha kupima au kuweka *provision* nyingine kwenye sheria ambazo zitamruhusu mtu wa kijijini aweze kupata hatimiliki ya kimila kwa haraka iwezekanavyo na siyo kusubiri ile milolongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ya Tume ya Taifa ya Upangaji wa Ardhi Vijijini inasema kwamba tuna vijiji 12,665 na taarifa ya Tume ya Ardhi inasema mwaka huu wa fedha 2021/2022 walipangiwa kwenye bajeti Shilingi bilioni 1.5 peke yake; na hadi Februari mwishoni walikuwa wamepewa Shilingi milioni 800. Katika hizo milioni 800 wamepima vijiji 239.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Sheria ya Ardhi ipitishwe mwaka 1999, hadi leo nilivyosimama hapa Bungeni kuzungumza, Wizara ya Ardhi imeweza kupima vijiji 2,560 peke yake, kati ya vijiji hivyo nilivyovitaja. Ina maana hii ni asilimia ngapi? Ni asilimia 20, bado vijiji 11,005. Kama kasi hii ya kupanga fedha, Shilingi bilioni 1.5 itaendelea hivyo, Wizara ya Ardhi itachukua miaka 140 kupima ardhi yote ya vijijini. Sasa hii ni hatari. Maana yake ni kwamba tutachelewesha maendeleo ya Watanzania kwa muda wa miaka 140. Iina

maana upimaji utakamilika mwaka 2,160, nani atakuwa anaishi hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo ndipo kwenye tatizo kubwa. Naomba sana wananchi wa vijijini, Serikali iweze kuwapa haki ya kumiliki ardhi tena kwa haraka, tusipoteze muda. Ninashauri hatua mbili Serikali itekeleze. Hatua ya kwanza Serikali ifanye marekebisho ya Sheria ya Ardhi ya Vijiji ili mtu yeyote mkazi wa kijijini ambaye anatambuliwa na *register* ya kijiji kama mwanakijiji, kama atataka ardhi yake ipimwe apate hati ya kimila, asisubiri mpango wa matumizi bora ya ardhi ya kijiji yote. Kwa hiyo, apate nini? Apate mambo matatu; kwanza, apate Muhtasari wa Mkutano Mkuu wa Kijiji kwamba anaruhusiwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji kupima ardhi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, muhtasari huo wa Mkutano Mkuu wa Kijiji uidhinishwe na Kamati ya Ardhi ya Baraza la Madiwani. Ukishaidhinishwa upate *approval* ya Mkuu wa Wilaya husika ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi ya Wilaya. Akishapata hivyo vitu vitatu, huyo mtu apimiwe ardhi yake bila kusubiri. Hiyo ndiyo itakuwa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia sentesi yako Mheshimiwa.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia. Hatua nyingine ya pili ambayo napendekeza kwa wale watu ambao wanalenga kuitumia ardhi kwa ajili ya kuweka rehani, kwa ajili ya kupata mikopo vijijini Waziri wa Fedha na Mipango, alete marekebisho kwenye *Finance Bill* ya mwaka huu 2022 ambayo itaruhusu sasa Watanzania wanaotaka kukopa kwa kuweka rehani mali zao vijijini, wapimiwe ardhi zao kwa approval ambazo nimesema hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ninaomba Serikali itekeleze hayo maoni ambayo nimeshauri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Kakunda. Namwita Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, Mheshimiwa Mwita Waitara na Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga, wajiandae.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana nami kwa kunipatia fursa ya kutoa mchango wangu. Nianze kwanza kwa kuwapongeza sana mtangulizi wa Wizara hii, Mzee wangu, Mheshimiwa Lukuvi alifanya kazi kubwa, lakini nampongeza Mheshimiwa Waziri, Mama yangu Angelina Mabula na Naibu wake Ridhiwani, mnafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri ambazo zinafanyika ndani ya Wizara hii, baadhi ya mambo yanatia dosari, hata ule uzuri wa mambo makubwa ambayo yamefanyika unakuwa hauleti ladha. Jambo hilo ni migogoro ya ardhi. Kila maeneo ndani ya Taifa hili huwezi kukosa migogoro sugu ya ardhi. Pamoja na kwamba kamati zinaundwa, lakini huwa migogoro ya ardhi ndani ya Taifa hili inachukua muda mrefu na hakuna suluhu, wala huoni kama kuna mwaka wa kuleta suluhu kwenye migogoro hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano. Nichukue mfano wa mgogoro mmoja ambao nadhani ni mgogoro kongwe ndani ya Taifa hili ni *GN* 28 ya kule kwetu Mbarali. Huu mgogoro tangu mimi niko binti, sasa hivi naelekea utu uzima, mgogoro huu bado na hatuelewi hata nini hatima yake. Kwa masikitiko makubwa zaidi, hii Kamati ya Waheshimiwa Mawaziri nane, imefika Mbeya mara mbili na wananchi walikuwa wanaisubiri kwa hamu mno wakijua kwamba sasa

ile neema iliyotangazwa na Mheshimiwa Rais kujua ni vijiji gani vitarasimishwa virudi kwa wananchi au vibaki kwenye hifadhi vitatajwa, Mbeya kamati hii imekuja mara mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara ya kwanza walipofika waliishia Mbeya Mjini, wakasema tutarudi tena. Wamefika mara ya pili mwezi uliopita, hakuna majibu. Wamesema sasa hivi tunauachia mkoa, watakuja kupitia upya. Kwa kweli inatia uchungu. Leo hii ukifika kule nyumbani kwetu Mbarali, muulize hata mtoto wa miaka mitano, akutajie matatizo matatu ya wilaya hii, atakwambia la kwanza ardhi, lapili ardhi, la tatu ardhi, atasahau hata shida za maji wala barabara. Ni kwa sababu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mgogoro huu tumepoteza ndugu zetu. Wanawake wamepoteza waume zao, watoto wamepoteza baba zao kupitia mgogoro huu, watu wanapoteza maisha. Siku moja alikuja Mbunge wa Jimbo letu la Mbarali, Mzee Mtega, alileta Taarifa Binafsi humu ndani, Waheshimiwa Wabunge walitokwa na machozi jinsi unyama unavyofanyika kisa mgogoro huu. Inasikitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro wa takribani miaka 15, kila siku wananchi hawajui hatima yao. Halafu wananchi wa Mbarali siyo mara yao ya kwanza kuhamishwa. Walihamishwa; vijiji 10 vilishahamishwa na watu hawapo maeneo hayo waovu, lakini sasa hivi ngoja nikutajie; maeneo kwa mfano, Msangaji, Upagama, Ukwaheri, Idunda, Ikoga, Kapunga, huku kote watu walishaondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti zilizoonyeshwa, ni kwamba wakibaki watu maeneo haya wataathiri Mto Ruaha, na maeneo hayo hakuna watu, sehemu kubwa watu waliondoka. Baada ya watu kuondoka maeneo hayo, walikubaliana kati ya mamlaka zilizokuwepo na wananchi.

Hawa watu waliondoka bila mtutu, wakaambiwa na wakaelewa. Baadaye wakakubaliana mipaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limekuja kutoka tangazo la *GN* 28, wamekuja hata lile eneo ambalo hawa wananchi walihamishiwa Luhanga na kwenyewe kukaonekana tena kuko ndani ya hifadhi; vijiji 33 vingine vipo ndani ya hifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi wana-Mbarali hatima yetu ni nini? Kwa kweli tunaumia. Kila siku tunapata misiba. Kweli Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi ishindwe kufanya maamuzi kwenye jambo hilo ambalo linatesa watu hivi! Siyo sawa. Wamekuja Waheshimiwa Wabunge mbalimbali humu ndani, kila siku *GN* 28, kila siku linaongelewa na taarifa zinaletwa, lakini hakuna. Yaani tunachukulia rahisi tu. Siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekit, tunaamini kabisa viongozi wetu wa juu ambao ni Waheshimiwa Marais huwa wanakuwa ndiyo wamiliki wa ardhi kwa niaba ya wananchi, na kwenye hili tayari kuna matamko mbalimbali ya viongozi wetu ambayo yametolewa kwa kuwaambia; ngoja nianze kwanza kunukuu. Februari, 2015 aliyekuwa Waziri wa Maliasili, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu alifika Mbarali, alitumwa na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne, alisema haya yafuatayo, nakukuu: "Mheshimiwa Rais wetu ameridhia, baada ya wananchi wa kata hizo zilizoondolewa, hakuna mwananchi yeyote atakayeondolewa katika vijiji vilivyobakia." Kwa hiyo, wananchi endeleeni na shughuli zenu za maendeleo, akaendelea: "ninaagiza viongozi wa Mkoa wa Mbeya, Njombe na Iringa muanze kuchukua hatua za haraka za kurekebisha tangazo hilo lililoleta mabadiliko ya mipaka ya eneo hili kwa ajili ya kupeleka Bungeni, kwa ajili ya kubadili sheria hiyo." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 4 mpaka tarehe 6 mwezi wa Kumi 2018 Hayati Rais wa Awamu ya Tano aliagiza Makatibu 11 waende Mbarali wakiongozwa na Katibu Mkuu aliopo Ofisi ya Waziri Mkuu, Mambo ya Sera na Uratibu Prof. Faustine Kazomola, huyu ndio alikuwa kiongozi wa kamati hiyo, walikaa Mbarali kwa siku hizo tatu; tarehe 4 mpaka tarehe 6 kushughulikia suala hilo. Baada ya hapo, Januari, 2019 tarehe 15, naomba ninukuu maneno ya Mheshimiwa Rais Hayati Dkt. Magufuli ambaye ndio alikuwa *guarantor* wa *land* hii hapa, alisema: "Vijiji vyote vilivyobainishwa viko ndani ya hifadhi, visiondolewe. Ninaagiza mamlaka husika zianze kufanya mchakato wa kuvirasimisha vijiji hivyo. Natoa mwezi mmoja mchakato wa kuanza mabadiliko ya sheria ili yapelekwe Bungeni." Tarehe hiyo hiyo ndiyo aliyoteua kamati ya kwanza ya Mawaziri nane kushughulikia migogoro hii na migogoro mingine ambayo haijapatta ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekit, sisi tulitarajia baada ya kauli ya Mheshimiwa Rais hii, kazi ya kwanza ya Kamati pamoja na migogoro mingine ambayo ipo maeneo mengine, kazi ya Kamati kwa Mbarali ilishatolewa maelekezo na maeneo ambayo ni hatarishi watu walishaondoka. Kuna shida gani Mbarali? Kuna shida gani Mbarali? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia, malizia Mheshimiwa.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Bahati Ndingo. Tunaendelea na Mheshimiwa Mwita Waitara, baadaye Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga, na Mheshimiwa Deus Clement Sangu, ajiandae.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Ninazo salamu kutoka Jimbo la Tarime Vijijini kwa Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan wakimpongeza kupata tuzo na kutambulika kama kiongozi mashuhuri duniani katika viongozi 100, na bahati nzuri amepeleka fedha za miundombinu barabara ya kutoka Tarime – Mugumu na Mkandarasi yuko *site,* watalii wataongezeka, watapeleka ujumbe kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii kama ambavyo wenzangu wamezungumza ni Wizara ambayo ingeweza kutuvusha sana na kuwafanya watu wakaendelea, lakini kwa kauli ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwamba kuna mambo manne ili nchi iendelee, eneo la ardhi bado kuna shida kubwa sana. Mheshimiwa Waziri lazima ajipange na wenzake Naibu Waziri kufanya kazi hiyo kwa kweli. Karibu kila jimbo kila mahali kuna migogoro mingi ambayo imedumu kwa muda mrefu zaidi na palipo na migogoro maana yake hakuna maelewano, hakuna maendeleo, ni ugomvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwangu kule Tarime Vijijini, tunayo madai ya wananchi wangu ya kulipwa fidia, ukienda eneo la Nyamichele tangu 2019. Nenda pale Murwambe, Matongo na Komarera kule kuna shida. Haya mambo ni muhimu yakafanyiwa kazi, kwa sababu eneo la Tarime kwa asili sisi watu ni wengi, ardhi ni kidogo sana haitoshi. Hata vita ya koo ambayo ilikuwa inapigana kule Tarime mnasema *Warenchoka* na *Wanchali* mpaka mkatubatiza majina kwa sababu shida kubwa ni ardhi, watu hawana sehemu ya kulima. Sasa kule Tarime ardhi ni finyu, haitoshi lakini wananchi wanajua kwa uhakika kwamba ndani ya ardhi yao kuna dhahabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fidia ambayo inalipwa, eti hekari moja Serikali inalipa Shilingi Milioni tano. Hata Waziri akipewa fedha hiyo akatafute ardhi hawezi kununua kwa kiasi hicho. Bahati mbaya wametengeneza migogoro wenyewe, wanachukua tangazo wanabandika kwamba ardhi hii tutaihitaji, yaani mwananchi akiona umebandika tangazo aache kulima, kujenga au kuendeleza chochote kile kwa sababu utamlipa. Hakuna mkataba, hakuna makubaliano, hivi ikitokea mwekezaji hataki eneo la mtu na hakuna makubaliano, unafanyaje? Hayo ndiyo madai yaliyopo pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nyamichele waliwaambia wasubiri watawalipa, hawakulipwa mpaka leo. Matokeo yake wale Wazungu wa Mgodi wa Barrick wamechimba *underground*. Watu mazao yao yalikatwa, nyumba zilibomolewa, watu wana shida muda mrefu sana. Katibu Mkuu Kijazi alipita kule Nyamichele, akanikuta Tarime, nikamwambia watu wa Nyamichele wanataka kauli ya kiongozi, tathmini inafanyika lini? Unajua walimsimamisha hata hakusalimia kabisa akafunga vioo akaondoka, nikapata wakati mgumu kwelikweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waambie viongozi kazi mojawapo ya Mheshimiwa Rais kumsaidia ni kutatua kero za wananchi, hata kama huna majibu. Wananchi wanalalamika, simama uwasikilize, utapokea hoja zao, utasema nimezibeba, naenda kuzifanyia kazi. Hayo maeneo ni vizuri fidia ikalipwa, Nyamichele, Komarera na Murwambe. Katika maeneo haya kuna mazao ya watu mengine nimeambiwa yalikatwa, kuna majina pale yapo. Mheshimiwa Waziri alikuwa Naibu Waziri kwenye Wizara hiyo, walikuwa na Mheshimiwa Lukuvi, walifanya kazi nzuri sana, siyo vibaya akiiga au akaendeleza walikoishia, kwa sababu anajua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapendeza sana wananchi wakilalamika, kiongozi aende awasikilize. Asiende Musoma Mjini, aenda awasikilize, kuna malalamiko mengi ambayo wananchi hawana majibu. Sasa kuna uchonganishi unafanyika pale Tarime kwenye eneo la mgodi. Wale *valuers* wanaowatuma, wanawaambia gharama ni ndogo imepangwa. Ukienda kwenye mgodi wanasema fedha zipo za kuwalipa, wanatuchelewesha. Wanaona viongozi wa Serikali hatuwasaidii, Wabunge hatuwasemei, mgodi una fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara waende ili waondoe changamoto hiyo, waongee lugha moja. Kile ambacho mgodi unasema lazima pia kauli hiyohiyo iende kwa wananchi. Wasiamini kwamba hatuwezi kuwasaidia ili waweze kulipwa fedha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni muhimu sana kama kuna makubaliano wanataka waingie na wananchi wenye maeneo yao na kumekuwa na tabia ya kuchelewa kuwalipa, kuwe na mkataba kwamba kama unachukua eneo langu unakaa nao miaka miwili, miaka mitatu, ikitokea wewe hujanilipa fidia na mimi sikujiendeleza unalipa *compensation* ya kuchelewesha muda. Mtu anakaa miaka 10, enelo lake hajawahi kulipwa mpaka leo na hakuna chochote kile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wanalalamika sana wananchi, ni muhimu kuwa na makubaliano. Nchi hii inaongozwa kwa sheria, tufuate sheria za ardhi. Kama unataka eneo langu tukubaliane, unalipa fidia, hulipi fidia, unipe muda ambao umenichelewesha kufanya kazi za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, mipaka ya hifadhi. Katika watu ambao kwa kweli wana mambo mengi ya kulalamikia ni pamoja na Tarime Vijijini. Eneo la Kata ya

Nyanungu, Kata ya Gorong'a, Kata ya Nyarokoba, Kata ya Kwihancha ni maeneo ambayo kumsikia mtu amepotea, siyo ajabu. Kwamba watu wamechukua ng'ombe za watu wameenda kupiga mnada mchana kweupe, siyo ajabu, kwamba mtu ameliwa na fisi, siyo ajabu, kwamba Kamati imeundwa na hakuna majibu, siyo ajabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais Hayati Magufuli alikuwa na nia njema na Mheshimiwa Rais Mama Samia ameunga palepale, ametoa maelekezo akafanya maamuzi. Yaani Mawaziri Nane wanashindwa kwenda kusikiliza wananchi wenye migogoro, wanaenda kukaa Musoma kwenye Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, kweli? Wanashindwa kwenda *site,* wanasoma *beacon* ambazo yaani wamepokea taarifa ya *SANAPA*. Yaani mimi Waitara namlalamikia hapa Amar, halafu wewe unakuja unachukua taarifa za Amar, unanihukumu nazo. *This is not fair*, siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitarajia kwamba katika kutatua hii migogoro, viongozi waende wakae chini, Mbunge, Diwani, Mkuu wa Mkoa, DC na wananchi wote wawepo ndiyo watu waseme migogoro na tutatue hizo changamoto. Hii habari ya kujifungia na kutuandikia taarifa siyo sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wemekwenda Musona na Mheshimiwa Waziri alikuwepo, lakini hawakwenda Nyamungo, Gorong'a, Kwihancha au Nyarukoba, lakini wataalam wake wamewaambiwa wananchi Mbunge wenu alikuwepo, alishirikishwa, je, Mheshimiwa Waziri anataka nyumbani kwangu wachome moto? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wakienda wakaweka *beacon,* wakahamisha watu, Mbunge maana yake ameridhia watu wahamishwe, lakini kama ningekuwepo na wananchi wakawepo, wale wananchi wamezaliwa pale

miaka ya 1980, miaka 1970 wanajua mipaka yao, wangesaidia maelezo kwa Mheshimiwa Rais kwa nia njema ili afanye maamuzi, watu waishi. Kwa kweli hakuna maendeleo kule, sasa kumekuwa na chuki kati ya watu wa hifadhi, wananchi, viongozi, hapaeleweki, duniani hatupo, ahera hatupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima watusaidie vizuri, siyo sawasawa kwa kweli na migogoro imekaa muda mrefu sana. Ukiona kila Mbunge hapa analalamika kila kona, hawa Mawaziri ni muhimu sana. Pia ni muhimu hili Bunge, mambo yote ambayo yamekaa muda mrefu, malalamiko ya majimbo mengi, ya wananchi wengi, Bunge litoe muda maalum wa changamoto hizo kutatuliwa. Tusiwe hewani hewani, kama tunawapa miezi sita, Mheshimiwa Waziri akafanye kazi na wenzake, alete majibu kwenye Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ilivyo kila mtu anajisikia. Nilisikia wanasema eti hawana hela ya mafuta kwenda kule Nyamongo, eti mtaalam hana hela ya kwenda kule kuangalia migogoro ya wananchi. Wananchi hawa ili tuwaongoze vizuri lazima tuwasikilize, lazima tutatue changamoto zao, usipofanya hivyo itakuwa siyo sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne, migogoro ya wakulima na wafugaji. Hii Wizara kama nilivyosema Mheshimiwa Waziri akifanya kazi vizuri na wenzake na uwezo huo anao labda maamuzi tu, ni muhimu sana kwa sababu haiwezekani Wabunge wa Bunge hili, unajua watu wanauana kule, mwenye ng'ombe ni adui wa mkulima, mkulima ni adui wa mfugaji na sisi ni viongozi, Serikali ipo, sheria ipo, ardhi haipangwi, hii haikubaliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima watu wetu waishi kwa ustaarabu. Kama kuna mtu anafuga tujue wapi wanafuga

ng'ombe, mbuzi, kondoo, maeneo yatengwe. Kama kuna sehemu watu wanalima tujue wanalima sehemu hiyo, iende, ndiyo uongozi wa nchi. Haitakuwa sawa kama tunakaa hapa watu wanauana, Watanzania wenyewe kwa wenyewe wanauana. Watu walewale, jamii ile ile halafu kuna Mbunge, kuna Diwani, kuna Viongozi, siyo sawasawa. Lazima tukubaliane, maeneo yapimwe, wale wafugaji wale siyo maadui wa wakulima, ila viongozi hatujachukua nafasi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inabidi tupange mpango vizuri, watu wanaofuga ng'ombe wafuge, au mfugo wa aina fulani wafuge, anayelima alime ili tuuziane. Hawa wanahitaji nyama, huyu anahitaji chakula, kuna shida gani? Tupangeni, jambo hili ni muhimu sana. Mbunge kusimama hapa anakutajia watu waliouwawa, hawajaugua, siyo bahati mbaya, kwa mapanga na sisi viongozi tupo, hilo lazima lifanyiwe kazi na Bunge hili kwani kazi yake ni hiyo kulinda watu wake, kuwasimamia Watanzania waishi kwa ustaarabu mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne, Mheshimiwa Naibu Waziri anafahamu, yeye alikuwa Naibu Waziri na ameenda kutatua mgogoro pale Mlitolegebasi. Watu walipigana mishale, wakapigana mapanga kwa sababu ya ule mgogoro, mpaka leo Mheshimiwa Waziri hajawahi kwenda pale na ule mgogoro upo. Kwa hiyo, wakati wa uchaguzi tunafanya kazi ya kugombea na kusuluhisha migogoro. Tumalize migogoro sasa kabla ya uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda wakati wa uchaguzi unaambiwa wewe umekuja kwa sababu unataka kula, Hapana. Tumesema mara kadhaa, tunawakumbusha tena, mahali popote katika majimbo yetu, kwenye mikoa yetu, kwenye wilaya yetu, kwenye vijiji vyetu, vitongoji vyetu, tarafa zetu, Waziri aainishe migogoro hiyo waifanyie kazi, tusifanye

kazi ya kuzima moto, muda wanao, nafasi wanazo, dhamana wamepewa, watatue changamoto za wananchi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili, Mheshimiwa Mwita.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Katika eneo hili ningependa nijue Mheshimiwa Waziri fidia ya Nyamichele, Komarera, Murwambe ni lini? Nitashika shilingi na nitakatalia mpaka Tarime Vijijini aifuate kule Nyanungu kwenye mgogoro wa ardhi, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwita Waitara. Tunaendelea na Mheshimiwa Asia Abdukarimu Halamga, atafuatiwa na Mheshimiwa Deus Clement Sangu na Mheshimiwa Cosato Chumi ajiandae.

Mheshimiwa Asia hayupo, Mheshimiwa Deus Clement Sangu.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii ambayo umenipatia ili niweze kuchangia mawazo yangu kwenye hoja hii ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hii tuzo aliyoipata kama Azimio la Bunge la leo lililofanyika hapa nami niunge mkono kumpongeza Rais wetu kuwa mwanamiundombinu bora. Tuendelee kumwombea, achape kazi kadri Mwenyezi Mungu atakavyomjalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya na

nilifarijika sana leo alipoanza kusoma hotuba yake ndani ya Bunge amesoma kwa kumtanguliza Mwenyezi Mungu. Naamini Roho Mtakatifu atamshukia na haya nitakayoyasema leo humu ndani, Roho Mtakatifu aliyemwomba amwongoze katika kusoma hotuba yake akamwongoze pia katika kuyatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa lililofanya nisimame katika Wizara hii leo ni jambo ambalo limekuwa sintofahamu kwa takribani miaka 13 sasa. Jambo lenyewe linahusu uwekezaji wa mwekezaji aliyekuja kuwekeza katika Shamba la Malonje ambaye anaitwa *Efatha Ministry*. Hili jambo ukiliongelea na akifika kule Mheshimiwa Waziri, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Lukuvi pamoja na yeye akiwa Naibu Waziri, wamepigana nalo jambo hili na miaka mitano hii ilivyopita palikuwa na utulivu kidogo, lakini ninavyoongea sasa hivi jambo hili limefufuka upya na hali ni mbaya sana kutokana na huyu mwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwekezaji huyu alikuja mwaka 2009, alipewa shamba lililokuwa la *NAFCO,* hekta 25,000, aliuziwa kwa Shilingi Milioni 600, kwa maana hekari moja aliuziwa Shilingi 24,000. Alipofika pale yeye alikuja kama mwekezaji anayekuja kufuga na baadaye makubaliano yalibadilika kwamba yeye atafanya shughuli ya kilimo. Sasa shida ilikuja pale ambapo alianza kuingilia mipaka ya wananchi wanaozunguka shamba lake hilo hekta 25,000. Sitaki kwenda mbali kwenye historia, lakini nataka niende kwenye matatizo yaliyojitokeza kwenye uwekezaji huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na shida ya unyanyasaji kwa wananchi, analazimisha kwenda kuingia kwenye vijiji ambavyo mipaka yake haipo. Kijiji kimesajiliwa, kimepewa hati kabisa, huyu mwekezaji anaenda analazimisha hata eneo la kijiji aendelee kulimiliki yeye. Naomba hapa Mheshimiwa Waziri anielewe, siyo kwamba yule ni mwekezaji, namwita dalali na nina sababu ya kumwita

dalali kwa sababu hekta 25,000 alizokabidhiwa, hajafanya uwekezaji unaofikia hata hekta 1,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile ardhi kwetu ina thamani kubwa sana. Ile ardhi inaweza kusaidia nchi kuondokana na upungufu wa zao la ngano kwa sababu ndiyo ardhi yenye rutuba kubwa. Sasa hivi nchi yetu tunaagiza ngano nje, tunatumia zaidi ya Bilioni 520 na uzalishaji wetu kama nchi tunazalisha tu tani 70,000 na mahitaji ni tani milioni moja. Eneo lile analomiliki yule *Efatha Ministry* linaweza likazalisha tani 44,000 na kuondoa nakisi. Ina maana nusu ya ngano tunayozalisha ndani ya nchi hii lile shamba linaweza kuzalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yeye alikuja kuchukua lile shamba, akafanya likawa *collateral,* akaenda kutafuta *financing* kwenye *financial institution,* baadaye aka-*deviate* zile *fund,* hamna kinachoendelea, ni mateso kwa wananchi. Kuna wananchi wangu wa pale Sikaungwi, juzi tu ameenda na *bulldozer,* zaidi ya ekari 70, ameenda kukatakata mazao, tena kwa kutumia vyombo vyetu vya dola, vina-*facilitate* mtu kufanya uhalifu wa kukandamiza haki ya wananchi wanyonge maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja hapa leo, Wizara iliwapa wale hati na nyaraka zote toka Wizarani ninazo hapa nitakabidhi mezani. Nawaomba jambo moja, kama huyu ambaye anahodhi ardhi ambayo haina manufaa miaka 13 iko *idle,* wanamwona ana maana kubwa na ana *muscles* kuzidi Serikali, niwaombe jambo moja, wawachukue wananchi wale 5,722 wa pale Sikaungu wawatafutie eneo kama walivyowatafutia watu wa Ngorongoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu hawawezi kwenda kuishi pale, hawana shamba la kulima na ni maisha yao, wale siyo wafanyakazi walioajiriwa, ajira yao ni kilimo, sasa wamempa mtu amehodhi, amechukua hati

ameenda kuchukulia fedha kwenye mabenki, wananchi wanakaa hawana mahali pa ku-*develop* mambo yao ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe mama yangu Mheshimiwa Waziri, jambo hili lina sintofahamu kubwa. Siyo Kijiji cha Sikaungu tu, kuna Kijiji cha Sandulula, Msanda Muungano, kuna Kijiji cha Songambele Azimio, Malonje kwa ndugu yangu Aeshi na pia Mawenzusi naye atasimama atasema. Hali ni mbaya, wananchi hawaelewi jambo lolote. Mwekezaji huyu kwa nini anafugwa? Amechukua hekari 25,000, haendelezi chochote, hamna kazi inayoendelea, yuko tu pale. Sisi tuna shida, mimi nimepiga hesabu zangu, kama tungepata mwekezaji *proper* kwenye ardhi ile tungeweza kupata mapato kama halmashauri kwa mwaka shilingi milioni 500. Kwa miaka 13 tungekuwa tumejenga vituo vya afya 13 kutokana na mapato ambayo halmashauri ingepata kwenye shamba lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri na Naibu nimeteta naye sana na jambo hili najua Waziri alikuwa Naibu Waziri analijua. Ilifikia hatua mpaka huyu mwekezaji anakata wananchi masikio, yaani masikio. Kuna mwananchi mmoja anaitwa Martin yuko pale Sandulula mpaka leo ni mlemavu anavyopigwa na yule mwekezaji. Mbaya zaidi kuna wananchi basi kwa sababu wana fedha na anaweza akahonga hapa na pale, aliweza mpaka kusababisha wananchi wakafungwa gerezani miaka mitano, wameenda na mahakama ikakuta hawakuwa na hatia, lakini wale wananchi wamepoteza miaka mitano gerezani. Wananchi wa Sikaungu hawana hatia yoyote, masikini ya Mungu wamerudi ni maskini, lakini kwa sababu wanajua haki yao hawaachi kupambana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suluhu labda kama Wizara itashindwa kuwatafutia sehemu ya Kwenda, wajiandae wale wananchi wako radhi 5,000 wote waje wawaue palepale,

wawazike Sikaungu. Kwa sababu haiwezekani, mwekezaji huyu ana ubabe gani? Kumekuwa na vitu fulani vya ajabu mimi naviona pale, mwanzoni mnakuwa timu ya watu wengi mna-*fight,* baadaye unaona wenzako wanarudi nyuma kwenye mamlaka hizi hizi za Serikali. Ukishaona hivyo ujue wenzako wamepigwa mlungula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi peke yangu, mimi Deus Clement Sangu niliyechaguliwa na wananchi wa Jimbo la Kwela nitasimama peke yangu, hata ikinigharimu Maisha, kwa sababu haiwezekani wananchi wananyanyasika sana. Ule mgogoro umeleta adha kubwa, wananchi mwaka huu hawajalima na kidogo walichokuja kulima amekuja kupita na *bulldozer,* eti anaweka mipaka. Mipaka si pande mbili mnakaa kama kuna mipaka mnaweka? Hivi wewe unaweza ukatoka peke yako ukaja kujiwekea mipaka? Haiwezekani jambo hili! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli mbaya iliyoniudhi, naomba niiseme na kwa kweli Mheshimiwa Waziri na Waziri wa Mambo ya Ndani nawaomba sana, kauli ya mwekezaji kuja kuongea, kudharau mamlaka ya nchi hii ambayo imekaa kihalali, sitakubaliana. Akirudia tena ama zangu ama zake kule jimboni. Yeye anasema kwamba, haya, mliyemtegemea amekufa, sasa narudi na kweli miaka mitano yote; Mheshimiwa Lukuvi ni shahidi, palikuwa kimya. Siku tatu baada ya Hayati Magufuli kufa akaja halafu anatamka kauli za kudharau mamlaka halali ya nchi hii, sitakubali. Kama wa kwanza kupigwa risasi kwenye shamba lile la Wanasikaungu nitakuwa mimi Mbunge wao niliyekuja kuwawakilisha ndani ya Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wamwambie kauli za kukashfu mamlaka za nchi hii iwe mwisho. Aishie huko huko, asije kudharau mamlaka, wananchi wanampenda Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia,

wanamuunga mkono, asije akafanya kwamba yeye ni mbabe kuliko Serikali. Tutamalizana huko huko *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongea kwa uchungu mkubwa, naona nchi ambavyo hatupigi maendeleo, tunalia humu Bungeni hata ndugu yangu Mheshimiwa Bashe nilimwambia haiwezekani, sisi tuna ardhi yenye rutuba, ardhi nzuri iko *idle* mtu mmoja amehodhi tu haendelezi, njooni tufanye maamuzi, nikamshauri Bashe amwandikie barua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tuna vijana wengi *graduates* hawana ajira, wanahangaika Jimboni kwangu. Tungeenda pale tukafanyia *block farming,* wakapewa mle mkopo na Benki yetu ya Kilimo. Nimeenda Benki ya Kilimo nikafanya mazungumzo, wakasema tunahitaji ku-*finance* kwenye sekta ya ngano, lakini watapata wapi ardhi? Kuna mabepari wamehodhi ardhi na hawaendelezi, vijana wetu wanarandaranda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe, kwa kweli nitalisimamia hili…*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Deus Sangu

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha tu, mama sitaunga mkono, nitashika shilingi mpaka aje atupe majawabu yanayostahili juu ya mgogoro wa lile shamba. Wananchi wa Sikaungu, Sandulula na Msanda Muungano wamenituma nije nipaze sauti humu ndani ya Bunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Deus Sangu. Tunaendelea na Mheshimiwa Cosato Chumi, ambaye

atafuatiwa na Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim na Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma wajiandae.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa haraka napenda kutumia nafasi hii kuwapongeza viongozi wenzetu walioteuliwa Mama Anjelina pamoja na ndugu yangu Ridhiwan ambaye kule kwenye Bunge *Sports Club* huwa tunamwita *super sub* yaani yule mchezaji anayeingia kipindi cha pili akishasoma mchezo, akiingia basi mambo yanakuwa vizuri magori yanatililika na ndiyo maana tukawa mabingwa kwenye michezo ya Mabunge ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, naamini hata huko kwenye ardhi, ataendeleza mazuri anayoyafanya tukiwa uwanjani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kumpongeza Katibu Mkuu, mzee Kijazi, ni mtu rahimu pamoja na timu yake na Naibu Katibu Mkuu wake. Pia napenda kuipongeza Wizara hasa ambavyo imeshusha huduma mpaka ngazi ya mikoa. Kwa mfano sisi watu wa Mafinga zamani ilikuwa lazima twende kwenye Ofisi ya Kanda kule Mbeya lakini sasa ofisi iko palepale Iringa, napongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imetokea nimepata huduma kwa baadhi ya Makamishna akiwemo Kamishna wetu wa pale Iringa ndugu Mtui, Kamishna Msaidizi wa hapa Dodoma ndugu Kabonge na Kamishna wa Dar es Salaam ndugu Kayela. Ni watu ambao wanafanya kazi vizuri na ni wasikivu, naamini na Makamishna wengine wote wanafanya kazi vizuri chini ya Kamishna wao ndugu Mathew ambaye kwa kweli ni mtu ambaye kama una jambo la wananchi wako anakusikiliza vizuri. Hivi ndivyo ambavyo inatakiwa tufanye kazi katika kuwahudumia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizi napenda kusema kwamba migogoro mingi ambayo watu wengi wameisema tunaweza tukaitatua tukiwa na mpango

bora wa matumizi ya ardhi na tukiiwezesha ipasavyo Tume yetu ya Matumizi Bora ya Ardhi lakini na hizo ofisi zetu ipasavyo, kwa sababu bila kupanga kupima na kumilikisha bado migogoro itaendelea kuwepo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Tanzania tuna *square km* 945,087 wakati nchi kama Vietnam wao wana *square km 391,690* lakini hawana migogoro, maana yake ni kwamba ardhi tunayo bwerere lakini kitu kinachotushinda pengine ni kuipangia matumizi bora ambayo itatuwezesha kupunguza migogoro. Ndiyo maana sisi Halmashauri ya Mji wa Mafinga tumejielekeza pamoja na kupima viwanja lakini tumeona ya kwamba tujielekeze katika kuwa na maeneo kwa ajili ya uwekezaji, kwa ajili ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetenga sasa eneo karibu heka 700 kwa ajili ya *Industrial Park,* maana yake ni kwamba sasa tunakuja mbele ya Wizara kuomba mtuwezeshe tuweze kupima, kupanga na kumilikisha, tukishakuwa na hii *industrial park* maana yake ni kwamba Wawekezaji watakuja, vijana wetu watapata ajira, Halmashauri itapata mapato lakini na Serikali nayo itapata mapato katika ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa kwa nini tumeamua hivyo, kwa sababu Mafinga na Mufindi ni Miji ambayo inakua kwa kasi, kuna viwanda vingi, lakini baadhi ya Wawekezaji wamejikuta wakati mwingine wanaingia katika mikono ya watu ambao sio waaminifu, pia wakati mwingine viwanda vinawekwa maeneo ambayo siyo vizuri kiusalama kwa sababu ni maeneo ya karibu na makazi ya watu, ni maeneo kwa sababu hayakupangwa kuwa ni maeneo ya viwanda kama Halmashauri tunashindwa kufikisha huduma muhimu kama za maji, barabara na hata wenzetu wa *TANESCO* inawawia vigumu kufikisha huduma ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba Wizara ituangalie Mafinga kwa macho mawili, katika suala hili la

*Industrial Park* na kwa kweli tumedhamiria, hapa ninapozungumza Mkuu wangu wa Wilaya Ndugu Saada Mtambule pamoja na timu ya Mkurugenzi wapo *EPZ*A kuweza kujifunza, kwa sababu tunataka kuwa *modal* ambao tutakuwa na *Industrial Park* ambayo itakuwa suluhisho pia kwa ajira za vijana wetu. Kwa hiyo ninawaomba sana Wizara ituangalie kama itakuwa ni *grant,* ama utaratibu wowote ambao utaona inaweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupanga, kupima na kumilikisha kunasaidia mambo mengi, kwa mfano kunaipunguzia Serikali gharama wakati ambapo ingekuwa imepanga hatuwezi kuingia kwenye gharama za kujipa hizi fidia, pia mara nyingi inapunguza migogoro, tukipanga pia tunakuwa na maeneo kwa ajili ya huduma mbalimbali. Kwa mfano, hapa katika eneo letu la Bunge, utaona ya kwamba eneo hili kadri huduma zinavyohitajika unaona kabisa tunahitaji eneo kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tukijadili hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu jambo hili lilijitokeza kwamba tuone umuhimu wa kuongeza au kupanua eneo hili la Viwanja vya Bunge, jambo hili kwa mujibu wa maelezo ilielezwa ya kwamba linapelekwa Wizara ya Ardhi ili wenzetu watusaidie kufanya uthamini ili kuona uwezekano kwa mujibu wa taratibu za Serikali kama wanaotuzunguka tunaweza tukawalipa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo, maeneo haya ya Bunge humu ndani tuna Muhimili wa Bunge, tuna Mheshimiwa Spika ambae ni Kiongozi wa Muhimili, pia yupo Mheshimiwa Waziri Mkuu ambae ni Kiongozi wa Shughuli za Serikali pamoja na Mawaziri wake, yupo Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Watumishi wa Serikali, kwa mfano leo hii wako Makamishna, wako watu wa Wizara ya Ardhi. Vilevile wakati Mheshimiwa Rais akija hapa kuhutubia Bunge au wakati wa Bajeti Kuu, Viongozi wengi wa

Taifa letu huwa wanakuwepo hapa katika Viwanja vya Bunge kwa maana ya kwamba Serikali huwa iko hapa. Wanakuwepo viongozi wastaafu, wanakuwepo viongozi wa vyombo vya dola, wanakuwepo Viongozi Wakuu wa Chama cha Mapinduzi sasa mimi nalitazama hili katika jicho la kiusalama zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwa jinsi ilivyo ndiyo maana nashauri kwamba mchakato huu wa kuongeza eneo la Bunge uende kwa haraka kwa sababu gani, tufikirie Serikali yote iko hapa, kama mtu ana nia ya kufanya jambo baya *just* ukitoka tu hapa mlango wa geti la Waziri Mkuu tayari unakuta pale ni maeneo ambayo ni maghala, kwa mfano mbele pale kuna maeneo ambayo ni bohari ya mafuta ambayo hata kiusalama kama limetokea jambo, *is high risk* na katika usalama wanasema, katika *security* huwezi ku-*compromise* mambo ya gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ninaomba wenzetu wa Wizara ya Ardhi pale ambapo wana wajibu wa kutusaidia kufanya tathimini na kufanya uthaminishaji basi wakamilishe hilo zoezi ili kusudi Bunge yale maeneo ambayo yanayotuzunguka yaweze kuchukuliwa kwa mukhtadha wa hilo jicho ambalo nasema ni jicho la kiusalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata jicho la kihuduma wananchi wetu wanakuja hapa kutaka kupata huduma mara nyingi *the most you can do* wakipata kibali wataingia watakusubiri kule kantini. Nakumbuka wakati wa mgogoro wetu wa nguzo na Serikali walipokuja watu wa nguzo ilibidi tukae pale kantini, lakini tukamuomba *OS* wa Bunge akatusaidia tupate ofisi tujadili lile jambo na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na baadaye likapata suhuhisho. Kwa hiyo, hata kihuduma vinginevyo utakuta tunakutana na wananchi wetu kule nje kwenye magari ili tusikilize hoja zao, kama wanataka kumwona Waziri kwa hiyo pia kihuduma na kiusalama ninashauri sana kile kipengele au ile *section*

ambayo wenzetu wa Wizara ya Ardhi wanalifanyia kazi walifanyie kazi kwa haraka na tuende mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili kutoka mwisho ni suala la Baraza la Ardhi. Wananchi wa Mufindi wanalazimika kusafiri kwenda Iringa wanapokuwa na shughuli zao za masuluhisho ya masuala ya ardhi, nimwombe Mheshimiwa Waziri na Serikali, imefika wakati sasa tuwe na Baraza la Ardhi pale Mafinga ambalo litahudumia Wilaya ya Mufindi, kwa sababu mtu kutoka Mgololo, Kitasengwa, Bumilahinga, Itimbo kwenda Iringa ni mbali, kwa hiyo ninaomba wizara ione na sisi kama Wilaya tuko tayari kutoa jengo kwa ajili ya huduma hiyo muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho kwa dakika moja ninaomba Serikali ingalie watu wanapouziana ardhi, zile gharama tunazolipa ili kufanya *transfer* kwa kweli watu wengi wananunua ardhi, kama mimi nikiuziana na Mheshimiwa Bonnah hapa, kwa sababu tunaaminiana naogopa kuhamisha ule umiliki kwa sababu ya zile gharama, hebu tuziangalie ili watu wafanye *transfer* na baadae weweze kulipa kodi za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nasisitiza tena kama nilivyosema asubuhi Mungu abariki viongozi wetu, Mungu abariki Taifa letu Mungu abariki Mafinga pia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Cosato Chumi, Waheshimiwa Wabunge wakati tunaendelea na michango kuna tangazo hapa. Mheshimiwa Waziri Mkuu hatakuwepo kuanzia leo tarehe 26 Mei kwa shughuli za kikazi nje ya Dodoma kwa hivyo Mheshimiwa Kapt. Mstaafu George Huruma Mkuchika ambaye ni Waziri wa Nchi Kazi Maalum atakuwa anakaimu nafasi za Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni hadi hapo Mheshimiwa Waziri Mkuu atakaporudi.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Mwanahamis Kassim, Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwijuma na Mheshimiwa Francis Mtega wajiandae.

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi kunipa nafasi hii kuweza kuchangia jioni hii ya leo. Mimi nichukue nafasi hii kwanza kumuombea Mama yangu Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayofanya nchi hii Mwenyezi Mungu ampe nguvu ampe afya, ampe uzima lakini ampe uvumilivu ampe na Subira, Mwenyezi Mungu tunasema Alhamdulillah basi Mwenyezi Mungu anakuwezesha kwa mambo mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite moja kwa moja nimpongee Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Naibu Waziri na Katibu Mkuu na Viongozi wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuitumikia nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nijikite moja kwa moja kwenye Wizara hii ya Ardhi, wenzetu hawa Wizara ya Ardhi wanafanya mambo makubwa, mimi ni Mjumbe wa Kamati hii tumezunguka maeneo mengi wanafanya kazi kubwa sana, migogoro hii itaendelea kuwepo na itakuwa ipo madhari sisi binadamu bado tupo kwenye dunia hii. Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi imeandikwa kuwa ardhi itapimwa nchi nzima na sisi tunatarajia ni hivyo kwa sababu nia ipo na sababu ipo ya kupimwa ardhi ya nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza migogoro, migogoro ni binadamu, sisi ndiyo tunayoitengeneza lakini na wale wanaosimamia kwenye kitengo hiki cha ardhi, pale wamefanya neno lililokuwa zuri basi tusema Alhamdulillah tuwashukuru tuwapongeze na Mama yangu, Dada yangu wanafanya kazi kubwa sana. Kwa kweli ardhi ilikuwa mahtuti iko *ICU* lakini leo ardhi inazungumzika, migogoro mingi imetatuliwa, mambo mengi yamefanywa, kwa hivyo tuseme

tu tuwaombee wenzetu waendelee na kazi hii kazi hii ni kubwa, kazi hii siyo ya mtu mmoja ni yetu sote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jukumu letu sote Wabunge kusimamia ardhi na kusimamia wananchi wetu tusiipe nguvu migogoro, kwa sababu tunalaumu migogoro lakini kuna migogoro mingine inatengenezwa, na watengenezaji ni wanasiasa. Hapa tunapigia kelele lakini mimi ni Mjumbe wa Kamati tumezunguka sana, hatujamaliza lakini tulikoenda kote ni kuzuri watu wanapewa hati zao wanapokea kina mama, baba, vijana, kwa kweli wenzetu wanafanya kazi kubwa, mimi nasema Alhamdulillah Mwenyezi Munge awawezeshe waendelee kuwatumikia watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizungumzia ardhi usimsahau Mheshimiwa Lukuvi. Mheshimiwa Lukuvi alifanya kazi kubwa sana ya nchi hii, alipewa Wizara ya Ardhi iko mbovu, huwezi kufanya ziara kamati ikienda kwenye sehemu ya ardhi kama utapokewa, ilikuwa ni matatizo makubwa lakini Alhamdulillah unapokwenda wananchi wanakuelewa wanaweka vikao wenyewe wanakuita mnazungumza mnapaga wanataka kupimiwa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mie niombe Serikali na Waziri wa Fedha yupo Wizara ya Ardhi hii iongezewe pesa, pesa ni ndogo wanayopewa hata tukiwalalamikia waje watupimie au watusikilize watu wanataka kupimiwa ardhi pesa ni ndogo wanayotengewa, kwa hiyo mimi nilikuwa naomba Serikali lazima isimamie ardhi. Ardhi ni kila kitu na wananchi sasa hivi ni waelewa wanajua kila kitu, kwa sababu ardhi ndio kila kitu, kilimo ardhi, ukienda kwenye maji ardhi, ukienda sehemu zote lazima tuwe na ardhi nzuri safi iliyokuwa haina migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lukuvi alifanya mambo makubwa sana, sisi tumekwenda Kigamboni tulipokewa kwa mapanga na kama Mbunge wa Kigamboni

yupo ananisikia, alitupigia simu tulifika kwenye Pantoni hatukushuka lakini wananchi walituzonga, lakini leo nenda Kigamboni utapokewa na ngoma utapigiwa kwa sababu ardhi imepimwana ambayo haijapimwa lakini itapimwa kwa sababu ni ilani ya Chama cha Mapinduzi na Waziri wetu ni wa Chama cha Mapinduzi na Naibu Waziri ni wa Chama cha Mapinduzi, kwa hiyo ni lazima ardhi itapimwa lakini tunaomba pesa Wizara ya Ardhi iongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite moja kwa moja kwenye *National House, National House* pia walifanya kazi nzuri. Ndugu yangu Mchechu alifanya mambo makubwa sana, huyu kijana alifanya mambo makubwa sana, kwa hivyo tumpongeze na tumuombee kwa Mwenyezi Mungu amerudi pale pana viporo tele alivyovianzisha sasa aviendeleze viporo vile lakini nimuombe Mheshimiwa Mchechu arudi Kigamboni, tulisema tutaupanga Mji uwe wa Kisasa kwa hivyo warudi pale waende wakaupange Mji wa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri nisema naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, tunaendelea na Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwijuma Mheshimiwa Francis Mtega, Mheshimiwa Jafari Wambura Chege ajiandae.

**MHE. HAMIS M. MWINJUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa hii na mimi niweze kuchangia kwenya hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Sina hakika kuhusiana na mambo niliyoandika yalivyo mengi kwa hiyo nitaenda moja kwa moja kwenye hoja yangu, kama muda utaniruhusu nitaleta pongezi zangu mwishoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukianza kwa nukuu kutoka kwa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, anasema: ‘‘Ili nchi

iendelee na ipate maendeleo inahitaji watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora." Kwa kichwa kizuri kama cha Mwalimu Nyerere ambacho tunakubaliana kwamba hata ambao hawakubaliani na siasa zake huko duniani wanakubaliana na ubora wa kichwa chake, kuiweka ardhi miongoni mwa vitu vinne muhimu kwa ajili ya maendeleo ya Taifa siyo kitu kidogo hiki wote tunakubaliana nacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo mimi ninachoona ni kwamba kwanza suala la ardhi kuwa miongoni mwa vitu vinne muhimu kwa ajili ya maendeleo ya Taifa, ni zawadi na laana. Ni zawadi kwa sababu ardhi tunayo kubwa na kama itatumika ipasavyo kwa sheria tulizojiwekea na wasimamizi wake wakafanya vile ambavyo tumewatuma kufanya, itatuelea maendeleo bila wasiwasi wowote, lakini ni laana kama yatafanyika kinyume chake.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa ardhi unafanya uwezekano wa kuepuka kabisa migogoro ya ardhi kutokuwepo, migogoro ya ardhi ni kitu ambacho tunatakiwa kuishi nacho, tuifanyie kazi tuisuluhishe kila wakati kuhakikisha kwamba wananchi wanyonge wanapata haki zao kama wananchi ambao wana nguvu kuliko wengine. Kwa hiyo, ni *ongoing* nisichokubaliana nacho ni jinsi ambavyo tunatengeneza migogoro na mingine ambayo pengine tungeweza kuitatua wakati ni midogo tunaiacha inakuwa milima mikubwa ambayo inakuwa migumu kuitatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna Mbunge hata mmoja kwenye Bunge hili tufuku wa Jimbo ambae hana mgogoro kimeo wa ardhi kwenye Jimbo lake, hiyo inakuonyesha jinsi ambavyo kuna matatizo makubwa ya ardhi kwenye nchi hii. Sasa pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri alisema kwamba mikutano 1,800 kwa ajili ya usuluhushi wa migogoro ya ardhi ilifanyika mwaka uliopita, lakini bado nimuombe Mheshimiwa Waziri afanye mikutano zaidi aendelee kwa nguvu nyingi asichoke mama yangu na ndugu yangu

Ridhiwani pia muendelee kwenda *site* kuhakikisha migogoro ya ardhi inaendelea kutatuliwa siku hadi siku, siamani kwamba kuna siku tutafika hatuna hata mgogoro mmoja wa ardhi kwenye nchi hii lakini angalau tuibadilishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro iliyokuwapo juzi na siku kabla ya juzi isiwepo leo na kesho. Katika Jimboni la Muheza tuna matatizo makubwa ya ardhi, mathalani naweza kuorodhesha migogoro karibu 15 hapa, lakini kwa sababu ya muda nina miwili ambayo ya mfano, kwanza kwenye Tarafa ya Amani, tuna mwekezaji *East Usambara Tea Company* ambaye anamiliki hekari 35,000 za ardhi, kati ya hekari 35 kulikuwa na viwanda vitano vyakuchakata chai ni viwanda viwili tu vinafanya kazi sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vitatu vilivyobaki vimebaki kuwa magofu ambayo yanafungwa yamekuwa majumba ya kifahari pamba na nyoka kule Amani. Kati ya hekari 35,000 ambazo Mwekezaji huyu anazimiliki ni hekari 5,000 tu ambazo zinatumika kulimia chai. Sasa kule Amani kila kitu kinaota, tunayo mashamba mpaka ya mpira huu unaotengeneza matairi, tuna mashamba ya iriki, mdalasini karafuu na kadhalika. Wananchi wa Kata zote Sita za Tarafa ya Amani wanamiliki robo heka, robo heka kwa sababu Mwekezaji ameshikilia ardhi ambayo haifanyii kitu kwa zaidi miaka 25 sasa! Unashirikia hekari 30,000 ambazo huzifanyii kitu katika ardhi ambayo Kata zote Sita hakuna hata hatua moja kwa ajili ya kujenga shule. Kwa mfano, Kijiji cha Magoda Kata ya Kisiwani wanataka hata eneo la kujenga Ofisi ya Kijiji hakuna ardhi ya kufanya hivyo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanataka eneo la kujenga Shule ya Msingi na Zahanati hakuna eneo la kufanya hivyo na kuna mtu ameishikilia hekari 30,000, *my good guess* ni kwamba amelichukua eneo ameenda kulitumia kama *collateral* kwa ajili ya kupata *financing* kufanya biashara zake

nyingine wakati wananchi wa Tarafa ya Amani wanapata shida! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Misalai katika Kijiji cha Misalai hakuna hata hatua moja kwa ajili ya kufanya shughuli za makazi. Shamba Ngeda wanataka eneo kwa ajili ya kufanya shughuli za kilimo lakini hawawezi, hakuna hata hatua moja. Mbomole wanataka kufanya ujenzi wa shule ya sekondari hakuna ardhi, wanataka kujenga zahanati na shughuli za kilimo lakini hakuna ardhi hata hatua moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nilisema mwanzoni, ardhi hii inasitawi kila kitu. Sasa mwekezaji anapoiwekea ardhi eka 30,000 ambayo haifanyii chochote huku ni kuwaonea wananchi wanyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kwenye, naomba niitafute ili nisikosee, ukisoma kweney misingi mikuu ya ardhi kitaifa, ukiacha wa kwanza ambao unasema ardhi yote ni mali ya umma na imekabidhiwa kwa Rais kama mdhamini na msimamizi mkuu kwa niaba ya Watanzania wote, wa nne unasema kudhibiti kiasi ambacho mtu mmoja au taasisi yaweza kumiliki na kutumia kwa mahitaji yake bila kuwaathiri Watanzania na wanajamii wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapofika mahali wananjamii wengine hawana sehemu hata ya kujenga ofisi ya kijiji ama darasa moja la shule ilhali kuna mtu ana ekari 30,000 ameziweka tu amekwenda kuzichukulia mkopo sehemu huku ni kuwaonea wananchi wanyonge na Kwenda kinyume na misingi ya umiliki wa ardhi ambayo tumejiwekea kwenye nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye taifa ambalo serikali yake inasimama kwa niaba ya wanajamii wote, na inasimama kwa niaba ya watu, linapotokea suala la ukinzani kati ya watu na maendeleo basi Serikali inachagua upande

wa watu. Sasa hili limekwenda mbali zaidi, hili ni watu na wanataka maendeleo halafu upande mwingine kuna mtu mmoja anayehakikisha watu hawa hawapati maendeleo.

Mimi niwaomba wawakilishi wa Mheshimiwa Rais kwenye upande huu wa ardhi, Mheshimiw Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Katibu Mkuu mfanya mnavyofanya, twendeni site mkawasikilize wananchi, mkawasikilize wasaidizi wenu kwenye halmashauri, na ikiwezekana na Kamishna wa Ardhi wa Mkoa ili kuona namna ambavyo tunaweza kuwasaidia wananchi wale wanyonge.

MheshimiwaMwenyekiti, wito wangu ni kumshauri Mheshimiwa Rais, kwamba mashamba haya ambayo hayatumiki yafutiwe hati na wananchi wagawiwe ili waweze kufanya shughuli zao za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mfano wa pili katika ya 15 ambayo ningependa kuitoa lakini nikasema nitasema miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wa pili ni kuhusiana na jinsi ambavyo watu ambao tumewapa mamlaka ya kutafsiri sheria za ardhi kwa ajili ya jamii nzima wanavyotukosea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2017 laliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati John Pombe Magufuli, Mungu amrehemu, alipita Mkoani Tanga. Miongoni mwa vitu alivyovifanya ni kufuta hati sita za yaliyokuwa mashamba ya mkonge kwa sababu yalikuwa hayatumiki. Kwenye mkutano wa hadhara pale Mkanyageni aliamrisha kwamba shamba lililokuwa la *Geiglits* ambalo lilikuwa katika Kijiji cha Muungano ligawiwe kwa wananchi wa maeneo yale; kwamba kila mwananchi apate eka tatu, na mwenye uwezo wa kuendeleza apate ekari tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2017 mpaka sasa hivi ni mwaka 2022, nikuambie kwamba zoezi hili halijafanyika hata

kwa asilimia 20. Sasa unapata walakini, maelekezo yalikuwa wazi, kwamba kuna eneo kuna wananchi, idadi ya kaya inafahamika kwa sababu Mheshimiwa Rais hawezi kufuta, na akaamrisha kwamba kila kaya ipate eka tatu. Vivyo hivyo mchakato ule haujaweza kutimia hadi leo. Sasa una watu, una ardhi, kila kimoja unajua ukubwa wake lakini zoezi hili linashindikana kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili pia nimuombe Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri na wasaidizi wao twende tukawasikilize wananchi. Moja, tupate vielelezo kutoka kwa wananchi, maafisa wa ardhi kule chini na tuone kitu ambacho tunaweza kukifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule chini kuna kamati ya wazee tisa kwenye Kijiji cha Muungano pale Kilapula, mzee mmoja anaitwa Dkt. Mhada amenitumia email 22, yaani imepita juzi tu, na Mheshimiwa Mnzava ni shahidi wangu, sija-*exaggerate* kituo chochote. Email 22 zenye vielelezo za kwa nini anahisi wananchi wanyonge wanaonewa na wanataka kudhulumiwa ardhi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisemi kwamba iamuliwe tu kwamba wakagawiwe, lakini twende tukawasikilize na tuone vielelezo ambavyo wanavyo na tuamua kwa *conscience* zetu zikiwa *clear* kabisa, tukiwa tumejitosheleza na vile vielelekezo ambavyo wanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi iko mingi sana Wilayani Muheza, na ninaomba Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri wanipe angalau siku tatu za kuambatana nao kule kuhakikisha kwamba tunakwenda kuitatua yote. Sina mpango wa kushika shilingi, kusema kweli kama mtaniahidi hilo wakati mnakuja kufanya majuisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na niwapongeze na Mheshimiwa Rais, na ninaamini mtafanya kazi nzuri.

Niwahakikishie, sisi tuko pamoja nanyi. Wananchi wa Wilaya ya Muheza wana Imani kubwa na Serikali yao ya Awamu ya Sita, chini ya Mama, Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Niwahakikishie kwamba kama tutawaondolea kero hizi ndogondogo basi mtashangaa na matokeo ya kuungwa mkono ambayo mtayapata kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma. Tunaendelea na Mheshimiwa Francis Mtega, Mheshimiwa Jafari Wambura Chege na Mheshimiwa Edward Ole-Lekaita wajiandae.

**MHE. FRANCIS L. MTEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuishukuru Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan. Niwashukuru sana viongozi wakuu wa kitaifa, nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Naibu Waziri, watendaji wote wa Wizara kwa kuwa na sera nzuri ya upimaji ardhi, urasimishaji na utoaji wa hati za ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nioneshe masikitiko yangu makubwa kuhusu migogoro ya ardhi; na kwa kweli mgogoro sugu wa ardhi uliopo Wilayani Mbarali ni GN namba 28. Ninamshukuru Mheshimiwa Bahati Ndingo ametoka kusema muda si mrefu; vijiji ambavyo vilihamishwa rasmi taratibu zote zilifuatwa na malipo yalifanyika. Isitoshe walilipwa mara mbili walipofanya uthamini mara ya pili, kwa hiyo tunashukuru kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilipeleka miundombinu sehemu ambazo wana Mbarali wanatakiwa sasa waishi kwa

amani na bila bughudha yoyote. Cha kushangaza na kusikitisha, wataalam wamekwenda kinyemela kuongeza mipaka bila ushirikishwaji wowote kwa wananchi. Kwa kweli kitendo hiki kimetuumiza sana, na mpaka sasa hivi ni mateso yanaendelea kwa wananchi wa Mbarali, achilia mbali vitendo vya kutisha, kama vile mauaji; mara tuokote nywele, mara kichwa, mara mifupa na viongozi wetu kupigwa sana na kuumizwa sana.

Mheshimiwa lakini pia ziko athari za kimaendeleo. Kwa mfano Mheshimiwa Rais ametoa fedha za kujengea Shule ya Sekondari Luhanga, shilingi milioni 600, lakini pia akatoa fedha kwa ajili ya vituo shikizi zaidi ya vine. Cha kushangaza ni kwamba wateule wake wamezihamisha zile fedha bila taarifa yoyote kwa wananchi. Wananchi wameshikwa na taharuki kubwa, wanashangaa; Mheshimiwa Rais anavyopenda wananchi wake, ameleta fedha halafu tena zimehamishwa, kwanini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, na majibu rahisi huwa wanasema kuwa haya ni maamuzi ya Mheshimiwa Rais. Sasa, matumizi mabaya ya jina la Mheshimiwa Rais kwa kweli hii inasikitisha sana na haikubaliki. Nimetembelea Luhanga, nimefanya kikao pale, nimeshuhudia mwenye wananchi kwa nguvu zao wamejitoa, wamechangishana; na ugumu walio nao lakini wameweza kujenga majengo ya shule ya sekondari, na wamekamilisha vyumba vitatu na ofisi moja; na matundu ya vyoo ilikuwa bado kidogo kukamilisha, mimi nikajitolea mifuko ya saruji ili wakamilishe kwa dhumuni la kunusuru watoto wale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu iliyopita watoto 60 hawaku-*report* shuleni katika kata ambayo iko jirani. Kwa kweli ni umbali mrefu, zaidi ya kilometa 60 kwenda na kurudi; sasa, watoto wanashindwa kuhudhuria. mwaka huu kati ya watoto 2019 waliochaguliwa kwenda kidato cha kwanza ni Watoto 49 tu wame-report, wengine wote wamepotelea

mitaani na wanachunga ng'ombe. Kwa kweli wanakosa haki yao ya msingi ya kupata elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, cha kushangaza ni kwamba, eneo lile wao wanasema ni hifadhi, mimi wiki iliyopita nilimfuata Mheshimiwa Waziri, kwamba hebu tuangalie kwenye kitabu, eneo lile sikuliona. Wakati huo huo ninafanya kikao pale kuna kijana alisimama, anauliza, anasema, hapa ardhi imeuzwa kwa matajiri, sisi vijana hatujapewa hata ekari moja. Mimi nimewasimamisha wenyeviti wa vijiji pale wajibu hoja, kwamba kwa nini mmeuza ardhi na imekuwaje vijana hawajapewa hata ekari moja. Viongozi wale walianza kuvutana vutana pale; haieleweki nani ameuza. Mheshimiwa Diwani akasema Mheshimiwa Mbunge tunaomba utuachie, hili tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, cha kushangaza, iwapo eneo lile ni hifadhi, imekuwaje matajiri waende wakanunue na kisha watengeneze mashamba? Wao hawaogopi kuhamkishwa?

Mheshimiwa Mwenyikiti, lakini madhara mengine ni kwenye anuani za makazi. Sote tunaelewa, sensa ya tarehe 23 Agosti itajumuisha pamoja na anuani za makazi. Sasa pale Mbarali kuna kata tatu ambazo sehemu kubwa ya vijiji havijawekwa kwenye mpango wa anuani za makazi mpaka sasa hivi ninavyoongea. Hata hivyo, cha ajabu ni kwamba, viongozi wangu walipolalamika kwamba mbona vijiji vingi havijaingizwa kwenye anuani za makazi mimi niliwajulisha kwamba hebu kaeni kwenye kamati ya siasa mje na muhtasari huku Dodoma mtakapokuja kwenye Mkutano Mkuu wa Chama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, walikaa kwenye kamati ya siasa, majibu yakawa ndiyo hayo, kwamba ni maamuzi ya Mheshimiwa Rais. Viongozi wale wa chama wakasema kama

ndivyo hivi sisi kesho tunakwenda Dodoma na muhtasari huu tukaoneshe. Cha kushangaza, asubuhi ile tunapigiwa simu kuwa baadhi ya vijiji wametumwa wataalam Kwenda kuandikisha anuani za makazi. Sasa tunashangaa, kwamba Mheshimiwa Rais anaamua kwa namna hiyo, kama si kumchafua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana kwamba wanancho walikabidhiwa yale maeneo ili waendelee kufanya kazi zao kama kawaida. Wapo waliojenga nyumba nzuri za maana, wako wanaobabaika mpaka sasa wanashindwa kujenga nyumba ilhali wana haki kabisa. Ingalikuwa wao wamehamishwa au wamelipwa fidia sasa hapo ni kweli wasingeweza kupewa anuani za kamakazi. Taratibu hazijafuatwa, sasa kwa nini wasipewe anuani za makazi? Na kama Serikali itaamua kulichukua eneo hilo basi taratibu zifuatwe. Kwamba wajulishwe, washirikishwe, walipe fidia halafu waondoke, kuliko kubaki wanateseka, kwamba hawana uhakika na maisha yao, kwamba tutabaki au tutaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kinachosikitisha zaidi ni usiri mkubwa katika jambo hili. Tumeona Mheshimiwa Waziri Mkuu, mwadilifu, mzalendo mkubwa kabisa, amekwenda pale Ngorongoro, amekaa na wananchi wale wafugaji, amewaelekeza hali halisi, baadhi yao wamekubali na wanaondoka vizuri tu kwa hiari yao. Kwa nini Mbarali kuna siri? Kuna nini nyuma ya pazia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile tume ya mawaziri nane walikwenda Mbeya; viongozi wa chama walipigiwa simu kwamba kesho wanakuja mawaziri, nami wakanijulisha. Jioni yake wakapigiwa simu kuwa ile ziara imeahirishwa, msije, lakini kumbe wanakuja. Sasa, kwa nini watuficHe? Wawakilishi wa wananchi tunatakiwa tuwepo, tusikilize ili tutoke na majibu sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vyombo vya habari ziliandika habari za kutisha wananchi, kwamba sasa vijiji 31 vinakwenda kwenye hifadhi, wananchi wakashangaa. Mimi nimekuja kufuatilia kwa Mheshimiwa Waziri, kwa kweli Mheshimiwa Waziri alikanusha habari za ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesi ya shamba humaliziwa shamba, tunaoumia ni wana-Mbarali. Wanapokwenda Mkoani Mbeya, Mbeya wenyewe wanashangaa kama ambavyo huku wanavyoshangaa. Lakini maumivu tunaopata ni sisi wana-Mbarali…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa tengele yako imeshalia.

**MHE. FRANCIS L. MTEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Francis Mtega. Tunaendelea na Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mheshimiwa Edward Ole-Lekaita, Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo wajiandae.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia Wizara hii ya Ardhi. Nianze tu kwanza kwa kuungana na wenzangu ambao tangu asubuhi wameshiriki kwa pamoja kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa tuzo na zawadi ambazo wenzetu wameweza kumuona na kumtunuku. Kubwa mimi niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo kwenye kila sekta ameweza kuweka mkono wake ili kusaidia, lakini lengo likiwa ni moja tu, kuwasaidia wananchi wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Wizara hii tu peke yake Mheshimiwa Rais ametoa zaidi ya bilioni 50 kwa ajili ya kuhakikisha angalau ardhi ya nchi hii inapangwa, kupimwa pamoja na kumilikishwa. Haijawahi kutokea kwenye ziada ya bajeti kutoa fedha nyingi kiasi hicho ka bajeti ya mwaka jana ambayo angalau imetumika kuanza kupanga, kupima na kumilikisha kwenye baadhi ya maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana fedha ikawa ni ndogo na tukawa hatuoni impact yake, lakini haya yote hatuwezi kuyaona ni kwa sababu ya ukubwa wa eneo la ardhi hii ambalo halijawahi kupangwa, kupimwa na kumilikishwa. Tunazungumza zaidi ya asilimia 75 ya nchi hii haijawahi kupangwa, kupimwa na kumilikishwa. Asilimia 25 pekee ndiyo iliyopangwa, kupimwa na kumilikishwa. Na zaidi ya asilimia 60 ya nchi hii haijapangwa. Kwa hiyo unaweza ukaona kwamba yawezekana fedha imetoka, Wizara ikaichukua ikafanya kazi lakini *impact* yake isionekane kwa haraka kwa sababu ya maeneo mengi bado hayajafanyiwa kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi leo nitajikita sana kwenye kutoa ushauri. Ninajua mchango mkubwa na kazi kubwa wanayoifanya Mawaziri hawa. Kwa sababu kama wenzangu walivyochangia, migogoro ya ardhi ni mtambuka. Hapa leo tukipanga na kupima maeneo yote nchi hii bado tukubaliane kwamba kuna baadhi ya maeneo kutakuwa na migogoro ya ardhi, haiwezi kwisha yote kwa pamoja. Tunachojitahidi sisi ni kuhakikisha ile migogoro ambayo tunaishauri Serikali, ni kuhakikisha angalau inapungua kwa kadiri inavyowezekana ili angalau kutoa haya ambayo yangekuwa yakichangiwa humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nitajikita kwenye sera katika ushauri wangu. La kwanza ninaloliona hapa ambalo linaleta shida kubwa humu ni Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995. Mimi nichukue nafasi hii kumuomba sana

Mheshimiwa Waziri, haya yanayozungumzwa, kitu pekee ambacho kinaweza kikamuokoa ni kuharakisha ile Sera ya Taifa ya Ardhi ambayo imeshapitwa na wakati. Sera ya Taifa ya Ardhi ndiyo ilizaa mabaraza ya ardhi. Mabaraza ya ardhi ngazi za vijiji, kata na wilaya yote haya kuna confusion ya sheria namna ya uratibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukiwa kuna mgogoro kwenye kijiji umetatuliwa na baraza la ardhi la kijiji na haujakwenda sawa sawa atalaumiwa Waziri husika; pamoja na kwamba na yale mabaraza hayawajibiki kwa Mheshimiwa Waziri moja kwa moja ilhali yametajwa kwenye sheria kwamba yanawajibika chini ya mkurugenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi niombe, sera ambayo itatupelekea mabadiliko ya sheria itaondoa hii changamoto iliyopo. Mimi niombe sana kwenye hili, Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI mkimbizane na Mheshimiwa Waziri wa Fedha ili tuone namna tunavyoweza kufanya *review* kwenye sera ili hatimaye tupate sheria nzuri. Haya mabaraza ya ardhi yote yasiwe na *confusion*. Baraza la ardhi la wilaya wanawajibika kwa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, mabaraza ya ardhi ya kata na vijiji yanawajibika kwa Waziri wa TAMISEMI. Hii *confusion* haiwezi kuwa sawa sawa. Kwa hiyo unakuta tayari huku wameharibu, ikija kufika kwenye baraza la ardhi ngazi ya wilaya, hata kama Waziri ataonekana ametatua bado inarudi kwenye Wizara ile ile ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi niombe, ili kuondoa hii *confusion*, kwa sababu imetajwa kwenye sheria, ni lazima tukimbizane kutengeneza sera uya ardhi na kupata sheria ambayo ita-regulate na itasimamiwa kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, tukubaliane; sehemu mbili ambazo zinaweza zikashughulika na changamoto ya migogoro ya ardhi ni mabaraza ya ardhi

pamoja na Tume ya Taifa ya Mipango. Tume ya Taifa ya Mipango, tutakubaliana hapa; kwa mwaka wa jana na mwaka huu peke yake imetengewa bilioni 1.5. kuandaa mpango wa matumizi bora ya kijiji kimoja yanagharimu zaidi ya milioni 11 mpaka milioni 15, kijiji kimoja. Leo mnawapa 1.5, maana yake nini; atakwenda kuandaa mpango wa matumizi bora ukigawanya pale ni vijiji 100 tu peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba, Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo hautakidhi na mpango huu ambao tunazungumza hapa, ambao Mheshimiwa Waziri wa Fedha umeuwasilisha. Wakati huo huo unakuwa kinyume na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Chama cha Mapinduzi hapa inasema, angalau kwa mwaka vijiji vinavyotakiwa kupangiwa matumizi yake visipungue 750. Maana yake ni kwamba, kwa miaka mitano, wame-project mpaka mwaka 2025 tuwe tuna vijiji elfu tatu, mia sab ana kidogo. Lakini sasa hawa watu mnawapa bilioni 1.5, kwa mwaka anapanga vijiji 100 peke yake. Maana yake ni kwamba anakwenda kinyume na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi na Mpango wa Tatu wa Mandeleo ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nimuombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tutafute namna ya kuinusuru hii Wizara. Ile Tume ya Taifa ya Mpango haya yote yanayozungumzwa inatakiwa iende *site*, ishughulike na kutatua migogoro iliyopo kati ya wafugaji na wakulima na migogoro ya mipaka iliyopo. Sasa haiwezi ikatatua kama haina fedha ya kufika kwenye maeneo husika. Hii ndiyo *instrument* ambayo inatakiwa iende ikashughulike na migogoro hiyo, haina fedha, wanakwendaje? Wanatatuaje migogoro?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi niombe, *solution* ya kwanza kabisa ni kuongezewa fedha. Tuwape fedha

angalau waendane na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi inavyosema pamoja na Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa. Vinginevyo tutafanya 25 hawatakuwa na fedha ya kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha, fedha ipo. Mheshimiwa Mdee alizungumza asubuhi hapa vizuri sana, fedha ipo na sehemu ambayo ipo, ukisikiliza Hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa nane, anasema, hakufikia malengo ya makusanyo ya kodi ya ardhi kwa sababu kuna Mashirika ya Umma hayalipi kodi. Wanadaiwa zaidi ya asilimia 70; na wanazalisha zaidi ya Shilingi bilioni 78 Mashirika ya Umma zaidi ya 114. Maana yake ni nini? Yale Mashirikia yakibanwa yakalipa ile Shilingi bilioni 78, tutapata Shilingi bilioni 10 iliyokuwa inaombwa na Tume ya Taifa ya Mipango kwenda kutekeleza jukumu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu haya ni Mashirika ya Umma, ni Mashirika ya Serikali, yanaingia kwenye Bajeti kila mwaka, yatenga fedha kwa ajili ya kulipa kodi ya ardhi na hayalipi, leo hii jioni naomba, kesho tutakapokuwa tunahitimisha, Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri Mkuu angekuwepo tungemwomba, watoe maelekezo na matamko ya haya Mashiriki ili yaweze kubanwa kulipa hii fedha. Kwa sababu vingenevyo, Wizara ya Ardhi kila mwaka inapanga bajeti na ikipanga bajeti inaonesha kwamba Mashirika yaliyopo yanatakiwa kulipa kiasi gani cha kodi ya ardhi, halafu unafika mwishoni, hayalipi ile fedha, unakwenda mwaka mwingine. Hawa watu mtawakamua kadri mnavyoweza lakini hawatafika lengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya ni Mashirika ya Umma, kwa nini mwananchi mnyonge tunamwambia lipa kodi ya ardhi? Shirika la Umma ambalo linatengwa kwenye bajeti, linapewa fedha ya Serikali, hawalipi. Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kigezo kimojawapo cha Mkurugenzi yeyote wa Shirika la Umma ambaye halipi kodi ya

ardhi ili angalau ile fedha iende kushughulikia kutatua migogoro ya wananchi, iende ikatumike kwa shughuli nyingine; na iwe ni kipimo kimojawapo cha kumtathmini kama kweli anaweza kufanya kazi ile. Kwa sababu haina maana kama mashirika mengine yanalipa fedha, halafu wengine hawalipi. Mashirika 114 nchi hii hawalipi, na tunakwenda kumaliza mwezi wa Sita hawatalipa. Wanabeba madeni, yanakwenda mwaka ujao, hawatalipa. Lini Wizara hii itafikia lengo? Lini itapata fedha ili iende kuweza kupanga na kupima maeneo ambayo hayajapimwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba ili tuweze kumnusuru Mheshimiwa Waziri na hii Wizara ya Ardhi, tuhakikishe angalau wale ambao wanatakiwa kulipa kodi kwa wakati, walipe kwa wakati na kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, sambamba na hili kwa Mheshimiwa Waziri, nilisema leo sitakuwa na la kulalamikia, nilitaka tu nishauri kwa namna ambavyo imekaa. Namwomba Mheshimiwa Waziri, tuliwahi kuzungumza toka mwaka 2021 kuhusiana na *Housing Policy*, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kumteua Mheshimiwa Mchechu kurudi kwenye Shirika la Nyumba la Taifa. Najua kwa namna anavyofanya kazi vizuri, ataanza kazi muda wowote wa ujenzi wa hizi nyumba. Shida yangu ni kwamba, anapooanza shughuli zile za ujenzi, kelele huwa zinakuwa nyingi kwamba bei za nyumba zinakuwa kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikisema sana, bei ya nyumba inaweza kuwa *regulated* na *Housing Policy,* lakini inaweza kuwa *regulated* kama tutaipitia tukaainisha maeneo yote namna ya ku-*regulate*. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri pamoja na watu wake wote ndani ya Wizara; Mheshimiwa Naibu mimi naamini kwamba wewe ni kijana umeingia na unafanya kazi vizuri, tuchangamkie hii ili yule atakapoanza Shirika la Nyumba kukimbizana na ujenzi wa

nyumba za gharama nafuu, mwananchi aweze kupata nyumba kwa gharama nafuu kadri inavyowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, naomba maeneo ya mpakani, ya maziwani na baharini tuone namna ya kuweka maboya, tuone namna ku-*identify,* kutenganisha mipaka kati ya Tanzania na zile nchi mbili ili angalau tuondokane na yale ambayo yanayotokea kule. Wananchi kule wanavamiwa, wanapigwa na maeneo mengine wanaumizwa. Naomba sana, mipaka ile, yale maboya yakiwekwa yatasaidia sana maeneo ya maziwa na baharini ili angalau mvuvi wa Uganda anapokuja akiona yale, ajue nikienda naenda Tanzania, huku ninapokwenda naenda kuchukua cha watu. Watanzania nao vivyo hivyo. Naomba sana, pamoja na maeneo mengine, mwone namna ya kulifanya hili kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jafari Wambura Chege. Tunaendelea na Mheshimiwa Edward Olelekaita, halafu Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo na Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, wajiandae.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi. Kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Rais kwa Tuzo ambayo Azimio la Bunge leo limepitisha. Nilifurahi sana kilichoandikwa kwenye tuzo ile, nanukuu: "*The First Female President in East Africa Region, the only Female President in Africa for 2022, for your dedicated services that proves the women ability.*" Mheshimiwa Waziri nikupongeze sana, tunataka tuone *the women ability* kwenye Wizara hii ya Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia Naibu Waziri, Wakili Msomi Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete. *Combination of*

*the women ability* na Wakili, tunatarajia kwa kweli Wizara hii migogoro tunayoisikia kutoka kila mahali itapata majawabu. Kwa kweli niwatie moyo, haya mnayoyasikia kutoka huku, tunawaambia tu kwamba kazi iliyo mbele ni kubwa zaidi, *but we will support you*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Dkt. Allan Kijazi, *very humble* na uzuri ametoka Wizara ya Maliasili na Utalii, na anajua kelele nyingi zilikuwa zinatoka Wizara ya Maliasili na Utalii kwa sababu ya migogoro mingi ambayo ipo. Kwa hiyo, sasa hii timu, *with that experience,* kwa kweli tunatarajia mengi zaidi na migogoro hii itapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ilileta mapendekezo ya sheria tumepitisha mwaka jana, na kwa kweli wameleta maboresho makubwa sana kwenye sheria ile ya migogoro kwa kupunguza nguvu za Mabaraza ya Kata ili waweze tu kusuluhisha tu migogoro kwa sababu ilionekana walikuwa wanafanya ambavyo sivyo kisheria. Wao wabaki kusuluhisha halafu Mahakama zile za ardhi zenye watu ambao wana uelewa wa kisheria wafanye kazi nzuri zaidi. Kwa hiyo, natarajia hayo yatakuwa ni mapinduzi makubwa yenye kuleta *harmony* kwenye migogoro ambayo ipo sasa. Pia walibadilisha sheria na Bunge hili lilipitisha sheria kuruhusu Kiswahili kitumike. Hii itasaidia wananchi kufuatilia hukumu zao kwa Lugha nyepesi kabisa wanayoifahamu. *Big up*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa lililozungumzwa hapa ni la migogoro. Ni kweli tuna migogoro mingi sana vijiji kwa vijiji, mipaka ya vijiji na Hifadhi za Taifa, wakati mwingine mikoa kwa mikoa kubwa sana, na tunashukuru sana. Ni kweli waliompongeza Mheshimiwa Lukuvi, kwa kweli tunatambua sana kazi yake aliyoifanya kubwa. Nakumbuka walikuja Mawaziri nane kule kwangu kule Kiteto Kijiji cha Arkyush kwa mgogoro ambao umedumu kwa miaka 20 kwa Pori la Mkungunero na vijiji. Kwa kweli inashangaza sana kwa

sababu *GN* iko *clear* sana na Mheshimiwa Rais Hayati Mkapa alisaini mwaka 1996, lakini eti ramani ambayo inachorwa na Maliasili na Utalii ndiyo inasema ile ramani ina-*extend* kwenda Kiteto. *It is a bit funny* kwamba ramani eti *GN* iliyosainiwa na Rais zinapishana, lakini hii yote inatokea kwa sababu wale walichora ramani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi msiruhusu mtu yeyote nchi achore ramani yake. Sheria iko *clear* sana, ninyi ndio *custodian* wa ardhi nchi hii. Mkishatutawanyishia mkasema hii ni ya Kijiji, hii ni ya Hifadhi, hii ni *general land,* ninyi mnabaki kusimamia. Mwenye shida yoyote anakuja kwenu. Siyo mtu anataka ardhi ya Kijiji, anachora ramani mwenyewe, anapeleka *GN* mwenyewe, haiwezekani. Msiruhusu tena. Najua migogoro mingi mnayopata ninyi inasababishwa na watu wengine. Kwa hiyo, mkisimama *firm* ninyi ndiyo *custodian* wa ardhi nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Kifungu cha 181 cha Sheria ya Ardhi, inasema, leo tukitunga sheria nyingi nyingi kidogo, ikatokea mgongano wa sheria hizi, *on lands' matter* Sheria ya Ardhi *takes precedent on lands' matter*. Kwa hiyo, wakati mwingine sijui migogoro inatokea wapi? Inatosha kwa Waziri wa Ardhi kusema Hapana. Akishasema hapana *definition* inayotokana na Sheria ya Ardhi ndiyo inakwenda hivyo. Siyo Sheria ya Wanyamapori. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine kijiji kipo miaka 20, Wenyeviti wamechaguliwa miaka 20, TAMISEMI inatambua, ina *CVL* lakini kuna mabingwa wengine wanakuja wanatengeneza ramani wanaingiza kwenye vijiji halafu inaanza migogoro. Nadhani migogoro hiyo muihamishe kutoka *field* ije kwenye Ofisi zetu hapa. Waje kwenu mkae TAMISEMI, Ardhi na Maliasili. Kaeni mnyongane Ofisini huku, *but don't bring the confusion* kwa wananchi, kwa sababu hakuna mwananchi anachora *CVL* ni Taasisi za Serikali wala hakuna Kijiji kinachojiandikisha chenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *this time* Mheshimiwa *Attorney General* ambaye namheshimu sana, *I think is the only man* ambaye amekuwa *DPP* akaenda *Judiciary* na sasa *Attorney General*. *Sometimes* migogoro inazuka, unakwenda Mahakamani, unashindwa ku-*enforce* eti kwa sababu unakuta ng'ombe, bingwa mwingine kauza na kesi inaendelea Mahakamani, tusikubali. Jana Mheshimiwa Mbunge wa Morogoro Kusini aliongea vizuri sana na naomba niwashawishi Wabunge hapa; hapa tumeletwa na wavuvi, wakulima na wafugaji. Ikija *issue* inayomgusa mkulima, mfugaji na wavuvi tusimame, wala hakuna Mbunge hapa ambaye ana wafugaji peke yake kwenye Jimbo lake, wala hakuna mkulima ambaye eti ana wakulima peke yake kwenye Jimbo lake. Sisi wote ni viongozi tusimamie migogoro hii bila kuvuta upande wowote

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nawapongeza wananchi wangu wa Kiteto. Kiteto imetulia sasa, lakini bado kuna vitu kidogo kidogo hivi; mara mfugaji ameingiza ng'ombe shambani, unaambiwa kuna mkulima ameingia kwenye maeneo ya kilimo. Hiyo ipo kidogo kidogo, lakini *to be exact, imetulia*. Nawapongeza sana wananchi wangu wa Kiteto. Nami nawaambia kupitia Bunge hili, mimi sina mtoto wa mgongoni na wa kifuani; wakulima, wafugaji wote wanaoishi Kiteto ni wa kwangu. Wote nawaomba mwendelee kutulia hivyo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi, Mifugo na Wanyamapori, tulikuwa tunaongea hapa na yule Mbunge wa Morogoro Kusini, migogoro hii siyo ya kwenu peke yenu. Mkitengeneza maeneo *hotspots* yenye migogoro, mkatengeneza ma-*champion* Wabunge hapa Bungeni, tutasaidiana tuende tuelimishe wananchi wetu na migogoro hii itapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesoma ripoti ya Kamati hapa na kwa kweli Wizara imekuja na *very ambitious plan* kwa kweli nzuri sana, wanataka kupima asilimia 50 ya Kijiji, lakini Tume ile ya Matumizi Bora ya Ardhi wana upungufu wa Shilingi bilioni tisa. Kwa kweli tuwasaidieni. Mheshimiwa Sillo rafiki yangu Kamati ya Bajeti hebu mtafute Shilingi bilioni 10 muwezeshe hii Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi ili Vijiji vipimwe. Vijiji vikipimwa, migogoro itapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwashawishi wote kwa kweli tupitishe bajeti hii ya Wizara hii wakafanye haya yote ili mwakani tukutane hapa wakati tuna furaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Edward Olelekaita. Tunaendelea na Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo na Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, ajiandae.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, Muumba wa Mbingu na Dunia kwa kutujaalia uhai na leo hii tuko hapa Bungeni, tunachangia Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Dkt. Angeline Mabula na Mheshimiwa Ridhiwan Kikwete, mwanangu kwa kazi nzuri wanazozifanya. Pia nawapongeza watendaji wote wa Wizara ya Ardhi kwa kazi nzuri ambazo wanaendelea kufanya kuiweka Wizara hii vizuri na kufanya Watanzania waweze kufurahia ardhi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu pamoja na hizo pongezi kuna mambo ambayo ningependa kuyazungumza kwenye Wizara hii. Kwanza kabisa napenda

kuzungumza kuhusu Tume ya Taifa ya Mipango ya Ardhi kama walivyoweza kuzungumza watangulizi wengine. Kazi za Tume hii ni kuipima ardhi ya Tanzania, lakini Tume hii haina meno ya kupima ardhi ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ardhi ya Tanzania ikipimwa itajulikana maeneo ya wafugaji yako wapi, maeneo ya wakulima yako wapi na itajulikana maeneo ya mambo ya jamii yako wapi; kama shule na Hospitali. Hii itapunguza sana mwingiliano na vurugu zilizopo kati ya wakulima na wafugaji. Kazi hii inashindwa kutekelezeka kwa sababu Tume ya Mpango wa Ardhi inapewa fedha ndogo. Haieleweki akilini, Tume ambayo inapima ardhi ya Tanzania inapewa Shilingi bilioni 1.4 na hata mwaka 2021 ilipewa Shilingi bilioni 1.9. Naiomba Serikali, kama kweli inataka kuondoa matatizo ya wafugaji na wakulima nchini Tanzania, iipe Tume hii fedha za kutosha. Migogoro mingi iliyopo ni kwa sababu ardhi ya Tanzania haioneshi mipaka ya mfugaji iko wapi, mipaka ya mkulima iko wapi; na mipaka ya mashamba ya mwananchi wa kawaida iko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Tume pia ina Bodi ambayo siyo ya Utendaji. Tume hii ina Bodi ya Ushauri. Ili Bodi hii iweze kufanya kazi, inatakiwa iwe *Executive Board,* lakini hii ni *Advisory Board*. Naomba Serikali ibadilishe sheria ili Tume hii iweze kuwa na Bodi ambayo itakuwa ni Bodi ya Wakurugenzi, ambayo itakuwa na meno na pia itaweza kutoa ushauri mzuri kwenye Tume na Tume iweze kufanya kazi zake vizuri. Pia Tume hii itakapokuwa imepata mambo hayo, itaweza kuwa na bajeti yake. Sasa hivi Tume hii haiwezi kupanga mambo yake ya Bajeti kwa sababu haina Bodi yenye meno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu kusisitiza, kama jinsi wachangiaji wengine walivyosema, Tanzania tuna Vijiji 12,319 lakini Tume hii tangu imeanzishwa imeweza kupima vijiji 2,565. Ukienda kwenye Ilani ya CCM kama wengine walivyosema, inasema mpaka kufikia 2025 angalau vijiji 80,000 nchini

Tanzania viwe vimepimwa, lakini kwenye mpango wa matumizi wa 2020 mpaka 2025 wenyewe umesema angalau asilimia 50 ya vijiji viwe vimewekewa mpango wa matumizi. Kutokana na hilo, naiomba Serikali iangalie ni jinsi itaweza kuipa nguvu hii Tume ya Taifa ya Mpango wa Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa kuzungumzia hapo hapo kwenye Tume suala la uhaba wa wafanyakazi. Tume hii ina wafanyakazi 79 tu nchini Tanzania. Ina uhitaji wa wafanyakazi 179, kwa hiyo, kuna upungufu wa wafanyakazi 100 kwenye Tume hii. Ili Tume iweze kufanya kazi mikoani vizuri, inatakiwa iongezewe wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kuhusu Kamati iliyoundwa na Mheshimiwa Rais; Kamati ya Mawaziri nane ambayo ilipita kuzungumzia migogoro ya ardhi. Kwanza kabisa, napenda kuishukuru Serikali pamoja na Mheshimiwa Rais kwa kuunda hiyo Kamati ya kushughulikia migogoro ya ardhi nchini Tanzania. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais, lakini pamoja na hizo pongezi, nimpongeze tu kwa Tuzo aliyoipata ya kuwa Kiongozi bora duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia Kamati ya Mawaziri nane kwa sababu Mawaziri walipita kukagua masuala ya ardhi na matokeo yake Serikali ilitoa vijiji 975. Katika vijiji 975, vijiji 925 Serikali iliwapa wananchi. Katika Mkoani kwangu Katavi vijiji 60 tulipewa. Sasa basi katika hivi vijiji 60 vya Mkoani kwangu Katavi, havijapewa *GN* namba. Pia kuna matatizo makubwa katika utekelezaji, kwamba kuna maeneo ambayo vile vijiji vimepewa lakini bado kuna mamlaka zinakwenda kuwafukuza wananchi na kuwachomea nyumba. Nitoe mfano Kijiji cha Kaseganyama Wilaya ya Tanganyika, eneo la visima viwili, wananchi wale wamechomewa nyumba, na mazao yao na kufukuzwa wakati walikuwa wameruhusiwa kukaa pale.

Mheshimiwa Spika, nimetoa mfano Kijiji cha Kaseganyama Wilaya ya Tanganyika, eneo la Visima Viwili, wananchi wale wamechomewa nyumba lakini pia wamechomewa mazao yao na kufukuzwa wakati walikuwa wameruhusiwa kukaa pale. Pia vipo Vijiji kwa mfano vya Kapalala, Sempanda, *operation* ya kuwafukuza inaendelea.

Mheshimiwa Spika, siyo Kapalala tu, zipo Kata za Ilunde na kule Inyonga bado kuna *operation* kama hizo za kuwafukuza zinaendelea. Vile vile Kata ya Kamsisi kule Inyonga nako pia wananchi wamechomewa nyumba pa wamefukuzwa kwenye maeneo ambayo tena kuweka hali kuwa mbaya, Serikali ya Kijiji cha Kamsisi iliwauzia wananchi yale maeneo na ikapata fedha ambazo iliweza kujenga zahanati, lakini leo hii watu wa *TAWA* wameingia pale wanawafukuza wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niombe mamlaka hizi zisiwe zinaingiliana, kama Serikali iliweza kutoa vile vijiji 920 ili wananchi wavitumie, tunashukuru sana na Mkoa wangu wa Katavi ukapata vijiji 60. Sasa kwa nini kunakuwa na mwingiliano wa mamlaka, kwa nini mamlaka nyingine ije kuwafukuza wananchi wakati walikuwa wameruhusiwa; na Kamati ya Mawaziri Nane ilipita na kuwakagua na kupewa ile ardhi. Sasa naona kuna mwingiliano wa mamlaka katika utendaji, haiwezekani, Serikali hiyo iwape wananchi vile vijiji kwamba wakae halafu Serikali hiyohiyo irudi kesho yake mamlaka nyingine iwaondoe na kuwachomea nyumba. Ningeomba sana Serikali ilirekebishe hili jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala ambalo ningependa kulizungumzia ni maeneo ya malipo kwa wananchi ambao Serikali inachukua ardhi yao. Kule Mpanda Mkoani Katavi kuna maeneo ambayo yana mgogoro mkubwa wa ardhi, maeneo ya Kampuni, Ilembo, Misukumilo, Mpanda Hotel, wananchi wametoka katika ile ardhi lakini wengine hawajalipwa malipo yao mpaka leo. Ningeomba

Serikali inapowahamisha wananchi kwa ajili ya kujenga mambo ya maendeleo ya nchi yetu kama shule au zahanati, basi iwe inaandaa malipo kwa wananchi hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili kwa sababu kumekuwa na mgogoro mkubwa katika maeneo hayo niliyoyataja ambayo yapo pale Mpanda Mjini. Wananchi waliachia ile ardhi na Serikali imeanza kujenga taasisi zake nyingi, imejenga kama Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Katavi, ipo kwenye maeneo ambayo wananchi bado wanadai ile ardhi; lakini mahakama imejengwa kule, vituo vya polisi na ofisi za Walimu, lakini unashangaa ni kwa nini maeneo hayo bado yana mgogoro wananchi hawajalipwa. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda w Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kengele ilikuwa imelia dakika moja nyuma.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kuunga mkono hoja ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimia Taska Restituta Mbogo. Tunaendelea na Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava na Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara ajiandae.

Mheshimiwa Mnzava hayupo, tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Thea M. Ntara na Mheshimiwa Jesca J. Msambatavangu ajiandae.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nianze kwa kuipongeza Wizara ikiongozwa na Dkt. Mabula na Mheshimiwa Ridhiwani. Pia niwapongeze watendaji waliopo kwenye hiyo Wizara Katibu Mkuu akiwa

ndiye kiongozi. Sasa licha ya changamoto nyingi ambazo zimesemwa bado wanajitahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita sana kwenye vyuo hivi vinavyohusiana na ardhi. Tuna Chuo cha Ardhi Tabora, kuna hiki Chuo kikubwa cha Ardhi hapo Dar es Salaam, kuna Nelson Mandela, kuna chuo kinaitwa *UDSM*, hivi vyuo vyote vinajihusisha moja kwa moja na ardhi. Sasa niseme hivi Serikali, niliongea wakati fulani, hivi Serikali wanaonaje wavitumie hivi vyuo katika kufanya *research* na kazi zinazohusiana na ardhi ili kupunguza upungufu huu wa wafanyakazi. Hivi vyuo vipo hapo lakini havitumiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumza mwaka jana, ni kiongozi mmoja tu anaitwa Mheshimiwa Sagini wakati akiwa *RAS,* nami nikiwa *RAS* Tabora, alikuwa ndiyo anatumia kile Chuo cha Tabora kufanya kazi zake kule Simiyu. Leo hii mikoa ina changamoto nyingi lakini unakuta hivi vyuo hawavitumii; mpaka nikajiuliza au kuna kitu hawakiweki vizuri ndiyo maana hawawatumii hawa watu. Hebu watumie hawa wa Chuo cha Ardhi, *MUST*, Tabora, *UDSM* na Nelson Mandela, hasa katika maeneo ya *IT* kule Nelson. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije niseme jambo lingine, niiombe Wizara ya Ardhi, wasaidiane au washirikiane na Wizara ya Fedha, Wizara ya Elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu, kuona namna gani wataongeza bajeti hasa katika hiki Chuo cha Ardhi kwenye *research*. Sasa kutokana na idadi ya wanafunzi waliopata mikopo kuwa wengi na lilikuwa ni jambo zuri sana, kwa hiyo fedha za *research* zikapungua sana, hivyo, unakuta hawa wanafunzi wa Chuo cha Ardhi wanakwenda kwenye *research* wanafanya *research* kwa wiki moja; hivi kuna *research* kweli ya wiki moja kwa mwanafunzi. Kinachotokea ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unisikilize, kinachotokea unajua ni nini? Watoto wale wana-*copy* au

wanagushi *researches* za kwenye mitandao, hawawezi kufanya *research* zilizokamilika; kwa hiyo, *forgery* inaanzia kwenye vyuo; ndiyo maana wakienda *field* kwenye halmashauri zetu, mahali panahitajika nondo 10, wanaandika nondo mbili. *Forgery* inaanzia chuoni, tumeshindwa kuwafanya hawa watoto wakafanya *researches* za uhakika kwa hiyo, wana-*copy* tunapata *degree fake,* halafu baadaye tunalaumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana, sasa tuangalie namna gani tunaweza kutumia mifuko katika kuongeza bajeti ya *research* kwa hao wanafunzi, hivihivi tunapoteana. Hao watu wathaminishaji, tunapata watu wa *procurement*, *Engineers*, sijui wengine wanawaita *Valuers* nasema wote hawa wanahitaji kufanya *researches* za kutosha. Sasa ardhi kuna hilo tatizo na naomba Mheshimiwa Waziri alichukue hilo. Vijana wanakwenda wanafanya *research* wiki moja kweli! Hili litatuangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo nije kwenye *National Housing*. *National Housing Corporation* wanafanya kazi vizuri sana, tulikagua hata wakati ule wamekwenda kufanya marekebisho kwenye sekondari, walijitahidi sana wakati tulilinganisha na lile Shirika lingine, walijitahidi sana. Hata hivyo, niseme, hizi nyumba za *National Housing,* mimi ni mdau nina nyumba pale Tabora, nikishuka pale nataka kuingia naangalia kushoto na kulia, nani ananiangalia naingia kwenye hii nyumba, yaani unaweza kusema ni magofu. Ukiangalia vijana wanaohusika kwenye *National Housing* hawafanani na hizo nyumba. Mheshimiwa Msechu, kuna kina Merkio, akina Deo, sijui akina Elias ni vijana ambao ukiwaangalia hawafanani na zile nyumba za *National Housing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa wakaangalie ni namna gani watazifanyia ukarabati na kazi hiyo wanaiweza akina Msechu, hebu wazibadilishe; tunataka wawe na

*uniqueness* ya *National Housing* na wanaweza kufanya hivyo. Mandhari yake nyingine hapa zipo Iyumbu zinaitwa *Satellite*, waende wakaziangalie, tunataka zilete mandhari, zioneshe kabisa kwamba hizi nyumba zinasimamiwa na vijana wasomi na wanaoweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niende kwa wafanyakazi wa *National Housing* na hasa vibarua. Wananiambia vijana wale, wanafanya kazi, lakini Mkurugenzi akaangalie wakifanya kazi wapate malipo kwa wakati. Akifanya hivyo kila mtu atasema hivyo sasa kweli tumempata Msechu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nikushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara. Tunaendelea na Mheshimiwa Jesca Msambatavangu na Mheshimia Deo Sanga ajiandae.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru pia kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii ya Ardhi na nitakuwa na mambo makubwa mawili. Niwapongeze kwanza kwa kazi nzuri pia ambayo wanafanya kwa sababu yapo mazuri mengi pia ambayo wanayafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka kuchangia kuhusiana na mpango wa matumizi ya ardhi na uendelezaji wa makazi. Kama Mbunge mmoja alivyokwishasema hapa; ardhi ni nguzo moja wapo katika nguzo nne ambazo Mwalimu Nyerere alisema, tunahitaji ili tuendelee, kwa sababu kila kitu kinafanyika kwenye ardhi. Sasa basi, kwenye upande wa makazi na matumizi bora nimeona kwamba wanasema mpaka 2025 inatakiwa vijiji vyote viwe vimepima na wamejiwekea namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miji tunayotoka pia kuna maeneo ambayo ni *peri urban,* haya sijaona mpango wake wamewekaje, yaani kwenye miji hakuna vijiji lakini tuna mitaa, lakini ile mitaa inaitwa mitaa kwa sababu tu ipo kwenye *municipals* au kwenye majiji; lakini ukiangalia hali halisi ni kama vijiji. Sasa sijui hii inaingizwa kwenye mpango gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni cha muhimu sana kukizingatia kwa sababu inatuletea shida hata kupeleka huduma kama hatuweki huu mpango wa matumizi bora ya ardhi mapema; hata kupeleka huduma kwa wananchi inakuwa ni kazi. Wakati ule Mwalimu Nyerere alianzisha zile *program* za vijiji vya ujamaa, *of course* yeye alianzisha kwa sababu ya mambo yake ya ujamaa na siasa za ujamaa na kujitegemea, lakini zilikuwa zina msaada kwa sababu hata wanapopeleka huduma wanawakuta wananchi wapo sehemu moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunataka kujenga barabara, unamkuta mtu alikuwa ni mwindaji, akaenda kuwinda mbali na wenzie, baadaye akajenga nyumba, akaanzisha familia iko mbali sana, sasa kule wanaendelea wanatengeneza familia wapo watu 200, wapo watu 150 kutoka kwa wenzao walipo ni kilometa zaidi ya 70 au 60; Serikali inalazimika kupeleka barabara mpaka kule, kuwapelekea shule lakini hawa watu wangekuwa sehemu moja kwenye kijiji ingelikuwa ni rahisi au kwenye mtaa, ingekuwa ni rahisi ku-*concetrate* kwamba tunawapelekea mahitaji ya muhimu pale ya huduma; lakini yale maeneo mengine wakatumia kwa ajili ya uwindaji au kwa ajili ya kilimo kama ambavyo wametumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamesema wanaimarisha *TEHAMA*, naomba katika zoezi la kuimarisha *TEHAMA* waangalie pia kuwapa mafunzo watu wao wa chini hasa kwenye kada hizi za chini kwenye halmashauri. Nasema hivi

kwa sababu wengi, leo ukienda kwenye halmashauri wanatoa risiti za kuwadai kodi za ardhi wananchi ambazo siyo halisi. Ukiwauliza wanasingizia mfumo, wakati mfumo ule anau-*feed* mtu, hakuna mfumo ambao unajiweka peke yake halafu una *generate data* peke yake, ni watu ndiyo wana *feed* zile *information* kwenye mfumo. Sasa inaonekana watu wanakuwa hawapewi mafunzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine tunaomba kwenye mambo ya MKURABITA, sasa hivi kwenye miji yetu MIKURABITA haipo tena, zile *program* za MKURABITA za kupima yale makazi ambayo hayakuwa rasmi haziendelei, sasa ujenzi holela unaendelea. Hata hivyo, kipo kipengele waliotoa kwenye Kamati zetu za Mipangomiji, cha kupitisha vibali vya ujenzi, wakaacha inawezekana walikuwa na nia njema kwamba vitolewe kwa wakati, viende na kasi na wananchi kwa sababu zile Kamati zina muda maalum. Hapa nafikiri wanatakiwa warudie waangalie ili kwamba Kamati zile zipewe *mandate* tena ya kuwa zinatoa vile vibali; kwa sababu tayari katika miji yetu ujenzi holela unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ninalotaka kuongea linahusiana na kodi ya ardhi *(land rent)* hasa kwenye taasisi; Taasisi za Dini, Taasisi za Shule na Taasisi za Vyuo. Ukiangalia hasa kwenye shule binafsi na kwenye vyuo binafsi. Suala hili limekuwa ni tatizo kubwa lakini katika hotuba ya Mheshimiwa Rais, alikuja hapa tarehe 22 Aprili, 2021, akatuambia kasome ile hotuba yake kitabu chake ukurasa wa 10, *paragraph* ya kwanza, ya pili mpaka ya tatu; alielezea ni namna gani ambavyo mazingira yetu ya uwekezaji wa biashara hayajaboreshwa; hasa kwenye Sera, Sheria na Kanuni zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akaahidi katika *paragraph* ya kwanza kuonesha anaboresha sera, sheria na kanuni. *Paragraph* ya pili na kuelezea hatua zinatakiwa kuchukuliwa ili kuvutia uwekezaji na sekta binafsi kuwekeza; lakini

*paragraph* ya tatu akasema, nchi yetu imekuwa ikilalamikiwa kwa kutokuwa na mazingira mazuri ya uwekezaji. Kwanza kutokuwa na kodi zisizokuwa na utulivu, lakini pia kuwa na sera ambazo zinabadilika badilika, hiki ni kitu ambacho hakivutii wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tuna watu wamewekeza kwenye elimu, uwekezaji kwenye elimu ni *investment* ya muda mrefu, *return* yake *on investment* ni zaidi ya miaka 10. Leo *land rent* unapokwenda kumchaji mtu mwenye shule binafsi, kwenye eneo la eka tatu katikati ya mji kwa mwaka anatakiwa kulipa milioni tisa, milioni sita inatoka wapi? Sasa uwekezaji umeanza kuwa kwa sababu hizi shule binafsi ndani ya manispaa lazima awe na eka tatu ndani yake kuna choo, viwanja vya michezo, madarasa, maabara, *library* vyote hadi choo kinachajiwa *land rent,* leo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakuwaje wakati hawa watu binafsi ni wawekezaji, wametupunguzia msongamano kwenye shule zetu za *public*; lakini hawa watoto ni watoto wa Watanzania, Watanzania hawa wanaosomesha kwenye shule binafsi wana haki kabisa ya kuhudumiwa kielimu na Serikali hii, lakini wameamua kulipa kodi, wameendelea kusomesha watoto wao kwa gharama zingine, kwa nini tuwaongezee mzigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie katika hizi shule binafsi, Serikali inatumia zaidi ya gharama za asilimia 97 kumsomesha mtoto kwenye shule ya *public,* lakini haichangii chochote kwenye shule ya *private*. Leo hii shule ya *private* inalipia fire, yaani shule ikitaka kuungua lazima ilipe ili ije izimiwe moto. Leo hatuna hata *grant* ya *temptation* tunayopata, unalipa *land rent* wakati fulani Katibu wa Wizara ya Fedha aliona kwamba suala la kuchaji kodi kwenye shule wakati ni taasisi zinazotoa huduma akazuia tukatolewa kodi ya *SDL;* lakini kodi hii imerudishwa kwa mtindo wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, vile vitu alivyoongea mama Samia kuangalia sera na kanuni zetu; kanuni mojawapo inayowatesa wananchi wa Tanzania ni ile kumpa *commissioner room* na kumpa *power* zaidi ya Bunge, nasema zaidi ya Bunge kwa sababu gani haiwezekani kwenye hati mtu aandikiwe hati hii utalipa kwa mwaka Sh.1,000,000 labda ndiyo itakuwa land rent yako; Kamishna anakaa anabadilisha mtu alipe milioni sita au milioni tisa nani hapo mwenye mamlaka kuu? Hivi ndivyo vipengele ambavyo Rais alisema viondolewe kwenye kanuni, sera zetu na sheria kama zinawakandamiza Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani leo tukafikiri viwanja vya michezo navyo vilipiwe kwa utaratibu upi? Tuwaangalie hawa watu kwa sababu ni wawekezaji wa ndani na tuwasaidie; na kwenye maeneo ya Makanisa, maeneo ya Vyuo, hawa wamechukua jukumu la Serikali la kuelimisha Watanzania, kwa nini tusiwasaidie kama hatusaidii hata kulipa mishahara, watu hawa hata fedha ya kukaguliwa, kuletewa mitihani, wanalipa mitihani, kukaguliwa lakini hawajalalamika. Unaposema watu hawa wanachaji fedha, basi umchaji kodi, ujue ile kodi inapelekwa moja moja kwa Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunawaomba ndugu zetu wa ardhi, kwa sababu wao ni msingi mmojawapo wa maendeleo kwa hiyo wasiposimamia vizuri sera hii na wakaweka kodi za aina hii maana yake ni kwamba huo mhimili hautasimama vizuri na hatutaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Ameshamaliza muda wake, ahsante sana Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nakushukuru sana. Naomba hilo lishughulikiwe.

**MWENYEKITI:** Haya, tunaendelea na Mheshimiwa Deo Sanga, baadaye Mheshimiwa Josephat Kandege ajiandae.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niwe mmoja wa kuchangia katika Wizara hii. Niungane na Wabunge wenzangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuwaletea Watanzania maendeleo; na hata Tuzo aliyoipata hii ni heshima kwetu kubwa sana Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nimpongeze sana Dokta, Waziri wa Ardhi kwa kazi nzuri anayoifanya pamoja na msaidizi wake Ridhiwani Kikwete, mchapakazi, songambele kazi ni nzuri, tunategemea atamsaidia Waziri kufanya kazi nzuri ya kuwaletea maendeleo Watanzania. Vile vile Katibu Mkuu Kijazi na wasaidizi wake, wanafanya kazi nzuri katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nielezee tu machache. Naishukuru Wizara ya Ardhi kwa kutupatia fedha za kupima ardhi, Halmashauri ya Mji wa Makambako, tunawashukuru sana mmefanya kazi nzuri na ndiyo sasa tunaendelea, lakini ombi langu kubwa Mheshimiwa Waziri, wako watu wanaokaimu katika nafasi mbalimbali sasa utendaji kazi unakuwa ni mgumu sana katika Halmashauri nyingi ikiwepo Halmashauri ya Makambako. Afisa Ardhi anakaimu zaidi ya miaka minne, tunaomba sasa athibitishwe ili kusudi afanye kazi yake kwa uhakika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wako watendaji ambao siyo waaminifu. Kwa mfano, kwa maksudi kabisa wako watu ambao wanatoa kiwanja kimoja zaidi ya watu wawili, hii ni

hatari sana. Wanagonganisha jamii ya Watanzania watu waanze kuichukia Serikali bila sababu. Tunaomba watu hawa wanaotoa kiwanja kimoja zaidi ya watu wawili wachukuliwe hatua za kinidhamu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo ambayo tuna matatizo ya fidia, hasa nizungumzie Jimbo la Makambako, baadhi ya wananchi imefika mahali aidha warudishiwe maeneo yao. Kwa mfano, eneo la kwanza ambalo lina tatizo ni eneo la Polisi kwa hiyo, tunakuomba Waziri ukae pamoja na Waziri wa Mambo ya Ndani muone namna ya kuwapa fidia hawa wananchi, maana eneo hili limetwaliwa kwa muda mrefu hawajalipwa fedha zao na sasa hawawezi kuendeleza kufanya kitu chochote. Ninaomba sana kwamba, jambo hili liweze kutatuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fidia ya pili ni eneo ambalo lilikuwa lijengwe soko la Kimataifa pale kwetu Makambako. Fidia baadhi ya watu walilipwa, baadhi ya watu 18 hawajalipwa, Wizara ya Viwanda na Biashara ndiyo ilikuwa inashughulikia kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri mkae pamoja ili muweze kutatua tatizo hili la wananchi wa soko la Kimataifa pale Makambako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ni eneo la Idofi ambalo Serikali ilikuwa inajenga *One Stop Center* imeshalipa fidia zaidi ya Milioni Mia Nane na kitu, bado hela nyingine wananchi kwa muda mrefu hawajalipwa. Ninaomba ukae na Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Mbarawa ili muweze kutatua tatizo hili wananchi waweze kufaidika na fidia yao ambayo wanaisubiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho katika fidia ni suala la umeme wa upepo, wananchi wa Makambako wanapata shida sana maeneo yale tangu yametwaliwa. Nilikaa na Waziri mwenye dhamana, Mheshimiwa Januari Makamba, alisema atalishughulikia. Sasa niombe mshirikiane

ili wananchi hawa waweze, kama imeshindikana waweze kurudishiwa eneo lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo Mheshimiwa Waziri napenda niliseme, tunataka Wizara ya Ardhi isimamie mpango bora wa matumizi ya ardhi ili mara nyingine Rais wetu aweze kupewa tuzo ya Kimataifa kutokana na matumizi bora ya ardhi. Tuzo hii atakayoipata itategemea na uchapaji kazi wenu, tuzo hii itakuwa ni faida kwetu Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo moja, Rais huyu wa Awamu ya Sita ni mteule na Mungu, huo ndiyo ukweli. Sasa siku nyingine nitawaambia kwa kirefu zaidi ili mujue huyu ni mteule na Mungu, leo naomba niishie hapa. Mheshimiwa Waziri chapa kazi, songa mbele, tuna imani kubwa na wewe na timu yako, pamoja na Naibu Waziri wako Mheshimiwa Ridhiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja ya ardhi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Deo Sanga. Tunaendelea na Mheshimiwa nilimtaja Josephat Kandege, Mheshimiwa Tauhida Galos, Mheshimiwa Francis Ndulane ajiandae.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kupata fursa ya kuweza kuchangia katika hoja ya Wizara hii, Wizara ambayo ni muhimu sana kwa Taifa letu.

Naomba niungane na Wabunge wenzangu ambao wamepongeza hotuba nzuri, ninampongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote kwa ujumla kwa kazi kubwa, nzuri, ambayo wanaifanya katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri akiwa Naibu Waziri, katika maeneo ambayo alipongeza kwamba, yamepimwa na kupangika vizuri ni pamoja na Makao Makuu ya Wilaya ya Kalambo, kwa maana ya Mji Mdogo wa Matai. Jitihada zile ambazo zilikuwa zimeonekena mpaka akasifia hapa katikati fedha hazijapatikana kwa hiyo, ule utaratibu uliokuwa ukitumika wa kuwezesha Halmashauri kupima maeneo yao vizuri naomba ile sifa ambayo alikuwa ametoa katika Wilaya yetu ya Kalambo kwa maana ya Mji Mdogo wa Matai isije ikaishia. Zile jitihada fedha ipatikane, tukipewa tunapima viwanja tunauza kwa wananchi na sisi tumekuwa waaminifu katika kulipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ambayo napenda nimuombe Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara ya Mifugo, washirikiane pamoja katika kutatua mgogoro wa *Ranch* ya Kalambo, hasa katika vijiji vya wananchi wa Katapulo, Kijiji cha Mimba, vijiji vingine vyote ambavyo vinazunguka *ranch* ya Kalambo ambavyo walitoa ardhi ile wakiamini kwamba, watakuwa wanaweza na wao kushiriki katika kufuga, kulima na kujifunza, lakini kwa bahati mbaya wamekuja wawekezaji ambao hakuna ambacho wananchi wa Mao, Mbuluma, wanaweza kujifunza. Kijiji cha Mbuluma na Mao wanakosa mpaka maeneo ya kuweza kuzika watu wao, ni wakati muafaka kwa Serikali kutizama namna gani itakavyowawezesha wananchi hawa kupata ardhi kwa ajili ya kilimo na mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee eneo lingine ambalo linahusu Muhimili wetu, kwa maana ya Bunge. Katika Kamati yetu ya Bajeti tulitoa mapendekezo tukiwa tunaona upo umuhimu kwa sasa, eneo la Bunge kuongezwa kwa maana ya kutwaa maeneo jirani. Katika hotuba ile ambayo tulikuwa tunawasilisha kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa maelekezo kwamba, Ofisi ya Bunge kwa kushirikiana na

Wizara husika waone utaratibu gani ambao utafaa, ili tuweze kutwaa maeneo yaliyo jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini upo umuhimu wa kufanya mambo haya? Kwanza ni suala zima la usalama. Bunge, kama Muhimili, ndiyo kama mti mkubwa ambao wananchi wote wa Tanzania wanatakiwa wakusanyike, lakini wametutuma sisi tukusanyike kwa niaba yao, kwa hiyo, eneo hili linahitajika kuwa na usalama. Maana sisi sote tunakubaliana kwamba, Mheshimiwa Rais ni sehemu ya Bunge na wakati mwingine anawaalika Marais wengine kuja kuhutubia Bunge hili, usalama ni jambo la muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haipendezi hata kidogo eneo muhimu kama hili likawa limezungukwa na maeneo mengine kama ambavyo ukienda upande huu unaambiwa kuna eneo la Soko la Mama Nchimbi, ukienda huku kuna Bohari, lakini pia ni ukweli usiopingika kwamba, eneo lenyewe unapoliongelea ni *square meter* 41,678 ni sawasawa na hekta 4.2 ambazo tunazidiwa hata miongozo ambayo inatolewa na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wanapotaka kujenga sekondari wanataka *at least* iwe eka 15. Sasa tunazidiwa hata na sekondari. Ni wakati muafaka kwa sababu, Bunge ndiyo tulitangulia Serikali ikafuata na sisi ni mashuhuda kwamba, ukienda kwenye Mji wa Serikali namna ambavyo maeneo yapo yakutosha na taasisi za Serikali zinaweza zikapewa huko ili mwananchi wa Tanzania akija kutafuta huduma aende kupata huko ambako uko Mji wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipendeze kama ikikupendeza kwa wakati mwingine tena utoe maelekezo hoja hii irejee Kamati ya Bajeti, tuwe na wakati muafaka wa kujadiliana namna gani ya kuweza kutwaa maeneo haya na Bunge liwe na eneo lake kubwa la kutosha. Nimepata fursa ya

kutembelea Mabunge mengine, nitolee mfano wa Bunge la kama Zambia, ukienda wana *zoo* ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wewe umekuwa ni shuhuda unahitaji wakati mwingine uende kushiriki shughuli za michezo, ukienda Jamhuri unaambiwa leo kuna tukio ambalo hutaruhusiwa Mbunge, unarudi kiunyonge, wakati katika hali ya kawaida sisi Wabunge tunatakiwa ofisi zote na huduma zote tupate tukiwa katika ukumbi huu na maeneo ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo haja pia ya kuwepo na hospitali yetu ya Bunge, tuna zahanati kwa Muhimili kama huu hailingani na hadhi yetu. Ifike wakati tuwe na eneo la kutosha, tuwe na hospitali yetu kubwa, nzuri, ili pale ambapo Mbunge anapokosekana kutibiwa hapa iwe ni ugonjwa ambao inabidi awe *refereed* kwa uhalisia, lakini kwa hali ilivyo tuna zahanati, imefika wakati tuwe na eneo la kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo taasisi za Serikali ambazo sidhani kwamba ipo haja hata ya kutoa fidia. Yapo maeneo makubwa huko nje ambako ndiyo wanatakiwa wakajenge ili kuboresha Mji, lakini ili kupisha Bunge, Bunge liwe na hadhi yake, juzi tulipata nafasi ya kutembelea Mahakama. Napongeza sana Mahakama wanajua kujinafasi, wamekuwa na eneo kubwa sana, tumeoneshwa mpaka sehemu ambayo kutakuwa na *swimming pool,* jambo ambalo kwetu sisi kila ukigeuka, ukienda nje huko ndiyo Wabunge wanalazimika ku-*park* magari yao, na siku za nyuma ilishawahi kutokea mpaka malalamiko Mbunge ame-*park* mara anakuta kuna kifaa kwenye gari lake kimeibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunatakiwa kuwa na ofisi za Makamishna, Wenyeviti wa Kamati na huko mbele ya safari hata Kamati hizi zinatakiwa ziwe na kumbi zake za mikutano. Sisi sote ni mashuhuda hata *canteen* yetu tuliyonayo wakija

wageni ukichelewa kidogo unakuta chakula hakuna, ifike wakati ikupendeze na nafasi uliyokalia utoe maelekezo ili tukutane na Wizara ya Fedha Kamati ya Bajeti, Wizara ya Ardhi na Wizara zote ambazo taasisi zake ziko hapa Jirani, tuweze kukaa tukiwa tumetulia tuone namna iliyo bora ya kutwaa maeneo haya ili Bunge liweze kujinafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipita huko nje msimu wa mazao unakuta kwamba, kuna Bodi ya Mazao Mchanganyiko, malori yanakuja kwa ajili ya kufanya shughuli ambayo katika hali ya kawaida shughuli hizo zilitakiwa zifanyike nje siyo karibu na Bunge. Usalama siyo mzuri kwa jinsi ambavyo tumezingirwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwa sauti hii na jinsi ambavyo nimeona unatikisa kichwa utatoa maelekezo ili Bunge tukutane na Serikali kwa maana ya Kamati ya Bajeti tujadiliane namna bora, ili kama kuna maeneo ya kutoa fidia itolewe fidia stahiki, lakini Bunge kama Muhimili ambao unajitegemea ambao ndiyo muwakilishi wa wananchi Tanzania lipate hadhi yake na eneo ambalo linalingana na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Josephat Kandege. Mheshimiwa Tauhida naona hayupo, Mheshimiwa Francis Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia bajeti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa tuzo muhimu ambayo ameweza kuipata ambayo inaendelea kuitangaza nchi yetu na kuendelea kuboresha mambo

mbalimbali katika nchi yetu, pili napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Ardhi pamoja Naibu wake kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja nijikite kwenye Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi. Mwaka 2006 katika Mkoa wetu wa Lindi Serikali iliridhia kuingiza mifugo kutoka katika Bonde la Ihefu, hii ilisababisha mifugo mingi kuhamishiwa katika Wilaya mbalimbali za Mkoa wa Lindi. Katika Wilaya ya Kilwa peke yake kati ya mwaka 2006 hadi 2007 mifugo isiyopungua Laki Moja iliingia katika Wilaya ya Kilwa. Pia hii ilisababisha sasa Serikali Kuu kupitia Wizara ya Ardhi pamoja na Halmashauri yetu ya Wilaya ya Kilwa pamoja na Taasisi ya *BTC (Belgium Technical Cooperation)* kuweza kushirikiana kwa pamoja kuweza kupima na kuweza kuboresha matumizi ya ardhi iliyopo katika Wilaya yetu ya Kilwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi iliweza kupimwa jumla ya hekta 337,500 kwa ajili ya kulisha ng'ombe wapatao 168,750, lakini kwa vipindi tofauti kati ya mwaka 2007 hadi sasa takribani miaka 15 iliyopita, mifugo mingi imeendelea kuingia katika Wilaya ya Kilwa pamoja na Mkoa wa Lindi kwa ujumla. Wilaya ya Kilwa peke yake mifugo inayokadiriwa kufikia 350,000 imeingia, vilevile wale waliokuwepo tangu mwaka 2006 wameendelea kuzaana na mifugo mingi imeingia kwa kupitia njia za holela, mingine imepita kupitia Pori la Akiba la Selous, mingine imeingia kutokea Mkoa wa Pwani, kwa hiyo, sasa hivi kuna takribani ng'ombe, ng'ombe peke yake wanakaribia 500,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, imesababisha hali kuwa ngumu sana ya maisha ya wakulima wetu, pia wafugaji wenyewe kwa sababu, mpango wa matumizi bora ya ardhi umeshapitwa na wakati kwa sababu una zaidi ya miaka 15 tangu ulipofanyika. Na kwa mujibu wa utaratibu mpango wa matumizi bora ya ardhi unatakiwa uwe *reviewed* angalao kila

baada ya miaka 10, kazi ambayo haijafanyika na hiyo imesababisha kuwepo na changamoto kubwa, mapigano ya mara kwa mara, lakini mifugo kuweza kutangatanga hovyo katika Wilaya nzima ya Kilwa na Wilaya zote za Mkoa wa Lindi. Kwa hiyo, sasa hivi tuna hali ngumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda utambue ndani ya miezi 12 iliyopita wananchi wanne walipoteza maisha, wawili katika Kijiji cha Nanjilinji, mmoja katika Kijiji cha Nakiu, pia katika Kijiji cha Kipindimbi kuna mwananchi mmoja alipoteza maisha kwa hiyo, jumla ni wananchi wanne walipoteza maisha ndani ya miezi 12 iliyopita, lakini pia kumekuwa na vurugu za hapa na pale nyingi. Kwa mfano, Tarehe 07 mwezi Aprili mwaka huu katika Kijiji cha Ngarambi, *WEO* wa Kijiji kile, Afisa Mtendaji Kata, alivamiwa na kundi la wafugaji lakini bahati nzuri alikimbia na badaye alijisalimisha katika Kituo cha Polisi kule Somanga, lakini na wale wafugaji walichachamaa baada ya kuwa mifugo yao ambayo iliingia kiholela katika Wilaya ya Kilwa ilipokuwa imekamatwa, baAdae walimvamia Askari wa mgambo ambaye alikuwa analinda ile mifugo na kumjeruhi, matukio ya namna hii yamekuwa mengi mno kiasi kwamba, yanawakatisha tamaa wakulima wetu, lakini yanawafanya hata wale wafugaji wasiweze kufuga ng'ombe wao na mifugo yao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niiombe Serikali katika hili ijitahidi kuweza kuona sasa katika zile fedha kidogo zilizotengwa kwa ajili ya maboresho au Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi waweze kutumia hizo fedha, vilevile zije Kilwa tuweze kuona namna ambavyo tunatatua ile migogoro. Nina imani kama mpango wa matumizi bora utafanyika katika Wilaya ya Kilwa ambao katika kipindi kilichopita ule mwaka 2006/2007 ulifanyika katika vijiji 35 tu wakati Kilwa tuna vijiji 90, ni imani yangu kwamba, tutapunguza kwa kiasi fulani hii migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina uzoefu na kazi ambazo zimefanywa za maboresho ya mpango wa matumizi bora ya ardhi kule Kilombero. Kulikuwa na mradi mmoja unaitwa *Land Tenure Support Program,* umesaidia sana katika Bonde la Kilombero hasa Wilaya za Malinyi, Ulanga pamoja na Mlimba. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba, tukitekeleza vizuri ule mradi basi haya mambo ya mauaji, haya mambo ya watu kujeruhiwa basi yatapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli niseme ningependa kwa kuanzia Kata ambazo zinaongoza ziko 12 ambazo ni Kata ya Somanga, Kata ya Mingumbi, Kinjumbi, Kipatimu, Kandawale, Mitole, Njinjo, Miguruwe, Nanjilinji, Kikole, Likawage pamoja na Kiranjeranje, ikikupendeza kupitia Wizara ya Ardhi basi tuanze na maeneo hayo ambayo yamekithiri kwa migogoro kila kukicha. Nashukuru Mheshimiwa Waziri wakati tunatekeleza ule mradi wa *Land Tenure Support Program* kule Bonde la Kilombero wakati ule ulikuwa Naibu Waziri na mara kadhaa ulikuja katika Bonde la Kilombero kuhakikisha ule mradi unatekelezwa kwa ufanisi. Na kwa kuwa, ulitekelezwa kwa ufanisi, ulitatua changamoto nyingi sana ambazo zilikuwa zinawakabili wananchi wa maeneo yale ya Malinyi, Ulanga, Mlimba pamoja na Kilombero yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niseme nikuombe Mheshimiwa Waziri basi na sisi utufanyie kama vile ambavyo *experience* inaonesha kule tuliweza kutatua ile migogoro ya wakulima na wafugaji, kwa sababu ule mradi kupitia wataalam wetu wabobezi, kulikuwa na Dada mmoja anaitwa Siyabumi Mwaipopo, sasa hivi sijui yuko Mbeya, sijui yuko wapi, walifanya kazi nzuri sana. Kwa kweli, nawapa hongera kwa kazi ambayo ilifanyika kule, Kilwa basi tunaomba Mheshimiwa Waziri utuletee ule mradi, hata kama siyo ule, lakini angalao ulete fedha basi ili baadae ule mradi utafanyika kwa mfumo ule wa *revolving,* kwa maana tutapata hela kupitia zile hati za kimila pamoja na kazi

ambayo itafanyika watu watalipia kidogokidogo na mwisho wa siku tutajikuta vijiji vyote 90 tuweze kuvikamilisha kuvipima, lakini vilevile kuweza kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi na pia kupima mipaka kati ya vijiji hadi vijiji ambayo iko mingi tu sasa hivi katika Wilaya ya Kilwa. Siyo katika Wilaya ya Kilwa tu hadi Kilwa na Wilaya za majirani kama Liwale na Rufiji kwa kweli hali siyo nzuri kuna migogoro ya hapa na pale kati ya vijiji vya Wilaya moja kwenda Wilaya nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ni imani yangu kwamba, kwa kupitia utaratibu huu wananchi watapata hati za kimila, lakini vilevile watadumisha usalama na amani katika maeneo yao. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri utusaidie katika hilo ili tuondoe hii hali ambayo inaendelea kukua ya mapigano ya mara kwa mara, watu wanajeruhiwa, wanakufa na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Waziri kuna suala la migogoro kati ya vijiji vyetu vya Wilaya ya Kilwa pamoja na Hifadhi ya Pori la Akiba la Selous. Kuna vijiji vinne katika Jimbo langu peke yake, kuna Kijiji cha Nakingombe, kuna Kijiji cha Ntepela, kuna Kijiji cha Zinga, kuna Kijiji cha Nakingombe, hivi vijiji vinne vinapakana na Hifadhi ya Taifa ya Pori la Akiba la Selous kwa hiyo, niombe Mheshimiwa, tuliliongea hili wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja mwezi Oktoba mwaka jana kwa uchungu na masikitiko makubwa sana. Kulikuwa na mgogoro mkubwa sana kati ya *TAWA* na wananchi wa hivyo vijiji, bahati nzuri ilikuja Tume ya uchunguzi, ingawa majibu hatujayapata mpaka leo na sasa ni ktakribani miezi Sita inakaribia tangu ile Tume ilipokuja kuchunguza ule mogogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba majibu tupate mapema ili wananchi watulie waendelee kufanya shughuli zao za kiuchumi katika hayo maeneo…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndulane, muda wetu umemalizika wa siku ya leo.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku hii ya leo. Waheshimiwa Wabunge nawashukuru sana, nawapa pongezi kwa kazi nzuri mliyofanya na michango ambayo mmeitoa. Naamini kabisa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Naibu wake wako makini sana hapo kwa kusikiliza yale ambayo yana tija na maslahi kwa nchi yetu na ninaamini watayatafutia ufumbuzi kadri inavyowezekana.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaahirisha Shughuli za Bunge, kuna Tangazo moja ambalo linatoka kwa Katibu wa Bunge; Waheshimiwa Wabunge wote mnatangaziwa kwamba, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira inawaalika Wabunge wote kushiriki katika Maadhimisho ya Wiki ya Mazingira yatakayofanyika kuanzia Tarehe 28 Mei, 2022 hadi Tarehe 05 Juni, 2022 ambapo Kitaifa yanafanyika katika Jiji la Dodoma. Shughuli zitakazofanyika ni kama zifuatazo:-

(i) Tarehe 28 Mei, 2022 ni siku ya uzinduzi ambapo kuanzia saa 12:30 asubuhi yatafanyika matembezi ya hiyari yatakayoanzia maeneo ya Bunge hadi makutano ya barabara ya Dar es Salaam na barabara inayoelekea kwa Waziri Mkuu na baadae kufuatiwa na shughuli za upandaji miti. Mgeni rasmi atakuwa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(ii) Tarehe 5 Juni, 2022 ni siku ya kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani ambayo yatafanyika kuanzia Saa 02:30 asubuhi katika Ukumbi wa

Mkutano wa Jakaya Kikwete, Jijini Dodoma na Mgeni Rasmi atakuwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Waheshimiwa Wabunge wote wanakaribishwa sana kuhudhuria sherehe hizi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho Saa Tatu kamili asubuhi.

*(Saa 01.45 Usiku, Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 27 Mei, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*